**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 14 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:-**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Maoni ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 205

**Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mpanda**

**MHE. CAPT. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (wakati huo) ya 2005/2006 iliyowasilishwa Bungeni, Halmashauri ya Mji wa Mpanda iliundwa na kutangazwa kuwa na hadhi ya Halmashauri ya Mji, na kwa kuwa, Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya la tarehe 28 Juni, 2003 liliidhinisha kuanza kwa Mamlaka ya Mji Mdogo kwa Mujibu wa Sheria Na. 7 ya mwaka 1982 (*Local Government District Authorities):-*

Je, ni kwa nini hadi sasa Hati ya kuthibitishwa kuundwa kwa Mamlaka ya Mji wa Mpanda haijatolewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said A. Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mpanda ilikwishaanzishwa kwa Mujibu wa Kifungu Na. 13 hadi kifungu Na.19 vya sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 ya mwaka 1982. Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mpanda, ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 137 la tarehe 8 Juni, 1990.

Kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ambacho kilifanyika tarehe 28 Juni, 2003, kilijadili na kuidhinisha kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mpanda. Hati ya kuanzishwa kwa Mamlaka hiyo ya Mji Mdogo wa Mpanda ilikwisha kutolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda tarehe 1 Julai, 2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 52 cha Hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2005/2006, iliyowasilishwa na aliyekuwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, yalitolewa maelezo kwamba Serikali ilianza kutekeleza utaratibu wa kuanzishwa kwa Mji wa Mpanda.

Uamuzi huo wa Serikali umeendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kutolewa kwa Tangazo la Serikali Na. 218 la tarehe 29 Julai, 2005. Tangazo hilo linaonyesha utaratibu wa kisheria wa kuanzishwa kwa Mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu inakamilisha hatua za mwisho ya utaratibu wa Kisheria wa kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Mpanda. Utekelezaji huu unafanywa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ambapo yafuatayo yamekwisha kufanyika.

(a) Kutenga sehemu ya eneo la ardhi ya Mamlaka Mpya ya Mji wa Mpanda kutokana na eneo la ardhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda na kuweka usahihi wa mipaka ya maeneo ya Mamlaka hizo mbili za Serikali za Mitaa.

(b) Kuandaa Bajeti maalum ya Halmashauri ya Mji wa Mpanda kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2006/2007 kiasi cha fedha kilichotengwa ni Shs. 82,000,000/=.

(c) Kugawanya mali zinazohamishika na zisizohamishika pamoja watumishi waliopo na Ikama kwa ajili ya Mamlaka hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba ucheleweshaji wa kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mji wa Mpanda kulitokana na uchaguzi wa mwaka 2005. Ilikuwa kwa kipindi hicho tungetekeleza uanzishwaji wa Halmashauri ya Mji wa Mpanda tungekuwa tunaingilia mipango ya Tume ya Uchaguzi. Lakini sasa hivi Ofisi yangu iko tayari na inaendelea na *process* ya kuanzisha kwa Mji wa Mpanda. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yenye matumaini kutoka kwa Naibu Waziri.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atalihakikishia Bunge hili na wananchi wa Mji wa Mpanda kwamba atanikabidhi Hati hiyo kwa niaba ya wananchi wa Mpanda mara tu baada ya Mkutano huu wa Bajeti kumalizika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Spika, hiyo Hati ikikamilika tutamkabidhi bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Na. 206

**Mradi wa Kufua Umeme Kilombero**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika mradi wa Shamba la *KATACO Korea Tanzania Cooperation* Wilayani Kilombero, kulikuwa na mpango wa kufua umeme kwa kutumia maji ya *Hydro Electric Power Generation* kwa kukinga Bwawa kutoka Mto Mngeta na kwa kuwa, bwawa hilo lilijengwa na kati ya *turbines* tano zilizokuwa zifungwe ni *turbines* mbili tu zinafanya kazi, na umeme huo unatumika kwenye Makao Makuu ya Shamba hilo:-

Je, Serikali haioni kwamba, ni vema sasa Kituo hicho cha kufua umeme kikachukuliwa na Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* ili *turbines* zote tano zikafungwa na umeme kusambazwa katika Tarafa nzima ya Mngeta kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwamba, kasi itaongezwa ya usambazaji umeme vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kituo kidogo cha umeme kilichopo Mngeta ni mali ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Rufiji *(RUBADA)*. Kituo hiki kilijengwa kwa ajili ya matumizi ya *RUBADA* katika mashamba ya Mngeta.

Mheshimiwa Spika, Wizara inafahamu na imekwishatuma wataaalam kutathmini uwezekano wa kupanua na kukitumia kituo hicho kwa ajili ya vijiji vya jirani kama Michombe. Wizara imeanzisha mawasiliano na *RUBADA* pamoja na mwekezaji wa Shamba la *Korean Tanzania Cooperation (KOTACO)* kuona uwezekano wa jinsi ya kutumia mitambo hiyo kuwanufaisha wananchi.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Napenda kutoa maelezo yafuatayo:- Kwanza, lile shamba haliko tena katika umiliki wa huyo mwekezaji ndugu Erick Williams. Ameishanyang'anywa umiliki huo na *RUBADA*. Shamba hilo mpaka sasa halina mwenyewe na nilishaongea hapa kwamba tunaitahadharisha Serikali isije ikaliuza shamba hilo kwa *outlet purchase* kama walivyokusudia. Hivi ninavyoongea wameishaenda huko wanataka kufanya hicho kitendo bila ridhaa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, swali ninalotaka kuuliza ni kwamba sisi Mwenyezi Mungu ametujali tuna mito mingi mojawapo ni huo mto Mngeta ambapo tumeweka hiyo bwawa. Kama hilo haliwezekani basi tunaomba Waziri aseme kama anaweza kujenga njia nyingine ya umeme kutoka Kihansi ije kuhudumia Tarafa ikitiliwa maanani kwamba ni Tarafa pekee katika Tarafa tano za Wilaya ya Kilombero ambayo haina umeme na sisi ndiyo tunafua umeme wa Kihansi na wa Kidatu. Watu watajisikiaje umeme unapelekwa sehemu nyingine wao wakakosa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, inatosha.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilishatuma mtaalam mshauri kwenda kukagua eneo husika na Kampuni hiyo inaitwa *ICON analysis* ilivyokagua eneo hilo tumegundua kwamba uwezo wa mtambo ni kuzalisha kilowati 360 kwa hivi sasa na kuna uwezekano wa kuufikisha kwenye hatua ya kuzalisha megawati 1. Mahitaji ya shamba lile pamoja na kijiji husika kutokana na

tathmini ni kilowati 50. Na kwa hivi sasa mradi huu wa kupanua uwezo wa mtambo uko chini ya *ERT*.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inashughulikia suala hili na nia yetu ni kuhakikisha kwamba umeme unafika katika kijiji cha Mngeta.

Na. 207

**Hitaji la Umeme Loliondo**

**MHE. KAIKA S. TELELE** aliuliza:-

Kwa kuwa, nishati ya umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu; na kwa kuwa, ni azma ya Serikali ya Awamu ya Nne kupeleka huduma hiyo katika Makao Makuu ya kila Wilaya:-

(a) Je, ni lini Serikali itaupatia umeme Mji wa Loliondo ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro?

(b) Iwapo Serikali itaona kuwa ni gharama kubwa mno kupeleka umeme Loliondo ukitokea aidha Arusha, Mto wa Mbu, Karatu au Musoma; je, Serikali haiwezi kufanya mazungumzo na Serikali ya Kenya ili nishati hiyo ipatikane kutoka Mji wa Narok ambao ni karibu na Loliondo kuliko kusubiri umeme wa gridi ya Taifa ambao upatikanaji wake ni wa polepole mno?

(c) Je, Serikali katika mipango yake ya kusambaza umeme nchini haioni umuhimu wa kutoa kipaumbele kwa Wilaya za mipakani kama vile Ngorongoro (Loliondo) ili kuweka na kutunza heshima kwa wageni wa nchi jirani wanaohudhuria vikao vya ujirani mwema vinavyofanyika mara kwa mara katika Wilaya hizo za mpakani ukiwemo Mji wa Loliondo ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuupatia umeme Mji wa Loliondo, ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro, kwa kujenga kituo kidogo cha kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya Mto Pinyinyi. Kituo hicho kina uwezo wa kuzalisha *MW 2* ambazo zinatosha kusambazwa katika Wilaya yote ya Ngorongoro, Loliondo na vijiji vinavyozunguka Mji huo.

Gharama za ujenzi wa kituo cha umeme cha Pinyinyi zinakadiriwa kufika Dola za Marekani milioni 2 na ujenzi wa laini ya KV 33 kutoka Pinyinyi kwenda Miji ya Loliondo na Wasso inakadiriwa kugharimu Dola za Marekani 653,000.

Upembuzi yakinifu wa mradi umekwisha kamilika na Serikali imetuma maombi Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji wa mradi huo.

(b) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali haijafikiria kuupatia umeme Mji wa Loliondo kutokea vyanzo vya nchi jirani ya Kenya kutokea Mji wa Narok kwa vile Benki ya Maendeleo ya Afrika ilikwishaonyesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

(c) Serikali kupitia Shirika la Umeme *(TANESCO),* imeupa kipaumbele mpango wa kuipatia umeme Miji Mikuu yote ya Wilaya za Tanzania, ukiwemo Loliondo. Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO* inafanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha azma nzuri ya Serikali inatekelezwa.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, namshukuru sana Naibu Waziri kwa maelezo mazuri na yenye kutia matumaini. Lakini naomba niulize kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa katika Mpango wa *TANESCO* wa kuupatia Mji wa Loliondo umeme ni hadi mwaka 2015. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba hii haiendani na kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Nne ya Kasi Mpya, Ari Mpya na Nguvu Mpya, katika kuupatia Mji wa Loliondo umeme? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa kuna maporomoko ya maji kati ya Kijiji cha Kisangiro na Mhoro na ni kilomita 60 tu kutoka Mji wa Loliondo. Je, utafiti wa haraka hauwezekani ukafanyika ili pamoja na utaratibu huo wa kujenga kituo cha umeme iangaliwe ni ipi yenye gharama nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nilivyoeleza katika jibu langu la msingi ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya Wilaya zote nchini zinapata umeme.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itafanya kila kitu kitakachowezekana kufanywa kuhakikisha kwamba umeme unafika Loliondo pamoja na katika Makao Makuu ya Wilaya zote zingine hapa nchini haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuhusu matumizi ya maporomoko ya maji ambayo yako jirani tumeyapokea na Wizara yangu itayashughulikia.

Na. 208

**Benki Kuu Kununua Dhahabu**

**MHE. PHARES K. KABUYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miaka ya nyuma Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa ikinunua Dhahabu ya Tanzania na kusaidia kuinua uchumi wetu:-

Je, ni sababu gani zilizoukwamisha mradi huo uliokuwa mzuri katika kukuza uchumi wa nchi kwa haraka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa kununua dhahabu uliobuniwa na Serikali mwisho mwa miaka ya themanini na kutekelezwa na Benki Kuu ulikuwa mzuri na wa manufaa kwa Taifa na kwa wachimbaji wa dhahabu wadogo wadogo. Kwani uliwapa wachimbaji hao soko la uhakika na kipato kizuri na kikubwa zaidi kuliko kile walichokuwa wakikipata kutoka kwa walanguzi.

Mheshimiwa Spika, mradi huo ulikuwa pia na madhumuni ya kidhibiti uuzaji na ununuzi holela wa dhahabu ili kuweka biashara hii katika misingi imara iliyoratibiwa. Aidha, uliazimia kulipatia Taifa fedha za kigeni zilizokuwa adimu katika miaka ile. Baadaye mradi huo ulisitishwa kwa sababu ulikuwa umeanzishwa bila matayarisho ya kutosha. Benki Kuu iliuanzisha mradi huo bila kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwekeza vya kutosha katika vifaa vya kutathmini dhahabu *(gold assay)*.

(ii) Benki Kuu haikuwa imeajiri wataalaam wake wa kutathmini dhahabu, utathmini ulifanyika na wataalam ambao hawakuwa wameajiriwa na Benki. Kwa hiyo, kulikuwa na wakati ambapo Benki ilikuwa ikipata hasara kubwa kutokana na mapungufu hayo.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Benki Kuu ilisitisha mpango huu kwa muda ili kuzingatia mambo yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa biashara hiyo inaendeshwa kwa udhibiti wa kutosha hasa katika vituo vya ununuzi vilivyokuwepo wakati ule.

(ii) Kutumia utaalamu wa kutosha katika ununuzi wa dhahabu ghafi.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado inaona umuhimu wa kuendelea kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu na inaandaa utaratibu mzuri zaidi utakaohusisha Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini na Benki Kuu ili kuweka soko la uhakika na kipato kizuri kwa wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amesema kwamba mradi huu ulikuwa wa manufaa kwa Taifa. Kitu chenye manufaa kwa nini kichukue miaka 20. Hayo maandalizi ya kuweza kufanywa ili dhahabu ziendelee kununuliwa yanatumia muda gani ili yakamilike?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema ni kwamba mwanzoni Benki Kuu ilianzisha mradi huu bila kufanya utafiti mzuri na ilipata hasara kubwa. Sasa hivi tumeishagundua kwamba ni vizuri mradi huu ukaanzishwa tena tunawasiliana kwa karibu kabisa na Benki Kuu, Wizara ya Nishati na Madini na Wizara yangu kuhakikisha kwamba mapema iwezekanavyo wachimbaji wadogo wadogo wanapatiwa huduma.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Benki Kuu baada ya kugundua kwamba mradi huu wa kununua dhahabu haukuwa na manufaa ikaingia ubia kwenye MEREMETA na *Mwananchi Gold Mines.* Je, kwa kutumia sheria ya *Immunities and privileges* kifungu cha 10 Waziri atakubali kuleta Mikataba yote ya ubia wa Benki Kuu ya MEREMETA pamoja na Mwananchi *Gold Mines*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, Mradi wa MEREMETA ni tofauti na wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha akitoa majumuisho yake ya Bajeti ya Serikali alielezea kwa kirefu. Lakini yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Mbunge tunayachukua tutayafanyia kazi.

**SPIKA:** Natumaini kweli itakuwa hivyo.

Na. 209

**Punguzo la Ushuru wa Majiko ya Gesi**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, umuhimu wa kuhifadhi mazingira unakwenda sambamba na nia ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kupunguza au kuondoa ushuru kwa majiko ya gesi yanayoingizwa hapa nchini ili kuhamasisha wananchi wengi hasa wa Mijini kutumia zaidi gesi badala ya mkaa na kuni?

(b) Je, punguzo la ushuru kwa gesi iliyoingizwa nchini kati ya miaka ya 2003 – 2005 limesaidia kuongeza kwa kiasi gani viwango vya gesi inayoingizwa nchini na Kampuni za Mafuta?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira sambamba na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Pia Serikali imeona kuwa ipo haja ya kupunguza au kuondoa kabisa ushuru wa forodha kwenye majiko ya gesi na umeme yanayoingizwa nchini. Hata hivyo, kwa kuwa suala la Ushuru wa Forodha kwa sasa ni la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali imekwishapeleka mapendekezo yake katika Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuifuta kodi hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kwa lengo la kupunguza viwango vya Ushuru wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa kwenye gesi inayoingizwa nchini ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Katika kipindi cha kati ya miaka 2003-2005 gesi iliyoingizwa nchini ni kama ifuatavyo. Katika mwaka 2003/2004 kiasi cha gesi iliyoingizwa nchini ni kilogram 3,248,609, mwaka 2004/2005 ziliingizwa nchini kilogaram 2,342,104 na mwaka 2005/2006 ziliingizwa nchini kilogram 3,841,207.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Vilevile naomba kuishukuru Wizara hii ya Fedha kwa kuwa ilipunguza ushuru wa majiko ya gesi hivi karibuni. Kwa kweli katika maonyesho ya sabasaba watu wengi waliitikia kwa kununua majiko ya gesi kutoka kwa kampuni ya *ORYX. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado watu wengi wana hofu kutumia gesi majumbani. Sasa kwa kushirikiana na Kampuni ya mafuta Serikali au Wizara ina mkakati wa gani wa kuhakikisha kwamba inatoa elimu ili kuwaondoa hofu wananchi ili waweze kuendelea kutumia gesi kwa wingi zaidi badala ya kutumia mkaa na kuni? Hilo la kwanza.

La pili, Wizara ya Nishati na Madini hivi karibuni imeelezea kwamba upo utaratibu wa gesi ya songo songo iweze kuanza kutumika majumbani na vilevile upo mpango wa kuwezesha nishati hiyo kutumika kuendesha magari.

Je, ni lini mpango huu utatekelezwa ili vilevile kuiwezesha Tanzania iwe ni miongoni mwa nchi za kwanza katika Bara la Afrika kutumia nishati ya gesi katika kuendesha magari badala ya petroli na dizeli ambayo ni ghali sana?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza, tuna mkakati baina ya Makampuni yanayoagiza gesi nchini na Wizara ya Nishati na Madini kutoa semina na kutoa elimu kwa wadau wote watakaotumia gesi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, linahusu Wizara ya mwenzangu. Naomba Waziri wa Nishati na Madini anisaidie.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini hivi sasa inawasiliana na Serikali ya China ili kuweza kufanya mpango madhubuti ili kuhakikisha kwamba gesi ambayo inapatikana hapa nchini inatumika kwa ajili ya matumizi ya nyumbani pamoja na matumizi ya magari.

Mheshimiwa Spika, ningependa Mheshimiwa Mbunge avute subira kidogo tukimaliza kujadiliana na wenzangu huko China tulete mipango hiyo hapa nchini ili kuyakamilisha na kuhakikisha kwamba tunanufaika na gesi ambayo tunayo hapa nchini. *(Makofi)*

Na. 210

**Tanzania na Jumuiya za Kiuchumi na Forodha**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, sheria za *W.T.O.* zinataka kila nchi mwanachama iwe ni mwanachama wa kundi moja tu la ushuru wa Forodha na kwa kuwa, Tanzania inajadili *Economic Partnership Agreement (EPA)* na nchi za Jumuiya ya Ulaya na hivyo kuwa na *Common External Tariff (CET)* na nchi za *SADC – EPA;* na kwa kuwa, hivi sasa kuna *EAC – Customs Union*:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa *SADC – EPA* na *ESA – EPA* ni hatari kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni busara sasa kuwa na *EPA* chini ya *EAC Configuration?*

(c) Kufuatia hasara iliyopatikana tangu Tanzania ijitoe kwenye *COMESA:* Je, Serikali haioni kuwa ni busara kurejea *COMESA?*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe Zubeir, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Zitto Kabwe kwamba, kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za Shirika la Biashara Duniani *(WTO),* kila nchi inatakiwa iwe kwenye kundi moja tu la ushuru wa forodha ili kuhakikisha kuwa faida za kundi moja haziathiriwi na fursa zilizoko kwenye kundi lingine la Umoja wa forodha.

Ingawa lengo la hatua ya mwanzo ya ushirikiano katika Jumuiya za *COMESA, SADC* na *EAC* ni Umoja wa Forodha, lakini madhumuni, matarajio na viwango vya ushirikiano wa Jumuiya hizi na ile ya Ulaya ni tofauti kutegemeana na sababu za kihistoria.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu busara ya kujadiliana *EPA* chini ya Jumuiya aya Afrika Mashariki ni kwamba, hapo awali kulikuwa na dhamira hiyo kwa nchi hizi tatu. Kenya, Tanzania na Uganda. Lakini Kenya na Uganda walijiunga na kundi la *ESA-EPA* na Tanzania ikaamua kujiunga na kundi la *SADC-EPA.*

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu hasara za Tanzania kujitoa *COMESA,* ikumbukwe kwamba, kila uamuzi una faida na hasara zake. Wakati wa kujitoa *COMESA* kulikuwa na faida na hasara ambazo zilikuwa zimeanishwa wakati huo, na Serikali ikaamua kuwa ingefaa kujitoa. Hivyo basi, ikiwa Serikali itarejea azma ya kurudi *COMESA,* pia itabidi uchambuzi wa kina ufanywe kwa faida na hasara zake.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Aidha, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba ni vizuri kila nchi kuwa katika kundi moja. Na kwa kuwa Tanzania kwa sasa ina *negotiate* kwa yote mawili. Na kwa kuwa, mimi ni Mjumbe wa Bunge lako kule *SADC* na kule *SADC* katika kundi la *negotiation* ni nchi saba tu zinahusika na Tanzania hatuko. Je, Serikali sasa inatoa kauli gani kwamba sisi tutaingia upande gani ili tusiendelee kupata hasara?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni kweli kila wakati unapofanya kitu kuna faida na hasara na kwa kuwa faida hiyo tumeiona na hasara hizo tumeshaziona. Je, sasa ni lini kulingana na faida na hasara zilizopo Serikali itafanya na kumaliza uchambuzi ili tujue kama tunarejea *COMESA* au tunaendelea *SADC?*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kweli kama ilivyozungumzwa unabidi kuwa katika kundi moja la forodha wakati una-*negotiate* na hii *EPA.* Lakini hili tatizo sio la Tanzania tu. Tuna nchi nyingi sana mpaka sasa hivi bado zingali katika tunaita *Regional Economic Operations Rates* nyingi. Mpaka sasa hivi bado inatafutwa mfumo gani kwa nchi hizo unazozizungumzia. Tanzania sasa hivi tunazungumza tukiwa katika *SADC (EPA)* ambayo ina-*include* Angola, Botswana, Lesotho, Mozambique, Namibia, Swaziland na Tanzania tumo humo. *South Africa* ni kama *observer* katika hilo kundi. Tunajua kwamba unayozungumza *ESA* haihusishwi *COMESA* tu peke yake. Kuna nchi kama 17 ambazo zenyewe zote zimechanganyikana. Lakini kuna tatizo unalolizungumza una maana kwamba katika hizo nchi 7 ambazo ziko katika *SADC (EPA)* nchi 5 ziko katika orodha ya *South Africa* na sisi tuko katika na tuna *Custom Union* ya *East Africa* ambao tuko nchi tatu lakini zitaongezeka mbili za Rwanda na Burundi tutakuwa 5. Sasa namna gani mwisho wa siku hizi nchi tutapangana hiyo bado maendeleo yanaendelea na ndizo *negotiations* zinakwenda mpaka sasa hivi. (*Makofi)*

Suala la pili, umezungumza faida na hasara zinazopatikana. Kweli sasa hivi kuna majadiliano, kuna *stakeholders* bado wanaendelea kuzungumza. Tanzania tulikuwa *COMESA* na tulikuwa *SADC* tukajiondoa *COMESA* na sasa tukabaki *SADC* peke yake. Lakini ukija kuangalia kuna bado nchi zingine ambazo ziko pande zote mbili *SADC* na *COMESA.* Kwa mfano kuna Congo, Malawi, Mauritius, Swaziland, Zambia na Zimbabwe zote ziko katika pande mbili ziko *COMESA na SADC.* Sisi Tanzania tuliamua kuchukua upande wa *SADC.* Sasa hivi kuna kikundi cha wadau walikuwa wamekutana tarehe 12 wanazungumza.

Sisi kama Serikali tuko kwa niaba ya wananchi na *stakeholders* mbalimbali. Hoja zitatolewa kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyozungumza tutaangalia faida na hasara tutazichambua mwisho wa siku tutaamua ni sisi wenyewe tutaamua kwa niaba ya wananchi.

Na. 211

**Watoto Kuwekwa Mahabusu**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu inaendeshwa kisheria na kwa kuwa, kuna baadhi ya watoto wanaofanya makosa ya kweli na wengine makosa ya kusingiziwa na kufikia hatua ya kuwekwa mahabusu na kwa kuwa, watoto hao wengine wakiwa chini ya umri wa miaka kumi na nane na wengine wakiwa wanasoma Shule za Msingi katika darasa la sita hadi darasa la saba na Sekondari katika kidato cha kwanza hadi kidato cha nne na kwa kuwa huko mahabusu huchanganywa na watu wazima wenye makosa tofauti:-

(a) Je, Serikali na sheria zake ina utaratibu gani wa kuwaweka watoto hao mahabusu?

(b) Kama itakuwa inawachanganya na mahabusu watu wazima. Je, Serikali haioni kama watoto hao wataathirika kisaikolojia?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga,Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inao utaratibu mzuri wa kuwaweka mahabusu watoto wanaotuhumiwa kwa makosa mbalimbali. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Watoto na Vijana ya Tanzania yaani *The Children and Young Persons Ordinance Cap. 13*, inayoelekeza kwamba mahabusu mtoto wenye umri kati ya miaka 12 na miaka 16 anapofikishwa Mahakamani kwa kutuhumiwa kutenda makosa ya jinai wanapaswa kuhifadhiwa katika Mahabusu za Watoto (*Remand Homes*) endapo watashindwa kutimiza masharti ya dhamana.

Iwapo mtoto aliyeko mahabusu, anatiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo anapaswa kupelekwa Shule ya Maadilisho (*Approved Schools)* iliyopo Irambo Mbeya kutumikia adhabu yake mpaka atakapofikisha umri wa miaka kumi na nane (18) ndipo ahamishiwe kwenye Magereza ya kawaida.

Katika nchi yetu zipo mahabusu za watoto tano (5) ambazo zipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Mbeya, na zipo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mahabusu hizi hazitoshelezi na hivyo baadhi ya watoto kulazimika kuhifadhiwa katika Magereza ya kawaida kinyume na taratibu za kuwahifadhi mahabusu watoto. *(Makofi)*

Pamoja na kuhifadhiwa katika Mahabusu za watoto na magerezani, mahabusu watoto wanapaswa kuainishwa na kutenganishwa kwa kuzingatia uzito wa makosa yao au kutenganisha waliotuhumiwa kwa makosa mbalimbali na watoto watukutu.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao inalazimika wahifadhiwe magerezani, Sheria ya Magereza ya Mwaka 1967 hairuhusu mahabusu watoto kuchanganywa na mahabusu watu wazima. Mahabusu watoto wanapoletwa magerezani hutenganishwa na mahabusu watu wazima katika sehemu tofauti za Gereza husika.

Pale ambapo gereza husika haliwezi kutenga sehemu maalum kwa ajili ya kuhifadhi mahabusu watoto, mahabusu watoto hutenganishwa na mahabusu watu wazima kwa kuwekwa kwenye mabweni tofauti na ya watu wazima.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuheshimu Haki za Binadamu ikiwa ni pamoja na mahabusu watoto waliopo magerezani nchini kote na kamwe haikusudii kukiuka haki hizo. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, nina suala dogo la nyongeza.

Amesema kwamba watoto hutengwa katika mahabusu. Kwa kuwa nina ushahidi wa kutosha je, nitakapompatia ushahidi huo Mheshimiwa Waziri atachukua hatua gani kwa watu wanaochanganya watoto na watu wazima?

**SPIKA:** Sijui labda ungesema moja kwa moja tu. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni swali lisiwe linauliza maoni, lazima liwe swali halisi linalouliza kitu halisi. Sasa inaelekea Mheshimiwa ana jambo lakini amelimezea. Kwa hiyo, ni vizuri tu kwa uwazi huo ushahidi auseme ili Waziri aweze kujibu na kuchukua hatua. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa kuna vituo vikubwa ambavyo vinachukua watoto wenye matatizo wanapokamatwa na watoto hawa wanawekwa ndani zaidi ya siku moja au mbili au tatu wakiwa wamechanganywa na watu wazima tayari kwa kuandaliwa kupelekwa Mahakamani. Naweza nikaongea katika Wilaya ya Ilemela katika kituo kikuu cha Polisi Kirumba watoto hawa hufanyiwa vitendo hivyo. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na hilo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza hilo eneo alilolitaja haliko chini ya Wizara yangu. Lakini tu kwa faida yake niseme kwamba watoto wanapokuwa wanakamatwa na Polisi wamefanya kosa mpaka sasa nchini mwetu bado katika vituo vya Polisi hatuna vituo ambavyo vinawekwa mkosaji mtoto, mkosaji mtu mzima. Lakini pale ambapo kituo cha Polisi ni kikubwa na kina vyumba vingi na hasa kwa sababu wakosaji akina mama ni wachache kwa hiyo zile mahabusu za akinamama huwa mara nyingi hazina watu. Kwa hiyo, mara nyingi vituo vya Polisi huwaweka watoto katika vile vyumba vya akinamama kwa sababu mara nyingi huwa vipo tupo katika vituo vingi ambavyo mimi nimebahatika kuvitembelea. Kwa hiyo, hata kule katika vituo vya Polisi bado jitihada kubwa kabisa inafanywa kutenganisha watoto wahalifu ambao wanafikishwa katika vituo vya Polisi na wahalifu watu wazima. ambao katika vituo vya Polisi.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nilikuwa na swali moja tu dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ni dhahiri makuzi ya watoto wenye umri uliotajwa hivi sasa ni mengi na imesababishwa na hali ya mazingira magumu yanayotokana na ugumu wa maisha

wakiwa uraiani. Na kwa kuwa mara zote watoto hawa wanapopatikana na hatia huwa nyuma kielimu na hata mafunzo mengine muhimu kama vile stadi za maisha na kadhalika. Je, Wizara inasemaje kuhusu kuandaa mipango kabambe ya kuwapa elimu watoto hawa wanapokuwa kule mahabusu yaani kwenye magereza yao ya watoto ili wanapokuja kutoka baadaye magerezani wawe tayari wamekwishakuwa wameshapata elimu pamoja na ujuzi ili waweze kwenda kutumikia baadaye. Kwa sababu wanapokuwa magerezani wanakosa elimu na umri unakuwa umekwishapita?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la awali kwamba hawa watoto kuna hatua mbili. Hatua ya kwanza ni wale wa miaka 12 – 16 ambao wanawekwa katika magereza maalum ya watoto na nimesema yako matano. Na kule wanaendelea kusomeshwa katika hizo shule za watoto. Akishafika miaka 18 anahamishwa kupelekwa katika gereza la kawaida. Nataka kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba hapa nchini tunalo gereza maalum la vijana. Hawa katika miaka 18 mpaka 25 yuko pale Wami. Hili ni gereza ambalo wafungwa vijana wanapelekwa pale na wanaendelea na masomo, wale ambao hawajamaliza Shule ya Msingi pale Wami wanaendelea na masomo mpaka wamalize Shule ya Msingi na wengine wanafaulu kwenda Sekondari na wanakwenda Sekondari. Wale ambao walishamaliza Shule ya Msingi pale Wami tunawafundisha stadi za kazi. Wanafundishwa stadi za kazi kwa *sylabbus* ya VETA ili akimaliza masomo pale atakuwa na ujuzi anakwenda kujiajiri mwenyewe.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna vituo vitano tu katika nchi nzima na watoto wanaokosa sio wale wa mikoa mitano tu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kuna mahabusu ya watoto mikoa yote Tanzania ili kuwatendea haki watoto wa mikoa mingine?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mpaka sasa tunazo Magereza ya watoto 5 katika mikoa 5. Na hizi zinahudumia watoto wa nchi nzima. Si kwamba ile mikoa mitano tu ndio watoto wanakwenda kufungwa pale lakini vinahudumia nchi nzima.

Ni kweli kwamba havitoshi lakini nafikiri Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana na mimi kwamba watoto wanachohitaji zaidi kwa kweli si kuwaongezea magereza watoto. Wanachohitaji ni malezi. Utafiti umeonyesha kwamba idadi kubwa ya watoto ambao katika jela hizi za watoto ni wale ambao wamekosa malezi ya baba na mama, zile familia ambazo zinatengana halafu watoto wanakosa malezi ya baba na mama. Ni watoto wanaotoka katika familia ya baba na mama walevi, ndio utafiti umeonyesha idadi kubwa ya watoto wamo katika magereza hizo.

Kwa hiyo ningependa kutoa wito kwa Watanzania wenzangu kwamba katika hili mwelekeo wetu sio kujenga au kuongeza magereza ya watoto lakini mwelekeo wetu uwe katika malezi bora ndio watoto wetu wawe Watanzania bora.

Na. 212

**Kituo cha Polisi – Kigongo – Busisi**

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kituo cha Polisi Busisi kilichopo katika kivuko cha Kigongo – Busisi Jimboni Sengerema katika barabara kuu iunganishayo nchi za Rwanda, Burundi, DRC, Uganda na Kenya ni muhimu sana kwa usalama wa maisha na mali za watu; na kwa kuwa, ofisi zake zina hali mbaya sana kama ilivyo kwenye kituo cha Polisi Buyagu kinachohudumia Tarafa ya Nyanchenche, Wilaya ya Sengerema ukiwemo mgodi wa Dhahabu wa Sota/Ngoma:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuviimarisha vituo vya Polisi Busisi na Buyagu hususan majengo ya ofisi na makazi ya askari wake?

(b) Je, ni lini vituo hivyo vitaboreshwa ili kutoa huduma bora iwiyanayo na hali halisi ya majukumu ya vituo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa William Ngeleja, Mbunge wa Sengerema swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga na kukarabati vituo, Ofisi na makazi ya Polisi hapa nchini. Aidha, pamoja na umuhimu huo wa kuimarisha majengo ya Polisi bado uwezo wa Serikali kutekeleza mpango huo ni mdogo hivyo miradi hiyo itatekelezwa hatua kwa hatua kutokana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa vituo vya Busisi na Buyagu, naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na viongozi wengine katika Wilaya yake kuhamasisha wananchi kujitokeza kuchangia na kuanzisha ujenzi wa vituo hivyo kama wanavyofanya wananchi wa Wilaya nyingine hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itakuwa tayari kuunga mkono jitihada za wananchi za kujenga, vituo; na makazi ya Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa huduma katika vituo hivyo utategemea sana kukamilika kwa ujenzi vituo husika na nyumba za kuishi askari wake. Kwa sasa maeneo husika yataendelea kuhudumiwa na vituo hivyo na kituo cha Makao Makuu ya Polisi Wilaya ya Sengerema. Aidha, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha Doria katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa wananchi kimsingi hawana matatizo kushirikiana Serikali katika kuimarisha miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa nyumba za askari Polisi, nashukuru hizi zingine kama ambavyo tumekuwa tukiona wanashiriki katika kuleta maendeleo katika maeneo yao.

Lakini pia kwa kuwa kimsingi jukumu la uimarishaji wa Ofisi za Polisi ni jukumu la Serikali na nguvu za wananchi ni nyongeza. Nilikuwa napenda kujua kama majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayaongezi mzigo kwa mwananchi katika mazingira ya sasa hivi ambayo tunayo ambapo Serikali imejitoa katika shughuli za biashara na hizi shughuli za ulinzi na usalama wa raia ikabaki kuwa jukumu la Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli jukumu la ulinzi na usalama wa raia ni jukumu la Serikali kupitia Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na hali halisi ya uchumi wa nchi yetu. Serikali ingependa sana kujenga vituo vyote vya Polisi hapa nchini. Aidha, kuhudumia sekta mbalimbali hapa nchini. Lakini tatizo ni uwezo. Tunapowaomba wananchi kushirikiana na Serikali kupunguza matatizo yetu si kwa nia kwamba mzigo huu tuutupie kwa wananchi. Nia ya Serikali ni safi tunataka kuongeza huduma kwa wananchi wake. Kwa hivi sasa Serikali inafanya kila njia kujenga vile vituo vilivyoko katika Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa. Kwa hiyo namwomba tena Mheshimiwa Mbunge aafikiane na wananchi wa jimbo lake ili tusaidiane kuhakikisha kwamba vituo hivi vinaimarishwa ili huduma zinazotakiwa zipatikane ipasavyo.

**MHE. DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana ni kutokana na uhamasishaji tulioambiwa na Wizara hii ya kwamba sisi katika Wilaya ya Ukerewe tulihamasishwa wananchi wakajenga kituo cha afya wakitegemea kwamba watasaidiwa zaidi hata kupata *armoury.* Tuna kituo cha Mliti wakatoa ekari 6 ambayo kwa Wilaya ya Ukerewe ni ekari nyingi kwa ajili ya kujenga bear Waziri aliyekuwepo Mheshimiwa Mapuri na mpaka leo hakuna msaada uliokuja. Je, tuendelee kuhamasisha au ndio mwisho wa habari?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimpongeze na nimshukuru sana kwa jitihada anazochukua katika kuhamasisha kujenga vituo katika eneo hilo. Nataka nimhakikishie kwamba nitayafuatilia masuala hayo ili tuhakikishe tunashirikiana naye kuhakikisha kwamba vituo hivyo vinavyoendelezwa huko pamoja na kushirikiana na nguvu za wananchi. Ahsante sana.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu imenunua kivuko cha zaidi ya shilingi bilioni 3 ambazo ni fedha nyingi cha Busisi na Kigongo. Na kwa kuwa itakuwa ni bora kuimarisha ulinzi ili kulinda kivuko hicho. Je, Wizara ya Usalama wa Raia iko tayari kushirikiana na Wizara ya Miundombinu ili wakati wa kujenga barabara kipande cha Usagara kwenda Geita waweke majengo ya Polisi kuimarisha ulinzi kama ilivyofanya kwenye daraja la Mkapa?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, siku zote Serikali iko tayari kuwahudumia wananchi wake hasa kuwahakikishia amani, usalama juu yao. Kwa msingi huo tutashirikiana na Wizara husika tuzungumze kama jambo hili linawezekana kufanya ili tulifanye kwa nia ile ile la kuwahudumia wananchi wetu.

Na. 213

**Barabara za Lami – Lindi**

**MHE. RIZIKI S. LULIDA** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara nzuri zinarahisisha mawasiliano katika eneo moja na jingine; na pia hurahisisha kupeleka mazao katika Soko:-

(a) Je, ni lini Mkoa wa Lindi utapatiwa barabara za lami kurahisisha mawasiliano katika Wilaya zake?

(b) Kwa kuwa, barabarba ya Kilwa – Liwale na Liwale – Nachingwea huwa katika hali mbaya baada ya mvua kunyesha; Je, Serikali ina mpango gani wa kuiongezea nguvu *TANROADS* – Mkoa wa Lindi ili iweze kukarabati barabara hiyo iweze kupitika wakati wote?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua umuhimu wa kujenga barabra za lami ili kurahisisha mawasiliano katika Wilaya za mkoa wa Lindi na vile vile mikoa yote. Hata hivyo kwa sasa Serikali imeweka kupaumbele katika kukamilisha kwanza ujenzi wa lami kwa barabara kuu zitakazounganisha nchi yetu na nchi jirani na barabara kuu zitakazounganisha Makao Makuu ya Mikoa yote. Kwa upande wa Mkoa wa Lindi barabara ya Kibiti – Lindi inajengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha barabara zote zinazounganisha Makao Makuu ya Wilaya nchini ili kuhakikisha kuwa zinapitika wakati wote.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilwa – Liwale ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Lindi na imegawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo: -

Sehemu ya Kilwa – Masoko hadi Nangurukuru yenye urefu wa kilometa 30, ni ya kiwango cha lami na ilijengwa mwaka 1990. Sehemu ya Nangurukuru – Liwale yenye urefu wa Kilometa 231 ni barabara yenye tabaka la udongo na changarawe. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo Wizara yangu imekuwa ikiifanyia matengenezo mara kwa mara. Kuanzia mwaka 2002/2003 hadi 2005/2006 jumla ya shilingi 480.1 milioni zimetumika kukarabati sehemu korofi na ukarabati wa madaraja na Njinjo na Nangale. Barabara hii itaendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida kwa lengo la kuifanya ipitike kwa muda wote wa mwaka.

Kuhusu barabara ya Liwale – Nachingwea yenye urefu wa Kilometa 136, nayo imekuwa ikarabatiwa mara kwa mara. Kuanzia mwaka 2000/2001 hadi 2003/2004 jumla ya shilingi 223 milioni zilitumika kwa matengenezo ya sehemu korofi na kutengeneza daraja la Kibutuka. Aidha, barabara hii itakabaratiwa kwa kiwango cha changarawe kipande cha kilometa 30 eneo la Mikunya hadi Liwale kwa gharama ya shilingi 721.49 milioni chini ya mradi wa *HIPIC* unaofadhiliwa na *OPEC Fund*. Mkandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu alichaguliwa tarehe 25 Machi, 2006 na kazi itaanza hivi karibuni. Mara mradi huu utakapokamilika, barabara hii itakuwa inapitika bila matatizo yoyote.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Miundombinu. Atakubaliana na mimi wakati akizungukia barabara za Mkoa wa Lindi alishindwa kusafiri kutoka Nachingwea kwenda Liwale kutokana na barabara haipitiki.

Pili, alizungukia barabara ya Ng'apa, Mtamba, Ngongo, Mtandanda Ngororo mpaka Milola na alishindwa kupita katika njia hiyo na akaahidi kuwa barabara hiyo itaanza kujengwa. Je, ni lini barabara hizo zitaanza kujengwa ili ziweze kupitika angalau kwa mwaka huu. Ahsante?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILITON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru ametambua kwamba nilitembelea mkoa huo na kupita barabara nyingi. Lakini vile vile ni kweli kwamba nilishindwa kupita barabara hiyo hasa sehemu hiyo ya Mikunya kutokana na ilivyokuwa imeharibika. Ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema sehemu hiyo ya Mikunya itakarabatiwa kwa gharama ya shilingi 712 milioni. Kwa kweli ni sehemu mbaya na baada ya ukarabati huo ambao nimesema utaanza hivi karibuni, basi nina hakika kwamba barabara hiyo itapitika wakati wote.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika kwa kuwa kilomita 231 za kutoka Nanguruku mpaka Liwale wakati wa masika ni ndoto kupitika; na kwa kuwa wakati huo huo wa masika kutoka Liwale kuja Nachingwea hufikika kwa pinde. Je,

Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kuunganisha barabara ya kutoka Ilonga kule Morogoro - Ndapata hadi Liwale ambayo ni kilomita 50 tu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHESHIMIWA DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hiyo anayoizungumza kutoka Ilonga Mkoa wa Morogoro kwenda mpaka Mkoa wa Lindi ni njia fupi na kwa kweli mimi nimeipita hivi karibuni nilipotembelea Mkoa wa Morogoro. Naahidi hapa kwamba Serikali ina mpango katika Bajeti zake za miaka ijayo kufungua barabara hiyo ili tuweze kufika Mkoa wa Lindi kutokea Mkoa wa Morogoro.(*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, ninayo matangazo, la kwanza ni kuhusu wageni, kwenye *Public Gallery* mkono wa kulia wapo viongozi 11 wa Mfuko wa Bunge la Vijana wa Afrika nawaomba wasimame ili Wabunge waweze kuwatambua karibuni sana kuona jinsi demokrasia katika nchi yetu inavyofanya kazi. Upande wa kushoto umekuwa ni utamaduni wetu napenda nimtambulishe Mrs Kilontsi Mporogomyi, karibu sana, asante sana.

Mheshimiwa Omar Kwaangw' Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii anawakumbusha Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 14 mwezi huu wa saba kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo saa tano asubuhi ukumbi Namba 231 Jengo la Utawala ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na Kikao leo saa tano asabuhi chumba Namba 227, ghorofa ya pili. Napenda pia kuwatangazia wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi kile Kikao tulichokipanga leo hakitafanyika kwa sababu kuna wajumbe kadhaa wameomba udhuru kwa sababu wanalazimika kwenda Dar es Salaam.

Kwa hiyo, Kikao cha Kamati ya Uongozi kitafanyika mapema wiki ijayo na pia Kikao cha Tume ya Huduma za Bunge kitafanyika wiki ijayo na tatu Kikao cha pamoja cha Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge nacho kitafanyika wiki ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Joel Bendera, Naibu Waziri, anapenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge ambao hawajajaza zile fomu kuhusiana na mbio za *VIP* za tarehe 22 Julai. Tunatazamiwa Waheshimiwa Wabunge kushiriki kwa rika mbalimbali. Mbio hizo zinaitwa *VIP Race*, sasa waliochukua fomu kuonyesha *size* ya fulana watakazovaa, viatu yaani raba na kadhalika ni Waheshimiwa Wabunge 190 tu. Sasa ninavyoelewa mimi kusiwe na hofu kwamba ukichukua fulana lazima ukimbie, ni kwamba utapata raba na fulana ukihiari kushirikiri ni vizuri lakini ukiwa na sababu huwezi, basi. Naona hiki ndiyo kikwazo watu wanagaili kutia saini hizi fomu. Kwa hiyo, tafadhalini mrejeshe hizo fomu ili ijulikane *small size*, *medium*, *large* wengine, *XL* na wengine kama Mheshimiwa Mgana Msindai *XXL* zote zipo. *(Makofi/Kicheko)*

Baada ya hayo nadhani ndiyo mwisho wa matangazo kwa sasa, Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007
### Wizara ya Maliasili na Utalii

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Kikao hiki cha Bajeti ni cha kwanza tangu Bunge letu lichaguliwe baada ya Uchaguzi Mkuu mwaka jana. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Ilemela kwa kunichagua kwa kura nyingi sana. Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa. Jakaya M. Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa kuniteua kuwa Waziri wa Wizara hii muhimu hapa nchini. Pia napenda kutoa shukrani zangu kwa Kamati ya Bunge iliyoundwa ya kushughulikia masuala ya Maliasili na Mazingira kwa ushirikiano walioonyesha tangu iundwe. Wizara yangu itaendelea kufanya kazi na Kamati hii chini ya Mheshimiwa Ndugai, kwa ushirikiano mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchache wa fadhila kama sitatoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa kuchaguliwa kuongoza nchi yetu chini ya uongozi thabiti wa Chama cha Mapinduzi. Ninampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Edward Lowassa kuwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa shughuli za Serikali. Aidha, nawapongeza Mawaziri wote na Wabunge waliochaguliwa na wananchi kuwaongoza. Mwisho napenda kuwapongeza Mheshimiwa Samwel Sitta kwa kuchaguliwa Spika wa kuongoza Bunge letu Tukufu, Mheshimiwa Anne Makinda kuwa Naibu wa Spika na Mheshimiwa Job Ndugai, kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, matukio muhimu, kutokana na uharibifu wa mazingira uliosababishwa na uvunaji usioendelevu wa mazao ya misitu, Wizara ilisitisha uvunaji katika misitu ya asili. Ili kuwa na matumizi endelevu ya mazao ya misitu, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uvunaji Bora wa Mazao ya Misitu. Nia ni kuweka taratibu za uvunaji zinazoeleweka hadi vijijini na kuwajibisha uongozi wa vijiji na wilaya katika kusimamia sheria kama wakala wa Serikali.

Vile vile, katika kutekeleza Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2002 Wizara ilifuta vibali vyote vya kusafirisha magogo na misandali nje ya nchi kuanzia tarehe 27 Januari, 2006 kama inavyotakiwa na sheria hiyo. Aidha, Wizara imechapisha Kanuni mpya kupitia Tangazo la Serikali Na.69 na 70 ya Gazeti la Serikali toleo la tarehe 9 Juni, 2006. Kanuni mpya zinatoa mwongozo mpya wa uvunaji wa mazao ya misitu na uchomaji mkaa unaozingatia usimamizi na uwajibikaji wa karibu zaidi wa Serikali na

Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji katika shughuli zote. Wizara imeunda Kamati za Uvunaji za Wilaya na itaziwezesha ili ziweze kutekeleza majukumu yake mara moja.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilizindua mradi wa kusaidia wavuvi wadogo wadogo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kuhifadhi Mazingira na Rasilimali za Mwambao wa Bahari *(MACEMP)* Mjini Kilwa Masoko, Machi 2006. Kwa kuanzia, Mradi huu utahudumia miradi ya wananchi wa Wilaya za Rufiji, Mafia na Kilwa na baadaye wilaya zote za Mwambao wa bahari ya Hindi na Zanzibar, ili waweze kujiongezea kipato na lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi Tanzania ambalo ujenzi wake uliwekewa jiwe la msingi na Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin Mkapa tarehe 16 Desemba, 2004 limekamilika na kuanza kutumika. Aidha Mkutano wa kwanza wa Tume ya Kisayansi ya nchi zinazosimamia uvuvi katika eneo la Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi *(South West Indian Ocean)* ulifanyika Dar es Salaam Juni 2006. Mkutano huu ulihusisha wajumbe 27 kutoka nchi za Mauritius, Seychelles, Somalia, Afrika Kusini, Kenya, Maldives, Comoro, Madagascar, Msumbiji, Reunion, France, Tanzania pamoja na Mashirika ya Kimataifa ya *FAO, UNEP* na *SIDA*.

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu ilipata mafanikio kutokana na kushiriki katika maonyesho mbalimbali ndani na nje ya nchi. Tanzania ilichaguliwa kuwa miongoni mwa nchi 10 bora zilizofanya vizuri kati ya nchi 180 zilizoshiriki Maonesho ya Utalii ya *ITB*-Berlin Ujerumani Vilevile, Wizara iliibuka kidedea katika maonyesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Mwalimu J. K. Nyerere mwezi Julai 2005. Aidha, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mashindano ya *Miss Tourism Model of the World, 2006* ambayo yamesaidia kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko nchini. Mashindano haya yatafanyika tena hapa nchini mwaka huu, baada ya Serikali kuridhika na matayarisho yake na kutoa kibali kwa wahusika wa mashindano hayo hapa nchini.

Mwezi Aprili 2006, Wizara ilikabidhiwa Kituo cha Makumbusho ya Dr. Livingstone Ujiji ambacho kilianzishwa mwaka 1927 kutokana na umuhimu wake kitaifa ambao ni historia ya biashara ya Utumwa na tukio la mwaka 1871 wakati Dr. Livingstone alipokutana na Bw. Henry M. Stanley katika harakati za kupambana na biashara ya utumwa. Sambamba na tukio hilo utafiti kuhusu njia ya utumwa kutoka Bagamoyo hadi Ujiji unafanywa ili njia hii iwekwe kwenye orodha ya urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Spika, Aidha Wizara imepokea taarifa muhimu ya kufurahisha kutoka *UNESCO,* Paris kuwa ombi letu la kuomba michoro ya Miambani ya Kondoa kuwekwa kwenye orodha ya urithi wa dunia limekubaliwa katika kikao cha kamati ya kimataifa ya urithi wa dunia kinachoendelea huko Vilnius Lithuania. Eneo hili limekuwa la saba kwa Tanzania, baada ya Magofu ya Kilwa, Hifadhi ya Serengeti, Hifadhi ya Kilimanjaro, Hifadhi ya Ngorongoro, Pori la Akiba la Selous na Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti 2005/2006 Sera na Sheria, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara kwa kutekeleza ilani ya uchaguzi, iliandaa

Rasimu ya Sera ya Malikale ili iweze kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri. Vile vile, iliendelea kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 na pia Rasimu ya Sheria ya Utalii. Kanuni za kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyama na mimea iliyo hatarini kutoweka duniani zilitayarishwa pia. Wizara ilipitia mapendekezo ya sheria ndogo ndogo za kuanzisha na kusimamia misitu ya vijiji katika Halmashauri 12 za Wilaya.

Mheshimiwa Spika,uhifadhi wa raslimali, kazi ya kupitia Mipango ya Uendeshaji na Usimamizi kwa Mapori ya Mpanga-Kipengere, Usangu, Ibanda-Rumanyika, Burigi-Biharamulo-Kimisi, Selous, Rukwa-Lukwati na Rungwa-Kizigo-Muhesi imekamilika. Aidha, Mpango wa Usimamizi wa Pori la Akiba la Selous umepitishwa. Hali kadhalika, zoezi la kuandaa mipango ya uendeshaji na usimamizi wa Hifadhi za Serengeti, Mahale na Kilimanjaro lilikamilika na Mipango ya Hifadhi za Ruaha na Mikumi iko katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutunza mashamba 16 ya miti yenye jumla ya hekta 85,000 kwa kuotesha miche 4,499,240, kurudishia na kupanda miti katika hekta 2,161 za maeneo yaliyovunwa na kunyunyizia dawa ya kuua wadudu katika hekta 167 zilizoathirika katika shamba la *Sao Hill* na miti imehezabiwa katika jumla ya hekta 2,074 za mashamba ya Longuza, Mtibwa na Rondo. Aidha, soroveya imefanyika katika hekta 2,300 za misitu ya Hifadhi ya Landikinya katika Wilaya ya Monduli na hekta 3, 848 za msitu wa Hifadhi wa Kisegese katika Wilaya ya Mkuranga. Makubaliano ya usimamizi wa misitu ya vijiji 24 katika Wilaya za Morogoro vijijini, Rombo na Handeni yamefanyiwa mapitio.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Taasisi ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ilikamilisha kazi ya utayarishaji wa mipango itakayohusika na usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari na mwambao na kuanza utekelezaji wa mipango hiyo. Kazi ya kuandaa mkakati wa usimamizi wa Ardhioevu nchini inaendelea. Rasimu ya kwanza ya Mkakati huo imekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uhifadhi wa misitu, Wizara ilifungua ofisi za Hifadhi za Misitu ya Lindimaji katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Tabora na Ruvuma. Shughuli za kuhifadhi misitu zimefanywa katika wilaya 18 za Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Morogoro na Arusha ikiwa ni pamoja na hifadhi mazingira asili ya Amani huko Tanga. Miche ya miti ya asili na mitiki zaidi ya 582, 654 ilikuzwa na kupandwa kwenye kingo za misitu, mashamba ya wananchi na ndani ya hifadhi na hekta 140 za mikoko zimepandwa katika delta ya mto Rufiji sehemu ambazo kulikuwa kumefanyika uharibifu mkubwa siku za nyuma.

Mheshimiwa Spika, Visiwa vya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara ndiyo maeneo pekee ya urithi wa utamaduni - Tanzania Bara yaliyoko kwenye orodha ya *UNESCO* ya urithi wa dunia. Katika kuhifadhi maeneo hayo ambayo yako hatarini kuharibika, Wizara iliendelea kuyaimarisha kuta za baadhi ya magofu ya majengo na makaburi, kutoa elimu ya ufundi wa uhifadhi kwa vijana ambao pia walipewa ajira ya muda kufanya kazi za ufundi. Aidha, mchakato wa kuingiza Mji wa kihistoria wa Kilwa Kivinje kwenye

Orodha ya Urithi wa Dunia umeanza. Gofu la Boma la Wajerumani la Kilwa Kivinje lilifanyiwa ukarabati wa awali kuimarisha baadhi ya kuta na paa.

Mheshimiwa Spika, Mbegu za miti, Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za miti iliendelea kuzalisha na kusambaza Mbegu bora za miti pamoja na vipandikizi. Hadi kufikia Aprili 2006, kilo 11,567 za mbegu bora za miti zilikusanywa. Kilo 7,150 za mbegu bora za miti ziliuzwa nchini na kilo 200 ziliuzwa nchi za nje. Aidha miche 29,224 ilisambazwa hapa nchini.

Ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbegu bora unakuwa endelevu, Wizara ilianzisha vyanzo vitatu vya mbegu bora za miti aina ya misindano na mikaratusi bora. Vile vile vyanzo vitano vya mbegu za miti ya asili ikiwemo miti aina ya mbuyu, mkangazi, mvule na mgunga vilitambuliwa.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Rasilimali, Wizara ya Maliasili na Utalii inalo jukumu kuu la kulinda rasilimali za Taifa na iliendelea na ulinzi wa rasilimali kwa kuimarisha uwezo wa kuendesha doria kwenye maji na katika nchi kavu. Watumishi walipatiwa vitendea kazi muhimu na vya kisasa pamoja na mafunzo yanayohusu mbinu mbalimbali za kupambana na uhalifu. Doria zilizofanyika zilifanikisha kukamatwa watuhumiwa 3,801. *(Makofi)*

Aidha, mali zilizokamatwa ni pamoja na magari 2, Meli ya mizigo, injini za maboti 20, mitumbwi 333, nyavu 26,863, pikipiki 1, baiskeli 87, bunduki 201, vipande vya mbao 36,979, nguzo za mikoko 2,010, misumeno 19, magunia ya mkaa 3,384, ng'ombe 13,213, samaki tani 3,305, majongoo bahari tani 4.0, zana haramu za uvuvi 364, baruti 5 na nyara za aina mbalimbali ikiwemo meno ya tembo matatu mazima na vipande 130 vyenye jumla ya uzito wa kilo 91.5, ngozi za wanyamapori na viumbe hai wa aina mbalimbali. Aidha, Wizara imeanzisha utaratibu wa kukagua maduka yanayouzia nyavu zisizoruhusiwa ili kuzuia uingizaji na uuzaji wake badala ya kuhangaishana na wavuvi mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti wa usafirishaji wa mazao ya misitu nje ya nchi, Wizara imeamua kuwa na eneo maalumu kwa ajili ya ukaguzi, upangaji wa madaraja na ufungaji wa lakiri katika Kontena zinazotumika kusafirisha mazao ya misitu nje ya nchi katika eneo la *Cheetah* Kurasini-Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kuimarisha ulinzi katika Makumbusho za Taifa zilichukuliwa kwa kukarabati jengo la Ofisi za Kijiji cha Makumbusho Dar es Salaam na majengo ya Makumbusho ya Azimo la Arusha. Vilevile, uzio kuzunguka eneo la Makumbusho ya Azimio la Arusha ulijengwa.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa ubora na viwango, ili kulinda masoko ya asali ndani na nje ya nchi, Wizara imekamilisha Mwongozo wa udhibiti wa ubora wa mazao ya nyuki. Vile vile, katika kuhakiki ubora wa mbegu za miti, Wizara imeendelea kuchambua na kupima ubora wa mbegu hizo kabla ya kuhifadhiwa au kusambazwa kwa wateja. Hadi kufikia Aprili 2006, Wizara ilipima ubora wa sampuli 860 za mbegu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi, Wizara ilizifanyia uchunguzi sampuli 333 za matope, maji, samaki na minofu ya sangara kutoka Ziwa Victoria kuona kama zina mabaki ya sumu. Sampuli 1,083 za minofu ya sangara, kamba miti, kamba koche, pweza na ngisi zilichunguzwa ili kuhakiki kiwango cha vimelea haribifu.

Vilevile, Wizara ilikagua na kuruhusu viwanda 15 vya kuchakata mazao ya uvuvi, Maeneo 18 ya kutunzia samaki hai na maghala 11 ya kutunzia mazao makavu ya uvuvi. Meli 11 na vyombo vidogo viwili vya uvuvi vilikaguliwa na kuruhusiwa kuvua na kuchakata kamba miti.Aidha, watumishi wapatao 42 walipata mafunzo ya muda mfupi na wavuvi 510 walipata mafunzo kuhusu njia endelevu za uchakataji na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi. Mafunzo kuhusu njia za kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi hasa dagaa yalitolewa kwa wavuvi wapatao 50 wa Mwalo wa Kasela, Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, Ushirikishaji Jamii na Elimu kwa Umma Sera zote za Maliasili na Utalii zimelenga kwenye ushirikishaji wa jamii. Wizara ilitoa Elimu ya Uhifadhi wa rasilimali za maliasili na malikale kwa jamii kupitia vipindi 93 vya redio na vipindi 15 vya televisheni.

Elimu ilitolewa kuhusu Kanuni za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori kwa wajumbe 239 katika maeneo ya majaribio ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori ya Ukutu, Wami-Mbiki, Makami, Tunduru na Songea.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa limetumia Shilingi milioni 805.6 kuchangia miradi 70 ya maendeleo iliyoanzishwa na wananchi kando ya hifadhi za taifa. Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro kupitia Baraza la Wafugaji lilitumia zaidi ya Shilingi milioni 500 kuendeleza miradi ya ufugaji na Mpango wa ujirani mwema nje ya hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kutekeleza mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu katika wilaya 15 kwa hatua mbali mbali, ikiwa ni pamoja na kuanzisha misitu ya vijiji, kuweka mipaka, kupima maeneo na kuandaa mipango ya usimamizi. Programu ya ushirikishwaji wa jamii kwa kuimarisha vikundi 29 vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi vilivyoanzishwa kwenye Bwawa la Mtera iliendelezwa.

Aidha, katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, mikutano ya kuhamasisha wavuvi na viongozi wa halmashauri kuhusu uanzishwaji wa vikundi vya kusimamia rasilimali ya uvuvi ilifanyika katika Wilaya za Moshi Vijijini yenye mialo 3, Mwanga yenye mialo 10 na Simanjiro yenye mialo 6. Jumla ya injini 20 zenye *horse power* 25 zimenunuliwa kwa ajili ya vikundi mbalimbali vya ulinzi wa rasilimali zilizoko katika Ziwa Victoria na Bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua umuhimu wa kuhamasisha jamii kuboresha lishe, kuinua kipato na kupata ajira kwa kutumia rasilimali ya uvuvi. Katika kutekeleza hilo, Wizara ilisambaza vifaranga bora vya samaki 43,000 kwenye mabwawa ya kuchimba katika Mikoa ya Dodoma, Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Tabora, Iringa na kupandikiza vifaranga 4,171 kwenye malambo ya asili katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Sinema za kuelimisha wananchi kuhusu uhifadhi wa wanyamapori zilioneshwa katika vijiji 7 vinavyozunguka Pori la Akiba Selous, vijiji 8 katika Pori Tengefu la Ruvu - Masai na vijiji 10 vinavyozunguka Pori la Akiba Maswa.

Aidha, kwa kutumia Majarida, Vipeperushi na Mabango wananchi waliweza kuelimishwa kuhusu shughuli za Uhifadhi. Katika Hifadhi Bahari na Maeneo Tengefu ya Mnazi Bay, Mpango ya Uhifadhi Shirikishi katika vijiji 10 ulikamilishwa. Vikundi vya Uhifadhi vya kujitolea katika Eneo Tengefu la Kisiwa cha Bongoyo na Mbudya vimeimarishwa kwa kupatiwa mafunzo, boti na injini. Kituo cha Elimu ya uhifadhi wa maliasili kwa jamii cha Likuyu-Sekamaganga kilitoa mafunzo kwa wananchi 161 kutoka katika Wilaya za Iringa Vijijini, Mafia, Mpanda, Ulanga, Sikonge, Urambo, Uyui, Babati, Mtwara, Namtumbo na Tunduru. (*Makofi*)

Elimu ya jinsi ya kudhibiti moto, ulinzi wa pamoja wa misitu ilitolewa kwa vijiji 53 katika Wilaya za Morogoro, Movomero, Kilosa, Kilombero, Kilolo, Handeni, Korogwe, Lushoto, Muheza, Pangani, Babati, Hanang na Mbulu na uhifadhi wa mazingira ilitolewa katika shule 45 katika Wilaya za Mtwara, Lindi, Rufiji, Mkuranga, Bagamoyo, Pangani, Muheza na Tanga. Vile vile, semina 6 kuhusu mbinu bora za ufugaji nyuki zimetolewa kwa wafugaji nyuki 450 katika Wilaya za Korogwe, Moshi vijijini, Kibaha, Kilosa, Morogoro Vijijini, Mbarali na Njombe.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuhamasisha jamii na mamlaka mbali mbali kuhusu uhifadhi na uendelezaji wa maeneo na majengo ya kihistoria ya Jiji la Dar es Salaam, Mji mkongwe wa Bagamoyo, kituo cha Makumbusho ya Dr. Livingstone Ujiji – Kigoma na vituo viwili vya Malikale vya *Olduvai Gorge Ngorongoro* na Engaruka Wilayani Monduli. *(Makofi)*

Aidha, majengo zaidi ya zamani katika miji yote nchini yataingizwa katika orodha ya majengo yanayolindwa kisheria ili yasibomolewe au kufanyiwa marekebisho makubwa bila ya idhini ya Wizara. Halmashauri za Wilaya zinatahadharishwa kuhusu kutokukiukwa kwa sheria hii wakati wanatoa vibali vya ujenzi wa majengo mapya katika maeneo yao.

Matumizi endelevu ya rasilimali, Sensa za uvuvi zilifanyika katika Ukanda wa Pwani, Bwawa la Mtera na Ziwa Victoria. Sensa hizo zimebaini kuwa katika Ukanda wa Pwani kuna wavuvi 29,754 wanaotumia vyombo 7,190 vya uvuvi na Bwawa la Mtera kuna wavuvi 1,451 wanaotumia vyombo 1,124 vya uvuvi. Ziwa Victoria kwa mujibu ya sensa ya Machi 2006 kuna wavuvi 98,015 wanaotumia vyombo 29,732 vya uvuvi.

Wizara iliendelea kusimamia uvuvi wa kibiashara wa kamba na samaki; utafiti umeonyesha kuwa kamba wamepungua. Meli 21 zilipewa leseni za kuvua kamba ambazo zilivua jumla ya tani 467 za kamba na tani 869 za samaki kwenye maji ya ndani. Aidha, meli 84 zilipewa leseni za kuvua kwenye Bahari Kuu (*EEZ*). Ili kuwa na usimamizi endelevu wa uvuvi katika Bahari Kuu, Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Bahari inarejewa ili utekelezaji wake uweze kuanza.

Katika kipindi cha 2005/2006 Wizara imeendelea kuboresha takwimu za uvuvi kwa kutoa mafunzo kwa wakusanyaji na wachambuzi wa takwimu. Wakusanyaji 59 katika ukanda wa Ziwa Victoria na wachambuzi 19 kutoka ukanda wa pwani walipewa mafunzo.

Utafiti

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina taasisi tatu za utafiti katika nyanja za wanyamapori, misitu na uvuvi ambazo ni *Tanzania Wildlife Research Institute (TAWIRI), Tanzania Forestry Research Institute* (*TAFORI*) na *Tanzania Fisheries Research Institute (TAFIRI).*

Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori iliendelea kufanya sensa za wanyamapori katika maeneo ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Mapori ya Akiba ya Maswa, Moyowosi na Kigosi pamoja na eneo la Ardhioevu ya Malagarasi - Muyovosi. Aidha, utafiti wa Mbwa mwitu unaoendelea kwenye Hifadhi za Serengeti na Ngorongoro umebaini kuwa wanyama hao walio hatarini kutoweka wameanza kuonekana tena na idadi yao inaongezeka. *(Makofi)*

Utafiti umeonesha pia mnyama adimu aina ya Kakakuona *(Greater Pangolin)* ameonekana katika Hifadhi ya Mahale. Aidha, aina ya nyani *Kipunji monkey* amegunduliwa katika milima ya Rungwe Kusini Magharibi mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Misitu iliendelea kufanya tafiti juu ya matumizi mbadala ya nishati ya kuni na mkaa; uchumi jamii na uhifadhi wa miti jamii ya *Commiphora* katika Mikoa ya Arusha na Manyara; ufanisi wa upasuaji magogo kwenye mashamba ya miti ya Rongai, Kilimanjaro Magharibi na Meru; sifa za mbao za miti isiyouzika kirahisi; na mikaratusi inayokua haraka.

Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Silikanti, samaki anayesadikiwa kuishi zaidi ya miaka milioni 60 iliyopita, unaendelea chini ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na umebaini kuwa kuna makundi mawili ya Silikanti; Kundi la Kusini ambalo linapatikana maeneo ya Kilwa na Lindi linafanana na lile la Madagascar na Comoro na kundi la Kaskazini linalopatikana maeneo ya Tanga linafanana na lile la bahari ya Kenya. Tathmini ya wingi wa samaki hawa katika Bahari ya Hindi utaendelea kufanywa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea na utafiti wa akiolojia mkoani Kilimanjaro na kutoa vibali vya utafiti wa akiolojia na paleontolojia katika maeneo 11 kwenye Mikoa ya Tanga, Mara, Shinyanga, Morogoro, Pwani, Arusha, Lindi, Iringa na Manyara. Aidha, utafiti wa viumbe wa baharini wasio na uti wa mgongo uliendelea chini

ya Shirika la Taifa la Makumbusho na kitabu kuhusu matokeo ya utafiti huo uliofanyika mwambao mwa Tanzania kinachapishwa.

Utafiti wa awali kuhusu kupungua kwa theluji katika Mlima Kilimanjaro unaonesha kuwa tatizo hili linatokana na ongezeko la joto duniani *(global warming).* Tatizo hili limejitokeza pia katika milima mikubwa k.m. *Everest na Swiss Alps.* Tafiti zaidi zinaendelea kufanywa ili kupata zaidi taarifa za chanzo cha kupungua kwa theluji hiyo.

Uendelezaji na Utangazaji Utalii

Mheshimiwa Spika, juhudi za kubaini vivutio vya utalii katika Mikoa mbalimbali ziliendelea. Hivi sasa Wizara imeandaa picha za video na za *DVD* kuhusu vivutio vya utalii vilivyoko katika Mikoa ya Mtwara, Singida, Kagera na Ruvuma. Aidha, taarifa kuhusu vivutio katika Mkoa wa Rukwa na Pwani inaandaliwa. *(Makofi)*

Katika kuhamasisha jamii kuhusu Utalii ikolojia na Utalii wa Utamaduni, Wizara ilifanya warsha iliyojumuisha wadau wakuu wa utalii wa utamaduni wapatao 78 kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa utalii wa utamaduni unaolenga kupunguza umasikini, Wizara yangu imefanya tathmini ya jumla ya vituo 24 vya utalii wa utamaduni katika Wilaya za Arumeru, Babati, Hanang, Monduli, Iringa, Morogoro, Temeke, Mwanga, Hai, Moshi, Mbeya, Ileje, Rungwe, Kyela, Pangani, Same na Lushoto. Tathmini hii ilifuatiwa na warsha ya wadau wote wa miradi ya utalii wa utamaduni kitaifa kwa lengo la kutoa mchango wa jinsi gani ya kuboresha utalii huu na kuusambaza nchi nzima.

Aidha, mchakato wa kuandaa mwongozo wa utalii wa utamaduni umeanza. Katika kuimarisha utalii wa utamaduni, Wizara imehamasisha wananchi kuanzisha miradi mitano katika Wilaya za Arumeru, Morogoro na Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi 15 za Afrika zilizoteuliwa kunufaika na mradi wa Shirika la Utalii Duniani ujulikanao kama *STEP Initiative*. Chini ya Mradi huo Wizara iliendesha zoezi la kubaini maeneo yanayoweza kusaidiwa kuanzishwa miradi ya utalii katika Wilaya za Ileje, Kyela, Morogoro, Mbeya na Rungwe.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa kushiriki katika maonesho 20 kwenye soko la nje katika nchi 16 na maonesho matatu kwenye soko la ndani. Aidha, vikundi 15 vya wakala, wapiga picha na wahariri kutoka Ulaya, Marekani, Mashariki ya Kati, Mashariki ya Mbali na Kusini mwa Afrika vilikaribishwa kutembelea vivutio vyetu na kuvitangaza nchini mwao.

Waandishi wa habari 8 na wapiga picha 12 kutoka China, Urusi na Afrika ya Kusini walitembelea vivutio vya utalii ili kuvitangaza kwenye nchi zao. Nakala 20,000 za majarida na 2,000 za *"CD-ROM"* ziliandaliwa katika lugha za Kichina na Kirusi na kusambazwa katika nchi husika. Tanzania kupitia uanachama wake kwenye shirikisho la

*"Cruise Indian Ocean Association"* ilifanikisha kutangaza utalii wa majini huko Marekani na nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki katika mikutano 11 ya kimataifa ya kudumisha uhusiano, ushirikiano na uwekezaji katika utalii ikiwemo ile ya Jumuiya ya nchi za Afrika ya Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za kusini mwa *Afrika (SADC).* Vile vile, Wizara imefanya vikao viwili vya *"Tourism Facilitation Committee"* kwa lengo la kurahisisha biashara ya utalii hapa nchini na kupunguza vikwazo mbalimbali vinavyokwamisha biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za utalii, Wizara iliendelea kuhakiki hoteli ambapo jumla ya hoteli 307 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Mara, Mwanza, Tanga, Dodoma na Morogoro zilihakikiwa. Wizara katika mwaka ujao wa fedha, inatarajia kuweka hoteli katika madaraja kwa kuzingatia viwango vya kimataifa na vya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mikoa mitatu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa liliendelea kuhamasisha na kushirikisha jamii za Tanzania ili zihifadhi na kuthamini utamaduni wetu. Kupitia tamasha la jamii ya Wabena lililofanyika katika Kijiji cha Makumbusho mwaka 2004, wanajamii hao waliamua kujenga jengo la Makumbusho Wilayani Njombe na tayari limejengwa ikiwa ni hatua muhimu ya kuanzisha makumbusho. Nawapongeza sana wanajamii pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa uamuzi huo wa busara na natoa wito kwa jamii nyingine ziige mfano huo.

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji Maduhuli pamoja na uhifadhi wa rasilimali, Wizara imeendelea kuchangia katika pato la taifa kwa kukusanya maduhuli kutokana na vyanzo mbalimbali vya maliasili, utalii na malikale. Lengo la makusanyo kwa mwaka 2005/2006 lilikuwa ni kukusanya Shilingi 32,884,260,000. Hadi kufikia mwezi Mei 2006, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi 33,319,942,800 ikiwa ni asilimia 101.4 ya lengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Watumishi Wizara imeendelea kusimamia vyuo vya mafunzo vilivyo chini yake ambavyo ni Chuo cha Usimamizi wa Wanyapori Mweka, Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori – Pasiansi, Chuo cha Misitu - Olmotonyi, Chuo cha Mafunzo ya Viwanda vya Misitu - Moshi, Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani, Chuo cha Uvuvi Nyegezi na Chuo cha Taifa cha Utalii. Vile vile Wizara inasimamia kituo cha Elimu ya Uhifadhi kwa Jamii cha Likuyu-Sekamaganga kilichopo Wilayani Namtumbo, katika Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Vyuo hivyo hutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada hadi Stashahada katika fani zinazolenga kuboresha uhifadhi, usimamizi na huduma katika Sekta ya Maliasili na Utalii.

Mchakato wa kuvipatia vyuo vya Pasiansi, Mbegani, Nyegezi na *FITI* (Moshi) usajili wa kudumu kutoka Baraza la Taifa la Usajili wa Vyuo vya Elimu na Ufundi *(NACTE)* unaendelea na Chuo cha Mweka, Misitu Olmotonyi, Chuo cha Taifa cha Utalii tayari vimepata usajili kamili na ithibati *(Full Accreditation*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora utekelezaji wa Mkakati wa Utawala Bora na Kuzuia Mianya ya Rushwa (2000-2006) katika Sekta ya Maliasili na Utalii, umekabiliwa na changamoto kubwa tatu. Changamoto hizo ni kutokuwa na watumishi wa kutosha wa kusimamia na kuendeleza rasilimali nchi nzima; uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sheria na kanuni za sekta; na baadhi ya watumishi wachache kutotekeleza wajibu wao ipasavyo na kuwajibika, kama taaluma zao na maadili yao ya kazi yanavyowataka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, shughuli za usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali zimekuwa zikifanywa katika mazingira ambayo husababisha migongano ya kiutawala. Aidha, sehemu nyingi zinazotakiwa kuwa na watendaji zimekuwa hazina watumishi kwa sababu ya uchache wa watu wenye sifa na taaluma ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua mbalimbali kutatua changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuomba nafasi za ajira mpya na mbadala. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara ilipata kibali na kuajiri watumishi wapya 34 wa kada mbalimbali na kuziba nafasi mbadala 90. *(Makofi)*

Aidha, Mpango Mkakati wa Wizara (2006-2009) umetayarishwa. Mpango huo umeainisha mahitaji halisi ya watumishi kwa ajili ya kuendesha na kusimamia sekta. Kutekelezwa kwa mpango huu kutasaidia kutatua changamoto zinazoikabili Wizara. *(Makofi)*

Katika jitihada za kupambana na janga la UKIMWI ambalo ni tishio kubwa kwa Taifa letu, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2004 – 2007. Hadi Machi 2006 jumla ya Shilingi 24,626,000/= zimetumika kwa kuandaa na kutoa mafunzo ya waelimishaji rika 65, kutoa elimu kwa watumishi na wadau wengine 52, kununua dawa za magonjwa nyemelezi na kuzisambaza na kuhamasisha wafanyakazi kupima Virusi vya UKIMWI (VVU) kwa hiari.

Mheshimiwa Spika Wizara itaendelea kutoa elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi na wadau na kusambaza vifaa vya kujikinga na ugonjwa huo. Aidha, huduma na matunzo kwa watumishi wanaoishi na Virusi ya UKIMWI (VVU) itatolewa kwa kuzingatia mwongozo utakaotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria; Ili kukabiliana na changamoto mbalimbali za mabadiliko ya Sera za uchumi na Maendeleo za kitaifa ikiwa ni pamoja na kujumuisha mikakati ya maendeleo kama MKUKUTA, Wizara inatarajia kukamilisha Sera ya Malikale, na kufanya mapitio ya Sera za Wanyamapori, Misitu na Ufugaji Nyuki. Sheria ya Utalii pamoja na Sheria Mpya ya Wanyamapori zitawasilishwa Bungeni. Vilevile,

Kanuni za Uanzishaji wa Mashamba ya Kufuga Wanyamapori na Biashara ya Viumbe Hai zitatayarishwa na Kanuni kuhusu namna ya kushirikisha wananchi katika Uhifadhi wa Wanyamapori *(WMA Regulations)* zitafanyiwa mapitio. Aidha, Wizara itatafsiri Sheria ya Uvuvi Na.22 ya Mwaka 2003 pamoja na Kanuni za Misitu na Uvuvi kwa lugha ya Kiswahili na kuzisambaza kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, Uhifadhi wa Rasilimali. Kazi ya kuandaa Mpango wa Uendeshaji na Usimamizi wa Mapori ya Akiba ya Maswa, Ugalla na Lukwika-Lumesule pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo inatarajiwa kufanyika. Aidha, Wizara itaandaa mipango ya usimamizi wa misitu ya hifadhi ya Geita, *Ilombero Hill* na *North East Mpanda.*

Mheshimiwa Spika, Wizara itaanza kutekeleza na kusimamia Mkakati wa Kitaifa wa Kuhifadhi Ardhioevu. Vile vile, itaendelea kutekeleza mpango endelevu wa usimamizi wa ardhioevu katika Mikoa ya Mbeya, Iringa na Arusha pamoja na kusaidia wilaya tisa katika Mikoa ya Mbeya na Iringa, Mapori ya Akiba ya Usangu na Mpanga-Kipengele katika kutekeleza shughuli zinazohusu uhifadhi na matumizi endelevu ya ardhioevu. *(Makofi)*

Aidha, Wizara inapitia mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa hapo awali na Kamati mbalimbali ya jinsi ya kuweka taratibu wa uendeshaji wa mapori ya akiba kupitia Shirika au Wakala inayojitegemea ili Wizara ibaki kuwa mtoaji wa Sera na Miongozo peke yake.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mbegu za Miti utaendeleza upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora za miti kwa kukusanya kilo 12,000; kuanzisha vyanzo 10 vya mbegu, kutambua na kuandikisha vyanzo 50 vya mbegu za miti ya asili na kuendeleza vyanzo 28 vya mbegu za miti ya aina mbalimbali. Vile vile, Wakala utakuza na kusambaza miche 15,000 ya miti aina mbalimbali na kupima ubora wa mbegu kwa kuchunguza sampuli 1,200.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa mashamba ya miti ya Serikali, Wizara itaendelea kutunza mashamba 16 yaliyopo kwa kukuza miche milioni 8,400,000 na kupanda miti hekta 6,221. Vile vile, itapogoa matawi katika hekta 3,799 na kupunguza miti katika hekta 1,705. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Serikali za Mitaa, Serikali za Vijiji na wadau wengine kuendeleza Kampeni ya Taifa ya Kupanda na Kutunza miti kwa kutambua vyanzo vya maji na kuhimiza kupanda miti kwa kila Wilaya kupanda miti milioni 1.5. Baadhi ya maeneo ya mabonde ya vyanzo vya maji kama bonde la Usangu yataingizwa katika Hifadhi za Taifa ili utunzaji madhubuti uwepo na baadhi ya maeneo ya wazi yatawekwa katika taratibu za mapori ya akiba ili kutunza mazingira yasiharibiwe na shughuli za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, biashara ya Mazao ya Nyuki imeanza kupata msukumo mpya. Hivyo, Wizara itatayarisha na kusambaza miongozo ya ubora wa mazao ya nyuki na kuwezesha wafugaji nyuki kuanzisha na kuendeleza manzuki katika wilaya 6 (Chunya, Uyui, Nchingwea, Rufiji, Kilindi na Njombe). Aidha, maeneo 4 ya hifadhi za

nyuki *(Bee reserve)* katika Wilaya za Manyoni, Handeni, Kondoa na Kibondo yatatengwa na wafugaji nyuki watawezeshwa kuanzisha na kuimarisha vyama vya ushirika ili viweze kusimamia uzalishaji na masoko. Elimu ya Ufugaji bora wa nyuki itatolewa katika Wilaya ambazo rasilimali za ufugaji nyuki hazijatumika kikamilifu Mikoani Lindi, Mtwara, Ruvuma na Iringa. Mapori ya maeneo ya wazi na ya Akiba yatatumika katika ufugaji wa nyuki badala ya uvunaji na uchomaji wa mkaa. Soko la Asali hapa nchini litakuzwa na kusakwa popote hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha uhifadhi wa rasilimali za bahari, mwaka 2006/2007 Wizara itatangaza maeneo ya visiwa vidogo vya Sinda, Makatumbe, Nyororo, Shungimbili na Mbarakuni kuwa Maeneo Tengefu. Aidha, itakamilisha utambuzi wa thamani wa maeneo mengine na hatimaye kuyatangaza maeneo yenye sifa za kuingia katika mtandao wa Hifadhi za Bahari.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa *MACEMP*, Wizara itaratibu majadiliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Comoro juu ya kuweka mpaka katika Bahari Kuu; Vile vile, itaimarisha Hifadhi za Bahari, na jamii pamoja na kuanzisha maeneo mapya yanayosimamiwa na jamii za pwani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kukarabati na kuimarisha magofu ya majengo na maeneo ya urithi wa dunia ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara kwa lengo la kuendeleza jitihada za kulinusuru eneo hilo kutoka katika orodha ya urithi ulio hatarini kutoweka kwenye kumbukumbu. Kabrasha jipya la maombi kuwezesha Mji mkongwe wa Kilwa Kivinje kujumuishwa pamoja na Kilwa Kisiwani na Songo Mnara litawasilishwa *UNESCO*.

Wizara yangu itaendelea kutekeleza programu ya uboreshaji wa Njia ya Kati ya Biashara ya Utumwa na Vipusa kutoka Bagamoyo Mkoa wa Pwani hadi Ujiji Mkoa wa Kigoma. Kazi ya upimaji pamoja na uchoraji wa ramani ya njia ya Kati ya Utumwa na Vipusa vitakamilishwa. Vilevile, katika kuhifadhi Mji mkongwe wa Bagamoyo, Wizara inakusudia kupima viwanja na kuandaa mchoro wa mpango mji.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Rasilimali; Wizara itaendelea na ulinzi wa rasilimali kwa kuimarisha doria, kutoa mafunzo kwa watumishi na kutoa vifaa vya kisasa. Vikosi 2 zaidi vya doria vitaanzishwa na kuendeleza vikosi 3 vilivyopo ili kuimarisha udhibiti wa rasilimali za misitu na nyuki pamoja na uvuvi. Wavamizi wapatao 100,000 wa misitu ya lindimaji na mikoko wataondolewa msituni katika mikoa ya Tabora, Tanga, Pwani na Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maziwa Makuu na mwambao wa Bahari ya Hindi, doria zitaongezwa kwa kuongeza siku za doria, kununua vitendea kazi na kuanzisha kituo cha doria katika Ukanda wa Kusini wa mwambao wa bahari ili kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Jumla ya doria 4,434 zitaendeshwa katika maeneo ya mwambao wa Bahari na katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Aidha, vyombo vya uvuvi baharini ikiwa ni pamoja na vile vya kigeni vinavyovua katika Bahari Kuu vitadhibitiwa kwa kutumia mfumo wa *Satelite* (kompyuta) ili kuratibu mienendo ya vyombo hivyo. Mitambo ya *Satelite* itatumika

katika sensa na ulinzi wa misitu, bahari na wanyamapori wetu. Tayari mitambo hii imekwishaanza kutumika katika ulinzi wa Bahari Kuu. Kupitia Mradi wa *MACEMP*, doria zitaimarishwa katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari *(EEZ)* kwa kutoa vifaa vya doria na kufanya doria kwa kutumia ndege.

Mheshimiwa Spika, Ushirikishaji Jamii na Elimu kwa Umma; Wizara itaendelea kutoa mafunzo kuhusu uhifadhi wa rasilimali pamoja na kuwashirikisha wananchi ili wanufaike na rasilimali hizo. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za uhifadhi wa wanyamapori uliojikita kwa jamii utaendelea kufanyika na maeneo 10 ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori yatapatiwa haki ya matumizi ya rasilimali ya wanyamapori. Tathmini ya Utekelezaji wa Kanuni za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori itafanyika ili kubaini kama wananchi wanaweza kusimamia maeneo hayo. Aidha, mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu katika wilaya 56 kwenye mikoa 18 utaendelea kuratibiwa. Ushiriki wa wananchi sasa utafanyika kwa mikataba na Serikali yenye majukumu bayana ili kuwezesha Serikali kuchukua hatua za kisheria kwa wahusika pale yanapojitokeza matatizo ya makusudi au uzembe wa Serikali za Vijiji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007 Wizara itatoa elimu kwa Maafisa ugani 300 na wafugaji samaki 300 juu ya uendelezaji na usimamizi bora wa ufugaji uwiano wa samaki katika Mikoa ya Mbeya, Iringa na Kilimanjaro. *(Makofi)*

Pia, elimu itatolewa kwa vikundi 60 vya wakulima wa zao la mwani ili kuwajengea uwezo wa kiujasiriamali na uundaji wa vikundi vya kuweka na kukopa ili waweze kunufaika zaidi na rasilimali za uvuvi. *(Makofi)*

Katika kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali ya uvuvi Wizara itaendeleza utaratibu wa kuanzisha vikundi vya ulinzi wa rasilimali kwa kuanzisha vikundi 120 katika Ziwa Rukwa na vikundi 60 katika Wilaya ya Muheza Mkoani Tanga. Vikundi vyote vipya na vya zamani vitatakiwa kuingia mkataba wa makubaliano na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaandaa na kutangaza vipindi 120 vya redio na televisheni, kuchapisha nakala 4,000 za majarida, vipeperushi, mabango pamoja na kuendesha mikutano, warsha/semina kwa wananchi na viongozi ili kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria, kanuni na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili na malikale. Aidha, uhamasishaji kuhusu upandaji miti, kudhibiti moto, matumizi ya majiko Sanifu, kilimo mseto, ufugaji nyuki na uhifadhi wa vyanzo vya maji utaendelea kufanyika.
Matumizi endelevu ya Rasilimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuendelea kuwepo kwa matukio ya wananchi kushambuliwa na mamba, Wizara kwa Mwaka 2006 imeruhusu uwindaji wa mamba 1500 kwenye mito, mabwawa na maziwa. Maeneo yatakayohusika ni Mto Ruvu, Rufiji, Ugalla, Malagarasi, Ruhuhu, Kilombero, Pangani, Zigi na Momba, Ziwa Rukwa, Bwawa la Nyumba ya Mungu na Hokororo – Liwale na baadhi ya maeneo katika Ziwa Victoria k.v. Buchosa, Butimba n.k. Jumla ya kampuni 20 na vikundi 10 vya walemavu vimepewa mgao wa mamba ili kuwinda kwenye maeneo tajwa.

Mheshimiwa Spika, Kunguru weusi wajulikanao kama *Indian House Crow* wamekuwa ni kero kubwa na ni tishio kwa wananchi hasa katika mikoa ya ukanda wa pwani kutokana na tabia zao. Kero hizo ni pamoja na kueneza magonjwa, kushambulia mifugo na kuchafua mazingira kwa ujumla. Kunguru hao wamezaliana kwa wingi na wanasambaa katika maeneo mengine ya nchi. Kutokana na kero hizo, Wizara imepanga kuwadhibiti kunguru hao kwa kutumia mbinu za kisayansi ambazo hazitakuwa na madhara kwa binadamu, mifugo, viumbe wengine wala mazingira. Baadhi ya mbinu hizo ni kuendeleza matumizi ya mitego, kutoa motisha kwa watakaowaua, n.k. Ili kutekeleza azma hiyo, Wizara imetenga Shilingi Milioni 50 katika mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja mbalimbali zilizowasilishwa, Wizara imeunda kamati ya kufanya tathmini ya uwindaji wa kitalii na kutoa mapendekezo ya kuboresha uwindaji huu kwa madhumuni ya kuwezesha wananchi kufaidika zaidi na rasilimali ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utafiti; Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori inatarajia kufanya sensa katika maeneo ya Hifadhi za Taifa za Serengeti, Ruaha na Katavi pamoja na Mapori ya Akiba ya Selous, Rungwa na Mkomazi.

Vilevile, Taasisi itaendesha mafunzo mbalimbali ya ufugaji nyuki kwa njia za kisasa ili kusaidia wananchi kuinua kipato chao.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Misitu itafanya utafiti kuhusu hifadhi ya vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini; matumizi endelevu ya mazao ya misitu yaliyo timbao na yasiyo timbao; utambuzi wa miti inayostawi katika maeneo mbalimbali ya kijiografia hapa nchini; uzalishaji wa vyahuzo *(cloning)* ya mikaratusi inayokua haraka; na kuendelea na tafiti za Kilimo Misitu na kusambaza teknolojia ambazo zimeshaboreshwa kwa wananchi. Katika kuboresha mazingira ya kazi, Taasisi imetengewa fedha ili kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa makao yake makuu Mjini Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi itaendelea kufanya utafiti wa uvuvi Bahari ya Hindi, Maziwa Makuu na madogo, mito na mabwawa. Baadhi ya tafiti zitafanyika chini ya miradi ya *South West Indian Ocean Fisheries Project (SWIOFP),* Marine *and Coastal Environment Management Project (MACEMP), Implementation of Fisheries Management Plan (IFMP)* na *Climate Impact on the Sustainable Fisheries of Lake Tanganyika Project (CLIMFISH).*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Shirika la Makumbusho ya Taifa litaanza maandalizi ya awali ya kuongeza ukubwa wa maabara na ghala za hifadhi katika Makumbusho ya Elimu ya Viumbe yaliyoko Arusha ili kujenga uwezo wa kuhifadhi mikusanyo ya viumbe na kutoa nafasi zaidi kwa watafiti. Aidha, Shirika litaboresha maonyesho ya ekolojia ya wanyama. Katika kipindi hiki pia, matengenezo ya magari aina ya *Royce Royce* yaliyokuwa yakitumiwa na viongozi wakati wa ukoloni na baada ya

uhuru yatafanyiwa matengenezo ili yaweze kutumika katika siku rasmi za sikukuu za kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji na Utangazaji Utalii; Wizara itaimarisha utalii ikolojia katika msitu wa Mazingira Asili Amani na Misitu ya Hifadhi ya Duluti, Rau, Kimboza na Shume-Magamba. Aidha, itaendeleza utalii ikolojia kwa kuanzisha misitu ya Mazingira Asili katika misitu ya hifadhi ya Nilo - Tanga, Milima ya Uluguru - Morogoro na *West* Kilombero *Scarp* pamoja na kutangaza Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki kuwa Urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Spika, ili kuharakisha utekelezaji wa Sera ya Utalii ya mwaka 1999, Wizara itakamilisha programu ya uendelezaji Utalii itakayobainisha dhima ya kila mdau wa sekta na kuanza maandalizi ya mwongozo wa utalii ikolojia. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itabaini na kuainisha maeneo ya uwekezaji katika Mikoa ya Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi. Katika kudumisha ushirikiano katika Sekta Ndogo ya Utalii, Wizara itahudhuria mikutano 11 ya kikanda na kimataifa na kuhakikisha kuwa maslahi ya Taifa yanalindwa. Aidha, Wizara itafanya vikao viwili vya *Tourism Facilitation Committee* na mkutano mmoja wa mashirikiano na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kupanua wigo wa vivutio vya utalii, Wizara itasaidia kusambaza utalii wa utamaduni katika Wilaya za Magu, Bukombe, Ukerewe, Mvomero na Kijiji cha Butiama. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, itatilia mkazo utalii wa mikutano na utalii wa fukwe. Tayari Wawekezaji toka Mashariki ya Kati wameonyesha nia ya kuja kuwekeza katika maeneo haya baada YA ziara ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na mimi mwenye kufanya ziara katika nchi hizo katika mwezi wa tatu na wa tano mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza na kuimarisha utangazaji wa utalii ndani na nje ya nchi, Wizara itachapisha nakala 250,000 za majarida kwa lugha za Kiingereza, Kiitaliano, Kijerumani, Kiarabu, Kichina, Kijapani, Kirusi na Kihispaniola.

Wizara yangu itakamilisha ujenzi wa kituo cha taarifa katika kituo cha Kumbukumbu ya Dr. Livingstone, Ujiji - Kigoma. Pia, uwekaji wa vionyeshwa katika vituo vya taarifa vya Isimila - Iringa, Kolo - Kondoa na Caravani Serai - Bagamoyo utakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kijacho Shirika la Makumbusho ya Taifa litaendelea na uhamasishaji katika jamii za Tanzania kuenzi na kuhifadhi utamaduni wake kwa kuzishirikisha jamii ya Wakerewe na jamii za Mkoa wa Morogoro. Aidha, Shirika litaendelea kusimamia maendeleo ya ujenzi wa Nyumba ya Utamaduni Dar es Salaam pamoja na kuboresha Kijiji cha Makumbusho ili kiweze kuvutia watalii wengi zaidi badala ya kutumika kama eneo la burudani kama ilivyo sasa. Uendelezaji wa Miundo Mbinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kujiandaa kuanzisha Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS)*, kazi ya ujenzi wa Makao Makuu imeanza. Kazi nyingine za ujenzi zinazotarajiwa kufanyika ni pamoja na kujenga ofisi mpya ya Makao Makuu ya Hifadhi ya Ngorongoro; ukamilishaji wa kuweka umeme wa *Grid* ya taifa unaopitia chini ya ardhi katika Makao Makuu ya Hifadhi ya Ngorongoro; uwekaji wa miundombinu eneo la Oldonyosambu (Tarafa ya Sale) kwa ajili ya wahamiaji wa Tarafa ya Ngorongoro; na kukarabati kilometa 400 za barabara na viwanja vya ndege vinane katika Mapori ya Akiba. *(Makofi)*

Aidha, *Crater* ya Embakai nayo itaanza kuendelezwa katika kiwango cha juu sawa na Ngorongoro ili eneo hilo liweze kunufaisha taifa kiu-talii.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kuleta ufanisi katika Wizara yangu, zimefanyika kwa ushirikiano na wadau mbalimbali. Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wananchi na wote waliotoa ushirikiano katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vile vile, natoa shukrani kwa washirika wetu wa maendeleo kwa michango yao ya kifedha na kitaalamu kama ifuatavyo: Denmark, Finland, Japan, Norway, Marekani, Ufaransa, Ubelgiji, Ujerumani, Sweden, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, *ADB*, *AWF*, *FAO*, *FZS*, *GTZ*, *IUCN*, *KfW*, *Trade Aid*, *MIGA*, *AFRICARE*, *UNESCO*, *UNDP*, *World Bank*, *WWF*, *ICCROM*, na mengineyo. *(Makofi)*

Katika kunipatia taarifa za ukiukwaji wa Sheria na Kanuni wananchi wengi wameshiriki katika kunipatia taarifa za siri. Taarifa hizi zimewezesha kuzuia utoroshaji wa mazao ya misitu, nyara za Serikali na matukio ya rushwa kwa baadhi ya watendaji wa Wizara yangu na watendaji wa Idara zilizo chini ya Halmashauri za Wilaya. Napenda kuwaomba wananchi waendelee kunipa taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu Bwana Saleh Pamba, Viongozi na Watumishi wa Wizara, Taasisi, Mashirika na Wakala kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa mwaka 2005/2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Shilingi 59,789,043,500. Kiasi hicho kinajumuisha fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida Shilingi 35,099,294,000, na kwa Miradi ya Maendeleo Shilingi 24,689,749,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI – MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu Na. 81sehemu ndogo ya (1) cha Kanuni za Bunge Toleo la 2004, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii Fungu 69 kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ambao ndio waliochambua Bajeti hii nao ni:-

1. Mhe. Hassan Rajab Khatib - Makamu Mwenyekiti;
2 Mhe. Bahati A. Abeid - Mjumbe;
3. Mhe. Halima M. Mamuya - Mjumbe;
4. Mhe. Prof. R. B. Mwalyosi - Mjumbe;
5. Mhe. Raynald A. Mrope - Mjumbe;
6. Mhe. V. M. Manyinyi - Mjumbe;
7. Mhe. Lucas L. Selelii - Mjumbe;
8. Mhe. Riziki O. Juma - Mjumbe;
9. Mhe. Elizabeth N. Batenga - Mjumbe;
10. Mhe. James D. Lembeli - Mjumbe;
11 Mhe. Emanuel J. Luhahula - Mjumbe;
12. Mhe. Lucy T. Mayenga - Mjumbe;
13. Mhe. Mariam S. Mfaki - Mjumbe;
14. Mhe. P. Ndesamburo - Mjumbe;
15. Mhe. M. H. Sakaya - Mjumbe;
16. Mhe. Abdukarim E. Shah - Mjumbe;
17. Mhe. Salum Khamis Salum - Mjumbe;
18. Mhe. Mohamed R. Soud - Mjumbe;
19. Mhe. Kaika S. Telele - Mjumbe;
20. Mhe. Anastazia J. Wambura- Mjumbe;
21. Mhe. Riziki Said Lulida - Mjumbe;
22. Mhe. Ernest G. Mabina - Mjumbe;
23. Mhe. Michael L. Laizer - Mjumbe;
24. Mhe. Mwanne I. Mchemba- Mjumbe;
25. Mhe. Juma S. Nh'unga - Mjumbe;
26. Mhe. Ali Said Salim - Mjumbe;
27. Mhe. Ali Khamis Seif - Mjumbe; na
28. Mhe. Aziza Sleyum Ally - Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, tutakubaliana kuwa hii ni moja ya Kamati zenye wajumbe wengi, wajumbe 29 kwa ujumla na inayofanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ambapo alielezea Dira na Muundo wa Wizara, utekelezaji

wa maoni, mapendekezo na maagizo ya Kamati kwa mwaka wa 2005/2006, pia alielezea kuhusu mapato na matumizi kwa kipindi cha fedha kilichopita, mafanikio na matatizo ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo katika kipindi cha fedha 2005/2006.

Aidha kamati ilipata maelezo ya kazi zitakazotekelezwa katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 na Maombi ya fedha za matumizi kwa mpango wa maendeleo na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2006/2007 yalifanyika.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha uliopita Kamati yangu ilitoa maoni na mapendekezo katika maeneo mbalimbali hasa yanayohusu Sekta ya Wanyamapori, Sekta ya Utalii, Uvuvi na Mambo ya kale (Tumejifunza Kiswahili kipya hapa, mambo ya kale sasa ni Malikale), Misitu na Nyuki. Nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, Wizara kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi baadhi ya maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika imeshauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Wizara ya Maliasili na Utalii ilichangia wastani wa asilimia 16 kwenye pato la Taifa. Mchango huu mkubwa unatokana na juhudi za Wizara katika kudhibiti makusanyo, kusimamia na kuendeleza Utalii na uuzaji wa mazao ya Maliasili ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa maduhuli, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 32,864,260,000/=. Sehemu kubwa ya makusanyo hayo yaliyotarajiwa ilitegemewa kutoka Idara ya Wanyamapori shilingi 12,659,320,000/=, Uvuvi shilingi 8,912,376,000/=, Misitu na Nyuki shilingi 10,106,150,000/= na Utalii shilingi 984,500,000/=. Hadi kufikia mwezi Aprili 2006 jumla ya shilingi 32,100,949,208/= zilikuwa zimekwisha kusanywa. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 97.7 ya makusanyo ya mwaka yaliyokadiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2005/2006 Wizara iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi 55,442,163,500/= kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na Fedha za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2006, Wizara ilikwishatumia jumla ya shilingi 37,413,838,900/=. Kiasi cha shilingi 18,028,324,600/= kilitarajiwa kutumika ifikapo mwezi Juni 2006. Mafanikio katika utekelezaji wa bajeti 2005/2006. Kamati yangu ilipata taarifa ya mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa Malengo na Majukumu ya Idara mbali mbali za Wizara hii. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na:-

Upande wa Idara ya Wanyamapori ambapo, visima vya maji katika mapori ya Ikorongo-Grumeti, Lukwika-Lumesule na Mkomazi-Umba vilichimbwa. Pia mafunzo mbalimbali yanayohusiana na sheria na taratibu za matumizi ya Wanyamapori katika maeneo ya Wami-Mbiki, Mbomipa, Ngarambe-Tapika, Ipole na Uyumbu, yalifanyika. Katika maeneo haya baadhi yake ni maeneo ambayo ni maeneo ya Uhifadhi ya Wananchi. Pia, doria katika mbuga za Taifa, mapori ya akiba na misitu zilifanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Idara ya Misitu na Nyuki, tunatoa pongezi kwa Wizara kwa kufuta vibali vya kusafirisha Magogo na Misandali nje ya Nchi, lakini

hata hivy Kamati inaishauri Wizara kuona njia bora ya kuwasaidia watanzania waliokwishavuna Magogo kihalali siku za nyuma ili kusafirisha mizigo yao hiyo nje ya nchi ili rasilimali hiyo isiharibike ovyo. *(Makofi)*

Pia tunaipongeza Wizara kwa kukamilisha mwongozo wa uvunaji bora wa Misitu na Nyuki na kwa kupitia Sera zake na Sheria zinazohusiana na masuala ya Misitu na Nyuki na Kanuni vile vile ili ziendane na wakati, Pia tunaipongeza Wizara kwa kuimarisha udhibiti wa usafirishaji wa mazao ya Misitu nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Idara ya Uvuvi:- Walifanya doria dhidi ya Uvuvi haramu wa Bahari na Maziwa, pamefanyiaka marekebisho ya Sera, Sheria, kanuni na taratibu za kuendeleleza sekta ndogo ya Uvuvi, kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za kimataifa za Uvuvi, Pia kaguzi zimekuwa zikifanywa kuhusiana na ubora wa mazao yatokanayo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Idara ya Utalii:- Idara hii ilishiriki katika maonyesho mbalimbali ya kimataifa, ikawasilisha waraka wa Sheria ya Utalii ya mwaka 2006 kwenye Baraza la Mawaziri, imefanya ukaguzi wa biashara ya Utalii na hoteli, pia imefanya mapitio ya hadidu za rejea kuhusu mradi wa ujenzi wa Chuo kipya cha Utalii.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mambo ya Kale:- Imeboresha vituo vya Mambo ya Kale na Makumbusho ya Taifa, imetayarisha picha na kumbukumbu mbalimbali za maeneo ya kihistoria, imeshiriki mikutano, semina za kimataifa, pia imefanya kaguzi, tafiti mbalimbali za Mambo ya kale.

Mheshimiwa Spika, Pia Wizara imejitahidi kutekeleza mambo mbalimbali yanayohusu Utawala na Utumishi, Sera na Mipango, Fedha na Uhasibu. Aidha, Kamati inasikitishwa na hamisho zisizotekelezeka za Watumishi kwa Idara ya Misitu na Wanyamapori ambazo zimeipaka matope Wizara machoni pa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha uliopita. Pamoja na mafanikio hayo niliyoyataja hapo awali, Kamati iliainisha matatizo yafuatayo:-

(i) Uhaba wa vitendea kazi na upungufu wa watumishi kwa idadi na ujuzi.

(ii) Uvunaji haramu wa maliasili unaotokana na kupanuka kwa biashara ya mazao ya Misitu, Wanyamapori na Uvuvi.

(iii) Ucheleweshaji wa fedha za miradi kutolewa na wahisani.

(iv) Makato ya bajeti ya Wizara ili kugharamia shughuli nyingine za kitaifa kama vile ukame, njaa na matatizo ya nishati.

(v) Kutowajibika kwa baadhi ya watumishi hasa wa ngazi za Wilaya kwenye baadhi ya Halmashauri zet, hivyo kusababisha uvunaji holela wa mazao ya Misitu.

(vi) Uwezo mdogo wa vyuo kuchukua wanafunzi ambao wangeziba pengo la watumishi ambao wanastaafu.

(vii) Dhana ya ushirikishwaji katika uhifadhi kuwa bado ngeni na haijafika sawa sawa kwa baadhi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe Maoni na Ushauri wa Kamati. Ili kufanikisha dhana nzima ya kutumia kikamilifu rasilimali hii ya Maliasili na Mambo ya kale katika Utalii, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo: Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uvuvi:-

- Hapa Nchini ufugaji wa samaki umekuwepo kwa muda mrefu lakini kwa kiwango duni sana, Hivyo kamati inaishauri Wizara iandae mipango madhubuti ambayo itawasaidia wafugaji wadogo wadogo ili kuwa wafugaji wa kisasa.

- Kamati inaishauri Wizara iendelee kudhibiti Uvuvi haramu katika maeneo ya Ziwa na Bahari, pia iweke misingi madhubuti ya usimamizi wa Biashara ya mazao ya Samaki.
- Kwa kuwa Sera ya Taifa ya Uvuvi inaelezea matumizi endelevu ya rasilimali ya Uvuvi, Kamati inaishauri Serikali kuboresha elimu ya Uvuvi kwa Umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Wanyamapori:-

- Kamati inaona kuwa bado kuna umuhimu kwa Serikali kuendeleza juhudi za kulinda Wanyamapori na kuendeleza juhudi za usimamizi wa Mapori ya akiba kwa kutenga fedha zaidi, watumishi zaidi na vifaa vinavyohitajika.

- Kamati inasisitiza umuhimu wa kuletwa Muswada wa Sheria Mpya ya Wanyamapori kabla ya mwisho wa Mwaka huu.

- Kamati yangu inashauri Serikali kuunda Wakala mpya wa kushughulikia masuala ya uwindaji wa Kitalii *(Agency)* ili kutoa fursa kwa Idara ya Wanyamapori kushughulikia Sera, Sheria na Uhifadhi kwenye Mapori ya akiba na hifadhi za Wananchi.

- Kamati yangu inakubaliana na uwepo na umuhimu wa Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori *(Wildlife Management Areas)*, hivyo inaishauri Serikali kupitia upya taratibu zilizopo ambazo ni kikwazo kikubwa kwa uanzishwaji wa Jumuiya hizi, na ushadidi ni uchache wa WMA ambazo zimeweza kuanzishwa hadi sasa.

- Kamati inapendekeza Serikali iongeze viwango vya ada na tozo mbalimbali kwa Kampuni za Uwindaji wa Kitalii, kwa vile rasilimali iliyopo ambayo inavunwa hailingani na Mapato tunayopata tukilinganishwa na Nchi nyingine za *SADC*.

- Kamati inashauri Serikali kuangalia upya Maslahi ya Watumishi wa Sekta ya Wanyamapori wanaofanya Kazi katika Mazingira magumu ya Wanyama wakali, Mbun'go na kadhalika, wapewe nyongeza maalumu ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, kwa Sekta ya Misitu na nyuki:- Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua iliyoichukua ya kufuta vibali vya kusafirishia Magogo na Misandali Nje ya Nchi, aidha kamati inaishauri Serikali ielimishe jamii kuhusu uvunaji bora wa mazao hayo ya Misitu na Nyuki, na kama tulivyosema kwa watanzania waliokuwa wamevuna kihalali, waanaliwe uwezekano wa rasilimali hiyo kuweza kuyafikia masoko husika.

Kamati inapendekeza kwamba Serikali itafute soko la uhakika la mazao ya Nyuki kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza kipato.Katika kukuza mwamko wa uhifadhi wa maliasili na mazingira, ni vema Serikali ianzishe mitaala ya kufundisha somo la mazingira na uhifadhi wa maliasili kuanzia shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Mambo ya Kale:- Kamati inaishauri Serikali iongeze utangazaji wa maeneo ya husika, pia itilie mkazo uzuiaji wa uharibifu wa mazingira katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Idara ya Utalii na Sekta ya Utalii kwa ujumla:- Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa Utalii unachangia pato kubwa la Taifa, Serikali iongeze juhudi za kutangaza nje ya nchi, vivutio vya utalii vilivyopo Nchini, pia bajeti ya kutangaza Utalii iongezwe kadri hali itakavyoruhusu.

Kamati pia inaishauri Serikali ianze sasa kutangaza na kuendeleza utalii uliopo katika mikoa ya Kusini na Magharibi mwa nchi yetu.

Nchi yetu imekuwa na vyuo vingi vya Utalii, Serikali inashauriwa iweke mkakati madhubuti wa kukagua ubora wa vyuo hivyo. Lakini pia Kamati inaiomba Wizara kuangalia malalamiko ya watumishi wanaofanya kazi katika hoteli za Kitalii ambao inasemekana wanalipwa kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa Utafiti katika Sekta nzima ya Maliasili na Utalii, Kamati inashauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya masuala ya utafiti

katika Sekta hii, msisitizo mkubwa utolewe kwa Taasisi za *TAWIRI*, *TAFORI* na *TAFIRI* bila kusahau Vyuo vya Kada mbalimbali vya maofisa katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Kuhusiana na maombi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007, Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2006/2007 ya Wizara ya Maliasili na Utalii, yameandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali yanayolenga katika kutekeleza Sera na mikakati ya utekelezaji wa MKUKUTA. Baada ya uchambuzi wa kina wa Kmati yangu, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya wizara Fungu 69, ya jumla ya shilingi 59,789,043,500/=. Hivyo Kamati inaliomba Bunge lako tukufu lijadili na kupitisha Fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; Kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mbunge, kwa ushirikiano ambao wameutoa kwa Kamati yetu. Pia tunamshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Saleh Pamba na tunatoa pole sana kwa msiba alioupata wa kufiwa na baba yake mzazi. *(Makofi)*

Pia tunatoa shukrani kubwa kwa Watumishi wote wanaofanya kazi chini ya Katibu Mkuu katika Wizara hii pamoja na Mashirika mengine ambayo yapo kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi yao ya uhifadhi wa maliasili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizoniwezesha kuiongoza Kamati hii kwa kipindi hiki hadi sasa na michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa. Aidha, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Utalii, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mbunge, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Mazingira, *NEMC*. Kamati yangu inaahidi kumpa ushirikiano wa hakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kukushukuru tena wewe mwenyewe, kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge Ndugu. Damian Foka na Makatibu wake wasaidizi wa Kamati hii Ndugu Lawrence Makigi na Michael Kadebe kwa kazi nzuri walioifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati, pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandali ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti. Sasa, namwita Msemaji Mkuu Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya ambaye ndiye Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Napenda, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni Kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kwa mujibu wa Kifungu 43(5)(b)(c) cha kanuni za bunge Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda nitoe shukrani zangu kwako wewe binafsi kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya kambi. Aidha nampongeza sana naibu wako, Mheshimiwa Anne S. Makinda kwa nafasi hiyo muhimu sana katika historia ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Urambo Magharibi na wanachama wa chama changu cha wananchi *CUF* kwa kunipitisha kwenye kura za maoni zilizopelekea uongozi wa chama Taifa kuniteua kuwa Mbunge Katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaahidi nitaitumia nafasi hii vizuri kuwakilisha mawazo yao na Watanzania wote kwa ujumla, kufanya kazi yangu kwa uadilifu na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri Mheheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge na Naibu wake Mheshimiwa Zabein Mhita, Mbunge kwa kazi wanayofanya ya kuiongoza Wizara hii. Kwa muda wa miezi sita wameweza kufanya mambo mengi yakiwemo kusafisha Wizara iliyokuwa kwenye hali mbaya, kupambana na ukiukwaji taratibu za uvunaji Maliasili na kuweka mikakati madhubuti ya kuboresha na kuleta ufanisi katika usimamizi wa uhifadhi wa maliasili za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utalii: Tanzania imejaliwa kuwa na vivutio vingi na mandhari nzuri ya kupendeza kupita nchi nyingi za Afrika na hata dunia nzima. Hata hivyo hatujaweza kutumia vya kutosha neema hizo ili kuliingizia taifa hili fedha nyingi za kigeni kuinua hali duni ya maisha ya Watanzania wengi. Pato tunalolipata katika utalii ni dogo sana kulingana na raslimali tulizo nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatakiwa kuwekeza kwenye Sekta hii ya utalii, kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutangaza utalii nje na ndani. Kwa sasa hivi Tanzania inapata wastani wa watalii 600,000 kwa mwaka, idadi hii ni ndogo sana ukilinganisha na nchi za jirani.Bodi ya Utalii yenye wajibu wa kukuza utalii endelevu ambao utaliwezesha taifa kuendelea kupata watalii wengi, kuongeza pato la taifa, kuongeza ajira na kuchangia katika juhudi za Serikali za kupunguza umaskini, haitaweza kufikia malengo yake kama Serikali haitatenga fedha za kutosha kuiwezesha Bodi hii kufanya kazi zake kikamilifu.

Kumbukumbu zinaonyesha kwamba tangu mwaka 1993/1994 hadi mwaka 2005/2006 Bodi hii haijawahi kupata hata nusu ya Bajeti inayoombwa Serikalini. Mwaka 1998/1999 Bodi iliomba kiasi cha shilingi milioni 1,283 lakini walipewa Shilingi milioni 402. Mwaka jana 2005/2006 waliomba shilingi milioni 3,539.4 kiasi walichepewa ni shilingi milioni 1,802.5 Hii inasababisha kushindwa kukabiliana na ushindani wa nchi jirani ambazo pamoja na kuwa na vivutio vya utalii vichache au hafifu zimekuwa zikitumia fedha nyingi kujitangaza.Kuna vivutio vingi sana hapa nchini ambavyo bado

havijafahamika na Serikali haijaeleza mpango wowote wa kuviendeleza na vingine vinafahamika lakini havifikiki kutokana na kukosekana kwa miundombinu mizuri katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, watalii wengi hupenda sana kutembelea mbuga za Kaskazini *(Northern Circuit)* kwa sababu ya kuwepo miundombinu mizuri na pia ndio maeneo yanayotangazwa sana. Hali hii inasababisha kuwepo na msongamano wa watalii eneo moja na pia kusababisha uharibifu wa mazingira ya mbuga zetu. Mfano mzuri ni *Serengeti National Park* ambayo mpaka sasa ina hoteli kubwa zaidi ya Nyota Tano na wawekezaji wengine wameruhusiwa kuendelea kujenga hoteli za kifahari. Wakati wa *Peak Season*, *Mbuga ya* Serengeti kwa siku moja inapokea magari 200 ya watalii. Je, Mazingira ya hifadhi hii yanaangaliwa kwa umakini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tufikirie uharibifu wa mazingira unaosababishwa na magari mia mbili kwa siku moja kitu ambacho kinaweza kusababisha baada ya muda fulani wanyama kuhama na kwenda nchi za jirani, kitu ambacho ni hatari sana kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, tunataka utalii endelevu, unaojali mazingira. Watalii waendelee kuja na uasili wa mbuga zetu ubaki pale pale.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua juhudi za haraka kukuza utalii maeneo ya Kusini na Magharibi kwa kuboresha miundombinu kama barabara, viwanja vya ndege, mahotel, mawasiliano pamoja na kupanua wigo wa shughuli za kitalii. Mfano, kuwepo na *Balloon Safari, Night Game Drive, Canoe Spot Fishing, Walking Safari* na kuanzisha *Cultural Tourism*. Pia, tunaishauri Serikali kuweka kiwango cha idadi ya watalii kuingia kwenye mbuga moja kwa wakati mmoja ili kunusuru uharibifu wa mazingira katika mbuga zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utalii wa kupanda Mlima Kilimanjaro huiletea nchi yetu pesa nyingi ambazo zinajenga uchumi wa nchi. Pamoja na Taifa kwa ujumla kufaidika, lakini kwa hali halisi ya kutokuutangaza kikamilifu wanaonufaika zaidi na mlima huo ni wenzetu wa Kenya kwa sababu ya juhudi zao za kuutangaza. Pamoja na kuwa na Mlima Kilimanjaro, tuna milima mingine kama Mlima Meru, Milima ya Usambara, Milima ya Uluguru, Milima ya Udzungwa na mingine yenye mandhari nzuri, lakini Serikali haifanyi juhudi zozote kutangaza maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watalii wanaopanda milima hulipa pesa nyingi zikiwemo za wasaidizi na waongoza njia. Lakini watu hao ambao wengi ni wenyeji wa maeneo hayo, hulipwa fedha kidogo sana na Makampuni ya utalii kwa kulinganisha na kiwango halisi wanachotakiwa kulipwa kwa siku.Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke sera itakayowawezesha wabeba mizigo na waongozaji wa watalii, waunde umoja wao na waweke viwango vya fedha watakazokuwa wakilipwa kwa siku kutokana na kazi zao. Kwa njia hii, tutaongeza tija kwa wazalendo kuweza kunufaika na kile kinachopatikana kutokana na Utalii wa kupanda milima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina hoteli zenye hadhi ya Kimataifa zikiwa katika Miji yetu Mikuu na nyingine zikiwa katika hifadhi za wanyamapori. Hapa ndipo uhusiano kati ya Sekta hii ya Utalii inapoweza kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika uhalisia wa mambo yalivyo katika Sekta hii ya Utalii ni kwamba, Tanzania bado haijaweza kuitumia vizuri Sekta ya hoteli katika kuhakikisha kuwa aina zote za bidhaa za vyakula zinapatikana hapa nchini ili kuweza kuinua hali ya kipato cha wakulima na wafugaji wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta hii ya Hotel inanufaisha zaidi wakulima na wafugaji wa nje kwa kuwa baadhi ya hoteli ambazo vyakula vinavyopikwa vinatoka nje ya nchi na hii ni hatari sana kwa wakulima wetu na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Kwa kuweka kumbukumbu sawa, Mheshimiwa Rais aligusia sehemu moja tu ya ajira katika hoteli kubwa kuwa zinashikiliwa na wageni. Hivyo, nadhani kama hilo limefanyiwa kazi, basi Serikali iangalie na tatizo la bidhaa za kilimo chetu kutotumika kikamilifu katika kuhudumia hoteli zetu. Huu utakuwa mchango mkubwa wa Sekta ya Kilimo katika vita dhidi ya Umaskini. Sekta hii huonekana kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na mwananchi wa kawaida badala ya kubaki kuwa mtazamaji tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utafiti unasaidia sana kwenye suala zima la utalii na uhifadhi wa maliasili, kwani unatoa *findings* ambazo *results* zinatumika na utawala kuboresha shughuli za utalii na uhifadhi wa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna uhifadhi endelevu wala utalii pasipo utafiti wa uhakika. Vituo vya utalii vya wanyamapori hapa nchini vimesahaulika, havitengewi fedha za kutosha kuendesha shughuli zake kikamilifu. Hali hii inasababisha Vituo vingi kufanya kazi chini ya uwezo wake na vingine kushindwa kufanya kazi kabisa kwa kukosa Watendaji na vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, milipuko ya magonjwa ya wanyamapori siku hizi ni mingi ukilinganisha na huko nyuma. Hali hii ni hatari sana katika swala zima la uhifadhi, kwani hata baadhi ya wanyama/viumbe wametoweka kabisa kwenye hifadhi zetu na hakuna utafiti wa kina kuhusu kutoweka kwa viumbe hao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vituo hivi kuwa na mipango ya kuboresha suala zima la uhifadhi na usimamizi wa maliasili zetu, wamekuwa wanashindwa kufikia malengo sababu ya kutopewa fedha za kutosha kwa ajili ya kujiendesha. Aidha, mapungufu makubwa yamekuwepo kwenye kugharamia mahitaji ya kila mwaka kwa kituo kikubwa cha utafiti cha wanyamapori *(TAWIRI)*. Mfano, mahitaji ya Taasisi kwa mwaka 2005/2006 yalikuwa Sh.1,270,000,000/=, kiwango kilichotolewa kilikuwa Sh.521,099,700/= ambayo ni asilimia 41 ya matarajio. Aidha, mchango wa Wahisani umekuwa ukipungua kutoka Shilingi milioni 700, mwaka 2000 mpaka Shilingi milioni 35 mwaka 2005/2006. Hii inaonyesha wazi kwamba Wahisani wameanza kukata tamaa baada ya kuona pengine matarajio yao ni kinyume na mambo yalivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo tulilonalo ni ukosefu/upungufu wa watafiti wa kitanzania wa kufanya utafiti unaohusu wanyamapori. Hili linaambatana na mafungu kidogo yanayotolewa ya kusomesha wataalam katika Sekta hii. Dhana ya uhifadhi, *conservation* inabadilika sana, hivyo Wahifadhi wetu wanatakiwa kwenda na wakati. Pamoja na hili, tunatakiwa kubadilisha sera za uwindaji ili izalishe zaidi kuliko ilivyo sasa, kwa kuuza fursa za uwindaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya utafiti wa wanyamapori hapa nchini inafanywa na wataalam wa kigeni kwa kutumia fedha za kigeni. Hii ni pamoja na *wildlife monitoring*. Hii ni hatari sana kwa usalama wa maliasili zetu, ni eneo ambalo tunatakiwa tufanye Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watafiti wengi wa nje wamekuwa wakifanya kazi peke yao bila ya usimamizi wa Idara husika, suala linalopelekea Watafiti kuwepo kwa muda mrefu kwenye Vituo bila kutoa ripoti za tafiti zao kwa muda muafaka. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliambia Bunge hili Kituo cha *ABRU* kinachofanya utafiti wa nyani kilichopo *Mikumi National Park,* kulichoanzishwa mwaka 1974, mpaka leo ni ripoti ngapi zimetolewa na kituo hicho kusaidia *management ya Park* hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kupiga marufuku uvunaji na usafirishaji wa magogo ya miti ya asili, biashara ambayo ilishamiri hapa nchini kwa muda mfupi ikageuza nchi yetu kuwa jangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kutambua mbinu na kuwajua vigogo ndani ya Wizara ambao ndio wahujumu wakubwa wa maliasili za Watanzania wakiendesha biashara haramu ya kusafirisha mazao ya msitu nje ya nchi, kama alivyonukuliwa Mheshimiwa Waziri mara kadhaa na Vyombo vya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuwatambua wahujumu hawa na kuwaacha kwenye nafasi zao wakiendelea kuhujumu maliasili za Watanzania haisaidii. Kwa kuwa vigogo hawa wanafahamika na wamejineemesha kwa miaka mingi wakitumia mali za Watanzania kujitajirisha wao binafsi huku Watanzania wakiendelea kuwa maskini na nchi ikiendelea kuwa jangwa na kusababisha majanga makuu kama njaa, kukosekana kwa nishati ya kutosha ya umeme na mengine, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya vigogo hao tangu Serikali ibaini jinsi wanavyofanya biashara hiyo haramu kuhujumu maliasili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna uhifadhi endelevu pasipo kushirikisha jamii. Mpango ulioanzishwa kwenye baadhi ya Mikoa mfano Morogoro, Iringa, Mbeya na Lindi wa kuhifadhi misitu kwa kushirikisha wananchi wanaozunguka hifadhi hizo, ni utaratibu mzuri sana ila *program* hii inasua sua kutokana na ucheleweshwaji wa fedha kutoka Serikalini. Fedha zinatoka *DANIDA* kwenda Hazina na toka Hazina zinakwenda Wizara ya Maliasili na kutoka Wizara ya Maliasili zinakwenda Wilayani. Ukiritimba huu na mzunguko umeathiri mtiririko mzima wa utekelezaji wa kazi na hivyo wananchi kuona kwamba wanadanganywa. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa utaratibu mzima wa utoaji fedha za miradi uwe wa haraka na usio na ukiritimba, ili kuwezesha utekelezaji wa haraka wa miradi hii na Serikali ifanye juhudi za kueneza *programme* hii kwenye Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo tabia ya Maafisa Misitu wa Kata na Tarafa katika maeneo mengi hapa nchini kutaifisha mazao ya misitu yanapokamatwa na Askari wa Vijiji/Kamati za Maliasili za Vijiji na kudai kwamba kazi ya Vijiji ni kukamata tu, baada ya hapo, mazao yaliyokamatwa yanakuwa mali ya Serikali bila kujali Askari hao wa Vijiji ni kiasi gani wameteseka na kuhatarisha maisha yao katika zoezi hili la kamata kamata mazao hayo ya misitu. Hili limekuwa tatizo na kukatisha tamaa wananchi wenye moyo wa uzalendo katika kulinda maliasili zao. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuharakisha kupima maeneo ya hifadhi za misitu zilizotengwa na Vijiji, ili kuwapatia wananchi hao hati ya kumiliki maeneo hayo na kuweza kunufaika moja kwa moja na maliasili wanazozihifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya, wamepewa jukumu kubwa la kusimamia misitu kwenye maeneo yao. Wakati huo huo Halmashauri zinategemea maliasili zilizopo kwenye misitu hiyo kupata fedha za kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti kwenye Halmashauri zetu, vibali vya kuvuna maliasili vinatolewa bila hata kujua hali halisi ya misitu hiyo, kwa kuwa wanaopewa leseni ni wafanyabiashara, hawana uchungu na maliasili hiyo hata kama wakikuta aina ya miti wanayotaka hakuna, watakata aina nyingine, ili mradi watengeneze pesa. Thamani ya pesa inayopatikana ni ndogo sana ukilinganisha na majanga makubwa tunayoyapata. Hali hii ndio iliyotufikisha hapa tulipo sasa. Serikali imeziamini sana Halmashauri bila kuziwezesha, kuja kushtuka misitu imeteketea na kilio cha ukame kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni Wizara kuchukua jukumu la kutoa vibali kwa wafanyabiashara kwenda kuvuna maliasili kwenye hifadhi za misitu ya Vijiji bila kuwasiliana na ngazi za Wilaya wala Vijiji husika. Hii ni kinyume na taratibu na sheria za uvunaji wa misitu.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali pamoja na kuwapa Halmashauri mamlaka ya kusimamia maliasili hiyo, Wizara husika ifuatilie mara kwa mara kutembelea misitu hiyo kujua ni nini kinachoendelea badala ya kutulia Ofisini wakisubiri taarifa kutoka kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza matumizi ya mkaa kama nishati, Serikali imeona njia mbadala ni kutumia mafuta ya taa na gesi kwa kupunguza ushuru wa bidhaa hizi. Wakati huo huo bei ya majiko ya mafuta ya taa iko juu. Ni wachache watakaoweza kumudu kuyanunua.

Pia, suala la kutumia *gas* kwa kupikia, ni wachache watakaolipokea kwa kutambua hatari za matumizi ya *gas* kwenye nyumba za familia, umeme ambao ndio nishati inayotegemewa na wengi unapanda bei kila leo haushikiki.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kuharakisha uchimbaji wa makaa ya mawe na kuanza kutumika kama njia mbadala ya mkaa wa kuni kwa matumizi ya majumbani, ndio litakuwa suluhisho la kudumu kunusuru misitu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania inakadiriwa kuwa na makundi milioni 9.2 ya nyuki wa asili yenye uwezo wa kuzalisha tani 138,000 za asali na tani 9,700 za nta kwa mwaka. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa, Tanzania inazalisha tani 4,860 tu za asali na tani 324 za nta kwa mwaka ambao ni asilimia 3.5 tu ya uwezo wa rasilimali ya nyuki iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijawahi kulipa umuhimu wa kutosha suala la ufugaji wa nyuki hapa nchini. Zipo jamii nyingi zinazojihusisha na ufugaji wa nyuki katika maeneo mengi, lakini wengi wao wameshindwa kujikwamua na hali ngumu ya maisha kutokana na Serikali kutokuwa na mpango ulio makini. Wafugaji wengi mpaka sasa wanafuga kienyeji kwa kutumia vifaa vya kienyeji na pia wanavuna kienyeji kwa kutumia moto kwa sababu ya kukosa elimu ya kutosha na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, hata hiyo asali kidogo wanayopata, wanaiuza kwa bei ndogo sana. Hakuna soko la uhakika kwa ajili ya mazao ya nyuki. Kutokana na hali hii, wafugaji wa nyuki hawafaidiki na kazi wanayoifanya, hali ya maisha yao ni duni. Serikali nayo imekaa kimya. Pia, Taifa linakosa mapato kutokana na zao hili ambalo lina soko zuri nje ya nchi kuachwa kiholela. Umaskini utaondokaje katika nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulipa umuhimu suala la ufugaji wa nyuki, kupeleka watalaam Vijijini wakaelimishe wananchi mbinu za kisasa za ufugaji wa nyuki na kutafuta masoko mazuri ya mazao yatokanayo na ufugaji wa nyuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wanyamapori ni Sekta nyingine ambayo inaliingizia Taifa fedha nyingi. Katika Sekta nzima ya maliasili kwa kipindi cha mwaka 2005 iliingizia Taifa kiasi cha Sh.12,665,063,222/=. Kwa kipindi hicho, jumla ya leseni 2,474 zilitolewa kwa wawindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 1974, *(Wildlife Conservation Act 1974)* inaonyesha kuwa utengaji wa maeneo ya uwindaji kwa watalii, Mkurugenzi wa Wanyamapori ndiye mwenye mamlaka ya kufanya kazi hiyo. Kulingana na misingi ya kisheria, mtu mwenye mamlaka ya kuweka utaratibu juu ya matumizi endelevu ya uhifadhi wa wanyamapori ni Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Maliasili.

Mheshimiwa Spika, malalamiko mengi ya matumizi mabaya ya mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Wanyamapori na kutolewa kwa vibali vya maeneo ya kuwinda na upendeleo kwa wageni, unyanyasaji unaofanywa na Maaskari wa Hifadhi kwa Jamii iliyozunguka hifadhi hizo, hali ambayo imesababisha hata wananchi kuwa na

wasiwasi kuwa mapato halisi yanayopatikana kutokuwa na uhalisia kamili, kwani wanyama wanaovunwa ni wengi mno na mapato ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iangalie upya sheria hii ili kuwepo na chombo angalizo jinsi utaratibu na leseni za maeneo ya uwindaji zitakavyotolewa na mapato yake yatadhibitiwa namna gani. Aidha, sera ya wanyamapori ya mwaka 1998, inataka kuwa raslimali za wanyamapori zitumike kisheria kwa hali itakayohakikisha kudumu kwake na matumizi endelevu ya raslimali hiyo kuendeleza jamii zilizozunguka hifadhi husika.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ilieleze Bunge lako kwamba, mpaka sasa kuna Watanzania wangapi ambao wametuhumiwa kwa kesi za kuhusishwa na ujangili wakati taarifa za mara kwa mara za vyombo vya habari imeonyesha kuwa majangili wa kweli wako nje na wanazidi kuendesha biashara hizo haramu kwa kushirikiana na Watendaji wa Serikali? Taarifa hizo nazo hazijakanushwa na Serikali. Ni dhahiri Bunge hili lina haki ya kupata taarifa ya Serikali kuhusu hali hiyo inayoathiri maliasili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Mkurugenzi wa Wanyamapori kuendelea kung'ang'ania nafasi hiyo, linatia doa Serikali ya Mheshimiwa Rais Kikwete. Hakuna mtu mwenye mali na cheo. Mbona Maofisa wengine wa Wizara hiyo waliokumbwa na hamishahamisha hiyo waliondoka wakati nao pia ni *presidential appointees*? Kuna nini katika Kiti chake hicho? Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kina kufahamu kama nchi hii pia kuna Miungu Watu wasiogusika katika nafasi zao. Kutokana na hali hiyo ya watu kugomea Maofisini kama ilivyo sasa *TANAPA,* ambako baadhi ya Maofisa wanapanga kwenda Mahakamani kupinga *transfers*! Inadhihirisha kwamba kuna Maafisa Waandamizi Serikalini wanamlinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo ndani ya Idara ya Wanyamapori, baadhi ya Wafadhili wamejitoa kwenye ufadhili, mfano ni *GTZ* waliotusaidia kwa miaka mingi katika uhifadhi wa wanyamapori na sasa wamejitoa kutokana na kukatishwa tamaa. Kambi ya Upizani inaiomba Serikali kulipatia Bunge lako Tukufu ufafanuzi kwa haya yafuatayo:-

(i) Ni lesseni ngapi zimetolewa kwa Makampuni ya kitalii ya uwindaji kati ya mwaka 2004 na 2006? Ni Makampuni yapi hayo kwa kila kitalu na zimetolewa kwa maeneo yapi? *(Makofi)*

(ii) Kati ya hizo, ni ngapi zimetolewa kwa wawindaji wageni na ngapi zimetolewa kwa wazalendo na leseni zinaruhusu umiliki wa eneo lenye ukubwa gani? *(Makofi)*

(iii) Ni fedha kiasi gani zimekusanywa kutoka kwa Makampuni hayo kama kodi kwa Serikali?

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine la Idara ya Wanyamapori kukumbatia wawekezaji wa nje wenye Makampuni ya Kuwinda na hata wale wanaoendesha mahoteli ya kitalii kwenye hifadhi zetu. Hata pale wanapokiuka sheria na makubaliano ya Mikataba yao, wananchi wakilalamika hawasikilizwi na hawa wawekezaji wanapata jeuri ya kuendelea kufanya wanavyotaka. Jeuri hii inatoka wapi wakati kuna Serikali na vyombo vyake kikamilifu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo haya yapo mengi na Wizara inayafahamu na bado wawekezaji hao wapo wanaendelea kuvuna. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia suala hili kwa makini, wananchi wapewe haki yao wanayostahili na wasinyanyaswe na wewekezaji ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, hifadhi za jamii za wanyamapori Tanzania ina hifadhi za jamii za wanyamapori 16 ambazo zimetengwa na wananchi wenyewe katika maeneo mbalimbali katika mpango mzima wa kushirikisha wananchi kuhifadhi na kusimamia maliasili zinazowazunguka.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kutumia mamilion ya fedha katika *program* hii, pamoja na wananchi hawa kuhifadhi maeneo hayo kwa zaidi ya miaka 10 sasa wakisubiri mpango wa matumizi endelevu wa maliasili hizo, mchakato wa *WMA* iwe asasi zilizoidhinishwa una ukiritimba mkubwa na wa gharama kubwa. Mpango wa uanzishwaji maeneo haya wazi ni tegemezi kwa fedha za Wahisani. Bila hawa, wananchi wetu hawataweza kumudu gharama za kutimiza masharti hayo.

Mheshimiwa Spika, tangu miradi hii ianze miaka ya 1980 na kuwa na miradi teule 16 mwaka 2002 hadi kufikia 31 Machi, 2006 ni miradi minne tu iliyopata hadhi ya asasi iliyoidhinishwa. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, ni lazima ikubali kuingia gharama za kupima Vijiji na kutengeneza matumizi ya ardhi kwenye Vijiji vilivyo na wanyamapori. Vinginevyo, mpango huu utabaki kuwa kitendawili.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kwanza kutambua na kuthamini mchango wa wananchi hao wanaofanya kazi ngumu sana kwenye mazingira magumu kuhifadhi maliasili zinazowazunguka kwa miaka mingi. Ni lazima Serikali ifikie hatua ya kuthamini kazi hiyo kwa kuwapatia mamlaka iliyotegemewa ya *Wildlife Management Areas. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Sekta ya Uvuvi inaingiza pato la wastani wa Dola za Kimarekani milioni 9.8 sawa na asilimia 2.5 ya Pato la Taifa, wakati Namibia wanaingiza wastani wa Dola za Kimarekani milioni 52. Namibia wanazo (*Fish Ports)* Bandari za Samaki na Viwanda vya Kusindika Samaki ambavyo vimeajiri sio chini ya watu 14,000.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna viwanda kwenye Ziwa tu wakati ukanda mzima wa bahari hakuna Bandari ya Samaki jambo ambalo linatukosesha ajira kwa vijana wetu, huduma ya kuuza mafuta kwa meli zinazovua, mrahaba kwa samaki wanaovuliwa na kusafirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wastani wa meli 140, kila moja inavua samaki wasiopungua *MT* 500 kwa mwezi, sawa na *MT* 70,000 ambazo ni sawa na kilo 70,000,000 kwa mwezi, wanauza samaki kwa wastani wa Dodla za Kimarekani tano kwa kilo, sawa na Dola za Kimarekani milioni 350 kwa mwezi. Meli hizi zina uwezo wa kutumia *diesel* wastani wa lita 1000 kwa meli kwa siku. Hivyo, zinatumia lita 140,000 za *diesel* kwa meli zote, mafuta haya wananunua huko huko *(high seas)* bahari kuu, kwa sababu Tanzania hakuna bandari ya samaki.

Mheshimiwa Spika, jinsi meli hizi zilivyonyingi, hivi sasa zinavua katika maeneo ambayo wananchi wengi wanavua, jambo lililosababisha upungufu wa samaki katika ukanda wa maili 20 za bahari na hivyo kupunguza ajira na kipato, lakini pia kuongeza utapiamlo miongoni mwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba zetu za nyuma, tulisema kuhusu hili la wamiliki wa meli hizi kulipia leseni kwa Dola za Kimarekani 18,000 tu kwa mwaka na tulishauri ada ipande mpaka Dola za Kimarekani laki moja kwa leseni angalau kama ilivyo Somalia ambapo hata Serikali yenyewe bado haijatengamaa vizuri.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ianzishe *Fish Ports na Fish processing plants* na kuhakikisha kuwa meli zote zinanunua mafuta, maji na huduma nyingine kwenye Bandari ya Samaki kwa njia hiyo, mzunguko wa biashara katika ukanda mzima wa Pwani utakuwa ni mkubwa sana kuliko ilivyo sasa. Kwa njia hii tungeongeza ajira Tanga, Mtwara, Zanzibar, Lindi, Mafia na Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo, Kambi ya Upinzani inapenda kuelewa kwa kina ni kwa kwanini tulishindwa kuchukua zawadi ya meli ya utafiti tuliyopewa bure na hata tungeletewa bure na Serikali ya Namibia mara tu baada ya kupata uhuru wao kama ishara ya kutambua mchango wetu katika ukombozi wa nchi yao?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo nawashukuruni wote kwa kunisikiliza. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kutoa taarifa tu kwamba, kengele ya kwanza ililia kwa makosa, Mheshimiwa Mbunge alianza saa 4.53. Kwa hiyo, utaona ilichelewa kwa sababu ilibidi tushauriane na kurekebisha. Sasa ninao Wasemaji 26. Lakini tutaweza kupokea labda 15 tu. Kwa hiyo, nawaita kwa mpangilio nikiweka umuhimu kwa wale ambao walikuwa hajachangia ukiacha Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella ambaye nampa upendeleo maalum, tutaanza nao. Wafuatao wote hawajasema hata katika hoja yoyote, Waheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Mohamed Said, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Saverina Mwijage.

**MHE. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii muhimu. Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Mheshimiwa Antony Diallo, Mbunge wa Ilemela kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa

Maliasili na Utalii na pia, kumpongeza Mheshimiwa Zabein Mhita, kuwa Naibu Waziri. Pia, ningependa kabla sijatoa mchango wangu, nitambue Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kuwakilisha maoni ya Kamati. *(Makofi)*

Lakini kwa namna ya pekee, nimtambue Waziri Kivuli ambaye amewakilisha ripoti makini ambayo ina uchambuzi wa kina. Haya ninayasema nikizingatia kwamba tunapokuwa ndani ya Bunge, tunawakilisha Watanzania na maneno yakisemwa ambayo ni makini kutoka katika Kambi ya upinzani ni lazima tuyakubali. Hiyo ndiyo itaonyesha kupevuka kwetu kisiasa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Sakaya, naomba nikupongeze sana, *you have done as proud* kwa wanawake ya kwamba, hata ukiwa upande wa pili, unafanya kazi yako vizuri. Kuna siku utarudi Kambi hii ya CCM. *(Makofi/Kicheko)*

Baada ya kusema hayo, napenda nichangie machache yafuatayo: Moja, Wizara hii itatuondoa hapa tulipo kama itafanyiwa kazi *seriously*. Ni Wizara hii ambayo nchi nyingine zinaionea Tanzania wivu. Tuna misitu, nchi nyingine hazina; tuna maji, nchi nyingine hazina; tuna mandhari ya mito, milima, maporomoko ya mito, mapango ya kila aina, yaani Tanzania katika Dunia hii ni sisi tuliobarikiwa na labda ndio maana tuna *Oldvai Gorge* ambayo inaashiria kuonyesha kwamba hapa ndipo kulikuwa na Bustani ya Eden ambayo Mungu aliumba akamweka Adam na Hawa ili aweze kumiliki viumbe vile. Hakuna mahali duniani unapoweza kupafikiria penye nafasi kama hii ambayo tuliyonayo. *(Makofi)*

Pili, ningependa kusema kwamba labda Wizara sasa itusaidie kufanya uchambuzi wa kisayansi. Kuna kitu kinaitwa *carrying capacity* katika mambo ya *population* ya kwamba, unaweza kuwa na idadi kubwa ya watu, lakini ukawa na uwezo mkubwa wa kuhimili hawa watu. Ama ukawa na idadi ndogo ya watu katika eneo na ukawa huna uwezo wa kuhimili, mimi nasema kufuatana na maliasili hii tuliyonayo, Tanzania ingeweza hata kuweka binadamu zaidi ya milioni 100 na bado tukaweza kuhimili kwa kutumia hii rasilimali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni vizuri Wizara hii sasa isiendelee kuhifadhi vilivyopo, lakini ifanye uchambuzi wa kina ya kwamba kama tungetumia uvuvi kwa makini, *carrying capacity* ya Tanzania kwa kutumia maziwa, mito na bahari ni kiasi gani tungeweza kuweka ajira ya watu wangapi, tungeweza kulisha watu wangapi samaki na tungeweza kupeleka nje kiasi gani tukaleta katika Pato la Taifa? Ningependa hiyo kazi ifanyike.

Mheshimiwa Spika, twende kwenye maeneo ya utalii. Ukichukua mbuga zetu zote kwa utalii wa kila aina na hasa utalii ule wa wawindaji, mimi nilikuwa katika Wizara hii na kwa sababu ninazunguka na niko *South Africa* kwa muda mrefu, hili ni ni eneo mojawapo ambalo tumeliachia, halijaweza kutuletea pato ambalo tunastahili. *(Makofi)*

Katika utalii utaratibu wa watu kuweka fedha nje makampuni watu watalii wanalipa huko huko halafu wanakuja hivyo walivyo, *in fact* katika utalii hao wengi tunaowapata ni *one donor tourist*, siyo wale watalii wa kweli kweli. Kwa hiyo, hilo nalo Wizara ifanyie kazi hatuwezi kuendelea kunufaisha watu wengine halafu tunawatuma Rais, Mawaziri kwenda kuwapigia magoti watu wengine ambao fedha zetu zimekwenda

kwao. Kwa hiyo, hiyo kazi nayo ifanyike ili katika kipindi cha mwaka mmoja mtakaporudi hapa mtueleze hiyo *carrying capacity* katika mambo ya uvuvi na mtueleze pia ni jinsi gani sasa tunaweza tukafanya mapinduzi katika utalii kwa kile ambacho tunakifanya sasa hivi tukikifanya vizuri kabla hata hatujaongeza kingine tunaweza tukapata mapato makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi, kama ningekuwa na muda ningeyaeleza. Lakini pia, ningependa kusema kwamba nakubali kwamba Wizara hii haipewi fedha zinazostahili kuweza kumudu majukumu yake. Labda katika Bajeti Serikali ifikirie kuongeza uwezo zaidi katika Wizara hii. Kwanza, uwezo wa kuwapa motisha wafanyakazi wao. Mimi nimeshapanda Mlima Kilimanjaro nilipokuwa Waziri wa Maliasili na Utalii nikiwa bado kijana kuliko nilivyo sasa. Upandaji ule unafika mahali hata vidole vyako unaviona vizito, lakini unakuta yule kijana anayebeba mizigo kumpandisha mtalii, atabeba maji atabeba mizigo yote na malipo yake ni kidogo. Mimi nilipopanda Mlima Kilimanjaro, niliteremka niliwaongezea mishahara, sijui sasa ni kiasi gani wameongezewa. Hili Waziri tu, atamudu. Kawaongezee mishahara wale watu wanaopanda juu ya Mlima Kilimanjaro wana kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Lakini ningependa kusema kwamba, yapo maeneo mengi ambayo yangeweza kuwa ni ya utalii. Mojawapo ni Jimbo la Ukerewe, Visiwa 38; eneo hili lina maajabu ambayo hayajatangazwa. Kwa sababu Waziri, anatoka karibu na kule niliko na huwa anakuja mara nyingi kwa sababu ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, nitajaribu kumtembeza aone. Moja, nitampeleka Waziri kwenye jiwe lililoko Kisiwa cha Ukara lenye tani kama kumi, ishirini, ni jiwe linalochezwa likaamrishwa na wenyewe. Linaitwa Bulebeka. Niliwapeleka wageni wangu wa Marekani hawakuamini. Mtu mwingine huwezi kuliamrisha, lakini ukiwaita watu wa ukoo ule ambao wanaishi pale Bwisha, anafika analiambia wasalimie wageni, jiwe linacheza mpaka atakaposema basi, imetosha. *(Makofi/Kicheko)*

Katika Kisiwa hiki hiki cha Ukara, yapo maajabu mengi na hawa walikuwa ni watu ambao wanahifadhi misitu kwa kuiita visaka. Wanaita kisaka. Wanahifadhi na walikuwa wanaamini sana uhifadhi. Sasa wakati mwingine tumekuwa na uhifadhi ambao hauendi na maadili ya wananchi. Kwa hiyo, napata taabu kuyaelewa mazingira hayo.

Kwa hiyo, ningependa hilo moja, tuna mahali ambapo ukisimama utaiona Mwanza na utaiona sehemu ya Kagera, inaitwa Handebezi. Kwa muda mrefu imekuwepo. Mheshimiwa Meghji aliwahi kuitembelea, tukamwomba, tumejitahidi kwa uwezo wetu kwa miaka mingi kuitengeneza, ni mahali panavutia sana. Kuna mapango mengi ya asili ambayo mengine yanakuja kutokea ndani ya ziwa. Tungeweza kabisa kufanya utalii katika maeneo haya. Tuna Pwani zinazopendeza katika Visiwa vyote. Ukiangalia Kaseni ya Ilangala utashangaa, ukiangalia *Beach* ya Rubya ambayo ina msitu, halafu ina mchanga halafu unaingia majini ni mahali panapendeza sana. Ukiangalia Kisiwa cha Ilugwa kile kinachoitwa Kulasi, kina Pwani na wananchi wake wanahifadhi wenyewe mazingira yao mpaka wanajenga vyoo Pwani ili mazingira yasije yakachafuliwa.

Kwa hiyo, mimi natoa tu rai ya kwamba, vivutio ni vingi kwa nchi hii. Ukienda Mafia utashangaa tu! Ukienda Kusini ukiangalia Milima ya Kusini, inapendeza! Kwa hiyo, tuondokane na kuangalia upande mmoja wa nchi, tusambaze utalii katika maeneo yote ili tuweze kuhakikisha ya kwamba hili ni tunda, haya ni mazao Mungu alitupa bure, hatukulipia, tuyaendeleze yote. Lakini mara nyingi jibu litakalotoka kwa Waziri ni kwamba wananchi wenyewe wajitahidi. Unamwambia mwananchi wa Ukerewe ambaye hata Mwanza hajawahi kufika, anakaa karibu na pango aendeleze. Sasa Wizara inafanya nini? Kama ni hivyo, mtuletee Ofisi ya Maliasili na Utalii kama Wilaya ya Ukerewe ili iweze kuchambua na kuyaendeleza haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kwenda kwenye uvuvi. Nasemea wavuvi wote wa Kojani, Mafia, Ukerewe, Mbambabay na wa Kigoma huko wote wanaovua samaki. Hili ni eneo ambalo halijaangaliwa kwa makini, bahati mbaya sikuchukua takwimu zao. Ukichukua Watanzania wanaokula samaki, tuko *below standard,* hatujafikia *kilograms* zinazotakiwa za kula samaki. Hiyo yote inatokana na kutowatazama hawa wavuvi kama wachangiaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, nimesema, mara nyingi kwamba, tunazungumza juu ya mahindi, pembejeo za mahindi, mtakuwa mnatafuna mahindi bila kitoweo? Kwa hiyo, lazima tunapoweka ruzuku kwa mahindi lazima ruzuku kwa uvuaji wa samaki. Lazima tuweke ruzuku kwa mifugo ili watu wale ugali kwa kitoweo. Sisi kwetu kule kula ugali na mboga za majani kwa kweli ni aina ya kakashifa kadogo kwenye familia.

Kwa hiyo, lazima Watanzania wote tuanze kuwa na *protein* na akili ziwe safi, ndiyo maana mimi napata tatizo kufikia kiwango cha kuwachukua watoto wote wanaoingia Sekondari. Napata watoto kila mwaka zaidi ya 2000 ambao wameshinda kwa kiwango cha juu kwa sababu ya samaki. Kwa hiyo, ruzuku ipelekwe, siyo kwa sababu tu ya kupeleka nje, lakini wavuvi waweze kuvua kiasi cha kutosheleza wananchi wa Tanzania waweze kula kiasi cha kutosha cha *protein* safi ambayo inatokana na samaki. *(Makofi)*

Lakini napenda tu kwa haraka niseme kwamba, wavuvi hawa hawalindwi, wavuvi hawa wamevamiwa *Lake Tanganyika* na wanavamiwa katika *Lake Victoria.* Kila siku Wilaya ya Ukerewe tuna matukio ya watu waliovamiwa na majambazi. Nahisi huu mtandao wa majambazi yanayoiba Benki, ndiyo hayo hayo! Kwa hiyo, Rais wetu kwa sababu ameshalivalia njuga na hili mumsaidie ili tuweze kufika mahali tujue mtandao. Mimi nina mashaka kama Serikali haijagundua mtandao wa majambazi yaliyopo ndani ya maji. Hawawezi kuwavamia wavuvi na kuwaua kila siku kama hawana mtandao!

Lingine ni kwamba, lazima kuwe na utaratibu wa uvuvi. Sisi sasa katika Wilaya ya Ukerewe ni kama shamba lisilo na mwenyewe. Anayejihisi tu kama anataka kuvua, anachukua nyavu anakwenda kuvua, anasahau kwamba Wilaya ya Ukerewe tuna kilomita 6000 za ardhi, maji ni mara kumi. Maji ndio shamba letu.

Kwa hiyo, Wizara iweke utaratibu wa kuwalinda wavuvi wa Mafia, Kojani, Ukerewe na huko kwingine katika maziwa ili wavuvi wapate haki ya kwanza kuweza

kutumia rasilimali iliyo karibu kwa sababu ndiyo njia pekee ya kujipatia kipato. Ukiwa na maji mara kumi ikiwa ndiyo Wilaya yako ndiyo mipaka yako, lazima kuwe na utaratibu siyo kila anayenyanyuka tu anakwenda kuvua katika shamba la mwenzie. Kwa maana hiyo, wavuvi wadogo wa asili waimarishwe, kuwe na mfuko na hilo nitahitaji maelezo kutoka kwa Waziri. Kuwe na mfuko utakaowekwa kwa ajili ya wavuvi, bila *condition* yoyote kama tunavyoweka mifuko mingine. Tunaweka mifuko na tunasema masharti yake ni haya, watu wanakwenda kukopa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ningependa kusema kwamba, Wizara hii ni ya muhimu sana na mwisho ningependa niseme kwamba, nitapenda Waziri aniambie hatima ya msitu wa Rubya katika Wilaya ya Ukerewe. Ikiwezekana, watu wanaohusika na misitu, wamekaa muda mrefu kwamba kimekuwa ni chanzo cha kupoteza rasilimali tuliyo nayo.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa kusema hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, atanielewa maana yangu. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kipekee kwa kunipa hii nafasi nami niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa vile ni mara yangu ya kwanza tangu Bunge hili limeanza Bajeti baada ya kutokuwepo kwa wiki mbili baada ya kuwa na ziara nje ya nchi kikazi, naomba nikushukuru kwa umakini wako kwa kutambua kwamba sijachangia.

Mhesimiwa Spika, awali ya yote, naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha wakati kama huu ambao tunazungumzia masuala muhimu na nyeti sana kwa Taifa letu la Tanzania. Ambacho ningeomba kutanguliza kusema mbele ya Wabunge wote na wananchi wa Tanzania, ni ule upendo wetu kwa Utaifa wetu kwa sababu kuna mengine tunasoma hata wakati ambapo hatujakuwepo au tunayaona humu ndani, kidogo yanaanza kuashiria hali ambayo siyo nzuri. Kwa hiyo, ningeomba Watanzania tuzidishe upendo ili tuweze kukaa pamoja na kutumia chochote kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote nizidi kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na timu nzima ya Serikali aliyoiunda ambayo inadhihirisha kabisa kwa matendo kwa falsafa ya Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya, kwani kwa muda huu mfupi tu mambo makubwa yameshaonekana na bado yanazidi kuonekana ambayo yanazidi kutupa sifa sisi sote. Pia, tunawapongeza sana Watendaji wote na timu nzima aliyoiunda. Vile vile natumia nafasi hii kuwapongeza Wajumbe na wanachama wa CCM wakati wa Mkutano Mkuu Maalum wa saba uliofanyika, kwa kuweka Uongozi mpya wa Chama Cha Mapinduzi, Chama kinachotawala. Ni Uongozi ambao unazidi kutia amani na kuzidi kuonyesha kwamba bado CCM itaendelea kutawala. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nije kwenye Wizara inayohusika na Bajeti ya leo. Nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na kutoa pole kwa taarifa tuliyoisikia ya msiba kwa Katibu Mkuu. Nawapongeze pia Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Nitakuwa sijatenda haki nisipowashukuru wale wananchi wa Hai hasa wale Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM walioniteua na hatimaye Halmashauri Kuu kuniidhinisha na wananchi wote kuja kunipigia kura na kuweza kuwepo hapa. Nawashukuru na kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Naomba nije kwenye hoja ya Wizara. Yangu mengi kwenye hii Wizara ni pongezi kwa kazi nzuri inayofanyika. Naipongeza sana Wizara kwa hatua ya kufuta vile vibali vya magogo, kwa sababu nchi ilikuwa imegeuka kuwa jangwa. Kwa kufuta vile vibali, nawapongeza sana na njia ya pekee kwamba, kule Wilayani kwangu Hai walikuwepo wavunaji wa misitu kutoka nchi jirani kwa muda wa dakika tano wanakuja na vyombo vya kisasa, mti umeshakatwa na kupakiliwa ndani ya magari. Lakini ile hatua ya kuzuia, imesaidia na ninazidi kuwapongeza sana na ninaomba tuzidi kuongeza jitihada ili kuzuia nchi yetu kuweza kugeuka kuwa jangwa. Pia, niipongeze Wizara kwa kuzuia kupeleka magogo nje ya nchi. Naomba tuzidi kuwa wakali ili nchi isije ikageuzwa kuwa jangwa. Naomba Wizara itusaidie sana kuhusu upande wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kuna hii biashara ya kupeleka wanyamapori nje. Labda uelewa, sifahamu lakini, nahofu kwamba tunavyozidi kupeleka wanyama wetu wa asili nje ya nchi, wale watalii baadaye watakuja kugomea huko huko wasije hapa nchini petu. Labda tuangalie utaratibu wa kuzuia hicho kitu.

Nikija upande wa wanyamapori, kuna bidhaa nyingi za wanyamapori ambazo kwa Taifa letu, wakati mwingine zinakuwa-*mis used* kumbe zina thamani kubwa sana. Ningeomba Wizara kwa kushirikiana na Idara zake kutoa elimu juu ya hizi nyara za Taifa ili iweze kueleweka vizuri kwa wananchi. Nikirudi kwa upande wa wanyama kwa upande wa Wilaya yangu ya Hai, niombe Wizara itusaidie. Kuna baadhi ya maeneo ya Masama Magharibi hasa Vijiji vya Lemira, tumbili wamekuwa ni wengi.

Mheshimiwa Spika, nilitoa taarifa kwa Afisa Misitu na Wanyama wa Wilaya, lakini ni kwamba ningeliomba Wizara nayo itusaidie. Wale wanyama wamekuwa ni wengi hata akina mama wakipika chakula wakiipua wanakuja wanachukua. Kutokana na ukame, wametoka kwenye mashamba makubwa ya kahawa wakahamia maeneo ya wananchi. Ningeomba Wizara itusaidie.

Mheshimiwa Spika, ningeomba pia nichangie kwa upande wa elimu ya utalii kwa Wizara yetu hii, kwamba, tuzidishe elimu ya utalii. Baadhi ya nchi nyingine ukienda, hata mwananchi wa kawaida kabisa ana taarifa za utalii uliopo ndani ya nchi yake. Naiomba Wizara iangalie ni jinsi gani ambavyo itaweza kutoa elimu kwa kupitia Chuo pamoja na vyombo vyetu vya habari kuwaelimisha wananchi juu ya utalii tulionao Tanzania ili kila mwananchi awe ni sehemu ya kuweza kuelezea utalii tulionao na kushawishi *Internal Tourism.* Sehemu nyingine, watu wanaotembelea maeneo yao kwa wingi zaidi ni wananchi wake yenyewe.

Pia, Tanzania ningeomba tuweze kufanya hilo na niipongeze Wizara, baadhi ya nchi chache nilizotembelea, utalii umekuwa ukitangazwa vizuri, ila ningeomba jitihada ziongezwe hata wenzetu wa *Tanzania Investment Centre* nao wamekuwa wakitangaza utalii wetu. Kwa hiyo, niipongeze Wizara pia iendelee kufanya hizo jitihada zaidi na nchi yetu izidi kufahamika nchi za nje. Niiombe Wizara pia kuibua maeneo mapya ya utalii. Kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Mama Mongella, pia, hayo maeneo mapya ya utalii yatazidi kuweka vivutio zaidi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Mama Mongella amezungumzia kule Ukerewe, lakini hata kule kwetu Hai kuna maeneo mengine mapya ya utalii bado hayajatangazwa vizuri. Kwa mfano, maeneo ya Rundugai kuna sehemu kabisa inaitwa Chemka. Kuna maji yanatoka ardhini mengi tu na yanachemka. Ni mfano mmojawapo, maeneo ya Masama kuna sehemu za Ngaseni huko kuna vitu vya asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara isaidie katika kuibua kwa watu binafsi pamoja na Wizara yenyewe ishiriki. Niipongeze Wizara kwa upande wa utalii kuzuia wale waongoza Watalii kutoka nchi za nje. Ile naipongeza Wizara sana, ilikuwa inanyima vijana wetu nafasi za kazi. Sasa kwa kuzuia, imetusaidia sana. Naiomba Wizara kwa njia ya pekee, kutoa mafunzo kwa ajili ya wale *guides* kwa mfano, ile *Machame Route,* tuna vijana wazuri, wako imara kabisa, wamejiandaa kwa ajili ya kuweza kuwaongoza watalii wapanda Mlima Kilimanjaro. Niiombe Wizara ishirikiane nasi tuweze kuwapatia vijana mafunzo ya kuweza kuongoza Watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yangu yamekuwa ni machache, lakini makubwa zaidi, naomba nizidi kuipongeza Wizara na kuipa moyo zaidi kwa kazi nzuri wanayoifanya. Bila kusahau, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Nazidi kumwomba Mwenyezi Mungu atujalie Taifa letu la Tanzania tuzidi kwenda vizuri, kwani hali ya uchumi inazidi kudhihirisha Tanzania ni nchi ya neema. Nawapongezeni sana na naunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie yangu machache ambayo yatakuwa manufaa kwa wananchi wetu. Kwanza nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi nami nichangie, lakini pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushika nafasi zote muhimu kuongoza Chama na kuongoza Serikali. Mgombea mwenza wake Mheshimiwa Makamu, Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu kuteuliwa na kupata baraka zetu ili naye kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa naye katika shughuli zetu za Serikali na ndani ya Bunge. Pia nawapongeza Wapigakura wangu wa Jang'ombe ambao wamenionyesha imani yao ya kunichagua kwa kipindi cha pili hiki ili niwaongoze na mimi nawaahidi kwamba nathamini juhudi zao na imani yao kwangu na mimi nitawatumikia kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Spika, suala la utalii ni suala nyeti kabisa. Ukweli, tunapaswa kuziangalia sehemu zote za utalii. Tukubali kama alivyozungumza Mheshimiwa Mongella, Mwenyezi Mungu ametujalia na kutupa baraka nyingi ili tuwe na sehemu

nyingi za utalii, kwa sababu ukizungumza katika Tanzania, unakuta tuna fukwe nzuri, tuna magofu ya historia na mambo mengi. Lakini bado tumemwachia Mwenyezi Mungu atusaidie bila ya jitihada zetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu elimu ikatolewa kwa wakazi wa karibu na bahari ili kuzitunza fukwe zetu ziwe vivutio zaidi. Katika ziara nyingi za Kamati ambazo tumefanya, nikiwemo mmoja katika Kamati ya Maliasili na Mazingira, ukweli tumejionea wenyewe uchafuzi wa mazingira lakini naamini elimu ikitolewa, basi hayo yataondoka. Napenda niipongeze Serikali kwa jitihada zake za kuzuia uvunaji wa magogo katika nchi hii. Uvunaji ulikuwa wa kasi kubwa sana kuliko upandaji. Kwa hiyo, nakubaliana na wenzangu kwamba matokeo yake ingefika wakati cha kukivuna hatuna. Sasa naipongeza Serikali kwa kuzuia uvunaji, lakini twende mbele na kurudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kati ya 2004 na 2005 tulizungumzia sana hapa suala la magogo ya wazalendo ambao yameshakatwa na yapo kwenye vitalu, yako kwenye ma-*godown* na mengine yalikuwepo mpaka Bandarini. Tukubali kwamba Serikali ilifanya makosa na kosa tulilolifanya wavunaji wengi au baadhi yao walikuwa ni wavunaji wa kutoka nchi za nje ambao hawastahiki kuvuna, wao wanastahiki kusafirisha thamani siyo kuvuna magogo. Kama sitakosea, tulipokwenda Kilwa tulikuta katika kiwanda cha Machina wanakata magogo ambayo kazi hiyo ingekuwa ifanywe na Wazalendo wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sasa masuala ya kibali kwa sababu hawakujipeleka tu, lakini walipata vibali na kila kitu na wakaweza kufanya kazi hizo, ninaiomba sana Wizara iwafirikie Wazalendo waliokuwa na magogo katika kipindi cha nyuma, sio wakataji wapya. Nakubaliana sana na Serikali kuzuia uvunaji, lakini tuwafikirie wale ambao walitafuta tenda na wakapata wakaenda Benki, wakachukua mikopo wakakata magogo ya miaka 2004-2005 matokeo yake wameshindwa kusafirisha na magogo hayo yapo mpaka hivi leo. Sasa Wazalendo hawa, ukweli tunawaweka katika hali ngumu.

Mheshimiwa Spika, nakiri mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba sisi Wabunge wako tunaomba angalau tumalize miaka mitano, tusife kwa mikopo ya Benki. Sembuse hawa Wazalendo ambao wamekopa, magogo yako chini karibu miaka mitatu, wanashindwa kufanya lolote! Ninaiomba sana Serikali ifikirie suala hilo ili kuwaokoa na malipo pamoja na faida ambayo wanatakiwa walipe katika Mabenki.

Mhesihmiwa Spika, naipongeza pia Wizara katika hotuba yake, imeona tatizo la udhaifu wa mbegu za miti na sasa wamechukua mkakati rasmi wa kuweza kuwapatia wananchi mbegu za miti bora. Kwa hiyo, naamini tukiwapa shinikizo, wananchi wanaweza wakapanda miti bora na tukapata mavuno bora hapo itakapokuwa tayari kuvunwa. Tunahitaji vijana wetu wapate elimu ili waweze kufanya kazi katika nchi hii. Lakini katika kuwapatia kazi hasa wale Watafiti wa Wanyamapori, ukweli ni kwamba mazingira ya Watafiti wa Wanyamapori yako katika hali mbaya sana. Baadhi ya sehemu ambazo tumetembelea tumekuta wengine wameondoka katika sehemu zao za kazi

kutokana na mazingira mabaya. Sasa mazingira mabaya hayo yako katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza ni ya utendaji yanafanya mazingira yashindwe kufanya kazi zake.

Lakini ya pili, tunapozungumzia, tunakwenda kuwafanyia utafiti wanyamapori. Nafikiri ni suala la kuangalia sana. Linategemea pia mazingira yawe mazuri ili yakapambane na wanyamapori, sio kwa kupigana, lakini kuwa karibu nao ili wawe marafiki wasiweze kudhuriana. Vinginevyo, kazi hiyo inakuwa ngumu sana kwa sababu hata mimi leo ukiniambia niende Morogoro kwa miguu, basi kazi hiyo itakuwa ngumu sana. Lakini utakaponipa gari, utakuwa umenipunguzia ule ugumu wa ile kazi. Waziri wa Elimu anahimiza vijana wasome na vijana wanajitahidi kusoma, tupate wataalam, *alhamdulillah* tunapata wataalam, lakini tuongeze nguvu kuwatunza wataalam wetu hasa wale wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo tunaweza kuwatunza na wakabakia hapa hapa nchini tukaweza kuwatumia kwa shughuli zetu zote za kujenga Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi watu tunaotoka katika Visiwa, tuko karibu sana na wavuvi. Ukweli, hali ya wavuvi wetu siyo nzuri na kinachongia zaidi hali isiwe nzuri pale Zanzibar ni kwamba, siku wavuvi watakapokwenda baharini, wakapata vibua, kila boti inayokuja imejaza vibua, basi ndoo Sh.200/= lakini siku wanayokuja na vibua watatu, ndoo Sh.5,000/=. Sasa tuangalie na hii yote inatokana na kutokuwajali wavuvi wetu. Tunasema mtu anapofanya kazi, anategemea kama ni shamba atoe mazao mengi zaidi hapendelei apate gunia moja kwa hekta moja, anapendelea apate hekta tano au sita kwa hekta moja. Lakini wavuvi wetu, wanaona bora wakapate samaki mmoja atapata pesa kuliko akienda akapata samaki wengi ndipo watakapokosa pesa. Hii inatokana na ulazima kwamba atake asitake auze. Kama hawakununuliwa, atawafanya nini? Lakini kama ingelikuwa tuna viwanda vya kusindika, basi tungewasaidia, lakini pia ni vizuri kuwatafutia vyombo ili waweze kuuza kwa hali ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, ulitwambia hapa kwamba sasa tunaanza na Bunge la kisasa. Kweli tunaona mabadiliko ya Bunge la kisasa, kasi na *speed* inakwenda vizuri. Sasa na hawa wavuvi naomba Wizara iwasaidie ili waweze kuvua kama wanavyoweza na wao kuvua.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, kwa kuwa kengele ya pili iko njiani kugongwa, naomba nikushukuru wewe binafsi, niishukuru Wizara pamoja na mikakati yote ambayo wanategemea kuifanya mwaka 2006/2007 na Mungu naamini atakuwa nasi katika kufanikisha hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, natamka kwamba naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji anayefuata, nimeombwa nitaje orodha nzima, itasaidia wale wanaojiandaa pengine kusafiri ama vipi, wajijue. Sasa mpangilio wa wachangiaji sasa baada ya Mheshimiwa Mohamed Soud kumaliza, Msemaji atakayefuata sasa ni Mheshimiwa Savelina Mwijage, halafu

Mheshimiwa Abdul Karimu Shah, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Suleiman Saddiq na tukibahatisha labda Mheshimwa Luhaga Mpina. Labda kama ninaowataja humu watakuwa hawapo ndio tutaendelea Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, sidhani kama tutamfikia Mheshimiwa Lwanji, pengine! Lakini hiyo ndio orodha. Nimeona vikaratasi vinakuja vinaulizia kama mtu fulani yumo, basi utaratibu ni huo.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika hotuba hii ya Maliasili. Pia, ninakushukuru kwa kuweza kunikumbuka, kwamba na mimi ni mmoja ambaye sijachangia katika awamu hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kukishukuru Chama changu kwa kunichagua pia kuwa mmoja wa Wabunge ambao wameteuliwa kufika hapa Bungeni na ninawashukuru wananchi wa Kilwa wa Chama changu kwa kunipendekeza kufika katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo yangu ni madogo tu. Kwanza ni kero za wananchi wa Kilwa wanazozipata kutokana na hii maliasili na utalii, hasa uongozi wao kama Maafisa Maliasili waliopo pale. Kihistoria, Kilwa sio maskini, japokuwa kwa sasa hivi katika takwimu Kilwa ni maskini. Kilwa sio maskini kwa maana ya kwamba, sisi tumezungukwa na bahari katika maeneo yote ya Kilwa kasoro sehemu chache tu. Pia, tumezungukwa na misitu ambayo pia ni utajiri mkubwa kwa hapa kwetu Tanzania. Vilevile, tuna vivutio vingi vya utalii kama vile magofu ya Songo Songo, Kilwa Kisiwani na sehemu nyingine ambazo zinazunguka pale Kilwa.

Lakini pamoja na hivi vyote tulivyonavyo, Kilwa bado Kilwa ni maskini wa kutupwa. Sasa naanza na maliasili bahari. Kutokana na kuzungukwa kwetu na bahari, wananchi wa Kilwa wanategemea hii bahari na ndio ajira ya vijana wa Kilwa, ndio ajira ya wananchi wote wa Kilwa. Ukiweka kilimo, ni sehemu ndogo kwa sababu maeneo mengi sio ya kilimo. Lakini hii bahari tulikuwanayo, wananchi wa Kilwa wanashindwa kuitumia kwa masharti kadhaa. Kwa mfano kwa umaskini walionao, wana nyavu ambazo wanazitumia ambazo hazistahili. Kwa hiyo, mara nyingi wakizitumia hizi nyavu hunyang’wanywa na Maafisa wa Waliasili. Lakini hapo hapo pamoja na kunyang’anywa hizo nyavu ambazo hazitakiwi, katika Wilaya ya Kilwa kuna meli kadhaa ambazo zinakuja zinavua pale kwa uvuvi huo kwa aina isiyotakiwa na wanaangaliwa na Maafisa hawa wa Maliasili, kwa kudai kwamba hawana usafiri wa kuweza kuvikamata hivi vyombo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna wananchi ambao wamenyang’anywa hizi nyavu ambazo wao wanazitegemea na hiki ni kipindi cha watoto wao kwenda Shule, wapate uvuvi, wapate pesa za kuwapelekea watoto Shule, wanashindwa kuwapeleka kwa sababu ya hali halisi ya umaskini na pesa wanapata hutokana na kazi ya uvuvi.

Naomba Wizara ichukue hatua katika eneo hili kuwarudishia nyavu zao wananchi wa Kilwa ambao wamenyang'anywa. Hivi ninavyozungumza, ziko meli tatu katika Wilaya ya Kilwa zinavua, kwa namba naweza kuzitaja hapa, kuna XIL 741 yenye jina la Mtoni, kuna meli nyingine inaitwa XE ina namba XLXA IL 722 inaitwa Aluwali, kuna na meli nyingine inaitwa Faraja, yenye namba XIL 868, iko hapo katika maeneo, inavua katika ukingo ambao wananchi wanavua na uvivu wao unaonyesha ni wa haramu, kwa sababu samaki wakubwa wanawachukua na wadogo wanawamwaga kwenye ufukwe na wanazagaa, wananchi wanawaona.

Je, hawa watu wanastahili kufanya hivyo vitu, wakati wananchi wa Kilwa wananyang'anywa nyavu zao kwamba wanavua uvuvi wa haramu? Naomba Wizara ikaangalie, hivi sasa labda wataondoka kwa vile mimi nazungumza hapa. Lakini mpaka asubuhi ya leo, hao watu wako pale na hizo meli zao. Naomba Wizara iliangalie hili. *(Makofi)*

Halafu pia nitazungumzia kwenye sehemu ya utalii. Kama nilivyoeleza, sisi tuna maeneo mengi ya utalii Kilwa, tuna mapango Kipatimu, tuna magofu na vilevile tuna wanyama wa kutosha katika maeneo mengi. Katika sehemu hii ya utalii kuna sehemu za wanyama zenye vitalu. Sasa nazungumzia vitalu.

Mheshimiwa Spika, vitalu vimegawiwa kwa nia njema kwa wawekezaji, lakini hawa wawekezaji wanawanyanyasa hawa wananchi wa Kilwa. Kwanza, wananchi wa Kilwa hawajui faida ya hivi vitu. Kama wangekuwa wanaijua faida, Kilwa isingekuwa maskini hadi hii leo. Hawa watu wamepewa haya maeneo na wanafanya shughuli zao, wanauza wanyama, watu wanakuja wanawinda pale kwa pesa nyingi, lakini wananchi wa Kilwa hawafaidiki na kitu chochote katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, linalonisikitisha zaidi, mtu akikutwa hata na nyama ya Sungura kipande kidogo tu, basi kisago atakachokipata utaomba dunia ufunuke. Lakini hao hao wanakuja na ndege zao katika misitu ile hatujui wanaingia kuchukua nini! Wanatoka wakiwa wamechukua nini katika misitu ile? Naomba Serikali itufahamishe, hizi ndege zinakwenda kwa ulinzi gani? Zikienda pale, nani anawaangalia wakiingia pale wanachukua nini na wanatoka na nini? Wakati mwananchi wa Kilwa akikutwa na kipande cha nyama, anatapa adhabu ya kipindukia. *(Makofi)*

Kitu kingine pia ninachotaka kuzungumzia katika maeneo haya ya misitu, Maafisa Misitu wamekuwa na tabia; kwanza, napenda kupongeza kwamba, katika eneo hili Waziri wa Maliasili, kwa kuruhusu wananchi ambao walikuwa wamewekeza pesa zao kwenye mbao, baada ya kuzuia msitu na kuweka sheria kuwaruhusu watoe yale mazao yao ambayo walikuwa wamevuna, kwa maana ya kwamba sasa hivi wanaweza kurudisha mikopo katika Benki, ambayo walikuwa wamekopa, kwa kipindi kile ilikuwa ni masikitiko kwamba hawa watu walikopa na wamezuiliwa mazao yao misituni. Waliweka watu kuwavunia, wanadai pesa zao, lakini walikuwa wanashindwa jinsi gani watawalipa wale watu, jinsi gani watarudisha mikopo Benki, jinsi gani wataweza kujikimu wao wenyewe. Kwa hiyo, namshukuru Waziri wa Maliasili kwa hiki kitendo na

ninategemea kwamba, hata wale Watanzania waliokuwa na mazao kama magogo itakuwa hali kadhalika kama Mheshimiwa Waziri alivyoamua sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo hayo hayo, Maafisa Maliasili wa Kilwa wamekuwa wakinyanyasa wananchi. Kipindi hicho cha kuzuia mbao zisitoke nje, walikuwa wanazunguka katika maeneo yanayovunwa mbao  na kuwakamata wananchi ambao mwingine unamkuta anaishi katika eneo lile ni Fundi Seremala ,ana mbao mbili, ana mbao tatu anamnyang'anya, anamkuta ana mbao moja anamnyang'anya, anakuta wengine labda wamevuna bila ya ridhaa ya Serikali wanamnyang'anya. Lakini je, hizi mbao zinapelekwa wapi?  Hizi mbao zilikuwa hazijulikani wapi zinapelekwa, ni chache tu ambazo zilikuwa zinaweza kufika katika Halmashauri ya Wilaya na zikaonekana, nyingine zilikuwa zinaishia huko njiani kwa kugawana wao wenyewe. Fikiria unamnyang'anya mtu ubao wake mmoja wakati wewe unasomba mbao kibao zisizo na uhalali, hii ni tabia gani? Naomba hili lirekebishwe katika Wilaya ya Kilwa.  Wananchi wananyanyasika kwa Mkoa mzima wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua wajibu wananchi katika maendeleo ya misitu pamoja na maliasili tulizonazo.  Kama ni hivyo, tunafahamu, basi mimi ninaomba kwa Bunge zima, kila mwananchi na kila Mbunge tuweke utaratibu wa kuzuia vitu vinavyotumika na wananchi pale kwa mfano mwananchi alikuwa amezoea kuvuna kwenye ile misitu kwenda kuwinda wanyama. Lakini unavyowekeza vitalu vyote kuwapa wananchi, mwananchi anabaki  hana mahali pa kuzungukia angalau apate hata yale mahitaji aliyozoea kuyapata katika misitu ile, bila ya kumpa eneo mbadala kwamba sasa hivi hiki kitalu tumekiweka hapa, tumewapa wananchi hawa na wawekezaji hawa. Ninyi mtakuwa mnatumia maeneo haya, kwa kweli mtakuwa hamtendi jambo la busara, kwa sababu wananchi wataendelea kuteseka wataingia humo humo kwa sababu hawajawekea kitu mbadala cha kukitumia badala ya ile misitu yao ambayo wamezoea kuitumia.

Sasa naliomba Bunge zima kwamba ili kuhifadhi misitu, naomba kila mmoja katika eneo lake, tuweke kama utamaduni anapozaliwa mtoto, basi kila mmoja apande mti pale kama ni nyumbani kwake mtoto amezaliwa, basi apande mti.  Kama ni jirani, basi mshauri anapozaliwa mtoto wake apande mti, ili tuweze kupata hiyo miti.  Vilevile, naishauri Serikali kwamba kuna nchi nyingine zimeweka mbadala kwamba msitu huu utumike, msitu huu tunauhifadhi, msitu huu ukishaendelea kukua unatumika mwingine tena, kwa hiyo, kuwepo na ile *rotation* ya kubadilisha kwamba hapa pakitumika mwaka huu, mwaka ujao utatumika msitu wa sehemu fulani ili kuweza kuhifadhi mazingira badala ya kukata miti yote kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsanteni.  Nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii.  Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, lakini nitakuomba radhi kwamba kwa kweli tangu nimekuja Bungeni, sauti yangu ni mbaya sana, inakwaruza na ndio maana nimekuwa nikichangia kwa maandishi. Lakini kwa kuwa Jimbo langu la Uchaguzi la Ngorongoro ndio kabisa liko ndani ya Wizara hii, kwa

kweli uzalendo umenishinda na ndio maana nimeona nijaribu kuzungumza hata kwa hali ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, nimpongeze Naibu Waziri, nimpongeze Katibu Mkuu na kumpa pole kwa matatizo yote yaliyompata ya kufiwa na baba yake mzazi. Pia, niwapongeze wataalam wote wa Makao Mkuu wa Wizara, Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara na Vitengo mbalimbali kwa kazi nzuri waliyoifanya hadi kufikisha Bajeti hii katika Bunge hili, mwaka huu wa fedha 2006/2007. *(Makofi)*

Napenda pia nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Ngorongoro kwa kuniwezesha kuja katika Bunge hili na wala sikupata misukosuko mikubwa, ni baada tu ya kura za maoni wakaona hakuna sababu ya Mbunge wao kupata misukosuko mikubwa hiyo wakanipitisha bila kupingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye Sekta ya Utalii. Wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, ya tarehe 30 Desemba, 2005, katika kitabu cha hotuba yake ukurasa 47 Mheshimiwa Rais alisema, "Utalii ni mhimili wa uchumi wa nchi yetu hivi sasa." Nami nataka nikubaliane naye, kwa sababu tumepata takwimu ya jinsi ambavyo utalii unaliingizia Taifa pesa nyingi za kigeni na hivyo kusaidia miradi mbalimbali ya wananchi na hivyo kuondoa umaskini miongoni mwa wananchi wetu.

Katika Jimbo langu la Uchaguzi peke yake, kuna vivutio vingi sana ambavyo kwa kweli vingetumika vizuri nisingekuwa na sababu ya kulalamikia umaskini katika Jimbo la Ngorongoro. Kwanza, tuna *creator* ya Ngorongoro ambayo imezoeleka sana duniani na napenda niwakaribishe Wabunge wote kutembelea huko kusaidia kuhamasisha utalii wa ndani. Hii ambayo tunatangaza sana ni utalii. Watalii wa nje ndio wanakuja kutembelea nchi yetu, lakini Watanzania wazalendo, raia wa kwetu, hawajazuiwa kabisa kuja huko Ngorongoro na maeneo mengine kutembelea maeneo hayo. Kwa hiyo *Crater* ya Ngorongoro kuna ya Mbakai *Crater*, nafurahi kusema kwamba katika *speech* ya Mheshimiwa Waziri, alisema *Mbakai Crater* sasa itaendelezwa vizuri ili iweze kutumika kama *Crater* ya Ngorongoro inavyotumika zaidi. Nawaambia kwamba, hii *Crater* ya Mbakai ni nzuri zaidi hata kushinda ile *Crater* ya Ngorongoro. Lakini kwa sababu miundombinu sio nzuri, barabara haziendi huko, hakuna huduma za kitalii, basi wageni hawaendi. Lakini kwa kweli ni kivutio kikubwa sana. Nashukuru kwamba, imetamkwa kwenye hotuba ya Waziri, pengine mambo yanaweza yakawa mazuri zaidi. Kule vilevile tunayo *Olduvai Gorge,* mahali ambapo mifupa ya binadamu wa kale ilipatikana karibu miaka milioni tatu mpaka nne iliyopita. Kule tunayo *lately foot print*, tuna *shifting sand, mount Liangai* ambayo ni maarufu kwa mambo ya *Volcano*, Serengeti na *Salei plains*, *Lake Natron* kwa ajili ya *flamingo, Rift Valley*, *Ngaresoli Water Falls, Northern Highland Forest Reserve* na tuna Seleloki. Kwa kweli maeneo yote haya ni vivutio vikubwa kwa watalii. Kama tungeweza kutangaza maeneo haya vizuri watalii wengi wangeweza kwenda huko na hivyo kutuletea fedha kigeni za kusaidia kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Ngorongoro, zaidi ya asilimia 80 ama ni hifadhi, kwa maana ya hifadhi ya Ngorongoro, ama ni *Game Controlled Area* na humo ndani kuna *Hutting Blocks*. Ndani humo humo kuna *Wildlife Management Aries* na nafurahi kusema kwamba, katika hotuba ya Waziri imetajwa. Ni maeneo vilevile ambayo kwa kweli tungeweza kushirikiana vizuri na hao watu na kuna Kampuni mbalimbali za kitalii, yako kwenye maeneo haya, tungeweza kushirikiana nao tungeweza kupata ajira kubwa kwa ajili ya vijana wetu wa Wilaya ya Ngorongoro na hata wa maeneo mengine.

Napenda niitumie nafasi hii niwashukuru watu wa *Otterbein Business Cooperation (OBC)* katika Vijiji vinane ambavyo mradi huu umezunguka, wamechukua vijana watano watano kutoka katika kila Kijiji na kufanya vijana 40, 30 kupata ajira kwa ajili ya hii tu pekee yake. Ningetoa wito kwa Makampuni mengine kwamba, wafanye hivyo ili kusaidia kuondoa umaskini na kuwapa vijana wetu ajira na hiyo pia itamsaidia Mheshimiwa Rais hata zile ajira milioni moja ndani ya miaka mitano iliyotajwa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi, hali hii pia ingeweza kusaidia kuleta ajira hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna hoteli moja iko karibu na Seronera huko, inaitwa *Nduttu Lodge,* hoteli ile pia nzuri, lakini sielewi ni kwanini hawaajiri wanawake, hata kidogo! Sijui ni hiari ya mwekezaji huyo au ni mwongozo wa Wizara, lakini hawaajiri jinsia ya kike, ni wanaume tu wako kule. Labda inawezekana kwa kuwa ipo porini, ndani sana, lakini hata huko hivi utakwenda wapi bila mwanamke? Kama ni maporini, wanawake wapo, wanaume wapo, sioni sababu kwanini hoteli ile isiwaajiri akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye uhusiano wa wanyama pori na mifugo, wanyama hawa wanategemeana sana, kwanza ni marafiki, na ndio maana mifugo yetu inakaa na wanyamapori, wanalisha pamoja, ukiondoa wanyama wakali wale wanaokula nyama kama simba na chui na ndio maana vijana wako mahiri kulinda mifugo yao, kama ambavyo na nyie mnalinda mali zenu. Lakini hatuna ugomvi nao, hata hao simba wakikorofisha, zamani ndio vijana walikuwa wanataka kupima ujasiri wao. Lakini hiyo hali sasa haipo, tunaishi kwa amani na tunaishi kwa kutegemeana. Chakula cha wanyama hao wawili, mifugo na wanyamapori ukiondoa wanyama wakali, ni majani mimea na matawi. Wanahitaji pia maeneo makubwa ya kulishia, pia kupata chumvi na majani na kunywea maji na kuzaliana, wanahitaji maeneo makubwa na ndio maana wakati Wamasai wanaondolewa kule Meru na Seronera ili kupisha hifadhi ya Serengeti ambayo mpaka leo tunanufaika nayo wote, ni jambo nzuri limefanyika.

Mheshimiwa Spika, Wakoloni walifanya mambo mawili mazuri. Kwanza, walifanya *negotiation* kwa zaidi ya miaka 13 na Viongozi wa Kimasai ili wakubali kwa hiari yao bila kusukumwa kuondoka katika maeneo yale na kwenda kwenye Ngorongoro *Highland*. Hicho ni kitu kizuri na ningeomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano nayo iwe inafanya hivyo. Kama kuna maeneo ambayo Serikali inataka kwa matumizi yake, kwa manufaa ya wengi, ifanye kwanza *negotiation,* ifanye makubaliano, wafikie muafaka na watu ambao wamewahi kukaa kule, kuliko tu pengine kutoa matamko na kusema ondokeni siku inayofuata. *(Makofi)*

Lakini jambo la pili walilofanya wale, walitekeleza masharti waliyopewa na Wamasai wale, kwamba, hatuondoki hapa mpaka mnapotupeleka muweke miundombinu tunayohitaji. Wekeni *vetinary centres*, wekeni mabwawa, wekeni majosho na mtutafutie madawa ya mifugo na yote hayo wameyafanya na wenyewe Wamasai kupitia Viongozi wao wakaenda kukagua wakaridhika na ndipo wakakubali kuhama.

Mheshimiwa Spika, katika uhusiano huu wa mifugo na wanyamapori, watu wanaoitwa Wahifadhi wa siku hizi, maana Wamasai hawa ni wafugaji kwa ujumla. Wamekuwa ni wahifadhi wa wanyamapori kwa miaka nenda kwa miaka rudi, lakini mtu anayeona hii hali, badala yake *they so called conservators, new consevators*, waliohitimu kwenye Vyuo, naona wanakuja wanaweka mtengano mkubwa kati ya mifugo na wanyamapori. Wanyama hawa nimesema wanategemeana.

Kwanza mifugo usalama wao utokana na wanyama wakali. Ni wanyamapori wenzao, lakini wale wanaokula majani. Kwa sababu wanyama wakali kama simba wanajua kabisa mifugo inalindwa na kwa hiyo hawendi tu akavamia mfugo hivi hivi. Anajua na yeye anaweza akapata shida, lakini ataishia sasa kuwatafuna wale wenzake, wanyamapori wanaokula majani, lakini hawana ugomvi. Asubuhi tunatoa ng'ombe kwenye mazizi, tunakuja kwenye malisho, tunakutana asubuhi tunalisha kwenye maji, majani, lakini jioni sisi tunakwenda nyumbani na mifugo yetu na hao wanabaki porini tunakutana tena kesho asubuhi. Ni mahusiano mazuri sana. Mimi nataka Wizara hii iendelee kuona uhusiano huo na isiendelee kutenga mifugo na wanyama pori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, kuna mikakati mingi mizuri zaidi na kabambe ya kuendeleza wanyamapori na sio kuendeleza jamii zinazozunguka maeneo hayo ambayo wanyamapori wapo. Sasa hii nayo sio nzuri. Jambo lingine nimesema kwamba kama Serikali inakuwa na mkakati wa eneo fulani, lazima kwa kweli ijaribu kufanya mawasiliano na wahusika ili wafikie muafaka kwa njia ya amani tu kwa kuwa nchi yetu ni ya amani, waweze kuchukua eneo hilo kwa amani. Mwaka 1975, kabla ya mwaka 1975 Wamasai walikuwa wanaishi katika *Crater* ya Ngorongoro, kule shimoni kabisa kule chini na wakati huo faru walikuwa zaidi ya 200 kwenye *Crater* ile ndogo. Ni kilometa za mraba kama 250. Eneo dogo, lakini lina kila aina ya mnyama. Sasa walikuwa wanaishi mle, lakini nadhani Serikali imefika mahali labda ni kwa nia njema, itaona kwamba eneo lile kwa kuwa ni dogo na mifugo yetu inazidi kuongezeka, wakasema watu hawa waondoke ndani ya *Creator*, waje huku juu kwenye *rim* ya *Crater.*

Sasa baada ya *negotiation* ya maelewano kufanyika, wakaleata Jeshi, watu wakaondolewa, maboma yale yakachomwa moto. Sasa hiyo sio vizuri na ndio maana hata hawa walioondolewa sehemu za Usangu, mimi nakubaliana, waondoke kwa sababu ni maeneo ya vyanzo vya maji, maeneo ambayo yana-*generate* umeme kwa ajili ya nchi ambayo inanufaisha watu wengi zaidi.

Lakini nafikiri, kwa kuwa sasa limekuja tatizo la ukame kwa kasi, nafikiri Serikali haikupata nafasi ya kuendelea kufanya *negotiation,* lakini hilo liwe sasa ni fundisho kwa wakati ujao. Tuweke malengo mazuri tu ya mwaka ujao, tuweke malengo mazuri tu ya muda mrefu, kuliko kuwaswaga watu. Sasa tatizo wa Wamasai wale, wameondoka,

wamekuja *rim* ya *Crater* lakini sasa hivi naambiwa kwamba, mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro inaweka kitu kinaitwa *zones* kwenye eneo. Kwa hiyo, kuna *zone* moja inaitwa *zone* ya *Crater*. Sasa nina hakika tena watasema ondokeni hapa kwenye *rim* ya *Crater*, nendeni *so many kilometres*.

Mheshimiwa Spika, nafikiri hawa Wamasai watakuwa wanahama, mwisho mtajikuta mnawarudisha Serengeti kama ambavyo mliwahi kuwatoa. Ni kuhamahama! Mimi hili naomba Wizara iangalie suala hili na kama kuna haja ya namna hiyo, basi ifanyike kwa makini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, mnawatoa watu hawa hapa lakini mnaendelea kujenga hoteli kubwa za kitalii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kwa kuniona na kwa kuwa sijawahi kuchangia kwa ajili ya matatizo yaliyonipata. Niliondoka nikaenda nyumbani.

Kwanza nakishukuru Chama cha Wananchi *(CUF)* kwa kunifikisha katika Bunge hili la Jamhuri la Muungano wa Tanzania. Nawashukuru walionipa kura za maoni, watu wa Bukoba Mjini.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wote waliotangulia kutoa hoja zote na Bajeti zao, nawashukuru sana. Mimi hoja yangu ya kwanza ninayoisemea ni wavuvi wadogo wadogo. Naona Serikali inawasahau hao wavuvi, wanapata matatizo makubwa hasa katika Ziwa Victoria. Wavuvi wanaweka nyavu zao wanasema zimekatwa, lakini nasikitika sana hizo nyavu unazikuta wanaziuza madukani na wavuvi wananunua mle wanapeleka ziwani. Wakishapeleka ziwani, wanakamatwa wanachomewa moto nyavu zao. Kwa masikitiko makubwa, naiomba Serikali, kama nyavu zimezuiliwa, Serikali ingefanya mikakati ya kuzuia hicho kiwanda kinachotengeneza nyavu haramu.

Mheshimiwa Spika, maliasili wakishakwenda pale Mwaloni, wakiwakuta wameshavua samaki zao, badala ya kuwakamata kuwapeleka Mahakamani, wanachukua zile samaki, wanamwagia mafuta ya taa na kuchoma moto. Sasa ninachoomba kuuliza kwa Wizara hii ya Maliasili, wana mikakati gani na hawa wavuvi ambao wako karibu na hilo ziwa?

Mheshimiwa Spika, lingine la kusikitika hasa, Kanda ya Ziwa hii kama Mama Mongella alivyosema, kutoka Ukerewe na Bukoba ni karibu sana. Yanayotokea Ukerewe ndiyo yale yale yanayotokea hata Bukoba na Mwanza. Nilikuwa nashauri na kuomba Wizara waweze kusaidia hawa wavuvi wadogo angalau zile nyavu zinazoruhusiwa kuuzwa madukani na kuweza kufanya kazi kwenye ziwa, ndio zitolewe madukani zisiuzwe kuliko kuwauzia wavuvi ambao hawazifanyii kazi na wanakamatwa, wanapigwa na wengine wanauwawa. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni la maliasili. Mkoa wa Kagera una misitu mingi sana. Una msitu wa Biharamulo, Kimisi, Msitu Mnene! Misitu hiyo imekuwa maficho ya majambazi. Serikali ina mikakati gani na misitu hiyo ya Kagera? Kulikuwa na vituo vya maliasili hasa Biharamulo, Kambi hiyo imeshavunjwa na majambazi wanajificha mle. Naomba Wizara ya Maliasili iangalie Mkoa huo kutokana na misitu hiyo. Kama kuna uwezekano, wangejenga Kambi hizo ili wawe wanaangalia misitu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kimisi ni sehemu nzuri sana, hata wakijenga sehemu ya utalii kwa ajili ya kutuletea uchumi katika nchi yetu. Naomba Mheshimiwa Waziri apaangalie. Katika Bajeti zote zinazosomwa au katika mikakati yote inayofanywa, wavuvi hawamo na hayo mapori hayamo. Naomba kuuliza, hii Wizara ina mikakati gani na Mkoa wa Kagera?

Mheshimiwa Spika, nimesikia wanaoongelea meli. Wavuvi wadogo wadogo watapata wapi meli za kuvulia samaki? Sana sana maongezi yangu yalikuwa ni ya wavuvi ili kuangalia tuwafanyeje, Serikali iwawekee mikakati ya kuwasaidia na kuhusu misitu ya Burigi, Kimisi na Msitu Mnene na Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo ya wavuvi, yananiuma sana kwa sababu ukishakwenda pale Mwaloni unasikitika sana wanavyopigwa, hawapelekwi hata Mahakamani. Wangekuwa wanawapeleka Mahakamani, sawa, sheria ingechukua mkondo wake. Hatukatai kusema kwamba nyavu sio haramu, ni haramu tunakubaliana nao, lakini ombi langu ni kuweka mikakati ya kutuletea nyavu zinazokubalika katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, wavuvi ni maskini, hawana uwezo. Sana sana wenyewe ukienda pale hasa kuanzia Muleba mpaka Bukoba Mjini, wanasema mnatuthamini kipindi mnatafuta kura. Mkishapata kura hamtukumbuki.

Kwa hiyo, nasimama na Wabunge wa Mkoa wa Kagera tushirikiane kwa pamoja na Wizara ya Maliasili wafike waweze kutusaidia kwa sababu katika maongezi yao sisikii wakisema chochote. Naomba watusaidie kuimarisha wavuvi wadogo wadogo ambao hawana uwezo wa kuwa na meli za kuvulia.

Mheshimiwa Spika, mengi sina, naomba Wizara hii isikilize kilio chetu sisi Wabunge wa Kagera na watusaidie. Nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema pamoja na wewe na Waheshimiwa Wabunge wote. Pia, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mawili, matatu katika Wizara hii adhimu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa Idara na Taasisi zilizokuwa chini ya Wizara bila kusahau Mameneja wa Vitengo kama vile hifadhi ya Bahari na vitengo vingine na watumishi wote wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii ambao ndio wanaofanikisha hayo

yote yanayoleta sifa katika Wizara hii ambayo nafikiri makusanyo makubwa yanatoka katika Wizara hii kutokana na vivutio vyake.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Hilda Ngoye kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mazingira la Taifa *(NEMC)*.

Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuliona hili, kwa kuteuliwa Mwenyekiti ndani ya Ukumbi huu ili iwe rahisi kumwona na kumweleza wapi panaathirika na yeye akiwa kama Mheshimiwa mwenzetu inakuwa rahisi zaidi kupeana mawazo na maoni kwa ajili ya usalama wa Taifa letu hili kuhusu suala zima la mazingira. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Mafia. Asilimia karibu 80 ya wananchi wa Mafia wanategemea uvuvi. Kwa mara ya kwanza kabisa baada ya malalamiko mengi, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri au Wizara kwa kutuletea miradi ambayo naamini kabisa wavuvi wa Mafia wataweza kupunguza kama sio kuondokana na umasikini tuliokuwanao. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imetuletea mradi unaoitwa RUMAKI (Rufiji, Mafia, Kilwa). Wameleta pesa nyingi kabisa na siku ya uzinduzi wa mradi huu kule Kilwa Masoko nilikuwepo kwa kushirikiana na mradi wa *MASEMP,* upande wa RUMAKI tumepata zaidi ya Shilingi milioni 930. Naamini hapo kila Wilaya itapata sio chini Shilingi milioni 300 ukiachia mambo ya utendaji. Hizi hela Mheshimiwa Waziri ndiye aliyezitoa, naomba azisimamie.

Mheshimiwa Spika, juzi nimepiga simu Mafia, wanasema Ofisi ya RUMAKI upande wa Mafia wanakusanya vikundi vya watu 30, wanatoa mchango au mkopo wa Shilingi milioni moja. Hivi umaskini huu utaondoka vipi?! Naomba sana Wizara iweke wazi taratibu za utoaji wa mikopo au misaada kupitia RUMAKI, *MASEMP* kwa pesa zote zitakazokuja kwa Wilaya ya Mafia, Kilwa na Rufiji na hatimaye Wilaya ambazo baadaye mtakazotoa misaada. Iweke wazi taratibu ili wananchi waweze kupata pesa hizi bila ya mivutano wala kuwasumbua na bila kuwawekea masharti magumu.

Naomba Wizara ituwekee taratibu hizo wazi, bila hivyo hizi pesa zitatumika kwenye Semina, kusafirisha watu, kufanya Warsha, kulipia gharama za uendeshaji na hakuna chochote kitakachoendelea. Naomba Wizara ilione hili na itufanyie mpango huu wa kuweka wazi ni jinsi gani taratibu za mikopo au ikiwa *grants,* basi wananchi wapate ili tuweze kuondokana na kiama hiki cha umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu Wizara ya Kilimo wana Mfuko wa Pembejeo. Hivi Wizara hii inashindwa nini kuanzisha Mfuko kwa ajili ya Wavuvi? Uvuvi umechukua sehemu kubwa sana na Serikali inapata mapato mengi sana kutokana na uvuvi ama wa bahari au maziwa au mito au mabwawa. Naomba sana, sasa hivi Wizara iandae Mfuko kwa ajili ya Wavuvi kama ilivyofanya kwa pembejeo, basi na sisi tuwe tunapata ruzuku kama alivyochangia Mheshimiwa Mbunge mmoja ili na sisi tuweze kufaidi matunda ya Wizara yetu na uhuru wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri, bado Jibondo kuna matatizo kati ya wananchi wa Kisiwa cha Jibondo na hifadhi ya bahari ya Mafia. Alishafika Jibondo ameona hali ya mazingira ya kule, lakini naomba sasa yeye kama Waziri twende Jibondo tusaidiane tumalize matatizo yale tupate kukaa na kufanya kazi vizuri, kwa upendo ili kuondokana na hizi kero ndogo ndogo za maneno maneno. Naomba twende Jibondo tukasaidiane kumaliza kero ya wananchi wa Jibondo pamoja na hifadhi ya bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie upande wa misitu. Naipongeza Wizara kwa kupiga marufuku uvunaji na usafirishaji wa magogo nje ya nchi. Juzi nilishtuka niliposoma gazeti la Mwananchi na kuona kwamba Wizara imeruhusu kwamba, tarehe 1Agosti, 2006 itakuwa ruksa kuvuna na kufanya kila kitu, lakini bahati nzuri siku ya pili yake nikakuta tamko la Wizara, Katibu Mkuu naye alikanusha jambo hili, ndio nikaona kumbe hawa Waandishi wa Habari wanataka kutuvuruga. Naomba sana Serikali iwe makini na Waandishi wa Habari wanaojiandikia taarifa hizi kwa ajili ya upotoshaji na kusababisha migongano miongoni mwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wameongea sana kuhusu suala la magogo. Nami naungana nao kuzungumzia magogo yaliyokatwa toka mwaka 2004. Naomba sana, ikiwezekana, hawa waliokata magogo waruhusiwe kupeleka huko wanakopeleka. Ni kweli wamekopa, kwa sababu mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira katika kipindi kilichopita, walikuja, tulikaa nao wakatuonyesha nyaraka zote na *LCO* ambazo wamepewa na matajiri zao huko nje na ndio maana wakaweza kupata mikopo katika Benki zetu. Wamepata mikopo, wamechukua mali, wamepeleka mpaka bandarani, lakini bahati mbaya ndio yakaja kuzuiliwa.

Mheshimiwa Spika, uzuiaji ule ulikuwa wa neema, ulikuwa wa kusitiri hifadhi yetu, lakini kwa kuwa mizigo hii ilikuwa imeshakatwa na haiwezekani tena yale magogo kurejeshwa, hayaoti kama mbegu, tunaomba basi jambo hili Serikali mlifikirie na ikiwezekana haya yaliyokatwa, basi wapewe kibali wayaondoe kwa sababu kuwepo hapa ndio kinakuwa chanzo kwa wengine wajanja wanaendelea kuyaleta na kuyaweka katika lundo lile lile. Lakini yakishaondoka na tukishazuia tena, mimi nafikiria hata kama ni kweli Wizara imesema tarehe 1 Agosti, 2006, itaanza kutoa subira kwanza yaondoke haya mpaka tuione ardhi yetu iko tupu, hakuna gogo lililobakia ndio tuanze kupanga utaratibu mpya. Bila hivyo, yatakuwa hayaishi, watu wanaendelea kukata, wanasafirisha na watu wa humo humo ndani kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, kuna baadhi ya watumishi wa Wizara yako sio waaminifu, basi naomba aendelee kusafisha Wizara.

Mheshimiwa Spika, hili jambo linauma sana. Naomba sana Watanzania hawa wasaidiwe. Sisi tulikaa nao, si jambo la kuficha na bahati nzuri Wizara ya Maliasili na Waziri wenyewe alikwenda kuangalia na kukagua pamoja na Watalaam wake, wakapima magogo mangapi, *cubic feet* ngapi zilikuwepo na yale ya haramu yamepigwa mnada. Sasa wale waliokuwa na vibali, waruhusuni waende ili walipe mikopo yao na Vijijini bado wanadai.

Mheshimiwa Spika, tulipotembelea Kilwa tulikuta wananchi wanalalamika, wanadai baadhi ya wafanyabiashara sasa sijui kama waliwapanga ama vipi! Lakini hili naiomba Serikali magogo haya yaliyokatwa yenye vibali na waliokuwa wameshalipia leseni zao yaruhusiwe yaondoke ili tuanze mikakati mipya ya uvunaji na usafirishaji wa magogo, lakini sio leo mpaka tuone ardhi yetu haina gogo lililobakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena kwenye uvuvi. Mheshimiwa Mwanawetu amezungumzia suala la nyavu. Hili suala ndio linalotusababishia migogoro. Tukichukua mfano wa Mafia, ndani ya hifadhi ya bahari hakuna mvuvi anayevua chini ya nyavu ya inchi tatu, lakini pale pale kwenye mpaka wa hifadhi ya bahari pamoja na eneo la kawaida, wavuvi wanavua nyavu za hata robo inchi.

Mheshimiwa Spika, hivi hawa Maafisa wanafanya kazi gani? Ndio maana watu wa sehemu ya ndani ya hifadhi wanalalamika. Kwa nini sisi tunakatazwa wenzetu wanaachiwa wakati wanaonekana lakini hawakamatwi. Hivi ndivyo migogoro inavyotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi huu uharamu wa nyavu unaanzia wapi? Tunataka Serikali ituambie. Nyavu inapokuwa haramu, wapi uharamu wake unaanza toka ilipotengenezwa au inakuwa halali inapotengenezwa, inapokuwa dukani halali inalipiwa ushuru, *VAT* na kila kitu, lakini ukiitosa kwenye maji tu, basi ndio inakuwa haramu?! Naomba sana hili suala mliangalie. Kama nyavu hairuhusiwi, isiingizwe nchini, wala viwanda visiruhusiwe kutengeneza, tuwe wazi. Tunamwogopa nani? Hawa wenye viwanda, kwa utajiri gani waliokuwa nao, watashindana na Serikali? Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri azingatie maoni yetu na sisi tuko pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekumbushwa suala la wanyamapori. Naomba nilizungumzie kwa haraka haraka. Tulitembelea baadhi ya hifadhi hizo na tumeona matatizo mengi yanayowakuta Maafisa Wanyamapori maporini huko. Tunaomba sana hawa wafanyakazi wawekewe bima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekwenda Lubondo, tumeona mke wa mfanyakazi aliyekuwa anatoka Zahanati nje ya eneo la hifadhi wakati anarudi manyani na masokwe mtu yalimvamia mwanamke yule wakampora mtoto wake wakamuua na mwishowe wakamla. Tunaomba sana *insurance* kwa wafanyakazi hawa iwepo na si hao tu lakini wale wote ambao wanaonekana mazingira ya kazi zao ni ngumu na zenye hatari. Naomba Wizara sasa hivi ifikirie kuwawekea bima watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kengele ya pili inigongee, napenda kuunga mkono hoja hii, lakini naomba haya tuliyoyasema Mheshimiwa Waziri wa Maliasili azingatie hasa kwa ndugu zetu hawa wa magogo na tunaomba Mheshimiwa uje Jibondo tumalize matatizo ya wananchi wa Jibondo ili tuweze kukaa kwa usalama na afya.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie Wizara hii ya Maliasili. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa hotuba yao nzuri na vile vile niwapongeza kwa kuchaguliwa kuongoza Wizara hii ingawa wameingia na matatizo, lakini nina imani watayanyoosha na kuendelea na kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja, lakini nina mambo ambayo ni lazima niyaseme. La kwanza, ni magogo. Naomba tusigeuke nyuma, tutakuwa nguzo ya chumvi. Tumeshaamua, hakuna kusafirisha magogo, hakuna wale waliokuwa na magogo, wapasue ziwe mbao wauze kama mbao, wasisafirishe kama magogo. Hatuwezi kuwa tunaamua hili kesho tunageuka tunaamua vinginevyo, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kuzungumzia, kwanza nimuulize Waziri wa Maliasili na Utalii, Sheria ya Wanyamapori tumeipitia, watu wameitwa kwenye Semina mbalimbali miaka mitatu iliyopita, hii sheria iko wapi? Itakuja lini Bungeni? Kuna nini kinachosababisha sheria hii isije? Nafikiria kucheleweshwa kwa sheria hii, ndio maana kunatokea malalamiko mengi hasa upande wa vitalu vya uwindaji. Imefika wakati sasa ni lazima tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa Bungeni zaidi ya miaka nane na kila mwaka tunaimba juu ya vitalu vya uwindaji, hii habari itakuja kwisha lini? Namwomba Mheshimiwa Waziri aishauri Serikali, kwanza sheria ije mara moja na apeleke *paper* kule *Cabinet* kuwe na mabadiliko na iteuliwe Kamati Maalum ya kugawa vitalu hivi vya uwindaji. Nimezungukazunguka hata kule nje, kuna *professional hunters* wanajitangaza. Mimi nimekuwa na kitalu cha uwindaji kwa miaka 29, nina uzoefu, njooni muwinde kwenye kitalu changu. Sasa miaka 29 hilo limekuwa koloni? Ni lazima tuweke utaratibu wa kukaa na hivi vitalu kwa muda maalum na watu wengine wawe wanapata. Ukiangalia wengi wenye hivi vitalu vya uwindaji ni watu wa nje. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Sio wazawa.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Haya, nimeambiwa sio wazawa. Kwa hiyo, mimi naomba sana tuangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, halafu bado tuna tatizo. Hawa watu wamejitangazia himaya zao kule, tuna uhaba wa Askari wa Wanyamapori ambao ndio wanatakiwa waende wawasimamie hawa.

Kwa hiyo, hawa watu wanajifanyia mambo wanayotaka. Sasa umefika wakati ni lazima tubadilike. Tunasema hapa tunapata mapato mengine kutokana na utalii na uwindaji, sio kweli. Sisi hatupati zaidi ya robo ya hela zile wanazopata wale jamaa. Kwa hiyo, ni lazima tugeuke, tuangalie upya. Hata ukienda kwenye hizi *camping site,* maeneo ya kujenga hoteli hakuna wazawa wanaopewa. Sasa ni lazima turudi tuangalie upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nizungumzie kidogo juu ya hawa Maafisa Wanyamapori na Askari wa Wanyamapori. Sasa hivi kuna mgawanyiko mkubwa sana. Sasa hivi kule Wilayani na kwenye hifadhi zetu, mambo hayaendi. Askari walishaacha kwa sababu hawapati haki zao, hawalipwi malipo yao na hawana vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna mgawanyiko mkubwa na huo mgawanyiko uliotokea pale Wizarani wa watu kuhamishwa halafu wanarudi tena, ndio wameigawa kabisa Idara ya Wanyamapori. Ningeomba Serikali iangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna watu wa Mkurugenzi na wengine ambao sio Wakurugenzi hata pale Makao Makuu. Ni juu yetu sisi Wabunge kuishauri Serikali hata iunde Tume. Zimeundwa Tume nyingi sana humu zipite maeneo yote, Idara ya Wanyamapori, hakuna kinachokwenda. Watu wanaongoza Idara kwa *computer*, hawaendi kwenye maeneo ya kazi. Serikali inahimiza watu waachie Ofisi waende kwenye maeneo ya kazi, hawaendi. Atatoka hapa anakwenda Singida kwa sababu kuna maonyesho au ufunguzi wa kitu fulani, anarudi.

Mheshimiwa Spika, nazungumza kwa uchungu kwa sababu mimi mwenyewe ni Bwana Nyama hapa. Sasa naona wanyama wetu wanavyokwisha, ujangili unavyoshamiri na watu wanakaa Ofisini, inaniuma sana. Mheshimiwa Diallo una kazi kubwa sana, ni lazima sasa utoke na ujidhatiti kupambana na hali hii. Najua utapigwa vita sana, lakini kwa sababu ulikula kiapo, mimi nakutakia kila la kheri kwenye kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda katika maeneo mengi ya hifadhi, hata ukienda kwa hawa wanaosindikiza wapanda milima, wanaumia na baridi kwa siku tano, wengine wanalipwa Sh.20,000/=, wanadhulumiwa na hawa *Tour Operators*. Nafikiri kule Maliasili hasa Idara ya Wanyamapori kunahitaji mtazamo mpya na kuweka mkakati wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mtoa Mada wa Kambi ya Upinzani kwa sababu amefichua mambo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunahitaji ukarabati mkubwa sana wa Idara ya Wanyamapori kama Polisi wamefanya hivi. Kama kwingine wamefanya hivi, huko wanyamapori kuna nini? Hatuwezi kukaa tunavumiliana sijui kama kuna urafiki, undugu au ujomba, hata hivyo nchi haiwezi kuendeshwa namna hii! Nasema hivi kwa makusudi ili iundwe Tume iende ikaangalie na ipite maeneo yote, mtaona ikishapita hiyo Tume mapato ya Idara ya Wanyamapori yataongezeka maradufu zaidi yasasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maliasili, kuna mambo mengi sana kwa mfano nilipita Morogoro juzi, kuna mambo haya ya *wet lands,* nikamkuta mtu mmoja na hata hakunificha, akaniambia nimepewa hii tenda, Bwana amelipwa Shilingi milioni 140 ile *consultancy.* Basi na hili naomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie. Hatuwezi kwenda kupeana vitu kienyeji, tenda za Serikali na mambo mengine yanatangazwa kwenye Magazeti, watu wanaomba, anayefaulu ndiye anapewa, lakini kwa huku, kwa kweli tunakoelekea ni kubaya sana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi maeneo yetu mengi wananchi wanalalamika hawana mahali pa kwenda kukata leseni wapate kitoweo kwa sababu maeneo hata yale yaliyokuwa *open areas* ambapo wananchi walikuwa wanawinda yamechukuliwa. Sasa wananchi wetu wanapata nini kutokana na hifadhi hizi? Tuna hoteli zetu hapa Dar es Salaam na maeneo mengine wanataka wapate vibali waanze kuwinda wanyama kihalali wawauzie wananchi. Hivi hamwendi kwa nchi za wenzetu mkaona? Hamjakwenda *South Africa,* Namibia, Zimbabwe ambapo hoteli, watu wanapata kitoweo wanakula jasho lao.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tunagawana vitalu na karibu tuviwekee uzio kwa sababu kama mtu anaweza kukaa na kitalu miaka 10, 20, 26 hela anayolipa hakuna, ni hela ndogo sana!

Mheshimiwa Spika, nazungumza kwa uchungu kwa sababu haya mambo yananihusu. Mheshimiwa Waziri kaingia pale kafanya mabadiliko imekuwa kosa. Sasa huyo Waziri kweli atakaa na hawa watamtii na Waziri alifuata sheria na mabadiliko yako kila mahali. Naomba sana na nazungumza kwa uchungu sana, Serikali ifuatilie juu ya mambo haya. Tukitaka uchumi wetu uongezeke au tukitaka tuwe tunapata kidogo kidogo na wanyama wetu wanakwisha na haraka, tuendelee na utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia kuunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia haumwezeshi Mheshimiwa yeyote kuchangia, kwa sababu ni dakika chache tu.

Nina matangazo machache. Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekuwa na shughuli kule Ikulu Dar es Salaam, kwa hiyo, wale ambao wanataka kuwasiliana na Serikali, aliyepo kama Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali ni Waziri wa Habari, Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib hadi hapo Waziri Mkuu atakaporudi. Nadhani itakuwa pengine saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku ya mwisho ya maonyesho ya Majarida ya Femina pale kwenye sehemu yetu ya hafla. Mnaombwa mkapate majarida mbalimbali ambayo pia yanaweza kufikishwa kwa Wapigakura.

Waheshimiwa Wabunge, jioni saa 11.00 kwa uchangiaji ataanza Mheshimiwa James Lembeli, atafuatiwa na Mhesnimiwa Mkiwa Kimwanga, atafutiwa na Mheshimiwa Aziza Suleyum Ally na pengine Mheshimiwa Chacha Wangwe, simuoni hapa. Kama Mheshimiwa Chacha Wangwe hatakuwepo, basi Mheshimiwa Blandesi unaweza kupata nafasi.Kama kawaida, tutamaliza saa kumi na mbili ili tuweze kusikiliza majibu ya hoja zenu kutoka kwa Mheshimiwa kwanza Naibu Waziri halafu na Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa muda wa saa moja na saa moja kamili tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi.

Kwa kuwa muda uliopo hautoshi kuendelea basi nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu hapa ilikuwa bado ni ndefu lakini ni dhahiri kwamba bado Waheshimiwa Wabunge wanne tu sana sana labda watano, kwa hiyo, nitasoma wale ambao kuna uwezekano.

Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe nadhani huyu hayupo lakini Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes na pengine Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq. *(Makofi)*

Sasa tunaanza na Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niwe mzungumzaji wa kwanza mchana huu katika kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu wake na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kwa bajeti nzuri kabisa ambayo kwa kweli imesomwa pia kwa ufasaha mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti ni nzuri, imewasilishwa vizuri japo inahitaji michango na mawazo mengine ili kuiboresha zaidi iweze kuleta tija zaidi kwa wananchi na uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimsingi naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwa vile nilikwishachangia mengi katika hotuba ya Waziri wa Fedha na ile ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, mchango wangu wa leo utakuwa na machache na nitajikita zaidi katika idara mbili za Wizara hii ya Maliasili na Utalii, Idara ya Utalii na Idara ya Wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuanza na Idara ya Utalii. Sekta ya Utalii duniani licha ya kuwa mhimili mkubwa wa nchi nyingi, Sekta ya Utalii ni sekta inayoongoza kwa kutoa ajira nyingi duniani kote. Hapa Tanzania Pato la Taifa linalotokana na Utalii, limefikia shilingi bilioni 824 mwaka uliopita, ajira katika maeneo mbalimbali hususan yale ya Kaskazini imeongezeka pia kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa sekta hii hapa nchini pia umetambulika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005/2010 pia inatambua

umuhimu wa sekta hii na naomba kunukuu sehemu ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005/2010.

Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako naomba kusoma: "Katika kipindi cha mwaka 2000/2005 sekta ya Utalii ilipiga hatua kubwa katika kuimarisha vivutio vya utalii na kuitangaza Tanzania na matokeo yake ni kuongezeka kwa kiwango kikubwa kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini, katika kipindi cha miaka mitano ijayo mwaka 2005/2010 Serikali za CCM zitachukua hatua zifuatazo ili kuendeleza utalii kwa nguvu zaidi na moja ya hatua hizo ni Serikali kujihusisha kwa ukamilifu katika kutangaza fursa za kitalii zilizopo hapa nchini na kuongeza bajeti ya kutangaza utalii ifanane na zile za nchi jirani."

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya kutangaza utalii imekuwa ni ndogo zaidi kuliko ile ya mwaka jana, mwaka 2004 Bodi ya Utalii Tanzania ilipewa shilingi bilioni 1,600,000, mwaka 2005 bilioni 1,800,000 na mwaka huu bajeti imepungua wamepewa bilioni 1,500,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi tayari Serikali imeshindwa kutekeleza yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ukizingatia kuporomoka kwa thamani ya shilingi ukilinganisha na dola, uwezo wa Bodi ya Utalii mwaka huu kuweza kuitangaza nchi yetu utakuwa ni mdogo sana. Nina wasiwasi kwamba huenda wakashindwa kushiriki katika baadhi ya maonyesho ambayo kila mwaka Tanzania imekuwa ikishiriki.

Mheshimiwa Spika, utangazaji siyo tu kushiriki kwenye maonyesho, lakini pia idara hii inatakiwa kuandaa makongamano, kutayarisha makabrasha, kuendesha tovuti yake na kadhalika, yote haya yanahitaji mabilioni ya pesa. Leo hii tunapozungumza *TTB* wameshindwa kutengeneza hata ramani ya kumwongoza Mtalii anayekuja hapa nchini afike maeneo ambayo anataka kwenda lakini kila siku viongozi wanaagiza Balozi zetu zilizoko nchi za nje tangazeni utalii wa Tanzania, hawana vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutengeneza ramani za Tanzania zinazoonyesha maeneo ya utalii ya Tanzania laki moja inakugharimu zaidi ya shilingi milioni 300, tayari wakitengeneza ramani laki moja bajeti itakuwa imepungua kwa kiwango kikubwa. Kujenga banda la maonyesho ya utalii pale London inagharimu zaidi ya shilingi milioni 250 na kwa taarifa nilizonazo mwaka jana Tanzania ilishiriki kwenye maonyesho yasiyopungua 10 kwa hali ilivyo mwaka huu haitawezekana kwa maana nyingine ni kwamba Tanzania haitaweza kupata kiasi cha pesa ambazo tulipata mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii inahitaji kuwekeza, usipowekeza kwa kweli utaambulia patupu na tusijilaumu mara kwa mara kwa kutoa visingizio mbalimbali kwamba nchi jirani wanatumia raslimali zetu kujipatia pesa wakati nchi ya Kenya mwaka jana ya Utalii ilikuwa dola milioni 10 sisi tulitenga dola milioni 1,500,000. Haiwezekani pamoja na *TTB* kufanya kazi katika mazingira magumu wameweza kwa kiwango fulani kuwadhibiti wafanyabiashara ya utalii ya Kenya leo hii hata ukienda Kenya na nchi za nje hawasemi tena njoo Kenya uone Kilimanjaro, wanachokisema leo hii wanasema njoo Kenya ufike Kilimanjaro haraka. Nafikiri *TTB* wanahitaji kupongezwa kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala la bajeti kwa *TTB* lipewe umuhimu na kipaumbele cha hali ya juu, tunataka Pato la Taifa linalotokana na utalii liongezeke kutoka 16% walau lifike 20%. Umaskini nchini upungue lakini tukiendelea kupunguza bajeti namna hii hatutafikia lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie Idara ya Wanyamapori. Kama nilivyosema tarehe 23 Juni, 2006 wakati nikichangia hotuba za Wizara ya Fedha na Mipango, Sekta ya Maliasili ni Sekta muhimu kwa uchumi wa nchi yetu inachangia 16% ikitanguliwa na Kilimo. Sekta ya utalii ni sekta ambayo kwa kweli inapenda mazingira, mahali ambapo mazingira yamechafuliwa hakuna utalii, Sekta ya Utalii haichafui mazingira kama sekta nyingine kwa mfano madini, sekta ya madini wengi wanaishabikia lakini inaharibu sana mazingira.

Mheshimiwa Spika, Idara hii ya Wanyamapori inaweza kuwa chanzo kikubwa sana cha Pato la Taifa na hivyo kusaidia kuinua uchumi wa nchi yetu. Mimi najiuliza nimesoma tarakimu hapa zinanipa wasiwasi, Idara ya Wanyamapori inasimamia *Game Reserves* zote hapa nchini na *Game Controlled Areas,* inamiliki eneo la kilometa za mraba 104,000 na ndani ya *Game Reserves* wanafanya biashara za aina mbili. Kwanza wanawinda lakini pili wanafanya *Photographic Safaris,* inakuwaje wanakusanya shilingi bilioni 12 ukilinganisha na Hifadhi za Taifa. Hifadhi za Taifa sasa hivi ziko 14 lakini kati ya hizo ni tano ndizo ambazo zinakusanya pesa na hao wanakusanya zaidi ya shilingi bilioni 35 na biashara yao ni ya aina moja tu yaani *Utalii Photographic Safaris*.

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine maneno yaliyozungumzwa asubuhi na yale ambayo yanaendelea kuzungumzwa kwenye Vyombo vya Habari ni lazima Serikali itupie macho Idara ya Wanyamapori kuna tatizo kubwa. Hakuna *transparency,* nafahamu *TANAPA* na Ngorongoro *tariffs* zao ziko wazi, mtu yeyote akitazama kwenye tovuti anajua kupanda Mlima Kilimanjaro anatakiwa kulipa dola 50 au 60 lakini Watanzania hata mimi sifahamu nyati mmoja akiwindwa mtalii huyo au muwindaji huyo analipa dola ngapi, haieleweki na ndiyo maana kuna makelele watu wanaona ndege zinaingia na zinatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usimamizi huko ndani kwa makampuni haya ya uwindaji hakuna anayefahamu, wana tatizo kubwa la watumishi askari na hata hao askari ukiwauliza leo hii wamekatazwa wasiwafuatilie hawa watu. Sasa kweli na taarifa zinasema wanyama wanapungua majangili yanaongezeka, sasa mimi nilikuwa naomba hili tatizo lililopo Wizara ya Maliasili na Utalii, Serikali basi ilitolee tamko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, panapofuka moshi kuna moto, siwezi kuamini mimi hata kama Waziri anakosea kumhamisha mtu, afisa wa chini yake anakataa kuondoka kwa visingizio mbalimbali, lakini kuna maafisa wengine katika Wizara hiyo hiyo nao pia wateuliwe wa Rais, wamehamishwa, wameondoka na wako kwenye maeneo yao ya kazi hakuna anayewatetea. Kelele hizi zitakwisha kwa Serikali kulitatua tatizo hili, vinginevyo mapato ya Idara hii ya Wanyamapori na Wizara hii ya Maliasili na Utalii yataendelea kuwa chini na hatutavuka kwenye kuchangia 16% tufike walau 20%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watumishi katika mapori hayo wanaishi katika mazingira magumu, naomba sana maslahi yao yaangaliwe na hapa napenda niwapongeze *Tanzania National Parks* na Ngorongoro kwa kweli wamejitahidi kwa kiwango kikubwa kuangalia maslahi ya wafanyakazi wao lakini bado wanahitaji kuongeza zaidi kwa sababu mapato ya *National Parks* na ya Ngorongoro yanazidi kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kengele ilie kabla sijamaliza, naiomba Serikali iangalie mtafaruku uliopo pale Wizara ya Maliasili na Utalii, wakubwa kwa wadogo wengine hata hawaangaliani sasa hali hii itaendelea mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nikushukuru kwa kunipa na mimi nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Anthony Mwandu Diallo, pamoja na Naibu wake kwa kutuletea hotuba ya bajeti mbele ya Bunge hili na sisi tuweze kuijadili. *(Makofi)*

Pia napenda kumpongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni, napenda kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi nitapenda nianzie katika sehemu ya Utalii. Katika miaka ya nyuma kidogo katika Mji wa Mwanza kulikuwa na kisiwa kimoja ambacho kilikuwa kikiitwa Kisiwa cha Saanane ambacho kiliweza kutoa angalau kuona aina ya wanyama katika utalii mdogo mdogo, lakini sasa hivi kisiwa hiki hakipo tena, kipo lakini hakipo tena kwa sababu kimekwishakuwa chakavu sana na Wizara ya Maliasili na Utalii ipo inaangalia hata kama kisiwa hiki tayari kilikuwa kimekwisharithishwa kuwa chini ya kundi fulani lakini bado kiko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, fukwe za kisiwa hiki cha Saanane sasa hivi haziridhishi, kisiwa ambacho kilikuwa kikipelekea kwa sababu Mji wa Mwanza hatuna Mbuga za Wanyama ni kisiwa ambacho kilikuwa kikipelekea watu wakati wa sikukuu wakienda kule kuangalia wanyama, jumamosi na jumapili wakienda kule kuangalia wanyama na pia kilisaidia kwa vijana wetu wa shule kwenda kuangalia ni kama mafundisho fulani ya utalii. Lakini kisiwa hiki sasa hivi kina hali mbaya, wanyama waliopo wana hali mbaya labda simba ndiyo kidogo mwenye hali nzuri.

Kwa hiyo, ningeiomba Wizara ya Maliasili na Utalii hata sisi wananchi ambao tuna visiwa kama hivyo wajaribu kuelekeza macho yao kule na ili waweze kukirudisha kisiwa kile katika hali inayotakiwa na pia watu wa Mwanza waweze kufaidika na wanyama hao ambao walikuwa wakiwaona na kuendelea na utalii wa ndani kwa sababu utalii wa Serengeti, Ngorongoro na mbuga nyingine za wanyama gharama zake ni za juu

sana ambapo watu wenye hali ya chini hawawezi kufika katika utalii huo, lakini kile kisiwa kiliwasaidia watu angalau kutoka Sengerema na Magu kuja kuangalia wanyama. Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii iangalie kisiwa hicho na ikipe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Misitu, kweli tunakubali kwamba misitu ikikatwa inaleta ukame, tunakubali kabisa kwamba uharibifu wa misitu umeshindwa kuleta mvua za kutosha na kusababisha nchi yetu kupata njaa. Tujiulize lakini ukataji huu ulikuwa ni ukataji wa aina gani? Kwa sababu ni pale ambapo tunazuia misitu kukatwa ambapo wafanyabiashara wakubwa ndiyo wanaoweza kuharibu misitu kulikoni wakazi wa kijijini. Kwa mfano, tunasema asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania wanaishi vijijini na wananchi hawa wanaoishi vijijini huishi kwenye nyumba za miti ambazo wanaweka miti na kukandika kwa tope na nyasi juu. Sasa kama tutazuia zaidi kukata misitu kwa manufaa ya ndani kama hawa wajengaji wataishi vipi?

Mheshimiwa Spika, hapa ina maana nyumba hii ukiijenga haiwezi ikadumu zaidi ya miaka mitano au sita, itakubidi ujenge nyumba nyingine na kwa sasa hivi Serikali haijalegeza bei ya manunuzi ya *cement* na mabati kupitia kwa watu wanaouza vifaa hivyo kwa hiyo tungeomba uharibifu wa misitu uzuiwe kwa wale wakataji wakubwa. Wasafirishaji wakubwa wakubwa wanaosafirisha magogo kwenda nje ndiyo wazuiliwe lakini hawa watu wanaotumia msitu kwa ajili ya kama vile kuni au mkaa wa kutumia matumizi ya ndani siyo mkaa wa kusafirisha nje ya nchi hawa tungeomba waruhusiwe lakini kwa sheria maalumu ili watu wetu waweze kuwapunguzia adha kwani ni pale tu walipotangaza zoezi la kusitisha ukataji wa miti na walipositisha uchomaji wa mkaa, gunia la mkaa lilisimamia shilingi 20,000/= katika Jiji la Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa tukitaka kujiuliza tunamrahisishia mwananchi maisha au tunamwongezea maisha na hapo hapo katika uchomaji wa mkaa huo kwa matumizi ya ndani yanamrahisishia mwananchi wa kawaida tunakubali Serikali imepunguza ushuru kwenye mafuta ya taa lakini tujiulize huyu mwananchi wa kijijini kweli ataweza kupikia mafuta ya taa muda wote? Huyu mwananchi mwingine anayeishi mjini ni kweli ataweza kupika angalau maharage kwa mafuta ya taa? Ni kitu ambacho hakiwezekani inahitajika mkaa kwa sababu utakapomwambia mtu huyo apike maharage na ndiyo mboga kubwa ya Watanzania wenye maisha duni utakuwa umemwongezea gharama mara mbili ya gharama ile ya mkaa.

Mheshimiwa Spika, tulipata njaa, tukasambaza vyakula vijijini lakini wakati tukizungukia huko vijijini unakutana na mtu anakwambia mimi nimepewa chakula cha msaada, lakini Mtendaji kanikataza kukata kuni sasa nitapikaje hiki chakula? Ni kweli ninayo haja ya kupika ninahitaji, nitafanya njia gani? Kwa hiyo, tunapojaribu kusema kwamba tunakataza jambo fulani tuwe tayari tumeandaa jambo mbadala la kuweza kusaidiana na lile kwa wakati ule ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchangia eneo la nyavu. Ukizungumzia Mji wa Mwanza kama hujamzungumzia mvuvi bado hujazungumzia Mwanza, ukiongea Mkoa wa Mwanza kama hujamuongelea mvuvi bado hujaongelea Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, wavuvi wa Mkoa wa Mwanza wana matatizo makubwa sana, najua ni wavuvi wote Tanzania wana matatizo lakini wavuvi wa Mkoa wa Mwanza wana matatizo sana na hili nashukuru Wizara ya Maliasili na Utalii imeliona na imesema katika hotoba yao ukurasa wa 9 kwamba italishughulikia.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda Wizara hii ya Maliasili na Utalii isiishe kushughulikia kwenye maandiko, kwenye vitabu kwa sababu Mwanza imekwisha kuwa sugu, wauzaji wa nyavu Mwanza wamekwisha kuwa sugu na hata walinzi wa usalama wa rais pia kwa hili imekuwa ni matatizo. Nasisitiza kwa sababu hizi nyavu haramu zinajulikana ni wapi zinatoka, ni wapi zinauzwa na hizi nyavu haramu zimesababisha mpaka kufikia jamii ya Watanzania hasa wakazi wa Jiji la Mwanza katika Kata ya Kirumba, eneo la Kigoto maana yake sasa imekuwa ni msako wa nyavu nyumba hadi nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha kushangaza sana wakati tunajua maduka yanayouza nyavu japokuwa Serikali sasa imeshtuka kuliona hili lakini lilikuwepo na lilikuwa linaeleweka kwamba nyavu haramu zinauzwa madukani, mvuvi hawezi kutengeneza nyavu haramu. Kama uwezo huu wa kuwasaka askari wa Maliasili wanaweza kuwasaka watu nyumba hadi nyumba kutafuta nyavu haramu naiomba Serikali kwa kuwa imesema kwamba itawasaka wauza nyavu hawa na iwasake mpaka kwenye ma-*godown* na makontena yanayoleta nyavu hizi kwa sababu hii inasumbua. Mwananchi ananunua nyavu dukani, huyu muingizaji kaingiza nyavu, nyavu hiyo inauzwa dukani, mvuvi anainunua na kuilipia Pato la Taifa lakini anapoingiza ziwani tu ndiyo inakuwa haramu, mimi naomba uharamu huu uanzie pale inaposhushwa nchini, ianze kuwa haramu na katika usakaji huu wa nyavu hizi uende jinsi inavyotakiwa ili kila muuzaji wa nyavu hili aweze kushughulikiwa kama wanavyoshughulikiwa wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la nyavu bado ni sugu, sielewi kwa sababu nimegusa usalama wa raia, sielewi kuna nini hapo katikati ambacho sikielewi kwa sababu utakuta mvuvi wa samaki ananunua nyavu akipiga hatua 25 au 30 anakamatwa na polisi kwamba amenunua nyavu haramu. Polisi huyo anapokamata hiyo nyavu harama hamwambii yule aliyemkamata kwamba twende unionyeshe ni wapi uliponunua nyavu hii haramu polisi atamchukulia hatua yule mtu lakini polisi alipaswa kujua hii nyavu haramu ameitoa duka gani, kauziwa shilingi ngapi ili kama kuwashughulikia, amshughulikie mnunuzi na muuzaji. Kwa mfano, bangi ni haramu, anakamatwa mvutaji, muuzaji na mlimaji hili hili suala lirudi kwenye nyavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia baada ya nyavu kuna jambo lingine la kusikitisha sana jambo hili la kusikitisha ni kwamba katika Jiji la Mwanza katika wavuvi hasa ni Mkoa mzima wa Mwanza Serikali kupitia *SUMATRA* na huyu ni kada wa *SUMATRA* ambaye sijui ana uhusiano gani na mvuvi kwa sababu tunaelewa *SUMATRA* iko chini ya Miundombinu lakini kuna bwana mmoja ambaye ni *agent* wa *SUMATRA,* bwana huyu anaitwa Mbondo. Mbondo huyu huwasumbua sana wavuvi, Mbondo huyu anaweza akafika kwa mvuvi tunasema sasa hivi tunawaondolea watu wetu umaskini lakini inafika

sehemu kumharibia mvuvi chombo chake sasa huyu mvuvi unapomharibia chombo unamwondolea umaskini au unamwongezea umaskini?

Mheshimiwa Spika, ningeiomba Serikali kupitia Halmashauri za Miji kwa sababu mitumbwi yote inayoingia ziwani imesajiliwa na ikapewa namba, wakiona umuhimu wa *SUMATRA* kwa kupitia wakala wao Mbondo awe pale ambapo tayari mtumbwi unasajiliwa aukague ndiyo uingie majini kuliko mvuvi kuuingiza mtumbwi majini baadaye unavutwa nchi kavu, baadaye unaharibiwa mtumbwi ule. Hapo tunakuwa hatuwaondolei wananchi wetu umaskini bali tunawaongezea wananchi wetu umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwa hili pia ningependa nipate ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwamba huyu Mbondo na *SUMATRA* anahusiana vipi na mvuvi? Hilo ningeomba nipate ufafanuzi ili niweze kuelewa na hata hao wananchi ninaowatetea waelewe hii *SUMATRA* na wakala Mbondo wanahusiana vipi na mvuvi?

Napenda kuongelea tena suala lingine ambalo katika maliasili limekuwa ni tatizo kidogo. Katika eneo la Mwanza wavuvi wetu wa Ziwa Victoria mara nyingi wanapokuwa ziwani wanashikwa, kule kuna majambazi wanawazuia huko maeneo ya uvuvi pia majambazi hao wakati mwingine wanaeleweka na wanapoeleweka watu wale wanakamatwa na kupelekwa kwenye usalama wa raia, kitu cha ajabu katika zoezi la usalama wa raia unasikia mtu huyu kakamatwa na ndiye anayejulikana kwamba ni jambazi sugu na anayesumbua wavuvi ziwani, kesho unaambiwa kapelekwa Sengerema. Kupelekwa Sengerema mtu huyu anaachiwa, ila namshukuru Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza kwa kusema suala hili atalifuatilia na ahakikishe mtu huyu amerudishwa kwa sababu anasumbua sana wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ama baada ya kusema haya nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii. Awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi yao nzuri na hotuba nzuri ambayo wametuletea kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili napenda niwapongeze watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Wizara hii kwa kweli nawashukuru tunafanya nao kazi kwa pamoja kwa sababu mimi ni mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, tunashukuru sana kwa ushirikiano wao na mengi ambayo tunashauriana wanayatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika suala la wanyamapori. Katika suala la wanyamapori katika Mkoa wetu wa Tabora mwaka 2002 tulikuwa tumepata matatizo ya tembo au tuseme mnyama tembo kwa sababu tuko watu wa aina mbalimbali, wengine ukisema tembo wanachukulia maana ile ile ya nyumbani walikotoka nayo. Lakini sisi kwetu tunasema mnyama tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Tabora tembo hawa huwa wanatokea Kahama. Wakitoka Kahama wanakwenda Urambo sehemu ya Kashishi. Nalisema hili kwa sababu najua sisi ndio tuna majukumu ya kukusemea. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi tutayasemea tu haya matatizo ya huko Urambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bado wanakwenda mpaka Nzega lakini tembo hawa wana matatizo makubwa sana ya kuharibu mashamba ya watu. Bado wanafikia hata kiwango cha kuua watu. Nzega pale ukienda katika mikutano ikifika saa kumi na mbili tu watu wote wana wasiwasi kutoka ndani na kujiuliza watafikaje katika maeneo yao. Kwa hiyo, inabidi lazima ukubali kuwa saa kumi iwe mwisho wa mikutano wako. Kwa hiyo, wananchi wanakosa amani.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kutoa ushauri kwamba hawa watu wa wanyamapori wawe wanatembelea kuona kwa sababu tembo ni wanyama ambao wanajulikana ni wanyama wa msimu. Kuna msimu ambao huwa wanasafiri kwa hiyo, msimu huo huwa ndio wenye matatizo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba kwa kwetu msimu ule wao wauangalie, ni muda gani na wao waweze kwenda *site* ili kuona wananchi wanaathirika kiasi gani. Lakini bado katika sheria yetu ya wanyamapori, kuna suala la kifuta machozi. Mkulima amelima shamba lake kubwa na mazao yameshakua lakini matokeo yake yeye anapewa kifuta machozi tu. Lakini hawaangalii mbele lile shamba lina ubora gani au baadaye atakuja kupata matatizo gani kuhusu njaa. Nilikuwa naomba sana sheria hiyo baada ya kuikalia kwa muda mrefu toka tumeanza kuomba, iletwe hapa ili tuibadilishe kusudi wananchi waepukane na adha hii. Wanyamapori ni wa kwetu, lakini wananchi na wao wapewe haki yao ya kulipwa haki zao ambazo zinaharibiwa na wanyama hao. Nategemea Mheshimiwa Waziri ataliangalia hili na kuweza kuleta sheria hiyo bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, wenzetu wengine wamezungumzia kuhusu bahari na maziwa, hata kule Peramiho kuna mabwawa, Tabora sisi hakuna bahari wala Ziwa lakini tuna misitu, nilikuwa nategemea sana katika suala la asali Mkoa wa Tabora ungeweza kupewa kipaumbele zaidi ili *SACCOS* zile ambazo zimeanzishwa kule wananchi wale waweze kwenda kupewa elimu ya kuvuna asali, kuangalia wale nyuki namna gani watazalisha asali kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka miwili iliyopita Mheshimiwa Waziri wa Awamu ya Tatu alikihamisha Chuo cha Nyuki kutoka Tabora kupeleka Moshi, hiyo haikuwa vibaya sana kwa sababu ndio Serikali imeamua, lakini wale ambao walipeleka Chuo cha Nyuki pale Tabora tulitegemea kuwa waliona umuhimu wa Mkoa wa Tabora katika bidhaa ya nyuki. Ukiangalia Tabora Uyui, kunazalisha asali sana. Pili, ukiangalia Sikonge unakwenda mpaka Mpanda asali ni nyingi sana ambayo inazalishwa. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nategemea katika hotuba hii watapewa kipaumbele sana Mkoa wa Tabora kwa uvuvi wao wa asali ili kuweza kuwasaidia katika bidhaa za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa naomba kuchangia sehemu ya utawala bora. Mimi napata wasiwasi kwa suala la utawala bora. Nategemea katika kila Wizara

inasimamia kwa dhati utawala bora kama jinsi ilivyojiwekea utaratibu wake. Lakini bado napata wasiwasi eti kusikia kuwa kuna viongozi ambao wakihamishwa wanashindwa kuhama, kuna viongozi ambao wanamsimamia yule mtu asiweze kuondoka. Sasa napata wasiwasi kwa sababu muda umepita, mtu mmoja ambaye anasababisha eti katika Bunge hili kila mtu akisimama aongelee suala hilo hilo, hivi amekuwa ni nani na hii Wizara inaongozwa na watu gani? Kwa maana hiyo , lazima tukubali Serikali yetu iwe na meno na Serikali yetu iwe na sauti, tusiweze kukubali mtu mmoja aweze kuleta mdahalo au hoja ambayo watu wote waijadili na kusikika katika Tanzania nzima na si Tanzania peke yake hata nchi za jirani. Kwa hiyo, bado hata wenzetu wanaona bado katika Serikali yetu kuna mapungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi sikupendelea suala hili kufika hapa Bungeni, Wabunge wamekaa wanalijadili kwa hiyo, inaonekana Waziri peke yake aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais yuko pale na watendaji wake bado wanaonekana kama ni Makatibu Tarafa tu. Nasema hivyo kwa sababu Katibu Tarafa yeye anatoa sauti yake, lakini anakuja *DC* naye anasema, akija Mkuu wa Mkoa anasema, akija Waziri atasema. Lakini huo si utaratibu mzuri, lazima tukubali Mawaziri wetu wanaopewa madaraka na Mheshimiwa Rais wazingatiwe na waheshimiwe na pia hata watendaji lazima kuwe na heshima kwa watendaji kwa kufuata utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hili mimi nasema hivi kama nitakuwa nimekosea nitawaomba radhi hata pale inaelekea Mheshimiwa Rais au Waziri Mkuu anapokwenda sehemu watu wakisimama na sauti zao mpaka wanapita hawana heshima bado au hawana nidhamu.

Kwa hiyo, yale ambayo anayasema Rais wala wao hawayafuati kwa dhati, lakini nilikuwa nawaomba yule aliyekuwa na nidhamu akisimama na kumheshimu Rais au Waziri Mkuu au Kiongozi Mkuu anayepita, basi akisimama asimame kwa dhati na moyo wake wa kujua kuwa nina haki ya kusimama kwa kumheshimu na kutekeleza maamuzi ambayo anayasema.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna kazi ya kuangalia watendaji wetu na kuna kazi ambayo inatakiwa, Serikali isifanye kazi kwa aibu au kuogopa mtu, lazima tukubali kuwa wawazi kwa kufuata sheria na taratibu za kazi. Kwa namna hii lazima muda mrefu tutakuwa tunajiona bado hakuna kinachokwenda, tutaandaa maneno mazuri, utaratibu mzuri na Bunge letu litakuwa ni Bunge la Wabunge wa kukaa na kulalamika kuhusu mambo mengine, hiyo sio kazi yetu kuja kufanya hapa. Sisi kazi yetu ni kuja kuwatetea wananchi wetu ambao wametuchagua lakini bado tunajisikia uchungu wa Bunge kuona kwa nini kuna suala ambalo linaleta matatizo katika Serikali na Serikali inakuwa kimya muda mrefu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri baadaye atueleze kuna tatizo gani huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema kuhusu suala la Tume au Kamati iweze kuundwa ili kuchunguza. Lakini bado nahisi kuwa hivi kwa nini tumuundie Kamati mtu mmoja tu ambaye anatusumbua, watu wanakaa wanaumiza vichwa vyao, wanapoteza fedha za Serikali kukaa wanaunda unda Kamati hizi. Haina maana, tunaye Rais, Waziri Mkuu na tunao viongozi ambao wanaweza kulitekeleza hili kwa haraka zaidi na

likafanyiwa kazi bila kuwa na kelele yoyote. Kulikuwa na Tume ambayo iliundwa katika Bunge lako lililopita. Tume ile mpaka leo sijaona matokeo yake wala kuletewa taarifa hapa kuwa hii Tume imeundwa ya kuchunguza mambo ya mashauri na mishahara ya walimu kuna hili, hili na hili na hili. Hakuna lililoletwa, sasa kuna maana gani ya hizi Tume kuundwa.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri akisimama atueleze kuhusu utaratibu wa Wizara yake na mambo haya yote ambayo yamejitokeza ili tuweze kuelewa na yawe yamekwisha, yasiwe yanaendelea tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya magogo ndio yale niliyosema ya utawala bora. Tukubali kwamba tunapokuwa na maamuzi, maamuzi yetu yaende kwa wakati na yazingatie sheria. Mimi nilishaona katika Halmashauri zetu hata katika Wizara mbalimbali watu wanakuwa wanafanya maamuzi, lakini hawaoni athari za mbele kuna tatizo gani, wanafanya maamuzi matokeo yake Serikali inakuja kulipa fedha nyingi za kodi ya wananchi. Kwa hiyo, wanapolipa kodi ya wananchi pale tayari wamesharudisha maendeleo ya wananchi wale wa Tabora kwanza ambao bado wanahitaji ile barabara kutoka Itigi na Manyoni kwenda Tabora itengenezwe, lakini matokeo yake mabilioni anakwenda kupewa mtu mmoja ambaye ungefuatwa utaratibu asingelipwa fedha zile kwa sababu amekwenda Mahakamani, amedai haki na ana haki ya kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la magogo. Mimi nilikuwa natoa ushauri, kama wale watu ambao walikuwa na magogo yao pale ambayo yanahitaji kusafirishwa, sheria inawaruhusu kuwa yale magogo yaondoke pale kutokana na kibali, muda wake ulikuwa haujakwisha, wakubaliwe wayapeleke. Lakini kama muda ulikuwa bado kibali kinaruhusu kuwa umekwisha hilo ni tatizo lingine, lakini kama kibali kilikuwa bado kinawaruhusu waendelee kuyaondoa magogo, naomba yale magogo wayaruhusu waweze kuyaondoa lakini kuwepo na utaratibu baadaye ambao utakaowabana watu hawa waweze kuondosha magogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata huu mwezi wa kwanza mimi naona unakuwa ni mwezi ambao bado hatujakaa tukajadili na kuona kuwa ni wakati gani ambao wanaweza kupeleka magogo kwa utaratibu uliokamilika. Lakini kama hawa watu tutawaambia kwamba sasa hivi magogo yaendelee kukaa pale na wanadaiwa kulipia yale magogo kukaa pale na wale watu wanakwenda benki kuchukua mikopo kwa kutegemea vile vibali ambavyo wamepewa, kwa maana hiyo hawa watu tukifuata sheria wanayo haki ya kuidai Serikali baadaye ili iweze kuwalipa na kama hilo lipo na tunaliona na wanasheria tunao kwa nini tusiweze kutumia wanasheria wetu ili kuepukana na matatizo.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kwamba lazima Serikali sasa hivi iangalie wale watu ambao hawafuati sheria walio katika Wizara, kukitokea tatizo lolote ambalo linatakiwa kulipwa fidia kwa mtu basi yule ambaye aliyesababisha, yeye ndiye alipe fidia ile sio pesa za kodi ya wananchi. Hili litasaidia sana kila mmoja katika maeneo yake kuwa makini katika kufanya kazi kwa sababu mtu anafanya kile kwa ugomvi wake na mtu au fulani, matokeo yake anakuja kuitia hasara Serikali na kuwaumiza sana wananchi wetu kwa kuweza kumlipa mtu pesa nyingi sana wakati zile zingetusaidia katika nchi

yetu. Matokeo yake ndio haya tunayoletewa mafungu ya ajabu wanasema hizi zinalipwa madeni. Lakini sasa ukikaa ukichunguza haya madeni gani yanayolipwa, unakuja kukuta ni zile hasara ambazo wamezitia watu wachache tu ambazo zinawasababisha wananchi wengi wazidi kukosa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza jioni hii. Kwanza kabisa namshukuru Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hiyo ya Maliasili na Utalii kwa juhudi wanazofanya. Nazungumza nikiwa upande huu unaoitwa wa kivulini, lakini lengo la kuwa hapa kivulini sio kulala ni kukaa kivulini macho kuangalia kinachoendelea maana yake hata sisi tutakuwa juani siku moja. Kwa hiyo, hatuna nia mbaya ya kuwa na hila yoyote na Serikali au Wabunge wenzetu tuna nia njema tu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana jinsi unavyolinda demokrasia ya *freedom of speech* ndani ya Bunge hili na kutupa fursa ya kuweza kuzungumza mbele ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi ingawa wakati mwingine sasa naweza kusema kwamba Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu ndiye Waziri Mkuu wa nchi hii, halafu naangalia kule kwa *Chief Whip* maana pengine atanikamata kwamba thibitisha, lakini hayo ni pamoja na mambo ambayo najua unayaangalia katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nikienda moja kwa moja katika Maliasili na Utalii, Utalii ni idara muhimu sana katika nchi hii kwa sababu inatuingizia fedha. Lakini vile vile naamini kwamba utalii ni sehemu ya mali tulizonazo Tanzania na unaendelea kwa manufaa ya Watanzania. Lakini napenda kuzungumzia jinsi Wizara hiyo inavyowaweka Watanzania katika mahusiano yake, nina mambo machache ya kuyazungumzia.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mara hususan Wilaya ya Tarime na Serengeti zimepakana na mbuga ya Serengeti, lakini mahusiano na Wizara hii na wananchi yamekuwa ni mabaya sana kwa sababu wananchi wamefanywa kuonekana kwamba wao hawahusiki kabisa na ile mbuga na wanaonekana kama ni watu hatari kabisa kwa ile mbuga wakati historia inaonyesha kwamba sisi kama Waafrika hapa tumeishi hapa miaka elfu nyingi na tumeishi na hao wanyama na tumewatunza, kuwahifadhi mpaka hawa wazungu wakaja kuwaona juzi. Hatukuwa na nia ya kuwamaliza kwa sababu ile *ecosystem* yenyewe inaonyesha kwamba wanapokuwa wamezidi basi hata wasipoliwa na binadamu wanaliwa na fisi na wengine wanakufa wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kuna tabia ya kupata kitoweo pale sasa hii ndio imekuwa balaa. Watu wetu wanakamatwa na kupigwa sana na hawaruhusiwi kukanyaga. Lakini hata mpaka wenyewe haueleweki kwa sababu mpaka uliokuwepo tangu miaka ya nyuma ya arobaini na hamsini hili shirika la *TANAPA* limekuwa likipanua mpaka kila kunapokucha na kuweka maeneo hasa yale ya vyanzo vya maji ambavyo wananchi walikuwa wakitumia ndani ya mbuga na mwananchi anapokuwa anakatiza kwenye ile mbuga akijiona yupo Tanzania anakamatwa na mifugo inakamatwa. Haya yameathiri sana hasa vijiji vya jirani kama Masanga, Gibaso na Kigonga, wananchi wanalia sana. Hilo suala Serikali inaweza kulimaliza tu kwa sababu ni kiasi cha kuwa

karibu na kuangalia kwamba je, wale wananchi ni kwa nini wanakuwa karibu na mbuga kufanya maendeleo yao?

Mheshimiwa Spika, ardhi ya Mkoa wa Mara imepungua kwa kiasi kikubwa. Haya mapigano ya koo mnayoyasikia yanasababishwa na sera za *TANAPA* kwa sababu wale wananchi wanaoishi Serengeti ni koo zilizotoka Tarime kwa hiyo maeneo yao ya kuendelea kupanukia ilikuwa ni Serengeti lakini sera ya upanuzi wa mipaka inayofanywa *unilaterally* bila kuwashirikisha imekuwa ikiwarudisha nyuma kwa nguvu na hata kuchoma vijiji vyao. Mnaelewa sakata lililokuwa linaendelea hapa kuhusu Serengeti na wanaambiwa kwamba wao ni watu ambao wametoka Kenya, wanabebwa na malori wanakwenda wanatupwa mpakani. Kule Kenya inasema haiwatambui wanarudi wanakwenda kubanana na wenzao kule Tarime. Sasa katika ile hali ya kutafuta nilime wapi, ugomvi wa ardhi unatokea ambao ni *land dispute* ambazo zinatokea kila mahali na Serikali ina uwezo wa kuzitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa naiomba Serikali ni kwamba kama basi haiwezi kuwaruhusu waendelee kupanukia ndani ya mbuga ya Serengeti kwa sababu hawawezi kwenda Kenya wala hawawezi kwenda Ziwa Victoria, huku Kusini Wasukuma wamejaa, sasa basi watafutiwe eneo lingine la ardhi ili hiyo migogoro ipungue na hiyo mbuga ya Serengeti iendelee kupanuka lakini nadhani hata wao vile vile ni wadau wanahitaji kupewa haki zao na vile vile mgao wao kutokana na kinachopatikana Serengeti. Kuna makampuni mengine ambayo kweli yameleta sera nzuri ambazo ni za kirafiki za kuwashirikisha wananchi. Kampuni kama sokwe asilia zinajaribu kuwashirikisha wananchi na kuwaonyesha kwamba wanaweza kufaidika na biashara za watalii, hizo ni sera nzuri na tunapenda Serikali iendelee kuzi-*encourage*.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ninachozungumzia ni kwamba kuna tatizo ambalo linaonekana linaendelea huko kutokana na uongozi na sisi tuliopo kivulini hapa tunaangalia tunasema kwamba sasa hiki chama kikubwa kimekuwaje, mbona kinatueleza kwamba wanatatua matatizo ndani ya vikao na Wazungu wanasema *don't wash your dirty, linen in public.* Sasa kuna mambo yanafanyika hapa ambayo yanaonekana kwamba ni ya aibu. Zile *blocks* ambazo hata sisi kule Mara tulihitaji tupewe kwa sababu haki ya kuwinda isiwe ya kibaguzi. Kama kuna uwindaji wa kitalii ambapo wazungu wanapewa *hunting blocks* basi na sisi watu wa Mara tupewe *hunting blocks* hizo ili tuwe tunawinda kama tulivyozoea lakini sisi tumepigwa marufuku yaani katika Watanzania wote wengine wanaoendelea kuwinda katika maeneo mengine kwa leseni lakini sisi kwa kuingiliwa na watu wenye *interest* mbalimbali haturuhusiwi hata kuwinda kihalali, leseni hatukati tumepigwa marufuku wakati mbuga hiyo tumeitunza miaka yote.

Naomba Serikali ilitupie macho hilo suala kwa sababu ni suala la kibaguzi kwa sababu kama ni kuwinda basi kama Serikali inataka kupiga marufuku uwindaji ipige marufuku uwindaji wote sio Wazungu waruhusiwe na Waafrika wazuiwe kuwinda. Hiyo ni *discrimination*. Katika ugawaji wa hizo *blocks* imeonekana kwamba kuna watu ambao wanapeleka *interest* zao binafsi katika ugawaji ule wa zile *blocks*.

Kwanza kuna Kamati inayoitwa *Block Allocation Advisory Committee* ambayo ni Kamati ya kushauri jinsi itakavyogawiwa. Maamuzi yake yanapelekwa kwa Mkurugenzi

na huyo anapotoka hapo anapeleka kwa *Permanent Secretary* ambaye ni Katibu Mkuu, Katibu Mkuu anapeleka kwa Waziri, Waziri ndiye ana uamuzi wa mwisho.

Kwa hiyo, zile *blocks* zinagawiwa na Waziri na Waziri aliyetangulia aligawa *blocks* tatu. Waziri wa sasa amegawa *blocks* sita lakini sasa tunashangaa ni kwa nini kufuata fuata watu wadogo ambao hawana maamuzi ya mwisho na kuwafanya sasa kumbe ni *interest* za watu kwa sababu hata ukiangalia zile bodi za pale hasa hii ya *TANAPA* ile ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, hasa ya Ngorongoro nizungumzie, sheria inasema kwamba uteuzi wa wajumbe wa Bodi si chini ya sita au si zaidi ya kumi na mbili, sasa mbona wameteuliwa kumi na tano ni *section* gani ya sheria imetumika kuwateua wao. Halafu ukiangalia wanateuliwa kwa namna ya upendeleo kwa kufuata undugu, ukabila hata ukiangalia majina yao. Sasa wapo watu wanaokaa kwenye ile mbuga. Wakurya, Wamasai wao hawamo mle wanatoka watu mbali wanakuja wanapangana ili kusudi waweze kupata ulaji mle. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo kama hayo ndio yanasababisha hapa kivulini tunaanza kuzungumza wengine wanatuona wabaya. Lakini haya mambo nadhani Serikali inaweza kuyarekebisha kwa sababu inaonyesha mfano mbaya ambao sio mzuri kwa sababu tutaanza kuwasema tena halafu ionekane kwa nini tunawasema. Hili suala linaonekana kwamba sio sahihi kwa sababu kama sasa Mawaziri wanafuatana fuatana na nini mbele za watu hiyo haifai.

Mimi nita-*shift* kidogo niende katika suala la maliasili na mazingira. Maliasili iliyopo hapa Tanzania ni pamoja na miti, sasa hii miti inaonekana imepungua Serikali imechukua hatua kali ambazo hata mimi nazipongeza lakini tuelekeze zaidi nguvu katika kuwafundisha wananchi wetu namna ya kutumia *biogas* pamoja na nguvu za jua kwa sababu wananchi wengi wana mifugo wanaweza kujifunza kutumia *biogas* kwa kupikia na kumulikia na wakasahau kabisa hata hizo kuni na majiko yale ambayo ni sanifu yanayotumia kuni kidogo yapatikane, viwepo viwanda vya *appropriate technology* kwa sababu sasa kama alivyozungumza mwenzangu hapa amesema hata wale akina mama ambao wana njaa wakishapewa chakula wanashangaa watapikia nini. Hili ni suala ambalo linasumbua sana.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Msemaji wa Upinzani amezungumza mambo mengi ambayo mimi sipendi kuyarudia, ila ningependa pia kugusia kuhusu uvuvi. Katika uvuvi wananchi wanateseka sana kwa sababu sasa wavuvi ambao ni wenyeji hawatambuliwi na wanazuiliwa. Kwa ujumla nikitoa mfano wa Mara kwa sababu mimi nakaa pale, kule ndio nakufahamu zaidi. Mbugani hatuhusishwi katika riziki, vile vile Ziwani haturuhusiwi kuvua, kwenye migodi haturuhusiwi kuchimba, sasa tutakwenda wapi ndugu zangu? Haya ni matatizo makubwa sana, tunaomba myaangalie kwa sababu kama hao wanaoondolewa huko kwenye migodi na kwenye mbuga za wanyama wanakimbilia Mwanza wanajaribu kuwa wamachinga kwenye Jimbo la Mheshimiwa Waziri. Nako kule wanatimuliwa kwa nguvu, sasa waende wapi? Mambo kama haya ndio yanaleta zile *social tensions* ambazo hazina umuhimu.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu kwa leo ni huo tu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu kupitisha barabara ya wananchi katika msitu wa Shaghayu, Wilaya ya Lushoto. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ilipeleka maombi ya kujengewa barabara kutoka Kata ya Mbaramo hadi Mlalo ili kuwawezesha wananchi wa Kata hiyo kupata mawasiliano na Makao Makuu ya Wilaya ya Lushoto. Halmashauri ilikwishatenga fedha kwa ajili ya ujenziwa barabara hiyo mwaka wa fedha 2005/2006. Barabara hiyo haikujengwa kwa sababu Wizara ya Maliasili na Utalii ilikataa kutoa kibali kwa kusingizia kuwa eti barabara hiyo itaharibu vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata ya Mbaramo wanayo haki sawa na Watanzania wengine ya kuishi wanapopenda na kupata huduma za kijamii. Hakuna eneo mbadala la kupitisha barabara hiyo isipokuwa kwenye msitu wa Shaghayu. Barabara hiyo ndiyo itakuwa mkombozi wa wananchi wa Mbaramo ambao ni wachapakazi wanaojitolea maendeleo yao wenyewe mbali ya makazi yao, wamejenga shule ya msingi, sekondari na zahanati kwa nguvu zao wenyewe. Vifaa vyote vya ujenzi wa mazao yao ya biashara huletwa au kutolewa Mbaramo kwa kichwa. Wananchi wa Mbaramo wanaiomba Wizara ya Maliasili na Utalii isiwe kikwazo katika juhudi zao za kujikomboa na kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvunaji wa msitu wa Shume, sehemu ya msitu huu ni wa kupanda *pime* na *cyprus*. Uvunaji wa msitu huu kufanywa na moja mwekezaji wa Kiwanda cha *Tembo Chipboard* na pili wananchini wenye viwanda vidogo vya mbao.

Mheshimiwa Spika, umekuwepo unyanyasaji wa wananchi wenye viwanda vidogo kwa kumpendelea mwekezaji ili avune miti zaidi. Mheshimiwa Zakia Meghji, alitoa agizo kuwa mwekezaji apewe asilimi 60 na wananchi wapewe asilimia 40. Utaratibu huu umeachwa bila sababu au maelezo kwa wadau. Wananchi hawa ndio wanapanda, kulinda na kupambana dhidi ya moto. Mwekezaji yeye hajafanya lolote katika kuboresha hali ya msitu huu. Lakini sasa mwekezaji ndiye anapendelewa dhidi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, hakuna haja ya kulumbana, kinachotakiwa ni kurejesha mgao ulioidhinishwa na Waziri Zakia Meghji, asilimia 40 wapewe wananchi. Hakuna sababu ya kupunguza idadi yao, wao wenyewe walikwishaelewana jinsi ya kugawana katika suala hili, wananchi pia wanayo haki yao. Tafadhali naomba kauli ya Waziri kuhusu masuala haya wawili.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, ushauri kuhusu Bodi ya Utalii Tanzania, nashauri bodi hii iongezewe fedha za kutangaza utalii hapa nchini. Uwepo utaratibu wa kudumu wa uchangiaji wa *TANAPA, NCAA* na Idara ya

Wanyamapori kwa viwango stahili kwa bodi. Wenye biashara za utalii zaidi ya hizo hapo juu, nao wawekewe utaratibu wa kudumu kuchangia bodi hii bila ya kuathiri mapato yao, kwa mfano dola moja ya Marekani kwa kila kitanda itozwe kwa ajili ya kazi za bodi. Wizara ibuni mpango/mradi wa uwekezaji kwa bodi kuwa na chanzo mahususi cha kupata fedha za kutangaza utalii kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, taasisi za utafiti, licha ya Serikali kuwa na azma ya kuongeza ruzuku kwa Taasisi ya Utafiti, wadau wengine wanaofaidi matokeo ya utafiti wawekewe utaratibu wa kudumu wa kuchangia taasisi hizo kwa viwango stahili (siyo shilingi milioni 15 kwa mwaka kutoka shirika kwenda *TAWIRI),* kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Wizara inafahamu ilivyowahi kuweka utaratibu wa uchangiaji kwa mfano, *TANAPA*, *NCAA* na Idara ya Wanyamapori *(TWPF)* kwa *TAWIRI*. Badala ya viwango kuongezwa, vimekuwa vinapunguzwa au kufutwa kabisa bila ya maelezo. Kwa nini bado Wizara ina mashaka kuhusu kusimamia uwekezaji katika tafiti za maliasili? Nashukuru.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Maliasili na Utalii na timu yake kwa kuwasilisha hotuba yake nzuri. Nchi yetu hii ya Tanzania inayo idadi kubwa sana ya maliasili. Tanzania zipo maliasili za baharini na nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, maliasili za baharini kama vile samaki wa aina mbalimbali, matumbawe pia inasemekana iko miti chini ya maji ya bahari iitwayo mivinje bahari. Serikali kama itakuwa na mikakati ya hali ya juu ya kuzitunza maliasili hizi, zitadumu na hazitatoweka na kupotea.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara hii ifanye utafiti zaidi wa kutafuta maliasili nyingine zilizomo baharini ili izijue. Serikali iweke ulinzi madhubuti wa baharini ili kuzilinda maliasili yetu zilizoko baharini. Maliasili zilizopo nchi kavu hapa Tanzania ni nyingi sana tena ni za aina mbalimbali mfano, miti, wanyama, mapango, ndege, wadudu, magofu, milima na kadhalika. Ili maliasili zetu ziendelee kuwepo na ziongezeke lazima Serikali iwaelimishe wananchi wake juu ya faida ya kuwepo kwa maliasili na hasara ya kutokuwepo kwa maliasili.

Mheshimiwa Spika, pia Tanzania tunazo fukwe nzuri ambazo watalii wanazipenda sana. Serikali izitunze na izitumie maliasili hizi vizuri kwa ajili ya watu wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Tanzania zipo mbuga nyingi kubwa ambazo zikitunzwa na kutumiwa vizuri Tanzania itapendeza zaidi na kuvutia watalii. Watanzania wanaweza kuondokewa na umaskini iwapo Serikali itazitunza na kuzitumia maliasili vivuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Napenda kuchangia katika suala la utafiti hasa utafiti wa wanyamapori *(wildlife research)*. Miaka ya 1980, ilikubaliwa ya kuwa watumiaji wa tafiti za wanyamapori *TANAPA*, *NCAA* na *Wildlife Division* wawe wachangiaji wakuu wa bajeti ya utafiti. Hii ni kwa sababu wao ndio wanafaidika na matokeo ya utafiti. Hii haijatokea, vile vile hii inafanya utafiti ufanywe na watafiti kutoka nje ya nchi. Hii ni hatari sana kwa ufadhili kwa sababu matokeo ya tafiti hizi hazionekani humu nchini. *Research reports* na *thesis* hazionekani humu nchini, hata *data base* ya *research data* iko nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba Wizara ifanye ni kuweka utaratibu ambao utawezesha watanzania washiriki katika utafiti. Mapendekezo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, *TANAPA*, *NCAA* na *Wildlife Division*, watoe mafungu ya pesa ambazo zilikuwa zimekubaliwa zitolewe na hizi taasisi.

Pili, *TAWIRI* ipewe pesa ya kutosha kwa ajili ya utafiti ili wafanye utafiti. Kwa wakati wowote wanafunzi wa *MSC= 4* na wa *Ph.D* = 4 kila mwaka kwa muda wa miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, kila mtafiti wa nje *(Research Scientists)* apate Mtanzania wa kumu- *understudy*. Hii itasaidia kujenga uwezo *(capacity) to conduct research.*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, wakati nilipokuwa nachangia kwa kuzungumza nilitoa shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kuruhusu kutoa mazao ya mbao msituni. Nazidi kutoa shukrani kwani walau kero ya wanamaji imetoweka.

Mheshimiwa Spika, muda uliotangazwa wa kutoa mbao hizo hautoshi. Tangazo lilitolewa tarehe 12 Julai, 2006 na mwisho wa kutoa mbao ni tarehe 30 Julai, 2006. Kizingiti kikubwa ni kwamba vifaa ambavyo vilikusanywa wakati misitu inafungwa bado havijarudishwa, hivyo basi wavunaji mbao hao japokuwa wameruhusiwa hadi sasa hawajaweza kutoka mbao kwani nyundo za kugongea mbao hizo bado hazijaletwa.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo naomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii aongeze muda. Vile vile awahimize watendaji wake wa Wizara wapeleke vifaa hivyo mapema iwezekanavyo. Naomba majibu tafadhili.

Mheshimiwa Spika, kipindi hicho hicho cha kuzuia ukataji wa mbao na magogo, wapo wafanyabiashara ambao walikata leseni ya kuvuna, kupasua mbao ambazo hazikuwahi kutumika kwa kuwa Serikali ilishapiga marufuku. Kwa kuwa wafanyabiashara hao walishalipa fedha taslimu si chini ya shilingi milioni kumi na hawakuwahi kupasua mbao.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara ina mpango gani kuhusu wafanyabiashara hao? Wizara itawarudishia fedha hizo au itawaruhusu kutumia leseni hizo katika mpango mpya wa uvunaji mbao utakaotolewa?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa utendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naomba kushauriwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, upandaji miti, bado kazi hii ni kubwa na inahitaji mikakati ya ziada kwa kuwa Halmashauri za vijiji, miji na Wilaya hazitengi fedha ya kutosha kwa kuanzisha bustani za miche ya miti katika maeneo yao, napenda kushauri kuwa Wizara itoe maelekezo kwa wataalam wa misitu, wasimamie kuhakikisha kuwa shule zaote za msingi, sekondari, vyuo na vijiji wanapewa jukumu la kuanzisha bustani za miche ya miti inayofaa kwa ajili ya wananchi wa maeneo yao. Utaratibu ufanyike wa kuwauzia wananchi kwa bei nafuu na kuipanda katika maeneo ya wazi, vyanzo vya maji, mipaka ya mashamba, milimani na kadhalika. Mathalani iwe ni lazima kwa kila mkulima kuweka mpaka wa shamba lake kwa miti inayofaa. Tusipozitumia taasisi nilizozitaja katika zoezi hili la upandaji miti tutachelewa.

Mheshimiwa Spika, miti aina ya *Eucalyptus*, naomba Wizara itoe ufafanuzi wa kitaalam juu ya utata uliopo juu ya ubaya au uzuri wa miti aina ya *Eucalyptus* ambayo inadaiwa kunyonya maji na kusababisha uharibifu katika vyanzo vya maji na kadhalika, wataalam wanatuambia kwamba zipo aina sabini za miti aina ya milingoti, *eucalyptus*. Wananchi wa kawaida si rahisi wananchi wa kawaida si rahisi kutofautisha ni ipi inanyonya maji na ipi inafaa. Ubaini huo, utasaidia katika kuwaelemisha wananchi kabla hawajajiingiza katika upandaji. Kwa maeneo ambayo wananchi wamepanda aina za miti inayonyonya maji, waagizwe kuiondoa na kupanda ile inayofaa kwa lengo la kuhifadhiwa mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kupitia *TANAPA* kwa kuamua kuanzisha hifadhi mpya ya Taifa ya Kitulo. Mkoani Iringa na Mbeya, hifadhi hii kama inavyofahamika ina vivutio vya aina ya pekee kama maua, mimea, misitu yenye miti ya kipekee, ndege na wanyama na kadhalika. Nchi yetu kwa muda mrefu imejizatiti mno katika utalii wa wanyamapori na Mlima Kilimanjaro na Meru. Utalii muhimu kama *site seing Eco-Tourism* na *Cultural Tourism* tumeusahau. Utalii wa aina hii unachangia moja kwa moja katika uchumi wa kaya. Watalii hulipia gharama zao kwa njia mbalimbali huko huko vijijini, watalii huishi katika maeneo ya vijijini na kulipa au kuchangia shughuli za maendeleo ya miradi ya wananchi. Mfano mzuri ni utalii unaofanyika utangazwe katika maeneo mengine hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ushauri, Hifadhi ya Kitulo ipanuliwe na kusambaa katika safu yote ya milima ya *Livingstone* katika maeneo ya Wilaya za Mbeya Vijijini, Wilaya ya Rungwe ukiwemo Mlima wa Rungwe kuelekea safu nzima kando ya Ziwa Nyasa, Wilayani Ludewa. Kwa kufanya hivyo vivutio kama *crater lakes* za Wilayani Rungwe na

vinginevyo vitapata umaarufu mkubwa Ecologia ya kuvutia katika safu hizo, itavutia watalii wengi sana.

Vile vile shughuli za kiuchumi zinazofanyika kama uvuvi katika Ziwa Nyasa, ufinyanzi wa vyungu vya aina ya kipekee na wanawake kando kando mwa ziwa vitapata masoko na hivyo kujipatia kipato. Ifahamike pia Ziwa Nyasa lina aina ya samaki wasiopatikana katika maziwa mengine wakiwemo samaki wa rangi nyingi wanaofaa kwa masoko ya nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, hifadhi hiyo itasaidia kuboresha miundombinu ya aina mbalimbali maeneo hayo ambayo ni duni sana. Uharibifu wa mazingira wa kuchoma mto ovyo, kukata miti utadhibitiwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, namshauri Waziri mwenyewe, viongozi wa *TANAPA* wapate nafasi ya kulitembelea eneo hili. Naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri wanayofanya na mikakati iliyoandaliwa kulinda, kuvuna maliasili na kuendeleza biashara ya utalii. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kuandaa mkutano Jijini Mwanza ambao ulishirikisha wadau wengi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Kanda Ziwa Victoria kubadilishana uzoefu na kupeana ushauri namna bora zaidi ya kunufaika na maliasili ya Kanda ya Ziwa hususan samaki. Utaratibu huu wa Mheshimiwa Waziri ni mzuri sana. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Wizara ya Miundombinu kuwaondolea kero wavuvi wadogo kero inayosababishwa na wakala wa kukagua vyombo vya majini katika Ziwa Victoria. Wavuvi wadogo wanalalamikia uharibifu wa mitumbwi yao unaofanywa na wakala huyo, kutoza fedha nyingi na wakati mwingine kuwadai rushwa. Nashauri uchunguzi ufanywe na wakati huu mkataba wa wakala huyo usitishwe na kazi hiyo kusimamiwa na wataalam wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru tena na naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa maandishi katika hoja tajwa. Lengo langu ni kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iyazingatie yafuatayo katika bajeti ijayo na nitaendelea kufuatilia. Kwanza, Serikali ieleze mkakati ulio nao kuzuia kukauka kwa Ziwa Victoria. Maji katika Ziwa Victoria, ni maliasili yetu ambayo kwa kweli pasipo maji ya kutosha sisi wananchi tunapata hofu kwamba kasi ya maji kupungua katika Ziwa hilo ni kubwa. Wakati huo huo hatujaelezwa mkakati wa Serikali ni upi kuzuia kasi ya Ziwa hilo kupungua maji. Kina cha Ziwa Victoria, katika mialo ya Muleba Kaskazini kinakaribia mita saba tangu yalipokuwa/miaka sita iliyopita maji hadi yalipo sasa. Kasi

hii ya Ziwa kupungua maji, wananchi wanataka/maelezo ya je, Serikali imeliona tatizo hilo na ina mkakati gani wa kudhibiti?

Mheshimiwa Spika, la pili, ni la wakazi wanaoishi karibu na Ziwa Victoria ambao ajira yao kubwa ni uvuvi. Hawa ni wavuvi wenye kipato kidogo, kwa maana nyingine wana mtaji mdogo. Ziwa Victoria ni miongoni mwa Maziwa ambayo yanachangia Pato la Taifa kwa kuvuliwa samaki wengi. Wavuvi wanaovua na kuuza kwa wingi ni wakubwa tu, hali ambayo inawaadhoofisha wavuvi wadogo. Wavuvi wadogo wamegeuka kuwa vibarua wa wavuvi wakubwa. Wavuvi wadogo wametupwa, wamebaki kama yatima. Naishauri Serikali ilitazama hilo kwa jicho la kuwalenga wavuvi wadogo. Naishauri Serikali, iwaangalie wavuvi wadogo ili wapate njia ya kufuata ili waunde makundi na makundi hayo yasaidiwe ili yasiendedelee kuwa vibarua wa wavuvi wakubwa.

Mheshimiwa Spika, la tatu, naishauri Serikali iajiri watumishi wenye utu na uungwana. Nalisema hilo kwa kuzingatia kwamba Serikali imemwajiri mtumishi wake mmoja ambaye hakika anawatia umaskini wananchi ambao ni wavuvi. Hivi ni haki kweli kuvunja mitumbwi ya wavuvi kwa madai kwamba hawakulipia ushuru wa maegesho ya shilingi 30,000/=? Je, thamani ya mtumbwi huo ni shilingi ngapi? Hakuna mtumbwi unaoweza kupatikana chini ya shilingi 70,000/=. Vile vile mtumishi anapovunja mtumbwi huo, je, magari yanapopatwa na makosa yakakamatwa yanaharibiwa? Mbona hushikiliwa hadi mhusika atakapotimiza masharti kisha kurejeshewa gari lake. Huu ni uonevu wa hali ya juu sana kuvunja mtumbwi wa mvuvi kwa madai ya kudaiwa egesho! Narudia kuiomba Serikali kwamba iajiri na ielimishe watumishi wake utu na uungwana! Uonevu ni dhambi kubwa. Haifai kosa la kutolipa likawa la kumtia mvuvi umaskini wa kudumu, kumvunjia mtumbwi. Kiwepo chombo cha kudhibiti tabia hizi ambazo zimekithiri katika maeneo ya mialo ya Kyamkwikwi, Rwazi, Bumbire, Iroba, Goziba, Kelebe, Makibwa, Kitua, Kinagi na maengine mengi. Vinginevyo wananchi wetu hawatakomboka na umaskini.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru Serikali ikifanyia kazi haya niliyoyaeleza kwa dhati na kwa uhakika. Ahsante sana.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, Kigoma imeathirika sana na misitu yetu ya asili kuvamiwa sana na ujio wa wakimbizi ambao walivamia kukata kuni na hata mbao, nashauri *strongly* mkakati wa kuanzisha *branch* ya wakala wa miti Kigoma na hususan Wilaya Kasulu ili kusimamia vilivyo upandaji miti katika maeneo yaliyoathirika sana na wakimbizi. Wizara yako inaweza kushirikiana na Wizara ya Mazingira ili kupata fedha kwa kazi hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukubwa wa eneo la Wilaya ya Kasulu naomba sana Idara ya Maliasili wapewe gari la kufanyia doria ili kulinda misitu yetu iliyobaki hasa mapori ya Nyamroha na *Banks* za Malagarasi.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 16 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kipengele 27 je, hiyo sensa ya wavuvi iliyofanyika ni kwa nini sensa hiyo haikufanyika

katika Ziwa Tanganyika? Kumbuka sensa hizi zinasaidia sana kupanga mipango ya kusaidia kundi hili na pia kupata *data* za ajira katika sekta hii.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Waziri, Maliasili na Utalii, katika Jimbo langu la Ruangwa tatizo namba moja ni kero ya mamba na boko. Wananchi wanashindwa hata kwenda shambani wakati mwingine! Hakuna ufumbuzi wa tatizo hili miaka nenda rudi. Risasi hakuna, mamba hairuhusiwi kuwaua! Je ni kweli?

Tatizo la pili, Ruangwa tuna misitu mizuri mingi, tunahitaji kufuga nyuki. Je, unaweza kutusaidia hili kwa kikamilifu ili nasi angalua tuwakumbuke wenzetu kwa mfano Tabora?

Mheshimiwa Spika, tatizo la tatu, Ruangwa hatuna kitoweo! Je, unaweza kutusaidia ili tuwe na mabwawa ya kufuga samaki ili tupate kitoweo na tuuze ili kuongeza kipato? Pia kuwafanya wapiga kura wetu wasiisogelee *Seleous Game reserve?*

Je, ni kweli *Paurosa* ni mti adimu hapa duniani? Kuna wafanyabiashara walikuwa wanazunguka zunguka maeneo ya mabwawa katika jimbo hili ili waifyeke hiyo miti? Kama jambo hili ni la kweli naomba tuchukue hatua za kulinda mali hii. Kama haipo naona ni vizuri watumwe wataalam ili kuja kufanya utafiti.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa mimi naunga mkono bajeti yako kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza sana Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake nzuri ilitoa mtazamo wa Wizara na Makadirio ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwapongeze Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na watendaji wakuu wote walioandaa hotuba hiyo kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya kuiandaa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, misitu ni uhai, misitu ni urithi mkubwa na zawadi kubwa tuliyoipata kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Lakini tusipoitunza na kuilea ipasavyo zawadi hiyo inaweza kutuponyoka na kutuletea madhara makubwa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya mpya ya Nanyumbu iliyopo mkoani Mtwara ilibahatika sana kuwa na misitu minene ya asili yenye miti aina ya mpingo ambayo huchukua miaka mingi kukomaa.

Mheshimiwa Spika, katika miezi ya hivi karibuni uvunaji wa miti hii ya mpingo umekuwa ni wa kutisha Wilayani kwangu Nanyumbu. Mipingo mingi imevunwa kwa kasi sana. Ningependa Wizara ya Maliasili na Utalii itoe maelezo kuhusu uvunaji huu wa mipingo, imerundikwa barabarani kati ya Chungu, Kata ya Nanyumbu na Masuguru. Je, ni nani wanaotoa vibali vya uvunaji huu wa kutisha? Natoa ushauri kwa Wizara kusitisha uvunaji wa miti ya mipingo ili iliyobaki iweze kukomaa kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uvunaji huo wa mipingo kuna uvunaji mkubwa pia wa magogo ambao usipodhibitiwa Wilaya za Masasi na Nanyumbu zitageuka kuwa jangwa. Naomba sana Wizara ya Maliasili na Utalii idhibiti utoaji wa vibali vya kuvuna magogo na hasa kwenye viwanda vya kupasua magogo na mbao. Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na hasa Mkurugenzi wake Bwana Noel Mahyenga amejitahidi sana kukamata malori yanayobeba magogo bila kibali lakini juhudi hizi hazitoshi kwani vibali vimekuwa vikitolewa.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kuwa tusipoziba ufa hutajenga ukuta.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kusema kuwa ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, pongezi na pole kwa Wizara katika maandalizi ya bajeti ya mwaka 2006. Mheshimiwa kaka yangu Anthony Diallo umekuwa Naibu Waziri wa Wizara hii katika awamu ya tatu, awamu ya nne umekuwa Waziri kamili, hii inaonyesha kuwa uliweka rekodi nzuri kipindi cha Unaibu. Hongera sana. Ni fahari kubwa katika nchi yetu kwa kuwa na maeneo makubwa ya mapori ya akiba na Hifadhi za Taifa 4.5% ya eneo la ardhi ya Tanzania, kuwa na wanyama ambao hawapo sehemu n yingine Barani Afrika na duniani.

Naupongeza mpango wa Serikali kuanzisha *Wildlife Management Area (WMA)* ili kushinikisha zaidi jamii katika kumiliki na kunufaika na maliasili. Nimepitia *The Wildlife Conservation Act, 1974* kipengele cha *Wildlife Management Areas, Regulation, 2005* inayoruhusu uanzishaji *WMA.,* nimeona vijiji vingi vimeruhusiwa kuanzisha *WMA.* katika Wilaya za Tarime, Urambo na kwingineko lakini vijiji vya Wilaya ya Meatu hakuna hata kimoja hata zile zilizokidhi vigezo kama Jinamo, Sapa, Makao, Paji Mwanzagaba na Mang'wina zinazo sifa.

Mheshimiwa Spika, eneo lipo zuri, tena *open area,* wanyama wengi karibu aina zote, tatizo nini? Naomba maelezo je, ni lini sasa vitatajiriwa katika mpango wa *WMA?* Vijiji vilivyo kando kando ya mapori akiba *(Game Reserves)* baadhi vimepungukiwa sifa za mpango wa *WMA.* Kwa mbinu shirikishi ina manufaa makubwa walau kilometa moja kuingia kwenye pori la akiba limilikiwe na kijiji kwa kanuni na sheria zile zile za *WMA.* Katika jimbo langu vijiji vilivyo mpakani mwa pori la akiba la Maswa ni Buga ya Bahyu, Nyanza, Butuli, Matale Mwamhongo na Mwaseng'ela.

Mheshimiwa Spika, sheria ya mwaka 1974 ya hifadhi ya mapori ya akiba na hifadhi za Taifa inazuia kuingia wala uwindaji Kirai kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Spika,wananchi wanahitaji wawinde walau kwa ajili ya kitoweo (nyama), wananchi wanahitaji wawinde kwa shughuli za utamaduni, mila na desturi na matokeo yake hakuna maelewano wala mahusiano kati ya askari wa *Game Reserves* na wananchi.

Mheshimiwa Spika, askari wa *Game Reserves* wanasimamia sheria wananchi nao kuona wananyimwa haki yao ya msingi. Wananchi wanakamatwa, wanateswa vibaya, wanatozwa faini kubwa na kufungwa jela miaka mingi.

Katika hili tunaowatesa sana ni wananchi, kutokana na sheria kupitwa na wakati, hakuna kazi ngumu kama kupewa kazi ya kuchemsha nyama, nyama inatokota halafu unanyimwa hata kuonja mchuzi, wananchi wangu mate yanawadondoka wanahitaji kula nyama na hata kwenye migodi ya madini kuna wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kifungu 34 katika ukurasa wa 32(b), kuzipa Serikali za Mitaa nguvu zaidi na kuwawezesha kumiliki na kunufaika na maliasili, sera ya utalii ya Taifa Septemba, 1999 katika ukurasa wa 17 na 18. Mikakati ya sera kwa ajili ya ushirikishaji wa jamii ni pamoja na kutoa kipaumbele kwa wananchi wa jamii hizi kwa upande wa mafunzo, nafasi za ajira na manufaa mengine ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *TANAPA* wa ujirani mwema, *Community Conservation Services* ni mzuri umesaidia sana kuharakisha maendeleo, lakini bado mpango huu hautoshi kuleta upatanishi, mahusiano mazuri kati ya watendaji na wananchi na wala hautoshelezi mahitaji ya Ilani, 2005.

Mheshimiwa Spika, nafasi za kazi mbalimbali zinapotangazwa vijana waishio kando kando ya hifadhi hayapewi kipaumbele, kinyume chake huletwa vijana toka sehemu zingine kitendo ambacho huwachukiza wananchi na kuona kama wanahujumiwa, pengine huona nafasi hizo zinajazwa hata bila kutangazwa, nashauri sana kipaumbele kwa watu waishio kando kando. Wapewe nafasi hizo za ajira.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamekuwa wakisubiriwa wavunje sheria ili wakamatwe na kupigwa faini kubwa na pengine kufungwa jela miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawapewi semina na wala mafunzo yanayokidhi na mwisho nazidi kushauri walau kilometa moja kuingia kwenye pori la akiba ili kutengeneza *buffer zone* kati ya shughuli za binadamu na zile za hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo ni kukidhi matakwa ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 pamoja na sera 1999, mwananchi atanufaika zaidi na mazao ya maliasili, majangiri yatapungua kwa kuwa jamii itakuwa imeshirikishwa zaidi na Pato la Taifa litaongezeka.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuanza vizuri shughuli za kulinda maliasili katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, moja, hotuba ya Waziri katika ukurasa wa 31 imeeleza wazi kuwa Serikali imeweka mpango kabambe wa kuendeleza kikamilifu rasilimali za ufugaji nyuki katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Iringa.

Naomba majibu kutoka kwa Waziri kwa kuwa Kata ya Gumbiro, Kata ya Ifinga na Kata ya Magagura tayari tumeanzisha vikundi hivi vya ufugaji wa nyuki, lakini hatuna kasma hiyo katika Halmashauri, je, Serikali Kuu iko tayari kuja kushirikiana nasi katika azma yake ya kuendeleza rasilimali nyuki kama ukurasa huo wa 31 unavyosema?

Mhesimiwa Spika, pili liko suala la ufugaji wa samaki katika visima vya asili vilivyoboreshwa. Tayari vikundi 15 vya vijana vinahitaji mpango huo wa kuendeleza ufugaji samaki kama Wizara inavyosema. Tunaomba sana Wizara itusaidie hilo ukizingatia tatizo kubwa la ukomo wa bajeti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii..

**MHE. LAWRENCE K. MASHA:** *Honourable Speaker, the tourism potential for the Lake Zone as a whole and Mwanza in particular is highly underdeveloped. Mwanza and the Lake Zone todate do not have a single four star and or five star hotel yet Mwanza is the closest urban centre to the Serengeti National Park and has great potential for game fishing.*

*Honourable Speaker, I would like to know what efforts are being made by the Ministry to attract investment to Mwanza and the Lake Zone in general within the Tourism Sector. Would it not benefit the country in terms of foreign exchange if the northern circuit was marketed inclusive of lake Victoria, that is Mount Kilimanjaro, Serengeti and then Lake Victoria or vice versa.*

*Honourable Speaker, the Fish Processing Factories gracing the Lake Zone have been muting millions of shillings though the sale of fish fillet abroad. Despite this fact many of the factories in Mwanza are accused of underpaying their employees as well as the fishermen who supply them with fish. Can the Honourable Minister tell us what oversight role the Ministry plays to ensure that our young men and women working in these factories are adequately paid and to ensure that the fishermen who supply fish to the companies are adequately and fairly compensated.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, moja, maliasili ya baharini inaweza kusaidia sana kuongeza Pato la Taifa pamoja na pato la mwananchi kama wavuvi wadogo wadogo watasaidiwa kwa kupatiwa vyombo vya kisasa na pia kupatiwa elimu ya uvuvi. Kinachofanyika sasa ni kuvua kwa uzoefu tu na sio kwa utaalamu. Je, Serikali ina mpango gani katika kuwapatia vifaa vya uvuvi vya kisasa pamoja na elimu ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali imekuwa na nia nzuri ya kuitangaza nchi yetu nje ya nchi kwa lengo la kuwavutia watalii wengi kila mwaka. Licha ya juhudi hizo,

Serikali haioni kuwa kuna haja pia ya kukuza utalii wa ndani pamoja na kuandaa utaratibu utakaowawezesha wananchi wetu kufika katika maeneo ya utalii.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitamke kuwa naunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja ninayo yafuatayo ambayo ama naishauri Serikali au naitanabaisha.

Moja, eneo la utalii ni nyanja moja inayochangia katika Pato la Taifa katika nchi yetu. Watalii wengi hupenda kutambelea maeneo yenye vivutio vya kipekee *(unique sites)*. Inashangaza Wizara ya Maliasili na Utalii, imeshindwa kutambua kuwa *Mahale Game Reserve* ni moja ya maeneo yenye mvuto wa pekee kwani wapo Sokwe ambao hawapatikani sehemu nyingine katika nchi yetu isipokuwa hapo na *Gombe Game Reserve.* Mbali na kuwa ni Hifadhi ya *Sokwe Mahale Game Reserve* inao Sokwe wa kipekee, wapo Sokwe weupe. Ifahamike kuwa Sokwe wengi duniani ni weusi, lakini pale Mahale wapo Sokwe wa aina mbili, wapo Sokwe weusi ambao wamezoeleka na wale weupe.

Mheshimiwa Spika, mshangao mkubwa ni kwamba pamoja na kivutio hiki cha pekee, hakuna juhudi zinazofanywa za kurahisisha usafiri wa kufikisha watalii kutoka Kigoma Mjini hadi Mahale (Kusini mwa MKoa wa Kigoma) mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kueleza mwaka 1999 kuwa ufanyike utaratibu wa *TANAPA* ichangie juhudi za wananchi za kutengeneza barabara ya kutoka Ilagala hadi Kalya kupitia Buhugu ambapo Mahale ipo. Katika ushauri wangu huo nilijibiwa kuwa uongozi wa Mahale uwasiliane na *TANAPA* pamoja na Wizara ya Ujenzi wakati ule na sasa Miundombinu ili juhudi za wananchi zipate nguvu ya fedha na *TANAPA* kwa nia ya kusaidia hasa ujenzi wa madaraja na makalvati.

Mheshimiwa Spika, ni vyema ieleweke wazi kuwa kuwapo barabara ya uhakika hata kama ni ya changarawe kutawezesha watalii wengi watafika Mahale na hivyo kuongeza pato la Taifa kwa pesa za kigeni na za ndani kwani huduma zitapanuka.

Mheshimiwa Spika, pili, ipo kero inayosababishwa na uongozi wa *Mahale Game Reserve* kwa wananchi na wakazi wa Kijiji cha Kalilani ambacho kinapakana na Hifadhi. Kijiji kimesajiliwa kwa mujibu wa sheria. Kinayo hati ya usajili iliyotolewa mwaka 1992 na mimi nikiwa Mbunge niliyekabidhiwa hati ile kutoka Ofisi ya Msajili wa Vijiji hapa Dodoma na kupeleka kwa uongozi wa kijiji cha Kalilani. Inasikitisha kuona kuwa uongozi wa kijiji unasumbuliwa pasipo na sababu na wahifadhi kwa hoja bandia ya mipaka.

Mheshimiwa Spika, mipaka iliyoainishwa katika hati ambayo niliyoelezea hapo juu ni mipaka halali inayotambuliwa na Serikali. Imekuwaje wahifadhi pale wawabughudhi wanakijiji mara kwa mara na hivyo kuwafanya wasifanye shughuli zao kistaarabu muda wote wanabudhudhiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara wakati wa majumuisho inipe majibu ya kuridhisha ni kwa nini wanakijiji wanasumbuliwa na wanakijiji wamefikisha hoja hizi kwa Mheshimiwa Zakia Meghji alipokuwa Waziri wa sekta hii na ufumbuzi ulitolewa kwa kuelekeza kuwa mipaka iliyotajwa kwenye hati iheshimiwe.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha mipaka haiheshimiwi, kwa makusudi na kwa nia ya kuwatoza rushwa wanakijiji wanabughudhiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara inipe majibu sahihi kwa nini wanakijiji hawapewi fursa ya kufanya shughuli kwa awamu na kwanini uamuzi uliotolewa na uongozi huko nyuma hauheshimiwi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mlima Kilimanjaro ni moja ya vivutio vya utalii na huingiza zaidi ya shilingi bilioni 15 kwa mwaka toka kwa watalii wanaopanda Mlima huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kupitia Bodi ya utalii na *TANAPA* pia makampuni binafsi yanayofanya biashara ya utalii hutangaza mlima huo pia katika kufanikisha upandaji Mlima Kilimanjaro makundi yafuatayo yanahusika, moja, Kampuni ya Utalii *(Tour Operators),* pili, waongoza watalii *(Guides)* na tatu, wapagazi.

Mheshimiwa Spika, makampuni ya utalii huleta wageni ni kuwakabidhi kwa waongoza watalii na wapagazi tayari kuwapandisha milima.

Mheshimiwa Spika, lakini waongoza watalii na wapagazi wanalipwa mishahara midogo sana na *tour operators.* Wengine wanalipa hadi shilingi 20,000 kwa siku tano yaani shilingi 4,000 kwa siku. Kiwango hiki ni kidogo sana. Hawa waongoza watalii na wapagazi wameunda vyama vyao na kuamua yafuatavyo, kiwango cha malipo kiwe kama ifuatavyo, *guide* alipwe dola 20 kwa siku, mpishi na *Assistant Guide* dola 18 kwa siku na *porter* alipwe dola 15 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, pia katika vikao vyao yaani kikao cha *Kilimanjaro Guides Association* na *Kilimanjaro Porters Association* waliamu yafuatayo:-

Kwanza, kila *guide* na *porter* lazima awe na mkataba wa *Tour Operators* unaoonyesha masharti ya kazi na mshahara kabla hajaruhusiwa kuingia Hifadhini. Hii itasaidia kujua kama mishahara yao inatosheleza kulingana na kazi wanayofanya.

Pili, vyama visimamie wakishirikiana na *KINAPA* kuhakikisha mishahara inalipwa mara wanapomaliza kazi na Wizara, *TANAPA, KINAPA* wanaohudumia watalii ni wale tu walio wanachama wa vyama vilivyosajiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa njia hii Serikali itapata mapato, vijana wetu watapata mapato mazuri. Wanaolipa mishahara ya hawa vijana ni watalii wenyewe na wako

tayari kuwalipa hata zaidi kwa kuwa ndio wanaokaa nao huko mlimani kwa siku tano ama zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa utaratibu wa sasa hivi, hawa vijana wananyonywa na *Tour Operators* huku Wizara ikiangalia bila kuchukua hatua. Wizara ilikiri hapa Bungeni kuwa hawa vijana wanateseka na kunyanyasika, sasa ni wakati wa kuchukua hatua naomba Waziri alitolee uamuzi wa kudumu mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mimi ni Mwenyekiti wa *Kilimanjaro Guides Association* naelewa matatizo ya hawa vijana na mateso wanayopata na jinsi gani hawalipwi. Najua ni watalii wangapi na vijana wangapi wamekufa huko milimani na sababu ya vifo vyao kwa miaka mitano iliyopita.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni mambo muhimu kwa maisha ya watu na ustawi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, utalii ni njia mojawapo ya kuliingiza Taifa pato. Ni vyema kuimarisha vivutio vyetu vya kiutalii ili kukaribisha watalii kumiminika nchini petu ili kukuza uchumi wetu. Lakini kiuchumi ipo haja ya kuangalia utalii usiathiri utamaduni wa nchi yetu. Aidha, Serikali iangalie ni kwa jinsi gani wazawa wanafaidika katika mahoteli ya kitalii. Upo ukweli kwamba kumekuwa na usiri wa ajira na kima cha mishahara kwa vijana wetu wanaofanya kazi katika hoteli za kitalii. Waajiri wengi katika hoteli za kitalii ni wageni kutoka nchi husika. Mishahara ya wazawa ni duni ukilinganisha na ile ya wageni.

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi bado halijapewa umuhimu mkubwa ambapo uvuvi ni eneo muhimu sana kuinua uchumi na vipato vya wananchi wetu. Tuweke mpango maalum wa kuwapatia zana bora za uvuvi, kuwe kuna mpango wa kuwakopesha wavuvi mitego bora. Bahari inao uwezo wa kutoa ujira kubwa. Mitego ambayo haifai ni vyema kukusanywa na wahusika kupewa mikopo ya mitego inayokubalika.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Wizara juu ya suala la uvunaji wa misitu asili. Ni hatua nzuri kuweka mkakati wa kuzuia uvunaji wa mazao kutoka misitu asili, lakini uzuiaji huo uwaguse wananchi wote. Inaleta unyonge kwa wananchi kuona ni wao wananchi wa kawaida ambao zoezi hili linawanyima fursa ya kujipatia kipato kutoka misitu asili, lakini watu wa daraja fulani wanaendelea kuvuna misitu hiyo asili.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote na Wizara hiyo kwa kazi nzuri wanazozifanya katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo naomba kuchangia yafuatavyo, moja, matumizi ya *future*. Hivi sasa fukwe zetu hasa katika fukwe za mwambao wa

kutoka Feri-Kigamboni hadi maeneo ya Pemba Mnazi kuna matajiri walionunua viwanja maeneo yaliyo karibu na fukwe wengi wao wamejanga wao hadi sehemu za matumizi ya jamii na baadhi kudiriki kuwapiga wananchi wanaopita maeneo yaliyo mbele yao. Ninavyoelewa kuna mita maalum hutengwa kutoka usawa wa bahari hadi fukwe kwa matumizi ya wananchi kwa ujumla. Je, Serikali hilo inalielewa? Naomba Waziri afanye ziara ya kutembelea Kata ya Mjimwema na aonane na Mwenyekiti wa Mjimwema kuthibitisha hayo.

Pili, matatizo ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya maendeleo. Suala la kupatiwa mikopo wavuvi wa Tarafa ya Kigamboni, Jimbo la Kigamboni hawajapata kabisa mikopo kutoka Serikalini. Naomba kipaumbele cha kuwapatia mikopo wavuvi wa Tarafa ya Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la kuimarisha doria katika maeneo ya bahari kupambana na wavuvi haramu wa mabomu na nyavu zenye tundu ndogo hivyo kusababisha samaki wengi wadogo/wachanga kumwangwa tu na kusababisha hasara kubwa na kupungua samaki katika uvuvi wa aina hiyo na kuua mazalio ya samaki.

Mheshimiwa Spika, tatu na mwisho, naomba suala la unyanyasaji wa matumizi ya fukwe nipate majibu ya maandishi pia ili jibu hilo nami na ngazi mbalimbali za uongozi uliopo katika Jimbo la Kigamboni tuweze kulitumia jibu hilo kusaidia kurekebisha unyanyasaji huo.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, naomba kutanguliza kuunga mkono hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Napenda kumpongeza Waziri, Naibu Spika, Katibu Mkuu Salehe Pamba na watendaji wengine wote kwa kutekeleza kazi za Wizara hii nyeti na ngumu.

Napenda kuzungumzia kuhusu wanyamapori. Wanayamapori ni mali inayoongeza uchumi wa nchi kama madini, mafuta, viwanda na na kadhalika, lakini kuifadhi wanyamapori wameachiwa Wizara hii tu wawe ndiyo wanashughulikia uhifadhi wa wanyama. Hata watumishi wengine wa Serikali, kama polisi na wanajeshi wanakuwa moja kati ya wawindaji wa wanyamapori kijangili.

Pili, wananchi katika baadhi ya maeneo huona kwamba wanyamapori si mali, bali ni hasara. Naomba elimu itolewe kwa wananchi ili wasaidie uhifadhi wa wanyamapori kwani hakuna wahifadhi muhimu zaidi ya wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia miradi ya wananchi inayofadhiliwa na mashirika ya umma. Napenda kutoa pongezi kwa mashirika yafuatayo *TANAPA, TWPF* na *NCAA.*

Mheshimiwa Spika, Mashirika haya wameonyesha ushirikiano mzuri sana na jamii, kwa sasa jamii wamefaidika sana na misaada waliopewa na mashirika haya. Kwa mfano *TANAPA* wamejenga shule nyingi nchini zahanati, barabara, miradi ya maji, nyumba za watumishi kadhalika *TWPF* nao wamefanya mengi katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, *NCAA* wametoa huduma kwa jamii ya wafugaji Ngorongoro na kutoa shilingi 700,000,000/= kila mwaka mbali na miradi ya afya, maji na barabara. Kwa pamoja napenda kutoa pongezi kwa mashirika hayo yote hongerni sana endeleeni kuwahudumia wananchi ili wanyamapori wafahamike kwamba ni maliasili muhimu.

Tatu, napenda kuzungumzia eneo lenye matatizo katika shirika hili au Wizara hii kuhusu vitalu vya uwindaji. Kuna migogoro kati ya wananchi na wawindaji hawa, wao n i wavunaji tu uhusiano na jamii siyo mzuri kabisa, naomba Wizara iangalie jambo hilo kwa umakini.

Naomba kuuliza *block* ya *TAWICO* kwa sasa ni ya nani na mwindaji aliyenunua toka Serikalini Bwana Mulla amelipa Serikalini malipo yote ya ununuzi wa *block* hiyo na kama hakulipa ni kwa nini? Mkataba wa malipo ya ununuzi wa Shirika hilo haikuwa na muda wa malipo?

Kwa kuwa shirika hili lina migogoro sana na wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya kitalu hiki, naomba maelezo kuhusu kitalu hiki kwani eneo lake lote liko kwenye jimbo langu. Wananchi wanakosa imani na kampuni hii na kuleta manung'uniko mengi kwamba wanalindwa na wakubwa jambo ambalo siyo kweli.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri majibu kuhusu swala la *TAWICO.*

**MHE. CELINA O. KOMBANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwako Mheshimiwa Waziri na Naibu wako pamoja na timu ya watendaji wako.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora, Mheshimiwa Waziri kuna baadhi ya watumishi wa Wizara yako ambao ni waaminifu sana. Watumishi hao huwa hawapokei rushwa wala kutoa rushwa, je, watumishi wa maliasili ambao wanakamata nyara za Serikali kama vile pembe za ndovu zenye thamani kubwa Wizara yako ina mpango gani wa kuwapa motisha wafanyakazi hao? Huoni kwamba ni wakati muafaka kupewa motisha kama askari wanaopewa *incentive* wakikamata jambazi? Je, utaratibu gani unafanywa ili kulinda usalama wao?

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaohamasishwa kando ya hifadhi za wanyamapori, hivi karibuni agizo lilitolewa na Wizara yako kuwahamisha wananchi waishio pembeni mwa mbuga/hifadhi za wanyamapori. Katika jimbo langu la Ulanga Mashariki wananchi wa kijiji cha Mbangayao, Kata ya Isongo ni mojawapo walioambiwa wahamie. Wananchi wao wamekaa kaltika kijiji hicho tangu zamani na sehemu hiyo ni barabarani (barabra ya Mahenge - Mwaya – Mbuga Selous) pia shule ya msingi na hduma mbalimbali zimeshawekwa katika kijiji hicho.

Mheshimiwa Spika, je, wananchi hawa watajibiwa? Je, sehemu watakayohamia miundombinu muhimu kama shule za msingi, zahanati, maji barabara na kadhalika Wizara itagharamia? Naomba niweke angalizo kwamba uhamisho huo ulifanyika haraka haraka bila kufanya tathmini.

Mheshimiwa Spika, vitalu vya uwindaji, Mheshimiwa Waziri kuna baadhi ya wanamiliki wa vitalu hawawathamini wananchi wanaoishi katika maeneo ya uwindaji, wengi wanajeuri kwa sababu wanapata vitalu toka *headquarter* (Wizarani). Lakini Mheshimiwa Waziri ieleweke kwamba mahusiano mazuri ni nguzo muhimu katika kuendeleza uwindaji. Nashauri wanaopewa vibali vya uwindaji wawaheshimu wananchi na watumishi na maliasili katika Halmashauri. Nashukuru watumishi wa Selous Ulanga wana mahusiano mazuri na wananchi na wafanyakazi wa Halmashauri.

Pia naomba asilimia ya uwindaji iongezwe kwa Halmashauri, fedha hizo zinasaidia sana kuongeza huduma za jamii kwa vijiji vinavyozunguka hifadhi za wanyama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itoe kipaumbele katika utangazaji wa vivutio vilivyo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, utalii ni biashara, kwa hiyo basi ni lazima tuwekeze kama njia nchi, mojawapo ni kuongeza uwezo wa *Tanzania Tourist Board (TTB)* kupanga na kuhudhuria maonyesho ya utalii ndani na nje ya nchi.

Pia kuwepo katika kila Ubalozi wetu wa nje, mtu akayetangaza utalii na apimwe uwezo wake kwa idadi ya watalii na biashara nyingine anazoingiza nchini kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuwe na sera na mikakati ya makusudi ya kuendeleza Watanzania katika sekta zote za utalii, maeneo ya kujenga hoteli kwenye mbuga zetu wapewe kipaumbele wazawa na maeneo ya uwindaji wapewe upendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pia kuwe na sera nzuri na endelevu hasa ndani ya idara ya wanyamapori. Idara hiyo ni ya kuangalia na kuondoa ukiritimba uliopo pale na kuleta mageuzi yanayoweza kusaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la kuangalia ni utaratibu wa maslahi ya Watanzania wanaoajiriwa na makampuni ya utalii. Wengi malipo yao ni kidogo sana niombe Wizara isimamie hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu maliasili na utalii.

Mheshimiwa Spika, pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, tatu naomba kuchangia maeneo yafuatayo, kwanza ni eneo la utalii. Kwa kuwa utalii unaipatia mapato makubwa Serikali, je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kujitangaza zaidi nje ya nchi kwa kuwa kuna vivutio vingi ambavyo watalii wengi wanaweza kuja kuona na hivyo kuongeza mapato ya Serikali yanayohusu utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira, kwa kuwa uharibifu wa mazingira unaendelea siku hadi siku pamoja na elimu inayoendelea kutolewa kila siku, je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kutunga sheria kali zaidi ili kudhibiti uharibifu wa mazingira ambayo inaweza kusababisha nchi yetu kugeuka kuwa jangwa, marekebisho ya sheria yaletwe Bungeni mapema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi, je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza watumishi wake kitaaluma na hasa waliopo katika Halmashauri za Wilaya hapa nchini kwa kuwapatia vitendea kazi vya kutosha, usafiri na kuboresha maslahi yao na hii itasaidia sana kuboresha utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa rasilimali na maliasili, misitu na wanyamapori vinaporwa na majangili, je, Wizara ina mpango/mkakati gani wa kuimarisha ulinzi ili rasilimali yetu isiporwe na kuhingizia Taifa hasara?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, *Inshallah* Mwenyezi Mungu aniwezeshe kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, utalii unasaidia sana uchumi wa nchi yetu. Pia unasababisha sana kuua utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wetu Watanzania unatoweka. Hii inatokana na Uhuru walopewa watalii wanapoing'oa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wetu Watanzania unakwenda katika nyanja tofauti. Kuna utamaduni wa mila ama dini. Hivi sasa utamaduni uliopo unatokana na wigo wa Watanzania kupitia utalii.

Mheshimiwa Spika, njia ya kwanza iliyopitisha ulevi haramu nchini petu ni utalii.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshuhudia watalii kuwa na maeneo yao ya kibiashara kama vile hoteli, Watanzania walio wengi hupata ajira katika hoteli hizo, lakini ni utumwa wanaoupata katika ajira hizo. Ni juzi tu Watanzania wenzetu walioajiriwa na hoteli ya kitalii walifanyiwa maovu hadi wakaamua kufanya mgomo.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Serikali ilione hili vinginevyo utalii utatuweka pabaya.

Mheshimiwa Spika, sasa niende katika wanyamapori. Wizara inafahamu fika wanyama wanahitaji maji. La kushangaza maeneo ya maji hayatoshi kukidhi wanyama wetu.

Mheshimiwa Spika, wanyama wanautofauti kimazingira nguvu. Wanyama wana lana hii ndio sababu tosha ya kuogopana. Inafaa Wizara ichukue hatua za kuweka maeneo ya maji katika maeneo yetu ya wanyama pori.

Mheshimiwa Spika, uwindaji, suala la kuwawinda wanyamapori sio mbaya, lakini lina hasara zake pale mwindaji amempiga mnyama silaha na bahati hakufa. Mnyama huyu atapata jeraha na hatimaye atakufa bure. Ni vyema sasa Wizara itafute mbinu ya kuhakikisha anapewa ruhusa awe wa asilimia kubwa ya kupata badala ya kukosa. Watu wasiruhusiwe kufanya mazoezi katika mapori yetu.

Mheshimiwa Spika, naitakia Wizara ya Maliasili na Utalii, ufanisi mwema.

**MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, samaki ni chakula chenye virutubisho muhimu mwilini *(protein).* Yapo maeneo mengi ambayo bado hayapati kitoweo cha samaki. Nashauri, idara ya uvuvi Wilayani zisikae kusubiri maswali na maombi toka kwa wananchi. Idara zihamasishe wananchi kujenga mabwawa na kuwapa vifaranga wa samaki. Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya za Kasulu na Kibondo zinahitaji utaalamu huo.

Mheshimiwa Spika, kuvamiwa kwa misitu ya asili kati ya Bukombe na Nyakanazi katika miaka ya 1969 hadi 1970, barabara ya Kahama mpaka Nyakanazi ilikuwa imepambwa na misitu ya asili. Hivi sasa misitu hiyo inaendelea kupungua kutokana na kuongezeka kwa wahamiaji ambao wanakata miti ya asili kwa shughuli zao mbalimbali. Je, kuna utaratibu wa kuhakikisha kuwa misitu hiyo niliyoitaja isitoweke?

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kuelekeza mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kanuni mpya ya uvunaji misitu, Serikali imechapisha kanuni mpya zinatoa mwongozo mpya wa uvunaji misitu na uchomaji mkaa kupitia tangazo namba 69/70 la Gazeti la Serikali toleo la tarehe 9 Juni, 2006.

Napenda kuishauri Wizara husika iwapatie nakala viongozi wa Serikali za vijiji vinavyozunguka maeneo ya misitu mikubwa, hifadhi za misitu na mashamba ya miti yanayosimamiwa na Serikali bila kusahau Halmashauri zetu za Wilaya. Mara nyingi

Halmashauri hazitoi nakala kwa viongozi wa vijiji na hivyo viongozi wa Serikali na hata Wizara kuifanya miongozo hiyo siri na kwa kutojua mwongozo wananchi au wafanyabiashara hutakiwa kutoa rushwa kwa utekelezaji wa huduma ambazo upo mwongozo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa mashamba ya miti pamoja na Serikali kugharamia kazi za utunzaji wa mashamba ya miti likiwemo shamba la mitiki la Lunguza, Amani Muheza, wananchi ndio wamekuwa walinzi wa mashamba hayo na wametumiwa hata katika kazi ya kuzima moto unapotokea ndani ya mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, vikundi vya wananchi hao wanapoomba wapewe ruhusa ya kuvuna miti iliyoanguka vibudu kwa nia ya kupata kipato kupunguza umaskini, maombi yao hayapewi uzito. Badala yake miti hiyo vibudu inaoza na kuliwa na mchwa badala ya kutumika kwa manufaa ya wananchi na kuwezesha Taifa kupata kipato.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara haioni haja ya kutathmini na kukubali maombi ya vikundi vya wananchi wanoishi kuzunguka maeneo ili kujipatia kipato na kama sehemu ya motisha ya ulinzi wanaoufanya?

Mheshimiwa Spika, uvunaji na uuzaji wa miti kutoka shamba la Lunguza, Serikali imekuwa ikitoa matangazo ya zabuni za kuuza miti kutoka shamba la Lunguza, je, utekelezaji wake umefikia wapi? Je, Serikali inasema nini kuhusu hoja mbalimbali za wananchi wa Wilaya ya Muheza kuhusu zabuni hiyo ya Serikali na kutoa nafasi kwa wazalendo kuvuna na kuuza miti ya shamba hilo?

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ya kuzingatia wakati wa uvunaji ili kuhakikisha kwamba maeneo hayo ya msitu yenye vyanzo vya maji havibaki wazi na kuathiri vyanzo vya maji na hivyo Serikali ina mkakati gani wa kupanda miti hiyo upya baada ya kuvunwa?

Mheshimiwa Spika, je, kuna utaratibu gani wa mgao wa mapato yanayotokana na mauzo ya miti kwa viwango gani kwa Serikali za vijiji na Halmashauri? Je, kwa mauzo ambayo tayari yamefanyika kutoka msitu wa Lunguza, vijiji na Serikali zao kwa miaka mitatu iliyopita mapato yametolewa vipi kwa kiasi gani kwa vijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza?

Mheshimiwa Spika, kuvuna miti iliyo kando kando ya barabara ya Lunguza hadi Kambai, licha ya kwamba miti ilivunwa miaka michache iliyopita kuondoa kivuli kando kando ya barabara hiyo bado giza limetanda na barabara haipati jua la kutosha kukausha ardhi ili barabarababa ipitike.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri miti zaidi ikatwe kuwezesha barabara hiyo kuonekana vizuri na hatimaye kutengenezwe ili iwahudumie wananchi wa vijiji vya Kambai na Segoma.

Mheshimiwa Spika, fidia kwa wananchi 1,128 wa hifadhi ya msitu wa Derema, Amani, Wizara ya Maliasili na Utalii mnamo tarehe 22 Julai, 2006 ilitoa ratiba kwa

wananchi wa vijiji vya Kisiwani, Kambai, Kwemdimu, *IBC*-Msasa na Kwezitu juu ya mpango wa kuwalipa fidia wananchi hao kwa awamu tatu kuanzia Julai, 2005 hadi Septemba, 2005. Ahadi hiyo ilitolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Mkuu wa Wilaya ya Muheza mbele ya Mbunge wao Herbert Mntangi wa Jimbo la Muheza. Awamu ya kwanza ya malipo ilifanyika mwezi Agosti, 2005 kwa wakati, wananchi wameshukuru awamu ya pili na awamu ya tatu hazikufanyika hadi Desemba, 2005, miezi minne nje ya ratiba.

Mheshimiwa Spika, fedha za awamu ya pili zilipokelewa katika akaunti maalumu Muheza mwezi Februari, 2006. Fedha hizo zimekaa hapo bila wananchi kulipwa licha ya wananchi na Taifa kuwa katika janga la njaa hadi Aprili, 2006. Inasikitisha sana, je, Wizara haikujua fedha zimekaa muda mrefu bila kulipwa?

Je, maombi ya mapendekezo ya wananchi kuhusu malipo ya fedha hizo wanachukua muda mrefu kiasi hicho kutolewa au ni kutojali shida za wananchi? Je, ni lini Serikali itamaliza kulipa fidia iliyobaki na kuwaomba radhi wananchi kwa ukimya unaoendelea kuchelewesha haki zao?

Mheshimiwa Spika, bei za fidia kwa mazao 26 Julai, 2005, bei zilizotolewa kufidia mazao ya wananchi zimelalamikiwa sana na wananchi kuwa ndogo sana. Mfano;

| **ZAO** | **MI** | **M2** | **S** | **DOS TShs/Mche** |
|---|---|---|---|---|
| Iliki | 2205 | 2000 | 100 | 3/= |
| Pilipili manga | 510 | - | 35 | 50(senti) |
| Mgomba | 1026 | 1015 | 70 | 1/= |
| Kahawa | 400 | - | 17 | 50 (senti) |
| Karafuu | 3600 | - | 450 | 3/= |

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Wilaya ya Muheza aliwaahidi wananchi kwamba Serikali itakuwa tayari kujadili malalamiko ya bei ndogo zilizotolewa. Je, ni lini Serikali itakaa na wananchi kujadili kero hiyo ya bei? Pamoja na hayo na imani kwamba Serikali inajali wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, pori la Moyowosi/ *Kigosi Game Reserve* lina ukubwa wa kilometa za mraba 21,430 (Moyowosi kilometa za mraba 11,800 na Kigosi kilometa za mraba 9,630).

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu pori hili limekuwa haliwapatii faida wananchi wanaoishi kwenye vijiji vinavyolizunguka kutokana na sababu zifuatazo: -

(i) Sheria zinazohusiana na misitu na mazao yake haziko wazi kwa wananchi;

(ii)Fedha zinazotolewa kwa vijiji vinavyozunguka Mbuga (Hifadhi) hazijulikani zinakokotolewaje hadi kufikia kila kijiji kupata shilingi 5,000/=;

(iii) Utaratibu mbovu wa wenye *plots* wa kuwaingilia wnanchi waliowekeza ndani ya hifadhi, kwa mfano warina asali, ufafanuliwe maana wananchi wanakamatwa ovyo. Tatizo siyo hilo tu, bali lipo tatizo la wenye *plots* wanawaajiri watu nje ya Wilaya inayomiliki pori. Hiyo ni kutokutenda haki kabisa; na

(iv) Hiyo asilimia 25 inayolipwa na Wizara kutokana na uwindaji wa kwenye hifadhi, imepitwa na wakati kwa sababu kinachopokelewa ni asilimia tu bila kujua kiasi cha fedha kilichopatikana kutokana na hifadhi. Hii ni dhuruma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Wizara kurekebisha hayo kwenye Mbuga inayohusika, bado inatakiwa kujikita katika mambo yafuatayo:-

(i) Kuwa na sheria inayoeleweka na usimamizi mzuri kuhusu hoteli zinazotakiwa ku-*promote* utalii, kuwatendea haki watumishi na malipo yanayostahili, tofauti na hivyo ni vurugu zinazotokea sasa kwenye hoteli ya kuwanyanyasa watumishi kama *Sea Cliff Hotel* ya Dar es Salaam.

(ii) Kwa makusudi mazuri kabisa ni vema Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizra ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kuwasaidia watu wanaohama hama lakini wanajishughulisha na kilimo. Wizara hizo ziweke utaratibu mzuri wa kuwasaidia hawa wananchi kuliko kuwaacha wakihangaika.

(iii) Kwa Wilaya kama ya Kibondo isiyo na Ziwa, wananchi wapewe msaada kuwezeshwa kwa ufugaji wa samaki kwa mambo yafuatayo, wapewe mafunzo ya kuchimba mabwawa, wapewe wataalamu wa kuwafunza ufugaji wa samaki na pia wapewe vifaranga vya samaki.

(iv) Kutokana na Wilaya kuwa na pori kubwa, wananchi wake ni warinaji wakubwa wa asali. Ili kuwasaidia wananchi hawa ni vema Wizara ikasimamia kutoa elimu ya ufugaji kwa wananchi, wananchi wapewe mizinga bora ya kufugia nyuki na pia wananchi wapewe vifaa vya kisasa vya kuhifadhia nyuki.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Wizara kutoa elimu ya upandaji miti kwa kushirikiana na Wizara ya Mazingira na hilo linaweza kufanikiwa kwa kuwatumia wanafunzi shuleni.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa asilimia mia moja. Aidha, nawapongeza kwa pamoja, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbozi ina maliasili lukuki na maeneo kadhaa ya vivutio wa utalii ikiwa ni pamoja na Kimondo cha Mbozi *(Mbozi Meteorite)* kilichoko

Mbozi Mashariki ambacho kwa hakika si pekee. Pia kuna Kimondo cha Ivuma ambacho kiko Mbozi Magharibi, Kata ya Ivuma.

Mheshimiwa Spika, vivutio hivyo vya utalii Jimboni Mbozi Magharibi, haviishii hapo kwani pia kuna nyayo za binadamu wa kale kwenye mwamba katika Kijiji cha Nkamgamo, kilometa 25 tu kutoka Mji wa Tunduma kuelekea Sumbawanga. Pia kuna maporomomko ya maji yajulikanayo kama Mpoma ya Mto Nyimahizi (Mtembwa) yaliyo mpakani mwa Kata za Myunga na Chitete. Vile vile kuna Mbuga ya Akiba ya Uwanda *(Uwanda Game Reserve)* yenye aina ya swala na ndege wasiopatikana sehemu nyingine popote duniani.

Mheshimiwa Spika, pia kuna chemichemi ya maji moto ambapo hupatikana aina ya viumbe pekee katika Kijiji cha Itumbula, Kata ya Ivuma. Vile vile kuna Ziwa Rukwa lenye kina kifupi kuliko yote duniani lakini lenye wanyama kama mamba na viboko pamoja na samaki wengi sana.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote niliyoyataja bado hayajabainishwa kwa umma wa Watanzania na Kimataifa, hivyo kutotambuliwa kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo hili pia kuna misitu asilia katika Kata za Ivuma, Chiluhumo, Chitete na Msagano yenye miti mbalimbali kama Mninga, Mninga Maji na Mpilipili. Kwa bahati mbaya sana japo misitu hii ni Misitu ya Akiba ya Taifa, sasa hivi kuna ukataji holela wa miti hiyo kwa ajili ya mbao. Mbao hizi ambazo husafirishwa usiku zinapasuliwa bila vibali vya Afisa Misitu Wilayani na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa Serikali na pia uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na uharibifu huu wa mazingira kwa *overgrazing* ya mifugo, ukataji miti na uchomaji moto, hivi sasa kuna tishio la kutoweka kabisa kwa swala wa mbunga ya akiba ya Uwanda iliyoko Kata za Kamsamba na Ivuma jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kufungua milango kwa utalii jimboni Mbozi Magharibi na kusimamia Hifadhi ya Maliasili jimboni humo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, narudia kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kunijalia kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Rais wa Awamu ya Nne kwa kuonyesha mfano bora wa uongozi kuliko awamu zilizopita. Nakupongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuongoza Bunge hili bila ubaguzi na kufanya haki sawa kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Pia nakupongeza kwa kuchapa kazi kwa viwango na *speed*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchagia kuhusu uvuvi. Serikali bado haijaweka mkakati madhubuti wa kuweza kuzuia uvuvi haramu wa kutumia nyavu ndogo au

mabomu kwa kuteketeza viumbe vidogo vidogo au kutumia baruti, wote ni mbaya sana kwa kuwa unaua matumbawe na viumbe vyote ambavyo ni maliasili yetu.

Je, sasa Serikali ina mkakati gani wa kuzuia hali hii isiendelee?

Mheshimiwa Spika, meli za kigeni zinatuibia tani kubwa za samaki wetu. Je, Serikali ina mkakati gani kuzuia wizi huu usiendelee kutupotezea mali yetu ya asili? Kwa nini Serikali iko kimya?

Mheshimiwa Spika, naomba sasa wavuvi wapewe ruzuku ili waweze kuwa na uvuvi wa kisasa ili wapate samaki wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanyamapori, naiomba Serikali iweze kuwazuia watalii wasipeleke wanyama wetu nje kwa kuzuia maliasili yetu kupungua kwa kasi kwa sababu hata Watanzania wenyewe wanachangia kufanya hivyo kwani ni biashara yao lakini sisi tunapoteza.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie utalii, umuhimu wa utalii kwa Taifa na wananchi wake ni jambo zuri sana lenye kuliingizia Taifa pato. Lakini penye uzuri na ubaya upo. Athari zake ni kupoteza utamaduni wetu na vijana huiga mambo ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, kutunza maliasili ni kuhifadhi misitu kwani misitu huleta mvua , misitu ndio uhai wa wanyama, ndege na binadamu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia ufugaji wa nyuki. Ufugaji wa nyuki ni mojawapo ya ajira . Kwa hiyo, Serikali iweke kipaumbele kwa suala la ufugaji wa nyuki ili kuondoa tatizo la umaskini.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake nzuri na naunga mkono hoja.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na awali ya yote, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Pili, napenda ktuoa pongezi na hongera kwa Wizara hii hasa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Anthony Diallo pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye Wizara hii nyeti. Pia nisisahau Katibu Mkuu wa Wizara hii na watumishi wote wa Idara mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unajielekeza moja kwa moja kwenye Hifadhi ya Bahari au Ziwa. Katika maeneo ya Maziwa Wizara hii inapata mchango mkubwa sana hasa kukuza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo haya ni sawa na Hifadhi za Taifa ambako kuna taratibu za uwindaji, hivyo taratibu hizo ziainishwe kwenye bahari na maziwa.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya zilizoko karibu na hifadhi hizi za Taifa zinapata mapato, hivyo tunaomba maeneo yaliyo kandokando ya Ziwa Victoria ambayo

minofu mingi ya samaki inatoka hapo, kwa mantiki hiyo utaratibu ufanyike wa kuwapa asilimia kama maeneo mengine ya hifadhi za Taifa zenye uwindaji.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ninakotoka kuna misitu mitatu na misitu hii ya Geita, Baraza la Madiwani lililazimika kuyafanya maeneo haya kuwa malisho ya ng'ombe na kilikuwa chanzo. Misitu hiyo ni kama ifutavyo, Msitu wa Geita, Msitu wa Ruanda na Msitu wa Miyenze.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iruhusu wafugaji wetu waendelee kupata ruhusa ya kupata malisho. Wizara kama itashirikiana, basi iruhusu kuingiza wanyamapori katika misitu hii na hifadhi hizi zikabidhiwe kwa wananchi. Pia kuwepo utaratibu wa kutuletea wataalam wa ufugaji nyuki katika misitu hii ili kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, najua kabisa kama mafunzo yatatolewa Wilayani Geita, nina uhakika yatakubalika na kupokelewa na wananchi kwa mikono miwili ili kuweza kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uvunaji wa magogo, naipongeza sana Serikali kwa kuzuia ukataji wa magogo. Lakini kuna wananchi waliopata vibali kwa njia halali na Serikali ikatoa kwa nia ya kuwasaidia wazalendo hawa ambao waliowengi wamechukua mikopo kwenye mabenki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeishafanya uchunguzi wa kina na kupata magogo yenye makosa na kuyapiga mnada. Hiyo adhabu inatosha kabisa. Hivyo naiomba Serikali iruhusu magogo yaliyo halali yasafirishwe ili wananchi hawa waweze kulipa mikopo yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namwomba Waziri atoe kibali cha kupata eneo ukiwa unatoka Geita kwenda Mwanza, upande wa kulia kutokea Magogoni hadi Buhalahala na kutoka Buhalahala hadi Kasamwa, kuna eneo ambalo ni dogo sana la hifadhi, naliomba ligawiwe kwenye Serikali za Vijiji vya Buhalahala na Kasamwa. Naunga mkono hoja.

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na kutuwezesha kuingia katika Bunge lako Tukufu, sasa kwa heshima kubwa naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Rais wa Serikali ya Mapanduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa ushindi mkubwa walioupata katika Uchaguzi Mkuu uliopita. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushindi walioupata na kuwa leo ni Wabunge kamili wa kuwawakilisha wananchi wa majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuchangia maeneo yafuatayo katika Wizara hii. Kwanza naipongeza Wizara hii kwa juhudi zake za kufanya ulinzi mzuri wa uvuvi haramu unaofanyika kwenye Bahari na Maziwa yetu.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoamini kwamba Mgodi wetu wa pili kwa sisi Watanzania ni Bahari na Maziwa tuliyonayo. Mwenyezi Mungu ametupa utajiri mkubwa wa mali za ndani ya Bahari na Maziwa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara sasa itumie nguvu zake katika suala la uvuvi kwa kupata meli za uvuvi na kupata viwanda ili kusafirisha minofu ya samaki.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili ni kuimarisha zile kumbukumbu zetu za mambo ya kale kama vile historia za Bagamoyo, Livingstone, *Zanzibar Slave Trade,* Ujiji kule Kigoma na mengineyo kwa kuimarisha uchumi kiutalii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uwindaji haramu wa mapori na mbuga zetu, naipongeza Wizara katika juhudi zake za ulinzi mzuri wa wanyamapori wetu, lakini, nashauri juhudi zichukuliwe zaidi kwani wawindaji hao haramu wanatumalizia wanyama wetu wengi ovyo ovyo hasa wanyama wengi wazuri na adimu wanapotezwa.

Mheshimiwa Spika, Mbuga zetu nyingi ni nzuri na ni kivutio kwa utalii, lakini uharibifu mkubwa wa mazingira udhibitiwe na hasa ule wa uchomaji moto ovyo.

Mheshimiwa Spika, walinzi wa wanyamapori watunzwe vizuri na wapate mafunzo na elimu nzuri kulingana na hali ya wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini, tunaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Anthony Diallo, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Pamba, pamoja na Wakurugenzi wote, Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Maliasili na Utalii kwa matayarisho ya hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongea viongozi, Waziri na Naibu Waziri ambao kwa kipindi kifupi wameweza kuielewa Wizara hii na kuchukua hatua za kuridhisha kurekebisha mambo pale walipoona kuna kasoro na kuleta maelekezo mazuri

Kitaifa kiasi cha kutoa imani kwetu sote kwamba Wizara sasa iko katika mchakato wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu napenda kuzungumzia zaidi sekta ya utalii ambayo ni sekta inayokua upesi sana. Kwa bahati, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira ambapo katika semina yetu tulielezwa kuwa utalii sasa unaongoza baada ya sekta ya kilimo katika kutuletea fedha za kigeni. Mpaka mwisho wa mwaka jana utalii uliingizia nchi kiasi cha dola za Kimarekani milioni 746 na hivyo kuwa ya pili baada ya kilimo na madini yaliingiza kiasi cha dola za Kimarekani milioni 400.

Mheshimiwa Spika, utalii pia unachangia asilimia 16 ya Pato la Taifa yaani *Gross Domestic Product (GDP)*. Hii ni sekta ambayo inaajiri watu wengi zaidi kwa maana hiyo utalii ni muhimu sana katika utekelezaji wa mpango wa MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya utandawazi, sekta ya utalii iko katika ushindani mkubwa Kimataifa kwani soko letu ni moja. Mataifa yanayojishughulisha na utalii hayana budi kutangaza sana *(promotion and marketing)* vivutio vyao katika soko hilo huria la Ulaya, Marekani na Asia ili kushawishi watalii kutembelea nchi zao na hivyo kuwaletea fedha toka huko kwao. Kazi hii hufanywa na Serikali au mawakala wa nchi husika, matokeo yake ni kupata watalii wengi kutokana na kampeni hizo. Kampeni hizi huwa katika maonyesho mbali mbali ya Utalii *(Tourist Trade Fairs)*, kutumia Balozi zao na makongamano ya Kimataifa.

Ni dhahiri kuwa gharama kubwa zinatumika duniani ili kushawishi watalii. Nitatoa mifano, Serikali ya Afrika Kusini inatumia shilingi bilioni 50 kwa mwaka kutangaza vivutio vyake, Namibia, wanatumia shilingi bilioni 14 kwa mwaka, Mauritius inatumia shilingi bilioni 12 kwa mwaka, wenzetu Wakenya wanatumia shilingi bilioni 10 kwa mwaka wakati Tanzania bajeti yake ya utalii ni kati ya shilingi bilioni 1.2 hadi 1.5 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya utalii ya nchi yetu haikidhi hata kidogo kiwango cha kutangaza vivutio vyetu na kwa namna nyingine ni kichekesho katika ushindani wa Kimataifa. Kadri tunavyofanya hivi ni wazi tunajidhoofisha wenyewe na tunajipuinguzia mapato ya fedha za kigeni bwerere.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii walitueleza kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na kwa namna nyingine tunaiaibisha nchi katika maonyesho makubwa ambapo wenzetu wanakuwa na mabanda makubwa, wakati sisi tunaonyesha katika kameza kadogo tu.

Mheshimiwa Spika, Bodi inahitaji shilingi bilioni 5 hadi 6 kwa mwaka ili kuweza kushinda na wenzetu kidogo.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Bodi ya Utalii ya shilingi ……. kwa mwaka huu bado ni ndogo sana. Ningependa Serikali iangalie upya suala hili ili walau mpaka mwisho wa mwaka zipatikane shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuendesha sekta hii.

Naamini zipo njia mbalimbali zinazoweza kutumiwa ili kupata fedha. Kuna msemo wa kiswahili usemao, ukitaka kupata pesa, lazima utumie pesa. Napendekeza tutumie pesa zaidi ili nchi iweze kupata fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ila naiomba Serikali iwekee maanani mawazo haya niliyotoa kwa ajili ya kuendeleza utalii Tanzania.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote tangu Uhuru Tanzania bado hatujafaidika ipasavyo kutokana na vivutio kemkem vya utalii tulivyonavyo nchi nzima. Tunachokipata kutokana na utalii ni kidogo mno kulinganisha na rasilimali tele tuliyonayo. Hali hii imesababishwa na udhaifu mkubwa na wa muda mrefu tulionao katika kuendeleza na kutangaza utalii. Nitatoa mifano michache tu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nguvu zetu zote tumezielekeza nje ya nchi kwa imani potofu kuwa mtalii ni mzungu, mchina, mjapani na kadhalika. Utalii wa ndani hatujaupa kipaumbele kabisa. Hivyo basi, hali ya hatari ikitokea nje ya nchi, kama vile mashambulizi ya ugaidi ya tarehe 11 Septemba, 2001 nchini Marekani, pato letu kutokana na utalii linaathirika vile vile.

Aidha nchi kubwa kama Marekani na Uingereza zimekuwa na tabia ya kutoa taarifa ziitwazo *advisories* kuelezea hali ya usalama wa nchi zetu kwa kutumia vigezo vyao. Matokeo yake ni wananchi wao kuacha kuja Tanzania na hivyo kuathiri vibaya pato letu kutokana na utalii. Njia pekee ya kuepukana na hali hiyo ya wasiwasi ni kukuza na kuendeleza utalii wa ndani. Kenya wameanza siku nyingi kidogo na wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Hatuna budi kufanya hivyo na sisi. Hatujachelewa sana ikiwa nia na ari stahili tunayo.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kusikia kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi 15 za Afrika zilizoteuliwa kunufaika na mradi wa *STEP initiative* ambao utayahusu maeneo mengi ya Kusini kama vile Kyela, Ileje na Rungwe. Licha ya kukosa miundombinu, tayari eneo la Matema Wilayani Kyela linavutia mamia ya watalii toka Ujerumani, Marekani, Uingereza na Afrika ya Kusini. Ni eneo lenye fukwe nzuri kando kando ya Ziwa Nyasa na lenye wasanii wa kijadi wa ufinyanzi wa vyungu na vyombo vingine vya ndani. Barabara ya Kyela hadi Matema ya kilometa 40 tu inahitaji kujengwa kwa kiwango cha lami kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi ili kuleta mapinduzi ya utalii Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta mapinduzi katika sekta hii upo umuhimu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukaa chini na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili uendelezaji na utangazaji wa utalii nje ya nchi usifanywe kiholela na kuwachanganya watalii licha ya kwamba suala la biashara ya nje ni la Muungano, utangazaji wa utalii nje ya nchi hufanywa kwa ushindani usio na tija kwa Taifa baina ya Serikali ya Muungano na Zanzibar. Wakati vyombo vya utalii vya Serikali ya Muungano kama vile *TANAPA* na *TTB* vinainadi Tanzania yote pamoja na Zanzibar vyombo vya

utalii vya Zanzibar kama vile Bodi ya Utalii ya Zanzibar vinanadi Zanzibar tu na vinahakikisha haviitaji Tanzania kabisa licha ya kwamba utaratibu huu unaibebesha Serikali mzigo wa gharama usio na sababu kwa kuwa na vyombo vingi vinavyofanyakazi hiyo hiyo, tunawachanganya watalii.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge, kwa hotuba nzuri, yeye pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Zabein Mhita, Mbunge. Pia nawapongeza wasaidizi wa Waziri wakiongozwa na Katibu Mkuu ndugu Salehe Pamba. Nachukua nafasi hii kumpa pole ndugu Pamba kwa msiba uliomfika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba nzuri napenda kutoa ushauri wangu kwa Serikali ili ifanye mambo kadhaa muhimu. Kwanza ni juu ya migogoro ya siku nyingi kati ya *TANAPA* na wananchi walio jirani na hifadhi za Taifa na pili ni kuhusu kuangamia kwa mti au mmea uitwao Msandali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro katika jimbo langu la Babati Vijijini, napenda nitaje maeneo yenyewe.

(i) Mgogoro kati ya kijiji cha Moyamayoka, Kata ya Magara na *Manyara National Park (TANAPA).*

(ii) Mgogoro kati ya Kijiji cha Gijedabung Kata ya Mamie na *Tarangire National Park.*

(iii) Mgogoro kati ya vijiji vya Ayamango na Gedamara, Kata ya Galapo na *Tarangire National Park*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na migogoro hiyo hapo juu kuna mgogoro unaohusu uanzishwaji wa *WMA* katika vijiji vya Kata ya Nkaiti.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni ukosefu wa ushirikishwaji na uelimishaji wa wananchi wa maeneo hayo. Naomba sasa Serikali ichukue katua za dhati kumalizia migogoro hii kiutawala na kiungozi.

Mheshimiwa Spika, suala la mti wa Msandali mti huu umepigwa marufuku kuvunwa, lakini katika jimbo langu bado unazidi kuangamia. Malori/magari yanazidi kuusomba kupeleka nje ya nchi. Serikali ichukue hatua za dhati kuukoa Msandali. Naunga mkono hoja hii, ahsante.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa hoja yao ya Makadirio ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Katika ukurasa 16 wa kitabu cha hotuba, *paragraph* ya pili ya kifungu cha 27 kuhusu uvuvi wa kibiashara wa kamba na samaki. Uvuvi wa maeneo ya bahari kuu si

suala la Muungano. Ibara ya 2(1) ya Katiba inaonesha tu eneo la Jamhuri ya Muungano ambalo linajumuisha eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Visiwani ambalo limeainishwa katika ibara ya 2(1) ya Katiba ya Zanzibar ambayo inaingiza bahari iliyovizunguka visiwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo sheria inayotaka kuanzishwa kwa Mamlaka ya Bahari Kuu itakuwa na matatizo. Ni kwa nini huwa na uchu wa kuongeza mambo katika orodha ya huu Muungano bila ya kwanza kufanya utafiti na kuondoa matatizo yaliyopo. Maoni yangu na ushauri wangu hapa ni kuwa sheria hii isiharakishwe kuletwa Bungeni ila kwanza matatizo hayo yatatuliwe.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa huo huo na kwa misingi niliyoilezea hapo juu, ni nini msimamo wa Serikali katika suala zima la *EEZ* kwa Tanzania Bara na *EEZ* kwa Tanzania Visiwani na ni wapi penye mgao wa bahari ya ndani, kwa madhumuni ya uvuvi yaani *equidistant mark* baina ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani?

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa 34 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuna suala zima la wizi wa samaki na kuhujumu bahari kuu ya Tanzania, hatuna ulinzi wa kutosha. Hata hivyo ningependa kujua ni meli ngapi zilizokamatwa ambazo zinavua bila ya kibali rasmi? Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho kimepatikana kutokana na faini kutokana na meli hizo?

Mheshimiwa Spika, je, Waziri haoni kwamba kuna haja ya kuwa na ndege au boti za ulinzi wa maeneo hayo kusaidia mitambo hiyo ya kompyuta?

Mheshimiwa Spika, kasi zetu za kutangaza utalii ni ndogo sana, watalii wanaoingia Tanzania ni kidogo sana hasa ukilinganisha na nchi za jirani kama vile Kenya. Wasiwasi wangu ni kwamba haraka zetu hizi za kufanya Jamuiya ya Mashariki inaweza pia ikatugharimu sana katika sekta hii. Sasa naomba kujua ni hatua gani madhubuti ambazo Wizara imeandaa ili kulikabili suala hili? Sambamba na hili ni kuwa utalii wa Tanzania tumeulenga zaidi. Kwa eneo moja tu ambalo ndilo tunalolipa kipaumbele wakati maeneo mengine mengi yapo ambayo miundombinu yao ni mibovu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalotaka kulichangia ni suala la samaki wa baharini. Bahari yetu ni kubwa na bado ni *semi vergin* ya kwamba haijashambuliwa sana kwa kuvuliwa. Lakini bado hakuna motisha kubwa kwa wavuvi wetu, vyombo vyao ni duni na hawana zana za kutosha.

Mheshimiwa Spika, motisha kama zile za kuwepo kwa bandari za uvuvi, viwanda hata vidogo vidogo vya kutengenezea samaki ni muhimu kuwepo katika bandari zetu. Naamini tukijitahidi kuyaboresha hayo, nafikiria yanaweza kusaidia sana katika kuwaendeleza wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni hayo machache naomba tena kumshukuru Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nimeomba kuchangia kwa maelezo pengine katika Wizara hii muhimu. Muda wa siku moja kwa Wizara hii muda huo hautoshi, ni vyema kwa siku zijazo muda huu ukaongezwa.

Mheshimiwa Spika, katika nchi hii kuna tatizo kubwa la ardhi, ni migogoro kati ya wakulima na wafugaji lakini Mpanda ni tofauti migogoro ni baina ya wananchi na wanyama kwa maana ya hifadhi ya wanyama na misitu. Nchi hii imepitia katika hatua nyingi za utawala katika kipindi cha miaka 40 ya Uhuru wetu. Serikali ni ile ile lakini mifumo ya utawala imekuwa ya majaribio kila wakati, tumepata kuwa na *native authorities* zikaondolewa, madaraka mikoani ikafutwa na sasa Halmashauri za Wilaya leo kuna Serikali nne katika Serikali moja, Serikali Kuu kila moja matunda inavyoona inafaa na wakati fulani chama kushika hatamu.

Mheshimiwa Spika, katika mabadiliko haya yapo maamuzi ambayo yalisukumwa na hoja za kisiasa na bila kuzingatia sheria watu wakaanza kujenga na kuishi katika mapori ya akiba *(Forest Reserves).*

Mheshimiwa Spika, leo unapoamua vinginevyo Serikali ile ile iliyoruhusu leo inawaondosha wananchi hao na kusababisha malalamiko toka kwa wananchi. Suala la kuhifadhi misitu ni la lazima na hakuna njia nyingine, lakini wananchi hao kama tutawaondosha bila fidia tutakuwa hatujawatendea haki kwa sababu wakati wanavamia misitu hiyo Serikali ilikuwepo na haikuchukua hatua ya kuzuia kwa sababu ambazo pengine zilikuwa zinachangia kuboresha hali ya kisiasa kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, hilo ni tatizo moja, tatizo la pili ni maeneo ya wazi ya kuwindia kitoweo kwa wananchi pia gharama kama zilivyotangazwa rejea *Government Notice No. 224* zimepanda mno na sijui vigezo vilivyotumika. Kama kupandisha gharama ni njia ya kuhifadhi wanyama kwa sababu wananchi wengi hawatakuwa na uwezo mimi napenda kutahadharisha kupandisha gharama za leseni ni kichochea cha kuwepo ujangili.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kupandisha gharama ipo katika uvunaji wa misitu ni vyema tukaangalia matokeo ya hatua hiyo, uvunaji holela umeendelea, miti imekatwa na Serikali haikupata mapato kwa kiwango cha ukataji wa miti ulivyofanyika baada ya kuongeza gharama za uvunaji. Wanaangalia wamefaidika vipi na maliasili hizi, wageni wamekuwa wakiwinda katika mapori ya Wialya ya Mpanda, Urambo na Sikonge kwa uchache ambao tunachangia mapori hayo zaidi ya vizawadi vidogo wanavyopewa vijiji vichache hivi, sasa ni lazima tuangalie mapato yatokanayo na uwindaji huo urudishwe katika maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu idadi ya watumishi hususan Wilaya ya Mpanda haitoshelezi, ni vyema kuangalia Ikama na eneo la kazi. Idara ya wanyamapori ikama ni watumishi 20, inayo 12 kwa mapori ya Wilaya ya Mpanda haitoshelezi, kadhalika watumishi wa idara ya misitu. Pamoja na mkakati wa kutumia *Village Game Scouts* tatizo liko vile vile, askari wa vijiji hawana vyombo vya doria kwa silaha, tunajidanganya katika eneo hili ni vyema likafanyika utafiti wa kutosha wa kurekebisha kasoro hizi na utendaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo na Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, pamoja na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko kadhaa kuhusu unyanyaswaji wa watumishi katika mahoteli ya kitalii hasa watumishi wanawake, pamoja na mishahara duni kwa watumishi hao. Baya zaidi ni kuwa wanalipwa mishahara iliyo chini ya kiwango cha kima cha chini cha kisheria. Nashauri suala hili lifuatiliwe kwa karibu kwani linasababisha wananchi kuwa wanyonge katika nchi zao.

Aidha, suala la kuajiriwa wageni kufanya kazi hotelini ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania lazima lipigwe vita sana. Wakati Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ameahidi kuwapatia kazi wananchi walaukazi/ajira 1,000,000. Juhudi zake zisirudishwe nyuma kwa kuwapatia kazi wageni kazi ambazo zinawezesha kufanywa na wananchi wetu. Nashauri Wizara hii ishirikiane na Wizara ya kazi kukabili tatizo hili. Haiwezekani *cashier* na wapishi watoke nje.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 31 wa hotuba ya Waziri anazungumzia biashara ya mazao ya nyuki kupata msukuma mpya na dhamira ya kusambaza miongozo ya ubora wa mazao ya nyuki. Napenda kuijulisha Wizara kuwa katika Jimbo langu Singida Kusini katika Wilaya ya Singida Vijijini wananchi wanajihusisha na ufugaji nyuki, hasa kata ya Mwaru na Kata ya Minyughe. Nashauri itembelee maeneo hayo na wapelekwe watalaam Mwatu na Minyughe kubaini au kutambua eneo hilo kuwa linashughulika na ufugaji nyuki na hivyo wapatiwe mafunzo na mbinu mpya za ufugaji nyuki pamoja na nyenzo za kisasa za ufugaji nyuki. Aidha watafutiwe masoko ya asali wanayoivuna.

Mheshimiwa Spika, nashauri na kuiomba Wizara isaidie Manispaa ya Singida kupata wafadhili wa kujnega hoteli za kitalii Mjini Singida hasa katika eneo la kando kando ya Ziwa Kindai ambapo pana mandhari nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake wa Wizara hii nyeti na muhimu katika kuchangia Pato la Taifa kwa juhudi wanazozichukua ili kuona kuwa mchango wa Wizara hii katika Taifa inaoana na mikakati ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie machache katika sekta ya misitu, wanyamapori na uvuvi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, misitu ni uhai, pasipo misitu mwanadamu na viumbe hai sidhani kama vingekuwepo. Maeneo ambayo yana uchache wa misitu hata mfumo mzima wa maisha katika maeneo hayo una matatizo. Faida za misitu hazina kikomo na itakuwa ni uongo kama nitasema kuwa zote nazifahamu, lakini baadhi tu ya faida hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokana na misitu tunapata mbao kwa maana ya kujengea/kuundia vitu mbalimbali ni kutengeneza samani *(furniture).*

(ii) Misitu huchangia kuwepo kwa mvua katika maeneo hayo.

(iii) Dawa za kutibu magonjwa mbalimbali zinazotokana na mazao ya misitu.

(iv) Misitu inahifadhi viumbe/wanyama.

(v) Misitu hufanya mandhari kuwa ya kuvutia na kuleta hali ya hewa nzuri.

(vi) Misitu huzuia mmomonyoko wa ardhi na kuhifadhi maji ardhini kwa wingi.

(vii) Wanyama na binadamu wanafaidika na matunda yatokanayo na misitu.

(viii) Binadamu hujipatia kuni na kutengeneza vito kutokana na mazao ya misitu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara hii kwa hatua za makusudi inazozichukua za kuzuia uharibifu wa misitu yetu, hatua ya kufuta uvunaji na uletaji wa magogo yanayosafirishwa kwenda nchi za nje ni ya kupongezwa. Serikali isirudi nyuma na uamuzi huo na mwingine ambao utakuwa ni wa manufaa katika kuhifadhi misitu yetu na bila kufanya uamuzi huo, nchi yetu itageuka kuwa jangwa.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua tu ni vipi Wizara au Serikali imeweka utaratibu wa kutumia mazao yatokanayo na misitu yetu hasa mbao hapa nchini. Baada ya kuzuia ukataji na uvunaji wa magogo hayo, bei ya mbao imekuwa ni ya juu sana na hata upatikanaji wake umekuwa ni mgumu sana. Wananchi wanalalamika sana kuhusu hilo, naomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri. Suala la mzungu mmoja kumilikishwa eneo kubwa la hifadhi ya wanyamapori nalo linazungumzwa sana na vyombo vya habari, Waziri anasemaje kuhusu hili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanyamapori, kumekuwa na utaratibu wa kuwauza wanyamapori wetu na kuwasafirisha nje ya nchi yetu. Kwa maoni yangu utaratibu huu uangaliwe upya na ikiwezekana usiwepo kwani ni kuwadhalilisha wanyama hao na pia ni maliasili tuliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, uvuvi nchi yetu pia imejaliwa maliasili ya samaki kwenye maziwa, mito na bahari lakini mali hiyo haitumiki vilivyo. Wizara ifanye mikakati ya

makusudi ya kwanza kuwawezesha wavuvi wazalendo kwa kuwapa nyezo za uvuvi kwa njia ya mikopo na hata kuwatafutia soko la samaki hao.

Mheshimiwa Spika, kuwapo kwa kiwanda cha kusindika samaki angalau kimoja kimoja katika maeneo ya maziwa na mikoa ya mwambao wa bahari ya Hindi kutawapatia wavuvi wetu uhakika wa soko la kuwauza samaki wao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaitakia kile la kheri Wizara hii katika utekelezaji wa programu zake.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Anthony Diallo, Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo imetolewa asubuhi ya leo. Ni kwa msingi huo naunga mkono hoja hii. Naahidi nitashirikiana na Wizara ili kuona kuwa malengo waliyojiwekea yanatekelezwa.

Naomba kuikumbushia Wizara kuhusu ombi la wananchi wa Siha, Kijiji cha Mese kwa kusaidiwa kuvuta umeme kupitia *TANAPA,* ili kuzuia uharibifu katika msitu wa asili unaotokana na uvunaji wa kuni kwa ajili ya kupikia. Kupitia swali langu, wakati Mheshimiwa Zakia Meghji akiwa Waziri wa Wizara hii alionyesha kuwa Wizara ingekuwa tayari kusaidia gharama za upelekaji wa umeme katika eneo hilo. Naomba kukumbushia ombi hilo kama tulivyoongea ofisini na Mheshimiwa Anthony Diallo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii inaliingizia Taifa pato kubwa sana kiasi cha 47%. Lakini Wizara hii haijapewa kipaumbele cha kutosha. Kwa mfano, miundombinu inayoelekea kwenye vivutio vya utalii ni mibovu sana. Hii imefanya watalii wengi washindwe kufika huko. Kwa mfano, Mlima Kilimanjaro umekuwa ukitangazwa kuwa uko Kenya na hivyo nchi hiyo kupata mapato zaidi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, barabara ni mbovu sana lakini pia utangazaji wa vivutio umekuwa ni tatizo sugu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi yetu kuwa na vivutio vingi sana vya utalii, bado havijaboreshwa na vingine havipo kwenye ramani ya nchi. Tunaomba Wizara ijitahidi kuboresha vivutio hivyo.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi zilizoendelea zimewekeza katika utalii kwa mfano, Switzerland, Afrika Kusini, Italia, France na kadhalika lakini pia nchi zinazoendelea kwa kasi sasa kama Thailand, Philippines na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwekeze zaidi katika sekta hii ili iweze kuongeza Pato la Taifa na hivyo kuleta maendeleo kwa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa/sugu kwa wafanyakazi katika sekta ya hoteli. Hoteli nyingi zimekuwa zikifanya ubaguzi kwa wafanyakazi hasa Watanzania. Mishahara imekuwa midogo sana na pia kufanya kazi katika mazingira magumu. Lakini pia wale *hoteliers* hawapandishwi vyeo kwa wakati. Kwa kuwa *hotels* za kitalii zimekuwa zikikumbwa na migogoro mingi ya kikazi kwa mfano ni juzi tu hoteli ya *Sea Cliff* ilikuwa na mgomo. Lakini pia zile kazi kubwa zimechukuliwa na wageni wakati kazi ndogo ndogo kama ufagizi, kutandika vitanda zimechukuliwa na wazawa.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona hifadhi za wanyama kama Gombe, Selous na Msisi hazijaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, wanyama wamekuwa wakigongwa sana katika hifadhi za wanyama. Kwa mfano ni mara nyingi wanyama wamekuwa wakigongwa katika hifadhi ya Mikumi ambayo barabara ya Morogoro/Iringa hupita. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi ni la muhimu sana hasa katika kuboresha maisha ya mvuvi kwani hili ndilo shamba lake na njia pekee ya kumpatia kipato.

Mheshimiwa Spika, samaki huingiza fedha nyingi nchini lakini cha ajabu mazingira ya wavuvi ni mabaya sana. Serikali iboreshe hali zao kwa kuwapatia vifaa vya kisasa vya uvuvi. Nashukuru sana.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia hadi kupata fursa hii na hata kuweza kuchangia mjadala uliopo mbele yetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii ikiwa ni bajeti ya kipindi cha mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia nimpongeze Waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Anthony Diallo na dada yangu Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa kazi nzuri na usimamizi mzuri kwa watendaji kwa kuandaa bajeti ya mwaka huu kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa na mimi nichukue fursa hii nitoe mchango wangu katika kuboresha bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara iyaainishe bayana maeneo maalum ya utalii na kuyapa kipaumbele, maeneo muhimu kama yale ya Pango la Amboni, Tanga, Ziwa Kitangili lenye vivutio vingi wakiwemo ndege wa kila aina ambao ndege hao wanafaa kwa maonyesho ya watalii wajao nchini mwetu, maeneo ya kale kwa makabila mbalimbali uanzishwe utaratibu maalum wa kuyahuisha maeneo hayo ili yatumike kama maeneo ya utalii.

(a) Mikakati ya uhifadhi Maliasili uainishe wa mamlaka za maliasili, zifanye kazi katika kulinda maliasili ipasavyo;

(b) Utunzaji wa miti na hata uhifadhi wa vyanzo vya maji upewe kipaumbele na hata jamii kuelimishwa umuhimu wa utunzaji wa miti na vyanzo vya maji;

(c) Wananchi wahamasishwe juu ya matumizi ya nishati mbadala ili kuokoa, mazingira (misitu) yetu, kuhifadhi mazingira kwa hifadhi ya misitu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wanyamapori na vivutio vingine vyote vilivyo ardhini kama vile vitu mbalimbali vyenye thamani vitunzwe na udhibiti uwe wa Kitaifa kwa kuzingatia maslahi ya kila eneo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, jimbo la Kalambo lina vivutio vingi ambavyo havijaendelezwa.

(1) Maporomoko ya Mto Kalambo;

(2) Maji moto Kizombwe Matai;

(3) Magofu ya ngome ya Wajerumani Kasanga Bismark;

(4) Msitu katika bonde la Lwanji linalosadikiwa lina Sokwe ni karibu na Ziwa Tanganyika eneo la Nyimba, Tarafa ya Kasanga. Wapo Wajapani wamekuwa wakifuatilia mienendo za sokwe hao; na

(5) Mapango ya kale maeneo ya Tatanda na eneo alilopumzika Livingstone.

Je, Wizara hii haina mpango wowote wa kuboresha hata eneo moja kwa ajili ya maeneo yote haya? Tunaomba mtuweke nasi katika ramani ya utalii kwa kutuboreshea maeneo machache tufaidi urithi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na tano.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri hasa ikizingatiwa kuwa ni hotuba yake ya kwanza. Nampongeza pia Naibu Waziri, wote hawa nawafahamu vizuri, ni wachapakazi wazuri. Lakini, pia naomba niwapongeze Wakurugenzi wote chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, sekta ya Utalii ni chagizo katika kuongeza Pato la Taifa, hivyo nawaomba sana, Serikali inawategemea sana na tunawategemea katika kuinua uchumi wa nchi yetu. Sekta ya Utalii haiwezi kukua na kujulikana bila kutangazwa, bado utalii wetu haujatangazwa vya kutosha, Balozi zetu zitumike kuutangaza utalii wetu nje, lakini pia tutumie ndege zinazotua hapa kwetu angalau huko wanapokwenda waweze

kututangazia utalii wetu, Bodi ya Utalii ifanye kazi ya kuutangaza utalii kwa bidii kama wanavyofanya wenzetu wa Kenya.

Mheshimiwa Spika, lakini je, ni lini hii tabia ya jirani zetu kuutangaza Mlima Kilimanjaro kuwa ni Mlima wao itaisha? Naomba nijibiwe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua nini hatma ya Sanane kulichopo Mwanza? Kuhusu kumbukumbu, je, Serikali kwa nini isichukue eneo la Kisesa linalojulikana kama Bujora linalomilikiwa na Kanisa Katoliki kwani eneo hili lina kumbukumbu nyingi za Kisukuma?

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri na naunga mkono hoja.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa kazi ngumu na nzuri wanayofanya ya kuendeleza utalii na kulinda maliasili ikiwa ni pamoja na kutumia maliasili zetu kwa mtazamo endelevu *(Sustainable Utilisation of Natural Resources).*

Mheshimiwa Spika, katika jimbo la Nkenge kuna vivutio vya utalii ambavyo naomba Wizara ivitangaze ili kuweza kuvutia watalii wa ndani na wa nje. Vivutio vilivyopo ni pamoja na Mapango yenye michoro na historia ya mambo ya Kale katika Kata Bwanjai, Msitu wa asili wa Minziro wenye vipepeo na wanyama wanaopatikana katika ule msitu peke yake duniani.

Mheshimiwa Spika, mabaki ya Kambi ya Wajerumani katika Kata ya Minziro, mabaki ya alama mbalimbali zinazoonesha kumbukumbu ya vita kati ya Tanzania na Uganda, msitu wa Kantare wenye aina ya nyoka pekee duniani na chimbuko la mibuni.

Mheshimiwa Spika, mbali na utalii wa kutembelea mbuga za wanyama, aina nyingine ya utalii ni *Cultural Tourism*. Mkoa wa Kagera una vivutio vingi vya *Cultural Tourism.* Naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuendeleza *Cultural Tourism* katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri kwa hotuba nzuri ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu ya Tanzania ina vivutio vingi vya utalii na Serikali inapata fedha nyingi katika Utalii kutokana na maliasili ya bahari mikoko kuna uharibifu mkubwa wa rasilimali hii ambayo inaharibu mazingira. Serikali iwashirikishe kikamilifu.

Naomba Serikali iangalie magofu ya Bagamoyo, Mji huu una historia kubwa katika nchi hii. Naomba Wizara unieleweshe kwa ufafanuzi kuhusu jumba ambalo

lilikuwa likitumika kama Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Bomani, jumba hili lina haiba yake na mvuto mkubwa kwa watalii. Sasa hivi haliishi mtu wala kutumika na limeanza kubomoka. Je, Serikali ina mpango gani wa kulikarabati? Naomba liangaliwe jengo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napongeza kwa dhati hotuba nzuri ya Waziri wa Maliasili na Utaliii na kazi nzuri zinazofanywa na Wizara hiyo.

Kuhusu upungufu wa wataalam katika sekta hii muhimu napenda kukufahamisha ya kwamba Chuo Kikuu cha Sokoine kinatoa wahitimu wa *BSC - Forestry, BSC - Wildlife Management, BSC - Environmental Sciences and Management* na *BSC - Agriculture*

Mheshimiwa Spika, aidha, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinaanzisha Shahada ya *BSC Hotel Management and Tourism.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania nacho imeanzisha Shahada ya *BSC Hotel Management and Tourism.*

Mheshimiwa Spika, natoa taarifa hii ili Wizara ianzishe mipango yake kuwapata wataalam, na kuona kama kina ulazima wa kuanzisha vyuo vingine kwa makusudi hayohayo.

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri kwa hoja aliyoitoa ya Maliasili na Utalii kwa mikakati iliyowekwa ili kuendeleza Wizara hiyo, hongera sana kwa maana hiyo, mimi naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa nichangie masuala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi haramu na utalii Kusini. Kwanza nianze na suala la uvuvi haramu Kusini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwapo na uvuvi wa kutumia sumu, mabomu na nyavu ambazo zinaharibu watoto wa samaki kwa kuvuliwa na kutupwa ovyo. Uvuvi huu umeshamiri katika bahari ya Hindi kwa upande wa Tanzania katika maeneo yaTanga, Dar es Salaam, Mafia, Kilwa, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kumekuwapo na uvuvi wa kutumia sumu, mabonu na nyavu ambazo zinaharibu watoto wa samaki kwa kuvuliwa na kutupwa hovyo. Uvuvi huu umeshamiri katika bahari ya Hindi kwa upande wa Tanzania katika maeneo yaTanga, Dar es Salaam, Mafia, Kilwa, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, uvuvi huu umeleta madhara makubwa sana kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kuharibu mazingra kwa vipi, naomba nichambue hivi, kijamii, uvuvi wa kutumia baruti na sumu huleta vifo, majeruhi, ulemavu wa binadamu.

Kiuchumi, kumekuwepo na upungufu wa samaki ndani ya Bahari ya Hindi kwa vile hata samaki wadogo wanauawa, kiutamaduni. Kwa siku za usoni kuna hatari ya kukosa samaki kabisa katika mwambao wa Bahari ya Tanzania na kimazingira, masalia ya samaki yanaharibiwa au yameharibiwa, hivyo kuifanya bahari yetu kukosa samaki kuzaliana na hivyo kuwa na upungufu wa samaki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kushughulikia kukomesha uvuvi haramu, lakini bado uvuvi huu unaendelea, nitoe mfano wa Mtwara na Lindi jinsi walivyoshughulikia Kimkoa, Kiwilaya na wananchi.

Kwanza Kitaifa, walipopita tarehe 3 Aprili, 1998 hadi 18 Aprili, 1998 baada ya hapo wavuvi hao waliendelea kufanya uvuvi haramu. Mkoa walipofanya *operation* pamoja na Wilaya tarehe 20 Aprili, 1998 hadi tarehe 10 Mei, 1998 bado waliendelea kufanya uvuvi haramu. Kampeni za *NGO* na wananchi wenyewe zinafanyika za kuzuia uvuvi haramu lakini bado wanaendelea.

Mheshimiwa Spika, ushahidi umepatikana kwa Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Mtwara kwa kuwakamata wavuvi 300 na vifaa kadhaa kama ifuatavyo:-

(i) Unga aina ya *Amonium Nitrate* kilo 202, *Magnum Blast Explosive* kilo 113, Tambi za kuwashia Baruti 36 na kadhalika. Vijiji vilivyohusika katika uvuvi huo mkoani Lindi na Mtwara ni Mtwara katika vijiji vya Msanga Mkuu, Ng'wale, Nalingu, Sinde, Mgao, Mkungu, Naumbu, Namgogoli, Tangazo, Mahurunga, Chuno, Shangani, Ufukoni, Kiyanga, Mbuo na Mikindani.

Mheshimiwa Spika, huo ni ushahidi tosha kuwa uvuvi huo haramu upo na majina yao katika kila kijiji yanafahamika.

Katika Mkoa wa Lindi Vijiji vifuatavyo vilihusika ambavyo ni vijiji vya Kijiweni, Mchinga, Mbanja, Kikwetu, Lindi Mjini, Tulieni, Kitumbikwela, Kilwa na Njia Nne. Kwa hiyo, huo ndio ushahidi wa uvuvi haramu na mimi nasema na kushauri kuwa wavuvi hawa lazima wafanyiwe mambo haya mawili.

Kwanza wavuvi hawa wapewe zana mbadala, badala ya kutumia mabomu na sumu, Serikali iwasaidie kuwapa nyavu sahihi na zana sahihi ili wasirudie tena kutumia vitu vya haramu.

Pili, kwa makusudi kabisa Serikali iweke *Speed Boat* hasa Mtwara na Lindi. Serikali iliahidi kufanya hivyo kwa mikoa hiyo lakini hadi sasa haijaleta kwa hiyo, tunaomba Serikali isaidie *Speed Boat* kwa ajili ya ulinzi. Wizara ya Maliasili na Utalii waungane na Wizara ya Mazingira wakae meza moja waweze kulitatua hili.

Mheshimiwa Spika, nije sasa kuhusu suala la Utalii. Kusini ni muhimu sana na vile vile watalii wanapenda kuja Kusini kwa sababu ni kwamba watalii sasa wanapenda kubadilisha vitu vya kuona, kwa maana sasa watalii wamechoka kuona wanyama na Mlima Kilimanjaro tu wanataka sasa kuona jamii na shughuli za kijamii kama kuona wakulima wa korosho, wakulima wa ufuta, mapori, maeneo ya Vita vya Majimaji, magofu ya Kilwa, mapango ya mawe na magofu ya Waarabu, Bahari nyeupe ya Lindi na Boko wengi waishio pamoja Kilwa na uwindaji vile vile mjusi , kwa hiyo nashauri kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ipanue wigo wake sasa wa utalii kwa kuelekeza utalii Kusini Lindi, Mtwara na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, tusaidie Kusini jamani katika kijiji cha Kilwa wanafika zaidi ya watalii 300 kwa siku, lakini wanakuja wenyewe tu wala hawajaandaliwa kimazingra yao ya kuishi kama watalii. Wengine wanakuja kuona alipozaliwa mjusi *Dinossars,* Lindi. Andaeni mazingira ya Kusini kwa ajili ya utalii, watalii wapo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara hii walioshiriki kwa njia moja au nyingine kuiandaa hotuba hii. Ni hotuba nzuri inayoonyesha matumaini endelevu ya uhai wa nchi, ardhi na Taifa letu. Hongera sana.

Napenda nitoe mchango wangu katika maeneo kadhaa, uendelezaji na utangazaji utalii. Mazingira ya Kwimba ni kame, haina pori wala misitu, iko mbali na ziwa na haina mito. Kwa ujumla ni sehemu ya nchi isiyo na vivutio vya wazi vya kitalii. Je, Wizara hii inayatambua maeneo kama haya ya Kwimba na ina mipango ipi ya kuyasaidia ili nayo yanufaike kutokana na mapato ya Wizara hii? Ni kwa namna gani Wizara hii inaweza kuyasaidia maeneo hayo yashiriki katika kuendeleza harakati za Wizara hii?

Mheshimiwa Spika, siyo mbaya maeneo kama haya yakafikiwa yakapigwa picha ili yakawa vielelezo vya uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za binadamu. Miaka ya 1960 hivi maeneo ya Tarafa ya Mwamashimba yalikuwa na misitu, mapori na wanyama wengi kama Simba, Tembo, Swala, Paa na kadhalika, leo huoni wanyama hawa. Itakuwaje miaka ijayo na je, itakuwaje miaka 100 ijayo? Picha hizo kama zitakuwa zinapigwa na kuhifadhiwa kwa kufanyia ulinganisho, somo tosha kwa umuhimu wa Hifadhi ya Raslimali ya Mazingira. Napongeza sana kazi iliyoanza kuafanywa na Wizara hii.

Ombi langu ni kuwa kwa vile wananchi wetu hawana utamaduni wa kusoma na kwa kuwa wananchi wetu hawana Redio na Televisheni na walivyonavyo hawavitumii, ninaomba mambo mawili, kwanza kuitumia sana Idara ya Maendeleo ya Jamii katika kutoa elimu ya kuhifadhi ya raslimali yetu na pili, Wizara ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili ianishe mambo muhimu kadhaa yawe katika mihutasari ya shule zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utafiti, napongeza sana Wizara kupanga taasisi ya tafiti wa misitu kufanya tafiti kuhusu hifadhi ya vyanzo vya maji kwa matumizi endelevu na kuweka muhimu katika miti ya asili.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu miti ya asili kimsingi ni miti inayokubalika katika maeneo hayo. Hata hivyo sambamba na kuweka umuhimu katika miti ya asili ni vyema tafiti ikabainisha umuhimu wa miti/ mimea hiyo kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Kufanya hivyo itamotisha wananchi kupanda na kuhifadhi miti hiyo wakijua faida zake. Ninashauri vile vile kijitabu kichapishwe kuonyesha aina ya mti unakopatikana hapa nchini na faida zake.

Naamini kufanya hivyo kutakuwa na faida kadhaa, wananchi kuifikia mimea hiyo kwa urahisi, kuwasaidia watafiti wengine kuifikia na kuendeleza utafiri kuhusiana na miti/mime hiyo na kuwezesha uendelevu wa miti hiyo kabla haijapotea.

Mheshimiwa Spika, nashauri watafiti wa Wizara hii wawe karibu sana na waganga wa kienyeji hasa kwa nia mbili wakiwa ni wadau wakubwa wanaweza kusaidia katika kutambua matumizi ya miti wakiwa ni wadau wanaweza kuwa msaada mkubwa sana katika kulinda na kuhifadhi mimea/miti hii.

Mwisho nashauri maeneo kama ya Kwimba niliyaelezea hapo mwanzo, yasaidiwe katika upandaji wa miti hasa miti ya asili inayopatikana katika maeneo hayo. Miti migeni ipandwe kwa uangalifu mkubwa sana ili isije ikasababisha madhara kwenye maeneo hayo. Naunga mkono hoja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge ninayetokea maeneo ya Pwani (Matemwe, Zanzibar) naelewa Wizara hii siyo ya Muungano, lakini kwa vile mwelekeo wa awamu ya nne ya kuona tunajielekeza zaidi na umoja kama Watanzania nimeshawishika kuleta suala hili mbele yako, kwa faida si ya Jimbo langu, bali kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, hapana shaka utalii unaleta fedha nyingi Kitaifa lakini matatizo makubwa yanayojitokeza katika maeneo ya utalii nayo ni makubwa vile vile. Mfano, silka na utamaduni wetu unapotea kutokana na vivazi na mwenendo wa watalii wanapotembelea mitaani, siyo siri wanakwenda nusu uchi katika maeneo yetu kule unawakuta wanachanganyika mno na watoto wadogo na vijana, hakuna aibu wanakumbatiana hakuna junaha wanafika hadi hata vijana kujisahau kama wako Afrika na utamaduni wetu, maeneo haya vijana wanakatisha kwenda shule mapema sana wanajiunga na kazi ambazo kwa mtazamo wangu kwa mimi wao haziwasaidii ama matembezi kutembeza watalii na kujishughulisha na mapishi au kutafuta makombe au vinyago kwa biashara na kadhalika. Hali ambayo kwa wazee wa kimaskini anaona mwanaye ndiyo ajira hiyo lakini hasara inayopatikana ni kwa huyu kijana kwa maisha yake ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, nazingira yanachafuka hali nzima ya mitaa inabadilika na kusema kweli hata heshima zao (watoto) zinaondoka.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo ya wafugaji kuna utaratibu wa kuwajengea mazingira watoto wao na kuhakikisha kuwa wanapatiwa elimu ili wasiwe wakosefu wa maisha ya baadaye, kwenye madini kunatolewa mirahaba, je, katika maeneo ya utalii yakiwa kama maeneo ya wafugaji au ya madini kwa maana yanachangia pato kubwa kwa Taifa. Je, maeneo yote ya utalii nayo mtayafikiriaje hasa kwa watoto?

Naomba suala hili litazamwe sana kwani baadaye nchi hii itafika wakati itagawanyika sana kimaadili, kiuchumi na kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kama hayo yatazingatiwa na ahsante sana.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:-** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia upande wa utalii.

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe unaojengwa Mbeya unatarajiwa kuibua vyanzo vingi vya mapato kiuchumi na kijamii. Wilaya karibu zote mkoani Mbeya zina vivutio vingi vya utalii ambavyo vikifufuliwa na kuendelezwa vinaweza vikaliingizia Taifa hili kwa kiasi kikubwa pato kiuchimi. Kwa mfano, Wilayani Chunya kuna vivutio kama vile milima, wanyamapori, fukwe kwenye Ziwa Rukwa, Mapango yenye historia kubwa tangu karne ya 15. Je, Wizara inaweza kuchukua hatua za makusudi kuendeleza vivutio hivyo ili watalii wapate fursa ya kuyatembelea?

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Wanyamapori hasa askari wa *TANAPA* wamekuwa wakilalamikiwa sana kutokana na ukatili wao wanapowakamata watu/wananchi kwa makosa madogo madogo na p engine wakati wananchi wanapoonekana kwenye hifadhi. Askari hao huwafunga kamba watuhumiwa na kuwaburuza vijijini bila huruma, naishauri Wizara ya Maliasili na Utalii ikemee na kuchukua hatua zipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika hifadhi ya mbuga za wanyamapori ya Lukwati Wilayani Chunya yapo maeoeo ya wazi *(open areas)* ambayo hayamilikiwa. Je, endapo wazalendo wataomba kumiliki baadhi ya maeneo hayo kama *hunting blocks* ni utaratibu upi unaotakiwa kufuatwa?

Mheshimiwa Spika, watumishi walioko kwenye hifadhi ya ziwa Rukwa hasa mabwana samaki na mabwana nyuki hakuna hata mmojawao aliye na chombo cha usafiri. Wizara inaweza kuwasaidia watumishi hao ili watende kazi zao kwa ufanisi?

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kutoa na kuandaa hotuba nzuri ya Makadirio ya bajeti kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu ziende kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mazingira, ikiongozwa na Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kuishauri Wizara hii ili pawepo na ufanisi mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nichangie hasa kwenye bajeti hii nikilenga jimbo/Wilaya ya Bukombe. Kwa kuwa Wilaya ya Bukombe inao wafugaji wa nyuki ambao Mungu kawajalia kupata asali na nta kwa wingi, tatizo ni ukosefu wa soko rasmi la zao hili.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isiandae utaratibu ambao unaweza kuwapa nafuu wafugaji hawa ya kupata soko? Naomba Wizara inichukue na kunieleza wapi asali na nta itauzwa kwa kuwa bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, katika suala la wafugaji wa nyuki ningependa kujua ni tatizo gani ambalo limezuia kuweka/kufungua ofisi ya wanyamapori Wilayani Bukombe?

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu kuu mbili kwanza upatikanaji wa vibali vya kuingia kuvuna asali, wananchi hulazimika kufuata kibali Kahama umbali wa kilometa 100 kwenda mara mbili.

Mheshimiwa Spika, unafikiri hali hii utatufikisha kwenye kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania, wakati anafuata kibali pengine mhusika asiwepo ofisini kesho tena arudi au alale pale pale. Pili, Bukombe ndiyo inayomiliki eneo kubwa la hifadhi ya Kigosi/Myowosi.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee msitu mkubwa ambamo linapita barabara la kwenda nchi jirani za Burundi, Rwanda na Uganda. Kwa kuwa upo msitu upande mmoja ni hifadhi ya Kigosi/Myowosi na ule wa Halmashauri.

Je, Serikali inaweza kuruhusu eneo la upande wa Kigosi/Myowosi pajengwe kituo kidogo cha Idara ya Wanyamapori kandokando na barabara hili ili kuondoa ujambazi unaosababisha wananchi kupoteza mali na uhai wao.

Mheshimiwa Spika, nichangie suala la watafiti wanaofanya ndani ya hifadhi ya Kigosi/Myowosi. Kwa kuwa baadhi ya watafiti hawa tulikutana nao wakakiri kwamba kweli ndani ya maeneo hayo zimo dhahabu nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isiliangalie kwa makini kujua faida tuipatayo sasa na kuwaruhusu/kukaribisha wawekezaji wachimbe kwa kufungua mgodi rasmi ndani ya eneo hilo. Naamini kama tutafungua mgodi humo tutakuwa tumeanzisha ajira nyingi sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niombe niongelee suala zima la uhifadhi wa maliasili zetu hasa misitu kwa kuwa Wilaya ya Bukombe tumezungukwa na misitu, napenda kuiomba Wizara itupatie gari idara ya misitu il waweze kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika,  inangawaje si taarifa rasmi nilizonazo, nilikia Bukombe tulitakiwa tupate gari cha kushangaza hadi leo hii hatujui gani hiko liko wapi, Mkoani au Wizarani. Naomba sana watendaji wangu wapatiwe gari.

Mheshimiwa Spika,  mwisho Wilaya yetu bado ina ujenzi wa shule za msingi na sekondari, madarasa yote haya yanahitaji samani kama vile madawati, viti, meza na kadhalika. Naomba Wizara wanieleze haya madarasa tutapata wapi mbao za kutengeneza samani hizi.

Je, haiwezekani kuandaliwa utaratibu wa kupata mbao hizi angalau kwa kibali maalum ili upauaji, madawati, viti, meza na kadhalika visije vikakwama na hatimaye kuzorotesha elimu Wilayani Bukombe na Mkoani Shinyanga kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii.  Ahsante.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimwia Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Maliasili na Utalii. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwenye maeneo machache. Utalii, katika Mkoa wa Kilimanjaro, Mji wa Moshi kuna msitu unaitwa Msitu wa Njoro.

Mheshimiwa Spika, misitu hii ni wa maliasili lakini kuna watu ambao wamegeuza msitu ule kuwa kichaka cha majambazi na kuna baadhi ya *tour operator* ambao wanatunza watalii  kuingia katika msitu ule. Je, Serikali inapata faida gani na msitu ule?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka *tour operator* kuhusu usalama wa watalii wakati wakitoa *output* usiku kuelekea/kutoka *airport*. Ningeshauri Wizara ya Maliasili na Utalii au Wizara ya Usalama wa Raia washirikiane, waangalie ni jinsi gani wanaweza kushugulikia tatizo hili sababu umeandikwa mpaka kwenye *internet* nchi yetu imekuwa siyo salama na hii inaweza kutupunguzia utalii.

Mheshimiwa Spika, kupandisha bei za *camping fee Kilimanjaro,* kupandisha bei sio tatizo lakini bei zikipandishwa *tour operator* waarifiwe mapema *at least  one year* kabla. Unakuta *tour operator* ameshauza kwa mwaka 2006/2007 bei inapanda ghafla.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi bei zinapanda kwa dola 10 kwa siku *camping fees* kuanzia Julai 1, 2007. Inakuwa vigumu kurudi kwa watalii walio-*book* tangu mwaka jana sasa hivi umwambie aongeze dola 60 zaidi, inakuwa ni vigumu sana, ningeshauri kama bei inatolewa unapata zaidi, basi *notice* itolewe mwaka mzima kabla ili *tour operators* wawatumie wateja wao bei kamili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ada ya *forest fees,* kuna kodi inatozwa na afisa misitu kwa njia za Londorossi, Umbwe hii *fees* ilizungumziwa katika Bunge lililopita la bajeti na Serikali ikasema ingelishughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, wageni/*tour operator* wanalipa *park fees, camping fees, forest fees* ni kwa nini yote isiwe chini ya *KINAPA?*

Mheshimiwa Spika, kuna afisa misitu wanakaa pale Umbwe bila vitabu vya *receipt* lakini wanatoza *forest fee,* je, Serikali inaweza kutueleza ni kiasi gani kimeshapatikana cha *forest fees?*

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanyamapori, napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kuwa muwazi na kutetea mali ya nchi yetu kwa kuweza kumdhibiti Mkurugenzi wa Wanyamapori lakini cha kusikitisha mpaka leo Serikali au anayehusika bado wanamtilia kifua na yupo kazini.

Mheshimiwa Spika, katika utawala bora, je, huyu Mkurugenzi ataweza kumheshimu bosi wake na atamsikiliza?

Mheshimiwa Spika, hii itapelekea hata wale wenyewe wasiwe na heshima za kazi katika Wizara hii. Tunaomba Serikali itamke ni jinsi gani itatatua suala hili ambalo limezungumziwa na kila Mbunge wakati wa kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikiliangalia hili, itatuletea heshima kwa Taifa letu kwa ujumla na dunia ambayo inayasikia haya na kuyasoma. Naomba kuwasilisha.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Ila ni tatizo moja la wafugaji wa Geita. Wilaya ya Geita ina idadi kubwa ya watu na maeneo yamebanana sana. Migodi mikubwa nayo imechukua maeneo na inasababisha uharibifu wa mazingira. Wafugaji maeneo yao yalichukuliwa na wakulima na wachimbaji ikabidi wakimbilie misituni (Hifadhi) kutokana na tangazo la Serikali wametolewa huko na hawana pa kwenda, matokeo ni vita kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wafugaji wa Geita wakiwa porini hawakati miti na ni walinzi wazuri wa misitu si ni vema wakaruhusiwa kuchungia huko kwani hawa madhara yoyote.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wafugaji hawa wamekuwa watoto yatima na wanaona kuwa Serikali haiwataki. Mimi naomba sana suala la wafugaji linahitaji kuangaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba taasisi zote za Serikali zilazimishwe kuotesha misitu yao. Inawezekana Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira zishirikiane, tuige mfano wa Kenya. Taasisi hizo ni Shule, Magereza, Majeshi, Polisi na kadhalika. Walazimishwe, asiyetaka aache cheo kama ni mkubwa.

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Mheshimiwa Spika, ningependa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake nzuri ya Makadirio ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kuchangia katika sekta ya uvuvi na utalii. Kwanza ni kuhusu uvuvi. Uvuvi hasa mikoa ya Kusini upo nyuma sana na kwamba wavuvi wanatumia nyenzo zile zile za kizamani. Mikoa ya Lindi na Mtwara tunaomba isaidiwe katika kupata zana za kisasa za uvuvi hasa boti na mashine zake. Mpaka hivi sasa mikoa hiyo haina boti hata moja na wavuvi wanatumia mitumbwi ambayo inahatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, wavuvi hawa hulazimika kwenda katika bahari kuu kwani sehemu za karibu zimetengwa kwa ajili ya hifadhi *(Marine Parks).*

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana kiwanda cha kutengeneza boti na vioo vya barafu vitengenezwe kwani toka viwanda hivyo viharibike miaka kadhaa iliyopita havijatengenezwa. Naomba sana viwanda hivyo vipatiwe vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa wa 16 chini ya kichwa kisemacho matumizi endelevu ya rasilimali, naona kuna habari isemayo ukanda wa Pwani kuna wavuvi 29,754 wanaotumia vyombo 7,190. Hivyo vyombo ni vya aina gani? Vyombo vilivyopo katika mikoa ya Kusini havifai kabisa. Hakuna mvuvi hata mmoja katika mikoa ya Kusini ambaye anamiliki boti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utalii, naomba mkoa wa Mtwara nao upewe nafasi ya kuchangia Pato la Taifa katika sekta hii ya utalii. Ningeomba Serikali ichukue hatua madhubuti ya kuanzisha biashara ya utalii katika mkoa huu. Mkoa una fukwe safi za kuvutia, *Marine Parks* hifadhi za wanyamapori. Kuna miundombinu ambayo itasaidia katika biashara hii. Kuna uwanja wa ndege ambao ndege yoyote ya abiria yaweza kutua, bandari bora kuliko bandari yoyote hapa nchini, umeme wa gesi ambao hivi karibuni utaanza kazi. Hivyo Mheshimiwa Waziri, naomba sana tupatiwe fursa ya kuchangia Pato la Taifa katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya makadirio haya kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Hongera nyingi kwa hotuba nzuri inayokidhi matumaini ya Wabunge wengi pamoja na wananchi. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo.

Hoja ya kwanza ni kuhusu Hifadhi ya Taifa ya Selous ina vivutio vingi sana na ni kubwa ya aina yake. Kuna wanyama wengi na mabwawa makubwa yanayotumika kama mazalio ya samaki na samaki wengi sana.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa ya miundombinu kwa mfano, barabara ya kupeleka watalii huko Selous. Aidha, wananchi wanashindwa kusafiri katika vijiji vilivyo njiani kuelekea *Selous Game Reserve*. Hakuna simu ya mkononi na minara haitoshi.

Mheshimiwa Spika ombi, naomba sana Wizara ikubali kwamba Selous kwa mfano, Hifadhi ya Selous inaweza kuingizia pato kubwa la Taifa kama tukiamua kulifanyia maendeleo kwa mfano, kupata barabara nzuri, minara ya simu za mkononi, hoteli na kuongeza juhudi ya kuitangaza hifadhi ya Selous duniani ili tuinue pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuna chemichemi ya maji moto mjini Utete Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji. Tunaomba Wizara isaidie kutangaza chemichemi hii ya maji moto. Maji hayo ni *medicinal* kwa magonjwa ya aina nyingi ya ngozi.

Hoja pili ni kuhusu kule Selous kuna mabwawa yenye samaki wengi wakubwa lakini askari wa hifadhi hiyo wana matatizo makubwa. Wananchi hawana proteini lakini Mungu kawapa Warufiji samaki wengi. Huko nyuma Wizara iliruhusu uvuvi kwa awamu katika ziwa hili kwa miezi miwili kisha hufugwa bwawa hilo na wananchi wakapewa kibali cha kuvua bwawa lingine. Hii Mheshimiwa Waziri ni uvuvi endelevu. Aidha, askari hawa huwapiga risasi wananchi badala ya kuwakamata na kuwapeleka polisi. Tunaomba Wizara irudishe mpango ule ule wa zamani wa kutoa vibali vya kuvua kwa awamu katika mabwawa yaliyomo katika hifadhi ya Selous.

Mheshimiwa Spika, aidha, askari wa hifadhi wafanye kazi kwa uadilifu. Nakushukuru kwa kupokea mchango wangu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia hoja hii, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake makini yenye umuhimu wa pekee kiuchumi katika nchi yetu.

Kwanza napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu sera inayotawala uwezekano wa kuongezwa au kupunguzwa eneo lililotengwa kama Hifadhi. Kwa mfano idadi ya watu katika vijiji vinavyopakana na *Mikumi National Park* vya Kata ya Mikumi yenyewe, Kata ya Ruhembe na Kata ya Ridodi imeongezeka sana tangu mwaka 1975. Matokeo yake wananchi wanahitaji eneo kubwa zaidi la kuendesha shughuli za kilimo ambazo ndiyo chimbuko la maisha bora kwa wananchi waishio vijijini.

Mheshimiwa Spika, imewahi kuruhusiwa wanyama kuwindwa na kuuawa wanapoongezeka katika hifadhi, lakini huwezi kuwapungza binadamu katika eneo fulani wanapoongezeka kuliko uwezo wa eneo walilopangiwa kuishi kutokana na kupakana na *National Park.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kulichunguza tatizo hili la haja ya mipaka ya *Mikumi National Park* inayopakana na vijiji katika Kata ya nilizozitaja ili wananchi wapate maeneo ya kutekeleza mipango ya Serikali ya MKUKUTA na MKURABITA?

Mheshimiwa Spika, naamini mipaka ikisogezwa kidogo itawahamasisha wananchi hao kuona Serikali yao inawajali na hivyo wataepuka kuharibu au kuhujumu hifadhi na zaidi ya yote watakuwa walinzi wazuri wa mipaka ya hifadhi kutokana na mahusiano mema baina yao na hifadhi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, la pili ni taarifa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwamba uzoefu umeonyesha kuwa mara nyingi askari wa *Mikumi National Park* wanawabambikia kesi wananchi, wanavijiji wanapakana na hifadhi, pale ambapo wao askari wanaponaswa na wanavijiji wakihujumu au wakivunja sheria ndani ya *park* wanayoilinda.

Mheshimiwa Spika, hali hii imejenga mahusiano mabaya baina ya askari wa *park* na wanavijiji *adverse relationship.* Kwa mfano, hivi sasa iko kesi katika mahakama ya Wilaya ya Kilosa ambayo ilianzia kituo kidogo cha polisi cha Ruhembe kesi hiyo ilikuwa inawatuhumu askari wa *Mikumi National Park* waliochoma miwa ya wanavijiji wa kijiji cha Ruhembe na moto huo ukavuka na kuanza kuunguza msitu wa *park.*

Mheshimiwa Spika, askari hao walioshuhudiwa na vijana na wanavijiji walipotajwa polisi kuwa ndio walioshitaki ndiyo watuhumiwa eti walikuwa wakichoma mkaa kambo ambalo ni la uongo.

Mheshimiwa Spika, hali hii imesababisha kinyongo kikubwa na hasira nyingi za wanavijiji dhidi ya askari wa *park* na taasisi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, hasira zimewazidi wanavijiji hasa baada ya vijana hao wasio na hatia kupelekwa rumande mjini Kilosa, pasipo na hatia.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kulifuatilia na kulipatia ufumbuzi suala hili na napenda kushauri suala zima litatuliwe nje ya mahakama hasa kwa kuwa hata eneo tajwa walipotuhumiwa vijana wanavijiji liko nje ya mpaka wa *Mikumi National Park.*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho katika mchango wangu ni la zoezi la kuainisha mipaka kati ya *Mikumi National Park* na vijiji/mji mdogo wa Mikumi nilivyovitaja awali.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Maliasili na Utalii washirikiane na Waziri wa Ardhi, kuirejea kwa pamoja *Government Notice No. 121* ya 13 Juni, 1975 inayoelekeza mipaka ya *National Park* imepangwa au imeanzia wapi na kuelekea wapi kuanzia barabara ya Mikumi - Iringa kwenye jiwe la kilometa 115. Mpaka huo uliowekwa kwenye miaka ya 1975 ndio tumike kuona au ku-*assess* vijiji vya Lumango, Ruhembe, Matambiko, Kodogobasi na Kitete viwekewe mipaka sehemu gani katika kupanua eneo la wananchi kupata eneo la kulima. Jambo hili likifanyika litaondoa tatizo la ardhi kwa wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumpa pole sana Waziri wa Maliasili na Utalii kumpoteza Katibu Mkuu wake na Mungu aiweke roho yake peponi.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja na kumtakia Mheshimiwa Waziri wa Maliasili utekelezaji wenye ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nami naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pongezi zangu kwa hawa wafuatao, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa, Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali wa Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Samuel Sitta, Spika na Mheshimiwa Anne Makinda, Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Wenyeviti wa Bunge, Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechaguliwa na wananchi kutoka katika Majimbo, Viti Maalum na ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru pia wapiga kura wangu wa Jimbo la Kondoa Kaskazini kwa kunipa imani kubwa. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kushika wadhifa huu. Naomba nimhakikishie kwamba nitatekeleza wajibu wangu kwa nguvu na uwezo wangu wote.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nimshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa msaada anaonipa na uongozi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu naomba nami nichangie hoja iliyo mbele yetu kwa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba, wachangiaji walikuwa ni wengi na sitaweza kujibu hoja zao wote, lakini hoja nyingi zilikuwa zinafanana. Napenda kutoa majibu kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge, wakati walipojadili hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, hoja yake ilikuwa Serikali ihamasishe ujenzi wa hoteli za kitalii katika fukwe za Bahari ya Mtwara ili kuwavutia watalii. Kuwa Serikali imejitoa katika shughuli za uendeshaji wa hoteli, jukumu la kuwekeza rasilimali katika maeneo yanayozunguka vivutio vya utalii, limeachwa kwa Sekta Binafsi. Kwa msingi huo, Wizara imeelekeza nguvu zake katika kutangaza vivutio hivyo na kuvutia wawekezaji. Mikakati ya sasa ya Idara katika kuendeleza utalii ni kuimarisha vituo vya utalii vilivyopo katika Ukanda wa Kusini ili viweze kuhamasisha ujenzi wa hoteli za kitalii. Aidha, Wizara imeanza mazungumzo na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Kituo cha Uwekezaji *(TIC)*, ili kupanga

mikakati ya kutenga maeneo ya uwekezaji katika Ukanda wa Pwani, ikiwa ni pamoja na fukwe za Mkoa wa Mtwara kwa ajili ya kuendeleza utalii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, hoja yake ilikuwa Wilaya ya Kilwa ipate mgao wa fedha zaidi unaotokana na mapato yatokanayo na utalii katika Mbuga za *Selou.* Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, hupata asilimia 25 ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii, kama yalivyo maeneo mengine ya uwindaji, yanayopakana na shughuli za uwindaji wa kitalii.

Vilevile Idara ya Wanyamapori, hupanga aina na idadi ya wanyamapori watakaowindwa kwa uwindaji wa wenyeji, baada ya Halmashauri husika, kuwasilisha maombi. Mapato yatokanayo na uwindaji huo, hubakia kwenye Halmashauri ya Wilaya husika. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, atumie utaratibu huu kwa kuwasilisha maombi ya aina hii ya uwindaji ili kuongeza mapato ya Halmashauri ya Wilaya yake.

Mheshimiwa Spika, Felix Kijiko, Mbunge wa Muhambwe alisema, Serikali iwaruhusu wananchi wa Lubanga, kuvuna chumvi iliyopo katika pori la Akiba la Muyowosi.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mgana I. Msindai na Mheshimiwa Lucas L. Selelii, sauti zenu zinakwenda mbali sana na ni kinyume cha kanuni.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Madhumuni ya kuanzisha Mapori ya Akiba ni kulinda mazingira ya maeneo ambayo yana utajiri wa aina mbalimbali za viumbe na mimea. Katika kusimamia maeneo ya aina hii, taratibu za kutumia maliasili zinazopakana ndani yake zinawekwa. Taratibu hizi ni zile zinazozingatia matumizi endelevu na kuhakikisha kwamba, hapatakuwepo na uharibifu wa mazingira. Pamoja na kuwepo madini mbalimbali katika Mapori ya Akiba, Sera za Rasilimali haziruhusu uchimbaji wa madini, chumvi au chokaa ndani ya Mapori au Akiba ya Hifadhi za Taifa, isipokuwa shughuli za utafiti zinazozingatia tahadhari za mazingira katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Clement B. Lyamba, Mbunge wa Mikumi, amesema kwamba, Serikali itoe kipaumbele kuwapatia ardhi wakazi wa Kidodi na Ruhembe, wakati wa zoezi la kurekebisha mipaka ya Hifadhi ya Mikumi. Zoezi la kurekebisha mipaka ya Hifadhi ya Mikumi, litafanyika kwa kushirikisha uongozi wa kijiji, pamoja na wananchi katika maeneo husika. Ili kutoa kipaumbele kuwapatia ardhi wakazi wa Kidodi na Ruhembe, Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, ambayo ndiyo yenye jukumu la kugawa ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mbunge wa Chalinze amesema, Serikali iweke mkakati wa kutangaza zaidi Hifadhi ya Saadani ili kuwavutia watalii na kuongeza Pato la Taifa. Mkakati wa Shirika la Hifadhi ya Taifa Tanzania *(TANAPA),* kuitangaza Hifadhi ya Saadani, kwa lengo la kuongeza wageni pamoja na mapato, hufanyika kwa njia mbalimbali, yakiwemo Maonyesho ya SabaSaba, Maonyesho

ya Nane na Maonyesho mbalimbali ya Kimataifa, yanayofanyika kwenye nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Shirika kwa kutambua umuhimu wa kutangaza zaidi Hifadhi ya Saadani, hivi sasa inaandaa vipeperushi maalum, kwa lugha za Kiingereza na Kiswahili, pamoja na mkanda wa *video*, utakaoonyesha vivutio mbalimbali vya utalii, vilivyoko kwenye Hifadhi ya Saadani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, amesema Serikali iwape mafunzo wavuvi wa Mwanza ili wafanye shughuli zao bila kuharibu mazingira. Kupitia Mradi wa Kuhifadhi Mazingira wa Ziwa Victoria, ambao awamu yake ya kwanza ilimalizika Desemba, 2005, pamoja na Mradi wa Utekelezaji wa Mpango wa Menejimenti wa Uvuvi Ziwa Victoria, Serikali imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali ili kuwaelimisha wavuvi wa Kanda ya Ziwa Victoria, wakiwemo wavuvi wa Mkoa wa Mwanza, ambayo yalihusu haya yafuatayo: Madhara ya kutumia zana haramu za uvuvi, ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia rasilimali za uvuvi, uvuvi na zana zinazokubalika kisheria, uhifadhi bora na salama wa mazao ya uvuvi na elimu ya kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, aidha, chini ya Mradi wa Utekelezaji wa Mpango wa Menejimenti ya Uvuvi Ziwa Victoria, jamii itajengewa uwezo wa kushiriki katika usimamizi wa rasilimali ya uvuvi kwa kupewa mafunzo ya uongozi, menejimenti ya uvuvi, ujasiriamali na menejimenti ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wafuatao walichangia kwa maandishi: Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, alisema Wizara iendeleze watumishi wake kitaaluma na hasa waliopo katika Halmashauri. Wizara inatekeleza Mpango wa Mafunzo kwa watumishi wake. Mafunzo yaliyotolewa yalikuwa yafuatayo: Madaktari wa Falsafa walikuwa wawili, Shahada ya Udhamiri 37, Shahada 47, *Diploma* 156 na Cheti 73.

Mheshimiwa Spika, Wizara inagharamia watumishi wote wasiokuwa na Elimu ya Kidato cha Nne kujiendeleza. Kuhusu watumishi wa Halmashauri, Wizara imekuwa ikilipa gharama za mafunzo kwa watumishi wa Halmashauri, kwa mfano, katika Chuo cha Misitu Olmotonyi na katika vyuo vingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Magharibi, amesema Kimodo cha Mbozi kitumike kama kivutio cha utalii. Wizara inakubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Kituo cha Kimodo cha Mbozi kimeshatambulika kama moja ya vivutio vya utalii na kipo kwenye orodha ya vivutio vya utalii na Wizara itaendelea kukitangaza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mbunge wa Karatu, amesema Mji wa Kaole hautunzwi vizuri wala kuwekwa katika utaratibu mahsusi kuwa kivutio cha utalii. Aliuliza je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kufanya eneo la Kaole kuwa eneo la utalii, ikiwa pamoja na miundombinu, ofisi stahili na kiongozi

stahili? Miundombinu kama vile Kituo cha Kumbukumbu na Taarifa, maji, umeme na simu, vimekwishawekwa. Uboreshaji zaidi wa Kituo cha Kaole, utahusishwa katika mpango wa uhifadhi, uboreshaji na utangazaji wa njia ya kati ya biashara ya utumwa. Kituo kina wataalam watatu, mwana ikolojia mmoja na mafundi wahifadhi wawili. Aliuliza pia je, nchi yetu ina wataalam wangapi wa ikolojia na tunawajuaje?

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Ikolojia cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kilitoa wahitimu wa kwanza katika fani ya ikolojia mwaka 1988. Mpaka mwaka 2005, nchi yetu imekuwa na jumla ya wataalam wa ikolojia 57, kati yao 42 ni wanaume na 15 ni wanawake. Aidha, wahitimu 25 katika fani ya ikolojia wameajiriwa katika Taasisi mbalimbali za Serikali na waliobakia wako katika Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, amesema maeneo ya Malikale, ikiwa pamoja na michoro ya mpangoni Bwanjai Kambi ya Wajerumani, Kata ya Miziro na kumbukumbu za vitu vya Kagera, yatumike kama vivutio vya kitalii. Wizara itafuatilia vivutio hivyo ili kuandaa utaratibu wa kuyatumia maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, ameuliza kama eneo la Bujora linahudumiwa na Serikali. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, itafuatilia suala hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo amesema, magofu ya Bagamoyo yaandaliwe ili yasiendelee kubomoka. Serikali inaandaa Mpango Shirikishi ili kutatua tatizo la ubomokaji wa majengo ya Bagamoyo. Aidha, hatua za ukarabati wa Boma la Bagamoyo, zinafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, amesema anataka kumbukumbu za mambo ya kale hasa Bagamoyo, **Silevuruti** na Ujiji ziboreshwe. Wizara ina Mradi unaolenga kuboresha vituo hivyo, hususan njia ya kati ya biashara ya utumwa kutoka Ujiji mpaka Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, amesema kwamba, bajeti ya *TTB* iongezwe kukabili ushindani na nchi nyingine. Wizara inatambua ufinyu wa bajeti ya *TTB* na itazama njia nyingine ya kuziba pengo la bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, pia amesema tutumie Balozi zetu kutangaza utalii. Wizara inafanya hivyo, kwa kuwapelekea vielelezo vya kutangaza na kuwashirikisha kwenye maonesho ya utalii, pia tunatumia Wakala katika masoko makuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, amesema tutumie vituo vya utalii ili kupunguza umaskini. Mikakati inayotumika ni kuhamasisha utalii wa utamaduni unaoendeshwa na wananchi na kushirikiana na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, amesema Jimbo la Kalambo, lina vivutio vingi ambavyo havijaendelezwa. Tayari vivutio hivyo, vimeainishwa Mkoa wa Rukwa ikiwa ni Maporomoko ya Kalambo na magofu ya Bismark ni kati ya vivutio hivyo. Serikali pia inaendelea kuhamasisha wawekezaji ili wawekeze katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, amesema tufanya mapinduzi ili Sekta ya Utalii ichangie zaidi katika uchumi. Tunachofanya ni kuhamasisha, kusaidia na kulinda makampuni za Wazalendo ili mapato ya utalii yabaki nchini. Tunahamasisha vilevile na utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, amesema tuimarishe Elimu ya Utalii miongoni mwa wananchi. Elimu inatolewa kupitia *TANAPA*, Redio, Maonesho ya Sabasaba na kadhalika. Wizara yetu inashirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ili elimu ya utalii iingizwe katika mitaala ili kuendeleza utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, amesema tuchapishe kitabu kinachoonesha aina ya miti nchini na faida zake, watafiti kupewa ushauri na waganga wa asili, pia upandaji miti wa asili Kwimba ufanyike. Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, tumepokea mapendekezo yako na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda na mimi naunga mkono hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa asilimia mia moja. *(Makofi).*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge, ambao wametoa maoni yao kwa njia ya kuzungumza, kuanzia asubuhi na wengine wameleta michango yao kwa maandishi. Kama Naibu Waziri alivyosema, kuna wengine walizungumza katika hoja za Wizara zilizopita.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda niwatambue waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ambao ni Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Abdulkarim E.H. Shah, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe na wa mwisho alikuwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Zabein M. Mhita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Loduvick J. Mwananzila, Mheshimiwa Fatma A. Makidadi, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Diodorus B. Kamala, Mheshimiwa Dr. Charles O.

Mlingwa, Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Celina O. Kombani, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Dustan D. Mkapa, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya na Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Prof. Feethan F. Banyikwa, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Sigifrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Brig. General Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Damas P. Nakei na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Dr. Lawrence K. Masha, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Kheri Khatibu Ameir, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mheshimiwa Vita R. Kawawa na mwisho alikuwa Mheshimiwa Stephen M. Wasira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, wachangiaji wote kwenye hoja niliyoitoa asubuhi, walikuwa na nia njema tu ya kuweza kutusaidia katika maeneo mengi kama ilivyotokea kwenye Kamati ya Maliasili na Mazingira. Ushauri wao tumeuchukua na kwa sababu ya kuzingatia muda, nitajaribu kujibu hoja moja moja kama zilivyonifikia na nina hakika kwamba, nitajitahidi kadri niwezavyo, ili niweze kufikia mahali pazuri na kuelewana.

Mheshimiwa Spika, naanza na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Job Y. Ndugai. Haya naamini ni maoni ya Kamati, kama ilivyo taratibu zetu. Kwanza, lilikuwa suala la kusafirisha magogo. Usafirishaji wa magogo nje ya nchi, umekataliwa na Sheria. Sheria kifungu kidogo kwenye Kanuni ya Sheria ya Misitu ya mwaka 2002, inazuia usafirishaji wa magogo nje ya nchi. Sasa mwanzoni kabisa, uzuiaji rasmi baada ya Kanuni na Sheria kutangazwa kuanza kazi, ilikuwa mwaka 2004.

Serikali ilipozuia wahusika ambao walikuwa wengi wao, kama walivyosema hapa Waheshimiwa Wabunge, walikuwa ni Waafrika, nikiimaanisha Wazalendo wa Tanzania, walikuwa ndiyo wanatumika kwenda kukata misitu. Lakini nyuma ya hao, biashara hiyo ilikuwa inaongozwa na wageni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, walikuwa wakitumika tu na wengi wao katika Makampuni ukijumlisha karibu 131 hivi, Makampuni matatu ukienda kuchunguza nani anayeyamiliki yalikuwa ndiyo yanamilikiwa na Watanzania. Yale mengine mengi yaliingia kama Makampuni ya wawekezaji. Lakini mengi hayakuwa na *asset* na ukifuata kweli sheria ya *TIC,* wengi walipewa kwa ahadi kwamba, wataleta mitaji. Lakini wengi walileta mashine kuu kuu, ambazo hazikuwa zinafikia hata kile kiwango cha chini kinachokubalika chini ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ile mara ya kwanza, ndugu zangu wakaja na hoja kwamba, wana magogo yameachwa porini, hiyo ilikuwa mwezi Juni, 2004. Waziri aliyekuwepo, akatoa *exemption*, wakatoe magogo. Wakatoa magogo na wakaendelea kukata magogo mengine na wakafanya ujanja wakitoa yale magogo ya zamani wanakata mapya, wanayachoma juu ili yaonekane kama ni magogo yaliyoachwa, yamepatwa na moto na kadhalika. Sasa huo mchezo umefanyika, wamepewa *exemption* karibu mara tatu na *exemption* ya mwisho ilikuwa mwezi Desemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa bahati nzuri, baada ya kuingia Awamu ya Nne, tuliahidi utawala wa sheria na taratibu. Niliiangalia upya Sheria ile, ndiyo nikakuta kanuni ya 50 inazuia usafirishaji wa magogo nje ya nchi. Sasa sikufanya kinyume zaidi ya hilo. Sasa hao wanaosema waliacha magogo tangu mwaka 2004 na wamekopa, ina maana hawajui biashara. Utakopaje uache magogo mwaka 2004, *interest* iwekwe tu na mabenki wewe umezubaa tu. Wameruhusiwa mara tatu haikufanya hivyo. Jamani *Bongo land* hii! Hatukupenda na sisi tuiingizwe kwenye mtego ambao hauna mantiki.

Mheshimiwa Spika, mimi nimetokea kwenye *business community,* naelewa siwezi kwenda kukopa kama sioni *prospect* ya kurudisha hizo fedha. Lakini wale ambao wamepata *order,* nimewaomba waniletee zile *letters of credit* kule *order* zilikotok zote zilisha-*expire*. Kawaida *letters of credit* ikiwa *valid* kwa miezi sita, huwa ni gharama sana kwa *importer,* kwa hiyo, zote zilisha-*expire*. Kwa hiyo, anayeeleza kwamba, hajalipa mkopo ni kawaida tuna matatizo ya kukopa saa nyingine hatulipi. Kwa hiyo, inawezekana kweli hawakulipa mikopo ambayo walikopa. Lakini kuanzia mwaka 2004, ina maana walikuwa hawalipi hiyo mikopo wakiwa wanafanya biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maamuzi tuliyoyatoa, tulifuata sheria kama alivyosema msemaji mmoja. Kama mkitaka sheria tuirudishe hapa Bungeni turuhusu magogo, lakini madhara yake wote tunayajua. Tumetumia mabilioni ya shilingi mwaka huu, kununua chakula. Sasa tukiruhusu *interest* za watu wachache, kwa bahati mbaya sana waliokuwa wanafaidika siyo Watanzania, tutajifikisha mahali hata *legitimacy* ya nchi kama Tanzania, nchi uhuru itakwisha. Nani anayependa uwe unaenda unaomba chakula kila siku. Kwa hiyo, Mheshimiwa Job Ndugai, busara iliyotutuma tufanye hivyo, tuliongozwa na busara ya kawaida kabisa, ambayo mtu yeyote ungemwuliza angeitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika upungufu wa usimamizi kwenye Wilaya, nakubaliana kabisa na taarifa ya Kamati ya Mheshimiwa Job Y. dugai. Kwa bahati mbaya sana, kipindi kilichopita tulijifikisha mahali, Wizara ilikuwa inaongoza kila kitu kutoka Makao Makuu.

Sasa *GN 69* na *GN 70*, tumerudisha madaraka kwenye Wilaya. Msimamizi wa uvunaji wa mazao ya misitu sasa hivi ni Mkuu wa Wilaya. Hiyo ilifanyika na ndiyo maana kulikuwa na vurugu tupu kwamba, mambo yanafanyika ukiwauliza wanasema wamepewa vibali kutoka Makao Makuu. Sasa tulijifikisha pale.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumewakataza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, kutoa vibali kutoka kwenye Wizara. Kwa sababu kwa kufanya hivyo, hatufuati taratibu za Serikali. Serikali inatoa matangazo yake kupitia Gazeti la Serikali. Hivi vibali nadhani wote mnajua historia ya wakati wa *RTC*, ilikuwa inafika mahali hata ukitaka kununua sukari lazima upewe kibali. Sasa hivi Maofisa nimewazuia, hawatoi vibali tena. Wakitaka kutoa vibali, lazima tutengeneze *GN,* ambayo inakuwa *vetted* na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na inapitishwa kwenye *process* na watu wengi wanaona. Hiyo inazuia mianya ambayo wafanyakazi ambao siyo waaminifu, wanaweza kuitumia.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na suala la usimamizi wa mapori ya akiba, tunapendekeza sasa hivi na tumeanza *process* ya kuanzisha *Executive Agency*. Sasa hivi Idara ya Wanyamapori, inakuwa sasa ni msimamizi wa sheria na wakati huo huo ndiyo inachukua jukumu la maamuzi, nani afanye hiki na nani afanye kile. Nadhani ni vizuri Wizara au Idara ya Wanyamapori, ikabaki kuwa ni msimamizi wa Sheria, badala ya kuwa mtendaji au o*perator*. Kwa hiyo, hilo nakubaliana na mapendekezo ya Kamati tulishayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kuhusisha jamii kwenye wanyamapori, napenda nitoe taarifa kwamba, tathmini itaanza kufanyika mwezi Septemba, tumeshapata fedha, *WWF* ndiyo wamepewa hiyo kazi ya kutathmini. Nina hakika kwamba, baada ya tathmini na baada ya Sheria mpya ya Wanyamapori kuletwa hapa Bungeni mwezi Oktoba, 2006, tutaoanisha vyote kama sera inavyotaka na mambo haya yatakwenda vizuri. Kwa nini sheria imechelewa? Imechelewa kwa sababu ya mambo mengi. Idara ya Wanyamapori au Sekta hii ya Wanyamapori inaongozwa na Sheria nyingi za Kimataifa, kuna *CTS,* kuna mambo mengi sana yanahusiana na jamii. Ukiangalia kihistoria, jamii iliachwa nje ya usimamizi wa maeneo ya wanyamapori tangu mwaka 1889. Sasa mnaweza kuona kwamba, jamii imekuwa *ignored* kwa muda mrefu. Kwa hiyo, *cumulatively* imekuwa ni tatizo sana kuihusisha jamii na ndiyo tunakwenda pole pole hatutaki kufanya makosa na tumetuma Kamati katika sehemu nyingi sana, kuchunguza wenzetu wanafanyaje?

Mheshimiwa Spika, nina hakika sheria tutakapoileta hapa Bungeni, itakuwa inajumuisha matatizo yote ambayo yalikuwepo na tuna uhakika tutatatua matatizo mengi.

Mheshimiwa Spika, tuongeze fedha za utafiti, lakini kama nilivyosema, nawaomba watafiti wetu walete *proposal* za *research*. Hatuwezi kupeleka fedha bila kuwa na *research problem,* bila kujua ni tatizo gani tunatakiwa kulitatua. Maana *process* ya *research,* nafikiri Waheshimiwa Wabunge wanafahamu, kwa bahati mbaya sanak *research* zetu nyingik wanaoleta *proposal* ni watu kutoka nje. Sasa wanapoleta inabidi tuwape na kwa sababu mara kwa mara wanakuja na fedha wametafuta wao wenyewe.

Lakini tuko tayari kuweka fedha nyingi zaidi kulingana na *protocol* tulizosaini na *SADC* na Jumuiya nyingine kwamba, tuwe tunaweka fedha za *research* karibu asilimia moja ya *GDP*.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwa Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya. Napenda nimpongeze kwa kuzungumza vizuri sana, ni kweli aliyoyaongea mengi ndiyo ilikuwa *feeling* ya Waheshimiwa Wabunge wengi. Kama alivyosema Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, uzuri tunachukua kutoka pande zote na napenda nimshukuru sana. Ila nitapenda kusahihisha maeneo machache ambayo ameyatamka, ambayo siyo sahihi. Ukurasa wa 19 *income* ya dola milioni tisa, anapo-*compare* na Namibia dola milioni 52. Ukweli ni kwamba, sekta yetu inaingiza dola milioni 150, kwa hiyo, tuko mara tatu zaidi ya Namibia, ila Kiwizara zinaonekana ni fedha kidogo, sekta binafsi inaingiza fedha nyingi zaidi. Kiujumla Sekta ya Wanyamapori, inaingiza asilimia tatu ya *GDP* ya nchi, kwa hiyo, ni fedha nyingi sana.

Halafu kuhusu *Deep Sea Fishing,* amezungumza meli 140, sielewi hii idadi ya meli aitoa wapi. Takwimu zinaonesha *the highest* tulitoa leseni kwa meli 84. Kuanzia mwaka 1999 walivua tani 350, mwaka 2000 tani 700, mwaka 2001 tani 800, mwaka 2002 walivua tani 700 na mwaka 2003 tani 700. Hizi takwimu tumezipata kutoka kwenye takwimu za *European Union,* ambao wengi *EU* na Japan ndio wanavua kwenye *EEZ* ya Tanzania.

Fedha za kupitia Hazina, ni kweli zilikuwa zinasababisha usumbufu sana. Zinatoka Hazina, zinakuja Wizarani halafu ndio zinapelekwa kwenye *Districts.* Kuanzia mwaka huu, fedha lazima zitoke Hazina, kwa sababu *Paymaster General* ni Hazina, yuko Hazina, zitakwenda *straight* kwenye *Districts*. Kwa hiyo, hiyo itapunguza urasimu uliopo na kwa sababu ya utaratibu uliopo sasa hivi wa *Zone Exchequer,* nina hakika matatizo yote hayo ambayo Mheshimiwa ameyasema, yatakwisha.

*Fish Port TAFICO* tunaiuza sasa hivi, lakini *conditions* zake ni kwamba, lazima atakayenunua *TAFICO* ajenge *Fish Port*. Wakati huo huo watu wanatafuta mwekezaji ili ajenge *Fish Port* Mbegani. Ni kweli tukiwa na *Fish Port,* meli zinazovua kwenye *deep sea,* itabidi zije hapa kuripoti, zichukue Maofisa wetu, wachukue mafuta, wachukue *supplies,* tutaingiza fedha nyingi na ajira kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Amezungumzia kwamba, magari 200 yanapita kwenye *National Park* kila siku. Ni sawa, idadi hiyo wakati mwingine huwa inazidi, ndiyo maana *TANAPA* na Ngorongoro, tume-*raise fee* ya kuingiza magari kwenye *Park.* Hayakuwa ya watalii hayo magari yote, mengi yalikuwa ya watu wanaobeba mizigo, kwa sababu ni *shortcut* kwenda Mwanza, kutoka Mwanza kwenda Arusha na kadhalika. Tume-*raise fee* ili kupunguza, kwa sababu hatuwezi kuchagua kwamba, wewe gari hii unaruhusiwa kupita hii hairuhusiwi kupita. Tunajaribu ku-*balance* kwa sababu *demand* inapanda kama *supply* ni ndogo na *supply* ikiwa kubwa *demand* kwa kawaida inakuwa ndogo. Kwa hiyo, tumejaribu ku-*balance* kwa kupandisha gharama ya kupita kwenye *National Park* ili tuweze kupunguza idadi ya magari. Hiyo tumeanza kuona, kwa sababu kuanzia Januari tumepandisha sana kiingilio kwenye *National Park* ya magari yanayopita kama *transit.*

Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, pia amezungumzia suala la dosari kwenye Wizara kwamba, kuna watu wanahamishwa, hawahami wanakataa. Napenda kuchukua fursa hii, kumwomba Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya na Mheshimiwa Mgana I. Msindai, waniachie kwa sababu kuna Sheria ya *Public Service,* Kanuni ya 107, inaniruhusu kufanya ambayo Waheshimiwa walikuwa wanayataka. Kwa hiyo, hilo naomba sana mniache lakini linahitaji *procedure* na nitajaribu ku-*involve.* Lakini sitaki kutoa hisia kwamba, Katibu Mkuu wangu, alifanya *procedure* ambayo haieleweki. Ni kwa sababu tu kama mnavyofahamu, wafanyakazi wa Serikali, kuna taratibu zake za kuwaondoa. Sasa ukikosea kidogo, inakuwa tabu. Lakini nina hakika, kilio cha Waheshimiwa Wabunge wanakizungumza kulingana na *Public Opinion* iliyoko kule nje. Naahidi waniache, tutaona uwezekano wa kulitatua kwa njia ambayo ni nzuri zaidi na isiyomwumiza yeyote.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kwamba, Watanzania wahusishwe kwenye uwindaji, ninakubali. Taratibu zimewekwa, kwa bahati mbaya sana mwaka 2005 *Hunting Blocks* zote zilikuwa *renewed* kwa miaka mitano. Juzi wakati Mheshimiwa Stephen M. Wassira, akitoa hoja ya kuomba fedha hapa, tulimlaumu sana kwa kufuta Mikataba iliyowekwa. Sasa hii Mikataba tayari imewekwa. Hatutaki kujiingiza kwenye masuala tena ya kupelekwa Mahakamani. Tuwe wavumilivu, bahati nzuri mwaka 2009 ikiisha, *Hunting Blocks* zote zitakuwa wazi na tutafuata utaratibu ambao utawanufaisha Watanzania wote na wawekezaji ambao wana nia ya kutusaidia. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, tusijiingize kwenye *legal wrangle* na watu ambao *legally,* wamepewa hayo maeneo.

Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, nakubaliana naye, tuna Sheria ya Uvuvi inatupa ruhusa ya kuanzisha Mfuko na huo Mfuko sasa hivi tumeanza kuujenga kwa ajili ya kusaidia *SACCOS* za wavuvi. Itahusisha si Ukerewe tu, bali na wavuvi wa *Lake Tanganyika*, *Lake Nyasa* na wavuvi wote waliopo pwani, mwambao wa Bahari ya Hindi. Kwa hiyo, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella kwa hilo. Jiwe la Ukala linalocheza, nina hakika kwamba, tutapeleka wataalamu wetu wacheze na nina hakika sidhani kwamba, watadensi. Lakini tutaiweka kwenye orodha.

Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, ametupongeza kwa kuzuia vibali vya kuuza magogo nje. Nakubaliana naye na tunamshukuru sana kwa kutupa moyo. Bahati nzuri wananchi wanatupa moyo kwa hilo kwa sababu wanajua hasara zake. Lakini pia lazima tukubaliane kwamba, kuna wakati mwingine *pressure* inakuwa kubwa sana. Nina hakika Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, kama mnakumbuka bajeti ya mwaka 2004, tuliokuwa humu *pressure* aliyoipata kutoka kwa Wabunge waliokuwa wanasema, magogo yaruhusiwe kwenda nje. Sasa *political pressures* za namna hiyo, kwa wakati mwingine ukiwa mzuri sana, zinaharibu, ukiwa mkali sana nako saa nyingine inaharibu. Lakini tutajaribu kuwa *in between*.

Mheshimiwa Spika, hatuzuii magogo kwa *GN 69*, utaratibu uliopo sasa hivi, hatutazuia kwa sababu hizo mbao tunazihitaji sisi kutengenezea fenicha na kadhalika.

Kwa hiyo, uchakataji wa magogo ndani ya nchi, hatutazuia ila tunachozuia ni magogo kwenda nje ya nchi. Kwa sababu wanasema kuuza magogo nje ya nchi, nchi yanakokwenda kama yanakwenda India, hulipi ushuru. Kwa hiyo, ni *zero tariff* kuingia India. Lakini ukipeleka mbao, wanakutoza ushuru kwa sababu gain? Unawanyima *labour*. Sasa hatutaki sisi tunyimwe *labour* hapa, kwa sababu ukichakata gogo maana kuna misumeno yetu itafanya kazi na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, tunajaribu kuangalia njia ya kutufikisha kama Ilani inavyotutaka, tupate ajira milioni moja katika kipindi ambacho tumekitamka kwenye Ilani.

Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, amezungumzia juu ya Wilaya yake ya Kilwa kutokuwa na mapato kutokana na wanyamapori na akasema kwamba, hana taarifa kama wananchi wa Kilwa watafaidika. Lakini Naibu Waziri, ameeleza vizuri sana, kuna asilimia 25 huwa inatolewa. Mfano, katika kipindi cha mwaka 2002, tulipeleka karibu shilingi milioni tatu, mwaka 2005 pia tulipeleka fedha. Tatizo ni kwamba, zinapokwenda kwenye Wilaya, tunapokaa kwenye Halmashauri hizi fedha hawaelezwi Waheshimiwa Madiwani. Sasa inakuwa ni tatizo sana. Kwa hiyo, kuna faida inayopatikana kutokana na shughuli za wanyamapori kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Kaika S. Telele, amezungumza sana akasema juu ya *negotiations* kwamba, iwe ni kitu cha muhimu, nakubaliana naye. Lakini historia ya Ngorongoro inatupeleka mbali sana, nitapenda baadaye nimwombe Mheshimiwa Kaika S. Telele, tukae kwa sababu historia ya Ngorongoro nimeisoma vizuri, naielewa fika, nikiwaeleza hapa tunaweza kuchukua muda mwingi sana. Lakini *negotiations* huwa zinatangulia, tatizo baadhi ya watu wetu wanatumia upole wa wananchi wetu kuwarubuni, kuwadanganya. Idadi ya wananchi Ngorongoro, *sustainability* ya Ngorongoro inakubali wasizidi elfu saba. Leo tunazoza wako elfu 55. Sasa *pressure* ambazo alikuwa anazieleza Mheshimiwa Mbunge mmoja asubuhi, hauwezi uka-*sustain* kwa sababu *pressure* ya watu elfu 55 na elfu saba ni vitu viwili tofauti, ndiyo maana wanyama walianza kupungua.

Sasa tumenunua eneo ambalo wale ambao walikuja kwa shughuli za kilimo, tutawahamishia kule na *negotiations* zimeshafanyika miaka karibu mitatu inaendelea. Bahati mbaya, utekelezaji ulikuwa mdogo kwa sababu walitaka tujenge zahanati na shule, kitu ambacho kinafanywa sasa hivi na Mamlaka ya Ngorongoro. Baada ya hapo tutawaomba wahame wenyewe, tutawapatia usafiri lakini kama ikibidi wakizidi kukataa, basi itabidi tufuate taratibu ambazo zinaturuhusu kisheria, lakini *negotiations* huwa zinatangulia.

Mifugo na wanyama kushabihiana. Nakubaliana na Mheshimiwa Kaika S. Telele kuwa, wanashabiana kama mifugo na wanyama wanachanganyikana pamoja. Lakini wakati wanyama unawatoa wanabaki peke yao na wanyama hawa wa porini wako peke yao, tayari kunakuwa na *fragmentation,* huwezi ukawarudishia tena wakawa kitu kimoja. Magonjwa yatakuwa tofauti, kwa hiyo, magonjwa ya wanyama yanakwenda kwenye mifugo ya mifugo yanakwenda kwa wanyama. Kwa bahati mbaya sana, mifugo kwa sababu wana mtu anaiangalia, kuna Daktari atawaangalia na sisi wanyamapori tutagundua kwamba, wameshapata madhara baada ya kuwaona wanaanza kufa. Sasa sio kweli ni mpaka pale ambapo kiikolojia wanyama wale wakiwa pamoja.

Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, amezungumzia juu ya Mafia. Nitakwenda Jibondo na nilishakwenda kule, naelewana, matatizo yako ulinieleza najua, hukutaka kuyaeleza hapa, kwa sababu yana madhara yake. La magogo, nadhani nimekueleza yanatosha.

Mheshimiwa Mgana I. Msindai, ameeleza vizuri sana suala la wafanyakazi wanaokataa kuhama. Nakuomba Mheshimiwa Mgana I. Msindai, niachie nimekuomba sana. Uhaba wa wanyamapori ni kweli kuna maeneo uhaba umezidi, lakini kuna maeneo wamepungua na kuna maeneo wameongezeka. Tembo mnyama kuna muda fulani walipungua, sasa BAKITA watanishtaki. Naomba nitumie neno lililo kwenye Kiswahili fasaha. Tembo mnyama, ilifika muda fulani wakabaki 50,000, leo tunazungumza wako 120,000. Hii ni kwa sababu ya ulinzi unaofanywa na Idara ya Wanyamapori. Sasa kuna maeneo ambayo wanyama wa aina fulani wamepungua na wa aina fulani wameongezeka.

Lakini pia lazima tukubali wale ambao tunalalamika, wanyama wanatuvamia ukweli ni kwamba, sisi tumeshawavamia, kwa sababu yale yalikuwa ni mapito yao ya wanyama. Wanyama huwa hawasahau, wanaweza kuwa wanakwenda mwaka huu huku, sasa wanaporudi mwaka unaofuata, unakuta kuna binadamu wamejenga pale. Sasa inakuwa tatizo sana. Maeneo hayo tutayaainisha na tutazungumza na Halmashauri za Wilaya ili tupate suluhisho. Hatuwezi kupuuza kwamba, sekta ya wanyamapori haituingizii fedha. Tumesema sekta hii inatuingizia karibu asilimia tatu ya *GDP.* Tukii-*manage* vizuri, tunaweza kupata fedha nyingi zaidi, kwa ajili ya kupunguza umaskini wa nchi hii na kupunguza nakisi kwenye bajeti zetu. Kwa hiyo, nina hakika kwamba, mambo mengine kwa kweli, binadamu tunazidi ndiyo, lakini kuzidi kwa binadamu, hakuna maana tudai ardhi zaidi. Leo unalima shamba la eka moja unapata magunia matano, halafu una *exploit nutrients* kutoka kwenye ardhi, baada ya hapo unaamua kuhama ukalime pengine wakati hapo umepaharibu, ambapo tungetumia mbolea vizuri usingepata magunia matano, ungepata labda magunia 40. Kwa hiyo, bado kuna ugani unahitajika kwa wakulima wetu ili tuweze kuwa katika hali bora.

Napenda nilielezee suala la *Water level* ingawa lililetwa kwa maandishi na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri. *Water Level* juzi tulikuwa Kampala, tumekubaliana na Waganda, kilichotokea ndugu zangu, *Water Level* ya *Lake Victoria*, Waganda waliamua kujenga *turbine* kuongeza, yaani kama kuupanua Mto Nile. Kwa sababu walijenga *unit* 11 na *unit* 12. Kwa hiyo, *intake* ya maji ikawa kubwa sana, kuweza kuziendesha zile *turbines* na kukawa na *design error.* Badala ya kuchukua maji *800 cubic metres per second,* wakawa wanachukua *16,000 cubic metres per second,* ni karibu mara mbili. Ndiyo maana *level* ya maji ikapungua kwa kasi sana. Tumekubaliana wanasema, *unit* 11 na *unit* 12 wataifunga kwa sababu wao wenyewe sasa hivi, wanapata matatizo kwa sababu maji hayaingii sasa, *as a result* kuna matatizo ya umeme sana Uganda sasa hivi. Lakini watajenga *power station* nyingine *downstream,* ambayo haikatazwi maana unaweza kujenga ukazi-*casket power stations as much as you can*. Kwa hiyo, hilo nina hakika, niliona nilielezee hapa kwa sababu linaleta matatizo sana hasa Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa James D. Lembeli, nakushukuru sana kwa maelezo uliyoyatoa kwa ufasaha. Najua utalii na sekta unaielewa vizuri sana, ulikuwa na sisi. Balozi hazina ramani, ni kweli Balozi nyingi hazina vifaa na mwaka huu tunachapisha karibu kila Balozi tutapeleka *kits* za *Tourism promotion* 5,000, kitu ambacho hatujawahi kufanya huko nyuma.

Mheshimiwa Mkiwa Mkiwa A. Kimwanga, ndugu yangu Kisiwa cha Saanane na mimi natoka huko huko, sasa hivi tumekikabidhi *TANAPA* ili kurudishia hali yake. Kawaambie Walimu, wajitayarishe tu kwenda kutembelea hayo maeneo, baada ya shughuli zote kumalizika. Tutanunua boti mpya na tutaunganisha watu wanaokwenda Saanane na wanaokwenda Rubondo, ili shughuli zote zifanyike kwa mara moja. Nakushukuru kwa hilo.

Mkaa umepanda bei, ni sahihi umepanda bein kwa sababu tukiwaachia ndiyo hayo madhara niliyoyaeleza ya ukame. Lakini *GN 70* inaelezea sasa hivi, utaratibu ambao ulikuwa unaueleza na nina hakika labda hiyo *GN* umeiona kwamba, tutakuwa tunatenga maeneo ya kuvuna na maeneo mengine yanaachwa ili uoto wa asili uweze kurudishia miti.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni elimu. Gunia moja likifika shilingi 25,000/= ukweli ni kwamba, tayari limekuwa ghali kuliko kutumia mafuta ya taa au ukiwa na jiko la *burner* moja la *kilowatt* mbili katika matumizi ya kawaida kwa siku 30, bili yako ya umeme haiwezi kuwa zaidi ya shilingi 32,000/=. Lakini magunia mawili, wenye familia nadhani huwezi ukamaliza wiki mbili, kwa hiyo, unatumia 50,000/=. Mimi ningependa mkaa tuutumie wakati umeme haupo au siku mafuta ya taa yamekosekana au siku ambapo huna pumba au matakataka mengine, ambayo tunayatumia kwenye upishi. Kwa hiyo, naomba hilo, nina hakika tutawaeleza wananchi baada ya muda kidogo, tutaweka matangazo kwa wingi ili waelewe. Kwa sababu saa nyingine, kutokujua nako kunakuwa ni gharama sana.

Wakala huyu Mbondo wa *SUMATRA*, kwa kweli ni kero, naifahamu mimi kwa sababu anasumbua pia wavuvi wangu. Lakini hilo tunazungumza na Wizara ya Miundombinu ili tutafute uwezekano wa kulitatua. Mheshimiwa Aziza S. Ali, amelizungumzia tatizo la tembo mnyama, kama nilivyoeleza ni hilo hilo kwamba, tumeingia kwenye maeneo ambayo yalikuwa mapito ya wanyama, tuvumiliane. *Compensation* kwenye sheria tunayoileta, tutaiongeza itakuwa sio kifuta machozi, itakuwa ni *compensation*, lakini tutaku-*compensate* kwenda mahali ambapo hukwenda kuwachokoza wanyama. Maana lazima kuwe na *safety valve,* la sivyo, fedha za walipa kodi zitaishia zote kwenye kulipa watu, ambao walikwenda kuchokoza wanyama, wamelima karibu na sehemu ambazo kuna wanyama wakali na kupata madhara.

Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, amesema uwindaji usiwe wa kibaguzi. Sio wa kibaguzi, sehemu za Bunda huko Ikizu, zilikuwa ni *game controlled areas,* zilikuwa na wanyama wengi sana, lakini wanyama tuliwamaliza. Asubuhi ukienda, Maafisa wetu wa Wanyamapori unakuta *landrover* iko juu ya mawe, usiku ina tairi inakimbia kwenda kuwinda. Tumewamaliza wale wanyama, sasa tusitake kuingia Serengeti. Kwa sababu

kihistoria, Serengeti hawajawahi kuishi watu wa sehemu anazozisema Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe. Mwisho, ilikuwa ni Mto Gurumet, miaka ya 1960 walivuka kidogo. Serengeti ilikuwa ya Wamasai na Wamasai waliokuwa Serengeti mwaka 1937, walikuwa ni familia 730 tu. Sasa walipohama baada ya utaratibu uliowekwa na Mkoloni, wakati ule mwaka 1957 kutangazwa kuwa sehemu ya Ngorongoro, wakahamishwa mwaka 1957 wakaletwa Ngorongoro, baadaye maeneo yale yakatangazwa.

Mheshimiwa Spika, yote hiyo ilikuwa inafanyika kwa ajili ya kuacha mali zetu za asili, ili wanyamapori waweze kuwa na uhuru wa kusogea na kwenda maeneo ambayo wangebaki mpaka leo. Lakini tusingekuwa na *Ngorongoro National Park,* wanyama wangekwisha. Maeneo mengi sana wanyama wamekwisha. Ukiendesha gari mfano kutoka Ruaha kwenda mpaka Mbeya, yale maeneo hayana wanyama na huko wanyama unawapata kutoka Tunduma, unaanza kuwapata ukifika Katavi, lakini kutoka Sumbawanga kuja chini wanyama hawapo.

Lakini hatuwezi kuachia kila sehemu tukawa na matatizo hayo, ni lazima tuwatunze wanyamapori kwa ajili ya utalii kwa Watanzania. Kuna Watanzania wanapenda kuona wanyama na kuna watu wa nje, ambao wanapenda kuona wanyama ni urithi wetu. Sasa itakuwa ni ajabu sana, tukipuuza urithi wetu ambao unatuweka na amani na upendo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, labda nimalizie moja, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, kuna *issue* moja aliieleza ya fedha, tenda ya shilingi 141 milioni, hiyo tenda imetolewa kwa Chuo Kikuu cha Sokoine. Naomba unisaidie, uniachie muda nitakujibu baadaye, kwa sababu inavyoelekea ni chuo cha umma, lakini walifanya *single source,* wameshindwa kunipa *proof* kwamba, walipata vibali kwa sababu kuna utaratibu *single sourcing* lazima wafuate utaratibu.

Mheshimiwa Spika, naomba nilikubali hilo kwamba, linawezekana, kuna makosa lakini nitakupa taarifa baadaye tukitoka hapa, nikipata taarifa kamili. Nakubali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nadhani nimewajibu Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia kwa kuzungumza na waliochangia kwa maandishi. Ambao hatukuwatolea majibu, tutawapa majibu tukiwa hapa hapa Dodoma kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … Sh. 4,133,939,700/=

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *programme* namba 10, *subvote* 1001, kifungu 250100 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia, pamoja na mambo mengi niliyozungumza na hayakujibiwa, nilisema Waziri aunde Kamati kuchunguza ubovu wa Idara ya Wanyamapori, sasa hajanijibu, naomba maelezo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kuwa, asubuhi wakati nasoma hoja yangu, nilieleza kwamba, sasa hivi tuna Taarifa ya Kamati, ambayo ilikuwa chini ya Ndugu Ntukamazima, ambayo Wajumbe wake walikuwepo Mheshimiwa Job Y. Ndugai na Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, mbali ya Wajumbe wengine. Kamati imetuletea ripoti safi, imekwenda nchi nyingi, wametuletea taarifa ambayo tutaitumia kurekebisha Muswada ambao tutauleta hapa ili kurekebisha dosari zote zilizopo. Hii ikiwa ni kutoa baadhi ya madaraka kutoka kwa mtu mmoja ili yawe yanafanywa na Kamati, ambayo imeruhusiwa kisheria, hiyo inatamkwa kwenye sheria.

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Mgana I. Msindai, inatosha hiyo au bado?

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Bado Mheshimiwa Mwenyekiti. Kamati iliyoteuliwa ilikuwa inashughulikia juu ya vitalu vya uwindaji. Mimi ninataka ubovu wa utendaji kazi wa Idara ya Wanyamapori. Naomba maelezo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimwa Mwenyekiti, ubovu wa Watendaji ni suala ambalo linakuwa *taken care of admistratively*. Huwezi masuala ya Watendaji ukaanza kuyaundia Kamati nje, Kamati ambazo zimetamkwa na Sheria ya Utumishi. Kwa hiyo, nilisema hapa kwamba, waniache. Nilimwomba Mheshimiwa Mgana I. Msindai, yeye mwenyewe atuache, tutafute taratibu ambazo kwangu mimi nadhani ni ndogo sana. Matatizo makubwa ni ya *procedure,* kuweka uwazi kama ni *Hunting Blocks* ziwe zinatangazwa kwenye magazeti, watu wajue, wa-*apply* kwa *criteria.* Kama kuna haya matatizo mengine kama Menejimenti ya *Game Reserves,* nimesema kwamba, tunaanzisha Wakala ambayo itakuwa na wataalamu na Menejimenti ambayo inaweza kuwajibika kwa wananchi wa nchi hii vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa hivi. Sasa Kamati nyingine nje ya hapo, kwa kweli tutakuwa tunavunja sheria sisi wenyewe, ambao ndio watunga sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgana I. Msindai, naona bado au unakubali?

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika na maelezo ya Waziri, sasa niko tayari kutoa shilingi kwenye bajeti hii. Kifungu hicho hicho, natoa shilingi Mshahara wa Waziri. Programu namba 10, *subvote* 1001.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa subiri kwanza, kaa. Nadhani hapa mlipishana kidogo tu, wewe unadai maelezo unachoita utendaji mbovu wa Idara ya Wanyamapori. Mheshimiwa Waziri amesema ubovu wa watendaji, ambacho si kitu kilekile. Nadhani kwa kile cha kwanza, sioni ugumu wowote kwa Serikali, maana ubovu wa utendaji si ubovu wa watendajim inawezekana nao wanakwamishwa na wanasiasa na mambo mengine. Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikiliza Mheshimiwa Mgana I. Msindai na asubuhi hii Wabunge wengi tu wamezungumzia kuhusu Idara ya Wanyamapori, tumesikia maoni yao, tutayazingatia watupe muda tuyafanyie kazi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* … … … … Sh.763,454,600/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 – *Policy and Planning* … … … …. … … … Sh.604,937,900/=

**MHE. SIRAJI J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la ufafanuzi tu kwamba, utalii wetu umejikita sana Kaskazini. Kifungu 1003 - *Policy and Planning, subvote* 250100 - *Basic Salary*. Ninachotaka ufafanuzi ni kwamba, utalii wetu umejikita Kaskazini ya nchi, pamoja na kwamba, nchi hii ina vivutio vingi katika maeneo mengine ya nchi hususan Magharibi. Wenzetu wa *Policy and Planning,* wanafanya nini katika ku-*diversify tourist destinations* za nchi hii, ili kufanya maliasili iliyoko Tanzania na utalii, viweze kutumika kwa kiasi kikubwa kuliletea pato la fedha za kigeni Taifa letu?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnapotaka kuuliza maswali yanayohusu sera, kifungu sahihi ni kile cha *administration and general,* ndiyo kuna mshahara wa Waziri. Huku kwingine ni hawa Wakurugenzi na nini na sisi sio kazi yetu kuwahoji Wakurugenzi. Kwa hiyo, nasikitika labda mfanye mawasiliano ili kuweza kupata ufafanuzi wa hilo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Wildlife* … … … …. … …. …. Sh. 8,648,682,000/=

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Programu ya 20, kifungu cha 2001, kifungu kidogo kabisa cha 270600 - *Land Operations*. Nilipeleka mchango wa maandishi na nikatoa malalamiko kule *Mahale Game Reserve*, ambapo uongozi wa *game reserve* unawasumbua wananchi wa Kijiji cha Kalilani. Kila siku wanajaribu kutaka kubadilisha mipaka nje ya utaratibu wa mipaka

iliyotolewa na ofisi inayotoa hati za vijiji. Mheshimiwa Waziri, wakati anajibu, wakati mwingine wana visingizio vya muda, amemaliza kutoa majibu yake dakika kumi kabla ya muda alioruhusiwa, lakini hakugusia kabisa hili. Sasa ningeomba anifafanulie, ofisi yake inasaidia vipi kuondoa bugudha wanayoipata wananchi katika Kijiji cha Kalilani?

**MWENYEKITI:** Kwanza, nisahihishe Mheshimiwa Waziri sio kwamba, alimaliza dakika kumi kabla. Ni kwamba, michango ya awali iliwahi kwa hiyo, alitumia muda wake wote mpaka akagongewa kengele. Mheshimiwa Mawaziri maelezo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa *concern* ya Mheshimiwa Mbunge, lakini kawaida haya maeneo yanapotangazwa yanakuwa *gazetted*. Kinachotokea ni kama hicho nilichokieleza hapo awali kwamba, wananchi wanatumia ardhi waliyonayo *to the point* kwamba, wana-*exploit nutrients* za ile *fertility* ya ardhi. Sasa haya maeneo ya *game reserves* au *national parks,* yanakuwa na rutuba. Kwa hiyo, wanalima mpaka wakati mwingine wana-*over shoot*. Sio sahihi kwamba, eneo hilo sisi tunahamisha mipaka.

Mipaka iko *gazetted* na iko kulingana na sheria. Matatizo ni hayo ya wananchi wakati mwingine ku-*lead ignorance* kwamba, hawaelewi mwisho wanaruhusiwa, inategemea pia na eneo lenyewe labda Mhifadhi wa eneo lile anaweza kumwachia mwaka mmoja akalima. Sasa kama kawaida ngamia akiweka kichwa anataka aweke mwili mzima. Sasa sio sahihi kweli kusema kwamba, tunawasumbua wananchi. Wananchi ndiyo hao hao wanatupa kura na tungependa sana tuwe nao bega kwa bega, kwenye matatizo yote. Sio sahihi kwamba, usumbufu unaofanyika kwa wale ambao hawavunji sheria, wengi wanavunja sheria na sheria lazima tuzilinde kwa sababu Bunge hili limetupa *mandate* hiyo ya kulinda sheria zetu.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri, hana taarifa nzuri. Katika maandishi niliyompelekea nilieleza kabisa kwamba, suala hili limewahi kushughulikiwa na Waziri aliyemtangulia na uamuzi ukatolewa na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kalilani alisafiri mpaka Dodoma hapa. Mimi na Mheshimiwa Zakia H. Meghji na Mwenyekiti yule, tulikaa tukalijadili na ofisi ikatoa uamuzi. Sasa anaposema kwamba, watu kama ngamia ukimruhusu kichwa anaingiza mpaka mwili, si kweli. Kwa sababu kwanza, kwa hatua kubwa sana kile sio kijiji cha wakulima ni kijiji cha wavuvi, sasa hawawezi kuchukua ardhi wakaenda wakavulia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, si ujipe nafasi mwenyewe ukaangalie halafu yaishe. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Wakati nawasilisha hotuba yanguh niliomba maelezo, niko kwenye progamu ya 20, *subvote 2001*, kifungu kidogo 260800. Niliomba nipate maelezo kwamba, Kituo cha *ABRU* kilichopo *Mikumi National Park,* mpaka leo kimetoa taarifa ngapi za kuweza kusaidia *management* ya *national park,* sikuweza kupata majibu? Pia katika kifungu hicho hicho kwa ujumla niliomba nipate taarifa za vijana wangapi ambao wamekamatwa mpaka hivi

sasa na wamefunguliwa mashtaka Mahakamani kwa masuala ya uwindaji haramu wakati wawindaji halisi wako nje? Asante.

**MWENYEKITI:** Hebu rudia hicho kituo kinaitwaje?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Kuna Kituo cha *ABRU,* ambacho kinafanya utafiti wa nyani, ambacho kiko *Mikumi National Park*, niliomba nipate taarifa kwamba ni taarifa ngapi zimetolewa na hiki kituo?

**MWENYEKITI:** La pili ulisema kuhusu vijana?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** La pili nilipenda kupata taarifa kwamba...

**MWENYEKITI:** Kwenye kifungu gani sasa hilo la pili?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Kwenye kifungu hicho hicho kwa pamoja, programu ya 20, *subvote 2001,* kifungu chote kwa ujumla, kwa sababu sielewi *specific* yote iko wapi. Ila hasa napenda kupata taarifa ni Watanzania wangapi, ambao wametuhumiwa kwa kesi za kuhusishwa na ujangiri, wakati majangiri sahihi wako nje, wanaendelea kuwinda na kufanya biashara haramu?

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Mbunge, nitaruhusu pale kwenye 260800 kwa sababu inahusu *training,* hilo lingine ni la jumla, ambalo halipo katika kifungu chochote hapa. Majibu kwa hilo la kwanza, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sikuweza kumjibu Mheshimiwa Mbunge hoja zote na ndiyo maana nikasema nitatoa kwa maandishi. Yeye alichukua nusu saa, mimi nilipewa dakika 40 kujibu hoja zote za Wabunge, nadhani sababu anaweza kukubali. Kituo hiki cha *ABRU*, kinatoa taarifa Wizarani mara nne kwa mwaka na wametoa gari kwa Idara ya *Ecology* ya *TANAPA* na wamesomesha sasa hivi kuna mwanafunzi anamalizia *Masters* ya *Ecology*. Kwa hiyo, wanasaidia kama alivyotaka kujua Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Programu ya 20, *subvote* 2001, kifungu kidogo 3017000 - *Feasibility Studies, Project Preparation and Design*. Wakati Wanakamati tulipotembelea Rubondo na *Port Ikoma*, wanakijiji walituletea malalmiko yao kuwa, mayai ya mbuni yanachukuliwa na wawekezaji na kusafirishwa nje na matokeo yake mbuni Serengeti wanakwisha. Lakini taarifa tuliyoipata kwa *DC* inasema, watu wa kule ni wakorofi, wanazungumza uongo.

Kamati kwa kushirikiana na wananchi, tukaenda mpaka *Guruneti*, tukatembelea ndani ya vyumba, tukayakuta mayai katika kila chumba ndani ya mifuko yamewekwa, inaonyesha yale mayai yanapalekwa nje. Je, kwa hili Waziri analitolea ufafanuzi upi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Mbunge, angetuletea mchango kwa maandishi au kwa kuzungumza,

tungempa majibu sahihi, lakini hatutaki kusema kwamba, hatuwezi kulijibu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, atupe muda ili tu-*consult* wahusika ili tumpatie taarifa.

**MWENYEKITI:** Nadhani ni *fair* kufanya hivyo. Anafuata Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, wengine mnasimama sijui vipi, tulikwishafunga orodha. Haiwezi kuendelea tu, ukifikiria jambo unasimama, Kamati ya Matumizi huwa unajiandaa kabla. Msemaji wa mwisho ni Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Programu ya 20, *subvote 2001*, kifungu kidogo cha 270300, kinachohusu magari. Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, imebidi waongeze hiki kiwango cha magari, kwa maana haya magari yanayopita mbugani, yasiweze kuharibu mazingira pamoja na mambo mengine. Matokeo yake ni kwamba, kiwango hicho kimeongezeka kutoka shilingi 30,000/= mpaka shilingi 200,000/= kwa gari. Lakini unapokuja kuangalia Mkoa wa Mara, baada hasa ya hii reli kuwa imeharibika, ina maana mizigo inatoka Dar es Salaam inashuka Dodoma, inaenda Mwanza inashuka ndiyo inaenda Musoma, kwa maana ya walaji. Sasa matokeo yake sasa, baada ya hizi gharama kuwa zimeongezeka toka shilingi 30,000/= mpaka 200,000/=, zile gharama si kwamba, zimeongezeka kwa yule mtu mwenye gari.

Yule mwenye gari naye amezibeba kama zilivyo, amepeleka kwa mwananchi wa kawaida na sasa kutoka na hali hiyo, ghafla vitu vimepanda katika kiwango kikubwa sana. Lakini vile vile katika mpango wa Wizara, ina mpango wa kufidia ile njia ambayo inaenda mpaka ziwani kutokea pale jirani na Ramadi. Kwa hiyo, matokeo yake sasa ni kwamba, Mara nzima sasa haitakuwa sehemu ya Tanzania. Kwa maana kote itakuwa imezungwa na mbuga za wanyama. Sasa kutokana na hali hii, sijui Waziri hilo analionaje, kwa sababu tofauti ya bei sasa imekuwa kubwa sana, kiasi kwamba, wale wananchi wa kawaida sasa hawataweza kuyamudu maisha yao kule waliko. Naomba majibu katika hilo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepandisha na tumepandisha kwa sababu ya kupunguza *pressure*. Sasa inakuwa kama utani wa kule anakotokea Mheshimiwa Mbunge, wanasema kwamba, ukikimbia unapigwa mshale ukisimama wanakupiga mapanga. Sasa tufanyeje, tunatakiwa tupunguze *pressure* na hiyo shilingi laki mbili siyo kwa gari dogo, gari dogo imepungua kutoka dola 30 hadi dola 50. Lakini kwa lori kuanzia tani saba na kuendelea, ambayo ukweli ni kwamba, yanaharibu barabara na bahati mbaya sana hatuna ruzuku kutoka Miundombinu kuwapa *TANAPA,* utengenezaji wa barabara wote unafanyika kwa fedha zao. Sasa ndiyo imepanda sio tena shilingi 30,000/=, ilikuwa shilingi 15,000/= wakati ule hadi 200,000/=, hiyo tukijua kwamba, tutapunguza idadi ya malori yanayopita katikati ya mbuga za wanyama. Wanagonga wanyama na wanaharibu barabara, sasa hatuna njia nyingine yoyote ambayo inaweza kusaidia idadi ya magari yanayopita pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali yetu ndiyo hivyo na hatuna ujanja mwingine.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba, hawana ujanja mwingine, kwa sababu magari yanapita katika njia hiyo, ndiyo maana barabara inaharibika. Sasa nadhani ni vizuri tungelinganisha kwamba, hivi kweli barabara ni muhimu kuliko wale watu, ambao sasa wanafika mahali kiasi kwamba, wanashindwa kumudu maisha yao. Kwa sababu hawana *alternative* ili mizigo iende kule, Musoma tunapata sukari kutoka Moshi, tunapata *cement* kutoka Tanga, tunapata ngano kutoka Arusha na hayo yote ni mahitaji ambayo ni muhimu kwa wananchi wa Mara na sasa kama hiyo ndiyo hali sasa watafanyaje.

Ni afadhali kidogo basi Musoma lakini kama watu wa Serengeti, ina maana hiyo mpaka izunguke ifike Musoma tena halafu ndiyo irudi Serengeti. Kwa hiyo, katika hali hiyo ni kwamba, hayo maisha hawatayaweza, kwa hiyo, kuna *crisis* kubwa, ambayo sasa imeanza kule. Sasa ni vizuri Serikali ingeangalia itafanya nini katika hilo, kwa sababu kutoka shilingi 15,000/= mpaka shilingi 200,000/=, kwa kweli hilo sio ongezeko la kawaida.

**MWENYEKITI:** Nadhani Serikali yetu huwa ni sikivu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hili suala tutalipeleka kwenye Bodi ili wajaribu kufikiria na kuangalia uwezekanao wa kutumia njia nyingine ya ku-*compensate* ili tuweze kutoa unafuu, ambao Mheshimiwa Mbunge anautaka.

**MWENYEKITI:** Nadhani unasimama kushukuru tu Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, anaposema litaenda tu kwenye Bodi, kwa kweli naamini hata kama litaenda kwenye Bodi, suala hilo haliwezi kupata majibu. Kwa sababu Bodi ndiyo iliyoyaangalia yote hayo, ikaamua kupandisha viwango hivyo vya malipo. Kwa hiyo, leo unapomrudishia afanye masahihisho wala hawatafanya. Kwa hiyo, ni vizuri tungeangalia kwamba, hilo tulifanyeje kabla hata hatujaenda kwenye hizo hatua nyingine.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Matumizi si Kikao cha kufikia maamuzi kuhusu lile analotaka Mheshimiwa Mbunge. Mnachodai hapa ni maelezo na mimi naona kwenye hili, Serikali imejibu vizuri kwamba, imepandishwa kutoka shilingi 15,000/= mpaka shilingi 200,000/=. Waziri amekiri kwamba, hii kwa sababu ya matatizo maalum ya Mkoa wa Mara, kwa sababu hii ni njia moja muhimu sana ya usafiri, kwa jinsi wanavyohusiana na Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha, wanakwenda kulifikiria. Amediriki hata kusema, atatazama njia nyingine za kufidia. Sasa jamani kweli hapo baada ya maelezo hayo, nitakuwa nakipeleka kikao kwenye

wajibu ambao sio wake kwamba, hapa tulazimishe mpaka Sera fulani ibadilike ,ambayo si kazi ya Kamati ya Matumizi. Nadhani tulidhike ha hilo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 – *Foresrty and Beekeeping* … …. …. … Sh. 9,514,488,100/=

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwi Mwenyekiti, *vote* 69, programu ya 30 - *Natural Resources Development, subvote* 3001 - *Forestry and Beekeeping*, kifungu kidigo 250100, mshahara upande wa Idara hiyo...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimekwishasema kwamba, mshahara tunao-*attach* sisi kama Wabunge, Serikali inawajibika kwa Bunge kupitia Mawaziri. Huwezi kuchukua mshahara wa Mkurugenzi wa Misitu, hairuhusiwi. Kwa hiyo, kama una jambo litafute katika kasma hizi ndogo, uone suala lenyewe kama linahusu nyuki, misitu au lolote lile.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* hiyo hiyo, *subvote* 3001 kifungu kidogo cha 250100.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Phares K. Kabuye hukuelewa, tunaendelea, nakuomba ukae chini. Jamani hapa ni mahali muhimu sana, panaangaliwa na watu wote na hii tabia inayoanza kujitokeza kwamba, Spika anatoa *ruling* halafu mtu anasimama anabishana naye, rudini kwenye Kanuni. Utaratibu wa kutokubali aliyosema Spika, umeelezwa kwenye Kanuni, lakini kwa sasa nikishasema ndiyo mwisho. Naomba msirudie tena, Kikatiba hatuwezi kuchukua mshahara wa Mkurugenzi, Wakurugenzi hawawajibiki kwetu, wanawajibika kwetu kupitia kwa Mawaziri. Kwa hiyo, ukikosa nafasi ya ule mshahara pale mwanzo, *administration and general*, huwezi kuendelea kila idara, nyuki unashika mshahara, misitu unashika mshahara, hatuwezi kuendesha hivyo. Kwa hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan A. Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo.

**MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti programu ya 30, kifungu 3001, kifungu kidogo 260500, ninaomba maelezo tu. *Military Procurements, Supplies and Services,* kwenye Idara hii maelezo yake ni nini, kuna *Military* humu?

**WAZIRI WAMALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani labda *terminology* iliyotumika ndiyo inayomshitua Mheshimiwa General. Lakini napenda nimtaarifu kwamba tuna vikosi ambavyo vina siraha vya kuzuia ujangiri wa baharini au majini na kwenye mbuga na misitu, na tuna nunua bunduki kwa taratibu zilizowekwa kisheria.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi *terminology* isingekuwa *military,* ingekuwa *para-military*.

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Waziri, ni kweli kabisa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 – *Fisheries* … … … … … … Sh. 6,834,257,700/=

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mhesimiwa Mwenyekiti, *subvote* 3002, *item* 270700 - *Naval and Marine Operations.* Asubuhi katika mchango wangu, nilizungumzia kuhusu habari za uvuvi katika eneo la Kilwa na wananchi ambao wamenyang'anywa nyavu zao na nilitaja kwamba, kuna meli katika ufukwe wa pwani, sio kule kwenye umbali ambao zile meli zinatakiwa ziwepo. Kitu hiki kinaendelea katika Wilaya ya Kilwa, kwa meli kuja pale haziendi mbali kule kunakotakiwa zile meli zikae au zivue, zinavua katika maeneo ya ufukwe. Sijapata majibu ya hili suala la wananchi kunyang'anywa nyavu zao na vile vile sijaelewa hizi meli nilizozitaja mpaka namba na majina yake, hatima yake ni nini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, *size* ya nyavu zinazoruhusiwa, inategemeana zinatumika maeneo gani. Nyavu zinazotumiwa na meli, zinaruhusiwa kuwa na matundu madogo zaidi kuliko zinazotumika ufukweni kwa sabababu mbili; meli haiwezi kuja karibu na ufukwe, ikifanya hivyo, itakwama kwenye mchanga, wanaovua kwa makokoro ya mikono, wanakuwa kwenye sehemu ambako wanaweza kusimama, yaani kwenye ufukwe, sasa ukitumia nyavu ndogo unaua mazalia ya samaki. Kwa hiyo, utaratibu ni kwamba, wanapovua maeneo ambayo yako mbali ya ufukwe, wanavua na samaki wengine. Sasa kuanzia mwaka huu, tumeweka utaratibu, wamesaini mikataba kwamba, kuna kitu tunaita *by-catch,* ina maana samaki watakaovuliwa ambao sio wale wanaohusika, inabidi wawaambie wananchi kuja kuwachukua kwenda kutumia, mara kwa mara wanapeleka kwenye shule zilizo karibu kwa ajili ya kitoweo.

Kwa hiyo, zile meli ambazo ameziona ni *lisenced,* meli za Tanzania kwa bahati nzuri zina bendera ya Tanzania na maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, yanaruhusiwa na Sheria ya Uvuvi, ila haturuhusu aina ile ya nyavu zitumike mwaloni au ufukweni, kwa sababu zitazoa na mayai ya samaki na samaki ambao ni wadogo ambao wanatakiwa ku-*hibernate.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi**,** nadhani umepata maelezo?

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo yake, lakini mimi nimeeleza kwamba, hizo meli zinavua maeneo ambayo hayastahili kuvua. Kwa taarifa zilizopo Kilwa na ndio maana nikaileta hiyo taarifa, ninaelewa kwamba, sheria inasema hizo meli zivue mbali na wale samaki wanaotakiwa, wanaokuwa wadogo wanatumika kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri. Lakini, hizi meli hazivui kwenye hayo maeneo na ndio maana wananchi wameweza kuziona, kuona majina yake pamoja na namba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko katika maeneo ambayo hazistahili kuvua. Ahsante. Ninaomba jibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa anachozungumza Mheshimiwa Mbunge, lakini sisi ndio tunaoiongoza hiyo Sekta na ndiyo walinzi wa ile sheria. Yale maeneo wanaruhusiwa kuvua. Kamba huwezi ukawapata katika eneo ambalo siyo hilo analolieleza Mheshimiwa Mbunge. Kamba wanapatikana kwenye maeneo hayo na ndio maana kama wapo *lisenced* kuvua Kamba, wakivua samaki wengine ambao ndio nilisema ni *by-catch*, hawaruhusiwi kuwachukua, wanatakiwa kuwagawia wananchi na wamekubali mwaka huu, wamesaini mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Mbunge, aking'ang'ana kwamba, hawaruhusiwi kuvua sehemu hizo, wakati wako *lisenced* kuvua sehemu hizo, kidogo siwezi kuwa na jawabu zaidi ya hilo. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Labda tu wawe wanawapa samaki sasa, maana yake hilo eneo wanalovua ili waelewane, nadhani hilo ndio tatizo. Basi, nadhani suala hapo ni kufuatilia haki iliyopo ya wananchi kupata samaki wao. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Programu namba 30, *subvote* 3002, kifungu kidogo 28500, hizi *Transfers and Subsidy to Institutions at the same Level of Government*. Nina-*assume* kwamba, Taasisi kama za Uvuvi, *TAFIRI* zinaingia hapa. Sasa, ninalotaka kuuliza ni kwamba, nimesoma kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 39, kifungu namba 63 kwamba, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi itaendelea kufanya utafiti wa uvuvi kwenye Bahari ya Hindi, Maziwa Makuu na Madogo, Mito na Mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaendelea kueleza kwamba, baadhi ya tafiti zitafanywa kutumia Mifuko iliyotajwa hapo. Lakini, nataka kuzungumzia Ziwa Nyasa, ingawa ni Ziwa kubwa, lakini haliko kwenye Mifuko hii iliyotajwa. Nataka kwanza nieleweshwe, je, kutakuwa na hela labda za Wizara, *other than* hizi za Mifuko hii ambazo utafiti utafanywa katika Ziwa Nyasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalisema hili kwa sababu katika Ziwa Nyasa, kuna samaki karibu aina tatu hivi, ambao walikuwa ni *commercial* na wananchi ndio walikuwa wanavua kwa wingi na walikuwa wazuri sana kwa kitoweo, wametoweka na Waziri wa wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, alitaja kidogo alipozungumza kwenye hotuba yake jana.

Kwa hiyo, tunataka kujua kama utafiti huu utakwenda kweli mpaka kwenye Ziwa Nyasa na ikiwezekana, je, wataweza vile vile kuangalia, kwa nini hawa samaki wametoweka na kama kuna uwezekano wa ku-*re-introduce* hao samaki, kwa sababu walikuwa ni wa muhimu sana kwenye mazingira haya? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri na nina hakika, mafungu siyo hayo tu, kwa sababu kama nilivyoeleza kwamba, tunaanzisha Mfuko Maalum wa shughuli za uvuvi. Sasa, tunaweza kuchukua fedha mle, kufanya *specific research* anayoisema, ambayo kwa kweli ina umuhimu kwa wananchi wa eneo la Ziwa Nyasa na maeneo mengine, ambako baadhi ya samaki wametoweka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Zimebaki dakika tatu tu, tutaingia kwenye *Guillotine*.

Kifungu 4001 - *Tourism*… …… … … … … Sh. 3,336,599,000/=

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Kifungu hicho, s*ubvote* 4001 na *item* 310700, ningependa kuulizia kuhusu hiyo *program design,* ambayo ilivunja Katiba katika *Tourism Development,* ambayo iliwafanya wananchi wa Mara wazuiliwe kuwinda wakati Watanzania wengine na watalii wengine wanaendelea kuwinda.

Mhehimiwa Mwenyekiti, hilo ndio ningependa nipate ufafanuzi na nijue ya kwamba, pamoja na kuvunja Katiba, ni *section* gani ya Sheria za Nchi, zilizoruhusu kufanya hivyo na kama hiyo *legislation* iliyoruhusu kufanya hivyo ililetwa hapa Bungeni na kuidhinishwa kwamba, Wananchi wa Mara tu wasiwinde, lakini wananchi wengine na watalii waendelee kuwinda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, unachosema ni kizito sana, kuvunja Katiba; unaweza kufafanua hii kuvunja Katiba?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Ninahusisha Katiba, kwa sababu Katiba ya nchi inatueleza kwamba, kusiwe na ubaguzi wa aina yoyote wa rangi, wa kabila, wa dini na nadhani hizo ndio sera ambazo zinaongoza nchi yetu. Ninaamini hivyo kwa vyama vyote, ndio maana nimezungumzia Katiba kwamba, ule ni ubaguzi kwa sababu, kama ni *conservation* kwamba, wanyama wasiuawe, hiyo kuwinda *(Hunting)* ipigwe marufuku, ibaki *Photographic Tourism* na aina nyingine.

Lakini kama *hunting* inaendelea na inaendelea kwa watu wengine, lakini watu fulani wanazuiliwa, hili ndio nimeona kwamba, ni uvunjaji wa Katiba na vile vile ningependa ufafanuzi kujua ni sheria gani iliyotumika kwa Waziri kufanya hivyo?

**MWENYEKITI:** Kiti hakikubali juu ya hilo, maana yake unatanguliza hukumu, wewe unasema uvunjaji wa Katiba. Eleza jambo lenyewe tu lililotokea. Ni kwamba, unavyoamini wewe, watu wa Mara hawaruhusiwi kuwinda ila watu wengine wote duniani wanaruhusiwa hapa. Si ndio unachosema, aeleze Waziri? Sasa, kama ni kuvunja Katiba au nini, yatafuata baada ya majibu. Siyo utangulize wewe hukumu kwamba,

Katiba imevunjwa. Hatuwezi kukaa hapa Wabunge wa Bunge hili, tukashuhudia kuvunjwa kwa Katiba. Kwa hiyo, swali lako ni hilo?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mwenyekiti, sawa, ninakubali mwongozo wako.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo niliyoyatoa wakati najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, nilisema kwanza, kwa bahati nzuri mwenyewe kasema, uwindaji ambao unafanywa na wageni ni wa *Trophy Hunting*, siyo wa kupata nyama.

Sasa, uwindaji wa kupata nyama uko kwenye *arrangement* ya *Wildlife Management Areas*, ambapo kuna baadhi ya vijiji vya Mkoa wa Mara, wameomba tuwaingize kwenye hiyo programu.

Tutakapowaingiza kwenye hiyo programu, watatakiwa kutunza kwanza wanyama waweze kuzaliana, waongezeke. Halafu watakuwa na maamuzi ya wanyama au swala wangapi, wawindwe kwa ajili ya kitoweo na wanyama gani waweze kumpa mtu ambaye anawinda kwa ajili ya *trophy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge, awe na subira, sheria hii tutaileta mwezi wa kumi na maeneo haya kama nilivyosema, *study* itaanza Septemba, tutaainisha maeneo yote hayo. Hakuna mwananchi yeyote, ambaye anazuiliwa kuwinda wanyama na kila mwezi wa saba kwa sasa hivi, wengi wameleta maombi na wanapewa leseni za kuwinda.

Mfano unataka Nyati mmoja au wawili, unashughuli zako, unaruhusiwa. Lakini unaruhusiwa kwa kufuata taratibu za leseni na kupewa vibali na *District Wildlife Officer,* kulingana na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo siyo kwamba, sheria ina ubaguzi wa aina yoyote, haina ubaguzi wowote.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 81(6) inasema, zikibaki dakika kumi kabla ya muda wa kuahirisha Bunge kwa siku hiyo na Kamati bado haijamaliza kufikiri, mafungu yote yanayohusika, Mwenyekiti atafunga mazungumzo yoyote, yaliyoruhusiwa katika aya (b) na (c) za Kanuni na papo hapo atawahoji kuhusu mafungu yaliyosalia kama yapo. Kwa hiyo, tunaingia hatua hiyo sasa.

Kifungu 4002 – *Antiquities Unit* … … … … … Sh. 1,262,935,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kifungu 1001 – *Administration and General* … … Sh. 200,000,000/=
Kifungu 1003 – *Policy and Planning* .. … … … Sh. 2,000,000,000/=
Kifungu 2001 – *Wildlife* … … … … … … …… Sh. 2,149,000,000/=
Kifungu 3001 – *Forestry and Beekeeping* … … … Sh. 6,982,750,500/=
Kifungu 3002 – *Fisheries* … … … … … … ..... Sh. 8,600,000,000/=
Kifungu 4001 – *Tourism* … … … … … … ..... ..... Sh. 1,971,300,000/=
Kifungu 4002 – *Antiquities Unit* … … ……… … Sh. 2,786,699,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu, Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2006/2007 kwa Wizara ya Maliasili na Utalii na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Makadirio hayo sasa yakubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo. Ni bahati mbaya mwisho wa wiki hii, yaani kesho, hatutakuwa na semina.

Semina iliyokuwa imepangwa, haikukamilika vizuri, lakini tarehe 22 Julai, 2006 na 23 Julai, 2006, yaani tarehe 22 Julai, 2006 itaanza saa 4.00 asubuhi na itakuwa ni siku ya Jumamosi, Wizara ya Maji.

Tarehe 23 Julai, 2006 kuanzia saa 5.00 asubuhi, ili kuruhusu wale wanaokwenda kwenye nyumba za Ibada waweze kwenda, ambayo itakuwa ni semina ya Kilimo. Kwa hiyo, Maji tarehe 22 Julai, 2006 na Kilimo tarehe 23 Julai, 2006, lakini kesho hatuna semina, ni utawala binafsi.

Tangazo la pili, nimepokea ombi kutoka kwa Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mbunge wa Tarime, kwamba anaomba muda zaidi wa kukamilisha taarifa yake ya kuthibitisha yale aliyoyasema wiki ilyopita. Yeye aliomba siku tatu, nimempa mbili tu.

Kwa hiyo, Jumatano tarehe 19 Julai, 2006 kabla ya saa 7.00 mchana, nitalazimika nitoe taarifa hapa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, atupatie uthibitisho wa yale aliyoyasema wakati Naibu Spika akiwa kwenye Kiti hapa, ili tuweze kuyapeleka sehemu inayohusika, kuona kama yanathibitisha ukweli wa yale aliyosema.

Kwa bahati njema leo ameukubali mwongozo wa Spika. Alikuwa anataka kufanya mengine tena. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, twende taratibu, bado miaka minne na nusu.

Basi, baada ya hapo kwa kuwa sasa naona muda wenyewe umefika wa kuahirisha Bunge, labda bado sekunde tu, kwa hiyo, siwezi kumsumbua Waziri wa Nchi. Naahirisha Kikao hiki cha Bunge hadi Siku ya Jumatatu Saa 3.00 Asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.44 usiku, Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 17 Julai, 2006 Saa 03.00 Asubuhi)*